**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Thelathini na Nane – Tarehe 7 Agosti, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:-**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa mwaka wa Fedha 2006/2007.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI (K.n.y. MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO) - MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA:-**

Maoni ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2006/2007.

**MHE. LUCY F. OWENYA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:**

Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2006/2007.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 355

**Umuhimu wa Barabara ya Mbelei – Mayo-Bumbuli**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa, zipo barabara Wilayani Lushoto na hasa Jimbo Bumbuli ambazo zimethibitika kuwa ni za muhimu sana kiuchumi kama ilivyo kwa barabara ya kutoka Mbelei- Kwesiwe-Baga-Mgwashi-Mayo-Bumbuli yenye urefu wa kilomita 50 inayopita kwenye maeneo yanayolimwa Mazao kama Chai, Kahawa, Nyanya, Viazi, Vitunguu, Pilipili, Mahindi, Maharage na kadhalika:-

(a) Je, barabara hiyo itatengenezwa lini na kufikia kiwango cha changarawe?

(b) Je, Serikali itaitembelea lini barabara hiyo ili ithibitishe na kuona umuhimu wake katika uchumi wa Jimbo la Bumbuli?

(c) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba, sasa kuna umuhimu wa kukubali kuipandisha daraja barabara hiyo iwe ya Mkoa na kuipunguzia Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto mzigo huo mzito?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara ya Mbelei-Kwesiwe-Baga-Ngwashi-Mayo hadi Bumbuli yenye urefu wa kilomita 50 ni muhimu sana kiuchumi kwa kuzingatia kwamba inapita katika maeneo ya kilimo cha mazao ya biashara na chakula na pia sehemu zenye huduma za Taasisi mbalimbali kama vile Zahanati za Mbelei, Baga-Mwashi na Hospitali teule ya Bumbuli na Kituo cha Utafiti cha Chuo Kikuu cha Sokoine katika msitu wa Mazumbai. Barabara hii ipo katika mpango wa matengenezo kwa kiwango cha changarawe kama ifuatavyo:-

Kutoka Mbelei-Kwesiwe-Baga-Mgwashi yenye urefu wa kilomita 26 ipo katika mpango wa matengenezo kwa kiwango cha changarawe chini ya Mpango wa Kilimo na Uboreshaji wa Masoko *(Agriculture System Marketing Development Programme*) ikiwa ni msaada wa fedha kutoka *African Development Bank (ADB).* Pia matengenezo makubwa yamefanyika katika sehemu ya Galambo-Bumbuli yenye urefu wa kilomita 5.0, matengenezo hayo yamefanywa na Wakala wa Barabara Mkoa wa Tanga. Sehemu iliyobaki ni Mgwashi –Galambo yenye urefu wa kilomita 19.0 ambazo zipo katika makisio ya mpango wa bajeti ya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2006/2007. Kiasi cha shilingi milioni 8 kimetengwa kwa ajili ya barabara hii.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto mpaka sasa imekwishatambua umuhimu wa barabara hiyo kiuchumi na kijamii, ndiyo maana Halmashauri imependekeza sehemu ya Mbelei-Kwesiwe-Baga- Mgwashi yenye urefu wa kilomita 26 kufanyiwa matengenezo makubwa kwa msaada wa fedha kutoka *African Development Bank*, kwa kupitia Mradi wa "*Agriculture System Marketing*

*Development Programme (ASMDP)"* kwa gharama ya shilingi milioni 700. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inakubali kabisa kwamba itatembelea eneo hilo la barabara wakati wa kukagua shughuli za barabara zinazopatiwa fedha kutoka Mfuko wa Barabara katika mwaka wa fedha wa 2006/2007.

(c) Mheshimiwa Spika, barabara ya Mbelei-Kwesiwe-Baga-Mgwashi- Mayo-Bumbuli ni miongoni mwa barabara sita za Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ambazo zimependekezwa kupandishwa daraja kutoka ngazi ya Wilaya na kuwa katika ngazi ya Mkoa. Barabara hizo zilipendekezwa katika kikao cha Bodi ya Barabara ya Mkoa kilichofanyika tarehe 26/9/2003 kama ifuatavyo:-

(a) Mlalo – Umba (Mng'aro) kilomita 25.9;
(b) Mbelei – Mgwashi-Bumbuli kilomita 50.0;
(c) Dochi- Mombo kilomita 20.0;
(d) Mlalo- Mlalo-Milingano – Mshewa kilomita 78.1;
(e) Soni – Mponde kilomita 14.0; na
(f) Vuga – Mponde – Wena Kilomita 22.5.

Mheshimiwa Spika, suala la kuzipandisha daraja barabara hizi linashughulikiwa na Wizara ya Miundombinu ili kuona kama upo uwezekano wa kuzihudumia katika ngazi ya Mkoa. Majibu yatakapokuwa tayari, hasa baada ya kupitishwa kwa Sheria inayotarajiwa kuwasilisha hapa Bungeni kupendekeza baadhi ya barabara kuwa za Mkoa. Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto itajulishwa ili iweze kuzikabidhi kwa Wakala wa Barabara wa Mkoa na kuweza kupunguziwa mzigo wa kuzihudumia.

Na. 356

**Majengo ya Mahakama ya Mwanzo Gairo**

**MHE. AHMED M. SHABIBY** aliuliza:-

Kwa kuwa, jengo la Mahakama ya Mwanzo Gairo lilithibitishwa na Msajili wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam tarehe 10/3/2006 kuwa haifai kwa matumizi ya Kimahakama; na kwa kuwa, Jaji Kiongozi wa Kanda ya Dar es Salaam alithibitisha pia kuwa, jengo hilo halifai na kwamba, lilijengwa kwa udongo mwaka 1926 likiwa kama Kanisa:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa, kuna sababu ya kujenga jengo jingine jipya?

(b) Je, Serikali haioni kuwa, inahatarisha maisha ya watumishi wa Mahakama na wadau wake?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mbunge wa Gairo, lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, majengo mengi ya Mahakama, hasa Mahakama za Mwanzo, ni machakavu na inawezekana kuwa mengine yanahatarisha maisha ya watumishi na wateja wanaofika kupata huduma za Mahakama. Serikali inatambua hatari hiyo na ndio sababu imeanzisha Mpango Endelevu wa miaka mitano wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama za Mwanzo. Mpango huu ulioanza Mwaka wa Fedha 2004/2005 utatekelezwa kwa awamu hadi kufikia Mwaka wa Fedha wa 2008/2009. Vilevile kupitia fedha za ufadhili za Maboresho ya Sekta ya Sheria kasi ya ujenzi wa Mahakama za Mwanzo itaongeza. Mahakama ya Mwanzo, Gairo ni moja ya majengo yaliyoingizwa kwenye mpango huu wa miaka mitano ya ujenzi na ukarabati wa Mahakama za Mwanzo.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, Mahakama ya Mwanzo ya Gairo, inafanana na Mahakama za Mwanzo za Idibo, Chakwale na Nungu, je, hizo nazo zipo katika Mpango wa ujenzi wa miaka mitano? Ahsante.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, mpango huu unahusu Mahakama zote za Mwanzo, na kwa hivyo Mahakama alizozitaja nazo zinahusika.

**SPIKA:** Naona leo Waheshimiwa Wabunge hawakuchangamka kabisa.

Na. 357

**Madai ya Walimu**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa, wapo walimu ambao hawajalipwa madai yao kama vile ya matibabu, nauli wakati wa likizo na kadhalika, kutokana na sababu ya kupotea kwa viambatanisho vya madai yao; na kwa kuwa, viambatanisho hivyo vimepotelea kwenye majalada mikononi mwa mwajiri:-

Je, Serikali haioni kwamba, kuwanyima walimu madai yao ni kutowatendea haki?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekuwa ikilipa madai ya walimu wa Shule za Sekondari, Vyuo vya Ualimu na Wakaguzi wa Shule yakiwa na viambatanisho. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kumnyima mwalimu malipo ya madai

yake, endapo ni kweli kuwa viambatanisho vya madai vimepotea mikononi mwa mwajiri ni kutomtendea haki.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa madai huwa yana mazingira tofauti, tunawaomba wenye madai ya aina hiyo watuletee ili tuyafanyie kazi.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. . Nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Kwa kuwa pamoja na kulipa madeni ya walimu ya muda mrefu. Vilevile Serikali bado inazalisha madeni mapya badala ya kwenda sambamba na wakati, pale walimu wanapohitaji haki zao. Je, Serikali ni lini basi itaacha tabia ya kuzalisha madeni haya ili walimu sasa wawe wanaenda sambamba kazi na dawa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, haina namna ya kuepuka kuzalisha madai. Kwa sababu kila mwaka tunaajiri walimu na kila mwaka walimu wanakwenda likizo. Kwa hiyo, sisi tutaendelea kupokea na kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyotujalia uwezo tutayalipa madeni hayo, kwa sababu ni haki zao.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nilikuwa na swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imekuwa ikiahidi kwa muda mrefu na hata katika Mkutano huu wa Bajeti kwamba malipo ya walimu ambayo ni stahili zao yatalipwa ndani ya mwaka huu wa fedha 2006/2007; na kwa kuwa tunafahamu kwamba mwaka fedha utaishia mwezi Juni, mwaka kesho. Je, lini Serikali itakuwa imeishawalipa walimu madai yao ambayo yamekuwepo na yameishathibitishwa ili swali hili lisije likaendelea kujitokeza mara kwa mara katika Mikutano yetu ya hapa Bungeni? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Ningependa tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba madai ya walimu yapo kwanza katika sehemu mbili. Yapo yale ambayo yanalipwa chini ya Ofisi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na yale ambayo yapo chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi hasa kwa ajili ya walimu wa Sekondari, Wakufunzi wa Vyuo vya Ualimu pamoja Wakaguzi hao ndiyo tumeishawahakikishia hapa Bungeni kwamba watalipwa mwaka huu wa fedha kuanzia sasa wakati wote Hazina itakapokuwa tayari, kwa sababu tayari kumekuwa na mawasiliano kati ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Hazina na tumekubaliana,watalipa Hazina moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, pia nilitaka tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kama alivyosema Naibu Waziri, kwamba haya madai yataendelea kuwepo, lakini tutajitahidi kadri ya uwezo wetu kila yanapotokea madai basi tunalipa.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali inaelewa kwamba upotevu wa viambatanisho hivyo husababishwa na watendaji. Je, kwa wale watendaji wanaopoteza viambatanisho hivyo huchukuliwa hatua gani? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli, ni kitendo kisichokubalika kabisa katika jamii cha kupoteza viambatanisho ambavyo ni kumbukumbu halali. Kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kweli panapojulikana kwamba hapo ni uzembe umetumika wahusika wanapaswa kuchukuliwa hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchukua nafasi hii pia kutoa wito kwa wale wote viongozi ambao wanahusika katika kuhamisha walimu kutoka sehemu moja kwenda nyingine, kwa kweli uhamisho ni jambo linalohitaji maandalizi ili uhamisho uende sambamba na uwezo wa fedha. Kwa hiyo, wajitahidi kadri iwezekanavyo kutokutoa uhamisho usiokuwa wa lazima ili kuepuka madai yasiyokuwa na mpango. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea kwenye Wizara ya Miundombinu, ninalo tangazo moja.

Waheshimiwa Wabunge, mnafahamu kwamba timu zetu mbili *Bunge Football* na *Bunge Netball* zilikwenda Kongwa *weekend* hii, na sikuweza kujizuia kuweza kutoa tangazo hili kwa sababu linafurahisha. *Bunge Football Club* imewafunga Ma-Veterani wa Kongwa magoli sita kwa bila. Naiomba Timu yetu ya Bunge hiki ndicho kiwango cha magoli sita, yeyote atakayecheza na sisi awe anafungwa magoli sita. *(Makofi)*

*Bunge Netball Club* imeshinda akinamama Veterani Kongwa *point 11* kwa *point 10.* Taarifa hii ni nzuri nimeipata kutoka kwa Kocha Msaidizi Mheshimiwa Mohamed Rajab, nampongeza sana, na *DC* wa Kongwa ametueleza kwamba timu zetu zilikuwa ni kielelezo katika nidhamu pia. *(Makofi)*

Na. 358

**Barabara ya Itigi - Mbeya**

**MHE. JOHN P. LWANJI** aliuliza:-

Kwa kuwa, barabara ya kutoka Itigi kwenda Mbeya imetengenezwa kwa kiwango cha kuridhisha kutoka Kirumbi hadi Kintanula, kazi hii imefanyika nusu tu na kuziacha sehemu zitokazo Itigi- Mgandu- Kiyombo-Kirumbi na kutoka Kintanula hadi Rungwa bila matengenezo yoyote walau kwa kiwango cha udongo:-

(a) Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara hiyo muhimu ili kurahisisha usafiri wa abiria na bidhaa kutoka maeneo hayo?

(c) Je, ni kwa nini Serikali imekuwa haitilii maanani barabara hii na kuyaacha maeneo hayo yenye rasilimali nyingi bila usafiri wa uhakika hasa nyakati za masika?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:

Barabara ya Itigi Mkoani Singida hadi Ruangwa Mkoani Mbeya yenye urefu wa kilometa 197 ni sehemu ya Barabara Kuu ya Mbeya - Makongorosi – Ruangwa – Itigi hadi Mkiwa. Sehemu kubwa ya barabara ya Ruangwa – Itigi ni ya udongo, isipokuwa eneo la Kitanula hadi Kirumbi ambalo lilitengezwa kwa kiwango cha changarawe kwa msaada wa Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB),* chini ya Mradi wa Matengenezo ya Barabara Kuu za Ukanda wa Magharibi/Kati (*Midwest corridor*) zilizoharibiwa na mvua za *El-nino.*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu umuhimu wa barabara hii. Hata hivyo kutokana na ufinyu wa fedha zilizotolewa na *ADB* kwa mradi huo haikuwezekana barabara yote ya Ruangwa – Itigi kufanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe. Shabaha ya Wizara ya Miundombinu kwa kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* ni kuendelea kuifanyia matengenezo barabara hiyo kulingana na upatikanaji wa fedha ili iweze kupitika kwa urahisi kipindi chote cha mwaka.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiifanyia matengenezo mbalimbali barabara hii kati ya Itigi – Mgandu – Kiyombo kutegemeana na uwezo wa kifedha. Kuanzia mwaka 2001/2002 hadi 2005/2006 Serikali imetumia jumla ya shilingi milioni 715 kufanya matengenezo kati ua Kirumbi na Itigi katika barabara husika, hali inayoonyesha wazi kuwa barabara hiyo haikusahauliwa.

Ni kweli kwamba nyakati za masika baadhi ya sehemu za barabara hii hupitika kwa taabu kutokana na kuwa barabara hii sehemu kubwa ni ya udongo. Lakini si sahihi kusema kusema kwamba Serikali haitilii maanani barabra hii, kwani matengenezo mbalimbali yamekuwa yakifanyika kwa kutegemeana upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha 2006/2007, Serikali inatarajia kutumia kiasi cha shilingi milioni 267 kufanya matengenezo mbalimbali katika barabara ya Rungwa – Itigi ikiwa ni pamoja na matengenezo ya kawaida, matengenezo ya vipindi maalumu, matengenezo ya sehemu korofi na matengeneo ya madaraja.

Aidha, barabara hii ya Rungwa – Itigi ni sehemu ya barabara ya Mbeya – Chunya - Makongolosi – Rungwa – Itigi mpaka Mkiwa ambayo ipo kwenye mpango wa kujengwa kwa kiwango cha lami. Kama nilivyoeleza nilipojibu swali namba 96 la Mheshimiwa Victor Mwambalaswa Mbunge wa Lupa, hadi sasa kilometa 115 kati ya Mbeya hadi Makongolosi zimekwisha fanyiwa usanifu na sasa tupo kwenye hatua ya kutafuta wakandarasi kwa ajili ya ujenzi. Sehemu ya barabara iliyobaki kati ya Makongolosi na Itigi hadi Mkiwa itashughulikiwa kutegemea uwezo wa Serikali kifedha kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa kipindi cha mwaka 2005 – 2010.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tayari nina ahadi ya maandishi kwamba barabara hii itashughulikiwa kikamilifu mara baada ya ujenzi wa barabara itokayo Mbeya hadi Makongolosi; na kwa kuwa wakati wa Bajeti Wizara hii iliahidi pia vilevile kwamba barabara inayotoka Makongolosi-Rungwa, Kiwele hadi Sikonge nayo iliahidiwa kujengwa mara baada ya kazi itakapokamilika pale Makongolosi. Je, Wizara ni kipaumbele gani inatoa ni kwa barabara inayotoka Rungwa-Itigi au barabara inayotoka Rungwa kwenda Sikonge au zinajengwa barabara zote sambamba kwa wakati mmoja?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, Serikali imeahidi kwamba itashughulikia barabara zote mbili yaani kutoka Mbeya-Makongolosi- Rungwa – Itigi mpaka Mkiwa na vilevile hiyo barabara ya Rungwa mpaka Ipole-Sikonge kwenda Tabora.

Mheshimiwa Spika, lakini matengenezo ya barabara hizi kwa kweli zitategemea uwezo wa kifedha. Uwezo wa kifedha ukiruhusu tutatengeneza barabara zote katika kipindi hiki ambacho tunacho.

Mheshimiwa Spika, lakini hatuwezi kupata uwezo kwa mara moja, kutegemea kwamba barabara zote zitatengenezwa sambamba inaweza ikawa ngumu. Kwa hiyo, kipaumbele kitawekwa katika barabara ambayo nimeieleza ya Makongolosi-Rungwa-Itigi mpaka Mkiwa wakati ambapo tunaendelea kutafuta tena fedha za Rungwa-Ipole-Sikonge mpaka Tabora.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa tatizo la barabara za Manyoni Magharibi zinafanana na barabara za Namtumbo katika barabara za kuanzia Mtwarapachani mpaka Mto Sasawara. Wakandarasi wake wamekuwa wakisuasua kuacha vifusi kwa muda mrefu mpaka leo hii kuanzia mto Msangasi, Liguseguse kuna vifusi vya muda mrefu.

Je, Serikali inaweza kwenda kutembelea na kuona kiwango cha wakandarasi hao wanavyosuasusa kutengeneza barabara hizo?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, nje ya Bunge nilishamwahidi Mheshimiwa Vita Kawawa kwamba tutakwenda tukague barabara hiyo, lakini sasa tuweke kwenye *Hansard* wazi kwamba ahadi hiyo itatekelezwa mara baada ya kikao cha Bunge. *(Makofi)*

Na. 359

**Barabara ya Tabora – Kigoma**

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, suala la barabara ya Tabora-Kigoma limesemwa kwa nguvu na mara nyingi na Wabunge wa Mikoa hiyo Tabora na Kigoma.

(a) Je, Serikali inaweza kutoa tamko la uhakika kuwa ni lini barabara hiyo itakamilishwa angalau kwa kiwango cha changarawe ili iweze kupitika wakati wote?

(b) Je, Serikali inajua ahadi ya kukamilisha ujenzi wa barabara hiyo iliyotolewa na Mheshimiwa Rais wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Ismaily Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa barabara ya Tabora hadi Kigoma na uwezo mdogo wa uchumi wa nchi yetu, Serikali imechukua hatua mbalimbali kwa madhumuni ya kujenga barabara husika kwa kiwango cha lami kwa awamu kama ifuatavyo:-

- Sehemu ya Kigoma – Uvinza, kilomita 46. Taratibu za zabuni za kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya usanifu wa barabara hii kwa kiwango cha lami zinaendelea kwa kutumia fedha za Tanzania. Aidha, Serikali imepanga kujenga sehemu hii ya barabara kwa kiwango cha lami kwa kutumia fedha za ndani.
- Sehemu ya Uvinza - Malagarasi kilomita 116. Usanifu wa barabara hii umekamilika. Umoja wa Nchi zinazotoa mafuta kwa Wingi *(OPEC)* umetoa fedha kwa ajili ya kuimarisha sehemu hii ya barabara ka kiwango cha changarawe baada ya awamu ya kwanza ya ujenzi wa makalvati kukamilika kwa kutumia fedha za ndani. Taratibu za zabuni za kumpata Mkandarasi zinaendelea. Aidha, mazungumzo yanaendelea kati ya Serikali yetu na Jamhuri ya Korea Kusini ambayo imeonyesha nia ya kufadhili ujenzi wa daraja la kudumu katika mto Malagarasi na kilometa hamsini za lami kwenye bonde la mto huo.

- Sehemu ya Malagarasi – Kaliau kilomita 104. Ukarabati wa barabara hii kwa kiwango cha changarawe unaendelea kwa fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* kwa gharama ya Jumla ya shilingi bilioni 2.752.

- Sehemu ya Kaliua - Urambo - Tabora kilomita 126. Usanifu wa kina wa barabara hii kwa ajili ya kujengwa kwa kiwango cha lami unaendelea kwa gharama za shilingi bilioni 332.77 zilizotolewa na Serikali ya Tanzania. Juhudi za kutafuta mfadhili kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami zinaendelea.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inajua ahadi ya kukamilisha ujenzi wa barabara hiyo iliyotolewa na Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni za Uchaguzi wa 2005 na juhudi zilizoelezwa hapo juu zinalenga kutimiza ahadi hiyo.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali ndogo la nyongeza kama ifuatavyo:- Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na pia ninaishukuru Serikali kwa hatua iliyofikia.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara tunayoizungumzia ni ya kuanzia Itigi – Tabora na Kigoma; na kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri wakati wa majibu yake hakuzungumzia suala la barabara ya kutoka Itigi kuingia Tabora.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba barabara hiyo nayo ya kutoka Itigi inatengenezwa kwa kiwango cha lami ili kuondokana na usumbufu wakati wa masika?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):**

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo hata wewe utakuwa umeona kwenye swali la Mheshimiwa Mbunge aliloulizia barabara ya Tabora hadi Kigoma hakuwa ameunganisha na Itigi kuja Tabora.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa sababu sasa ameliuliza swali hilo la Barabara ya Itigi hadi Tabora nataka nimweleze kwamba na sehemu hiyo ipo katika mpango ambao nimeeleza hapo awali. Kwa kweli barabara hii tayari usanifu umeshafanyika barabara imefunguka kwa magari na inapitika na iko katika mpango huo na kama tulivyoeleza hapa Bungeni barabara hii tokea Itigi, Tabora na Kigoma Serikali inajaribu kutafuta fedha na tulitaja kwamba moja ya vyanzo ambavyo tunavifuatilia ni Benki ya Abu Dhabi ambako wameahidi kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii mradi tu tutimize masharti fulani fulani ikiwa na kulipa madeni ya nyuma ambayo Serikali yetu inadaiwa na Benki hiyo kazi ambayo imeshaanza kufanyika na Waziri wa Fedha.

**SPIKA:** Nimemwona Mheshimiwa Zitto Kabwe na nimempa nafasi yeye kwa sababu ya mchanganyiko tu lakini pia ili kumkaribisha maana yeye na wenzie *Engineer*

Manyanya na wengine walikuwa wawakilishi wetu kwenye kuangalia uchaguzi wa *DRC Congo.*

Nimearifiwa kwamba Waheshimiwa Wabunge wote waliokwenda *DRC* wamerudi salama na kama mnavyojua mazingira ya *DRC* lolote lingeweza kutokea. Kwa hiyo, tunamshukuru Mungu.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi mambo ya *DRC* tutayaongea zaidi wakati wa Wizara ya Viwanda na Biashara. Naomba niulize swali dogo la nyongeza.

Barabara ya Itigi, Tabora, Kigoma ni barabara hiyo hiyo ambayo inakwenda mpaka Manyovu kwa maana ya Itigi, Tabora, Mwandiga, Manyovu. Na kufuatia majibu ya kutia matumaini ambayo Naibu Waziri ameyaeleza ningeomba atie matumaini pia kwa kipande cha Mwandiga, Manyovu hali ikoje na Naibu Waziri anadhani kwamba eneo hili au kipande hiki cha barabara kitakamilishwa lini? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Spika, barabara ya Mwandiga/Manyovu ipo kwenye mpango na kwenye Bajeti imeonyesha kwamba fedha zipo kwa ajili ya kutengeneza. Lakini Mheshimiwa Mbunge atakumbuka kwamba katika kikao chetu na Wabunge wa Mkoa wa Kigoma tulizungumzia suala hili na tukaahidi kwamba barabara hiyo katika mwaka ujao wa fedha itaongezewa fedha ili iweze kutengenezwa kwa kiwango cha lami kwa kutumia fedha zetu za ndani kwa umuhimu wa barabara yenyewe. Kwa hiyo, napenda nirudie ahadi hiyo kwamba barabara hiyo ipo katika mpango wa kutengenezwa.

Na. 360

**Ujenzi Katika Maeneo Ambayo Hayapimwa**
**Dar es Salaam**

**MHE. CHARLES N. KEENJA** aliuliza:-

Kwa kuwa, inakisiwa kuwa, asilimia zaidi ya sabini na tano ya ujenzi katika Jiji la Dar es Salaam umefanyika katika maeneo ambayo hayakupimwa na baadhi ya maeneo hayo ni hatari, na kwa kuwa, katika maeneo hayo huduma za jamii na uchumi ni duni sana:-

(a) Je, Serikali imekusudia kuchukua hatua gani ili kudhibiti na kurekebisha hali hiyo ya ujenzi?
(b) Je, kwa nini Serikali isichukue hatua za kupima maeneo mengi na makubwa ya miji ili kuweka miundombinu; huduma za jamii na za kiuchumi?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Keenja, Mbunge wa Ubungo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kutambua makazi yaliyojengwa bila ya kupimwa mijini na kuwapatia wananchi leseni za makazi (*residential license*) ikiwa ni utekelezaji wa Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999 fungu la Na. 23. Kazi ya kutambua makazi yaliyojengwa bila kupimwa inafanyika kwa mafanikio katika Jiji la Dar es Salaam, Mwanza na Manispaa za Dodoma na Morogoro. Mfano, katika Jiji la Dar es Salaam, kazi ya utambuzi ilianza mwaka 2004/2005 na hadi Juni 2006 jumla ya miliki 220,131 zilizoko kwenye makazi holela zilikuwa zimeshatambuliwa na leseni za makazi 30,212 zilikuwa zimesajiliwa na kutolewa katika maeneo hayo. Hata hivyo, leseni za makazi hazitolewi kwenye maeneo ya hatari kama mabondeni. Aidha, baada ya makazi hayo kutambuliwa inafuatiwa na kazi ya kuyarasimisha *(regularization*), na kurekebisha miundomsingi.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa na kuanza kutekeleza upimaji wa viwanja na kuweka huduma muhimu za jamii kama vituo vya mabasi, shule na soko kwenye maeneo ya pembezoni mwa miji. Mpango huu una lengo la kudhibiti ujenzi holela unaoendelea kwa kasi katika miji mikubwa na kupunguza msongamano wa watu katikati ya mji. Kwa mfano, mradi mkubwa wa kupima viwanja 20,000 uliotekelezwa katika Jiji la Dar es Salaam kuanzia mwaka 2002/2003 kwa kutumia fedha za mkopo. Hadi Juni, 2006 jumla ya viwanja 31,000 vilikuwa vimepimwa na vinaendelea kugawiwa kwa wananchi. Upimaji wa viwanja unafanyika kwa pamoja na uwekaji wa miundomsingi kama barabara na kadhalika. Mradi kama huo unaendelea kutekelezwa katika Jiji la Mwanza, Mbeya na Manispaa ya Morogoro. Viwanja vinavyopimwa vitagawiwa kwa wananchi kwa njia ya kuchangia gharama.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba ujenzi holela unaendelea kwenye maeneo ya hatari katika miji ya Mwanza, Dar es Salaam na hata Morogoro na katika miji yetu yote. Kama kungetokea mafuriko kama yanayotokea Ethiopia ama vimbunga kama vinavyopiga Madagascar na Uchina tungepoteza maisha ya watu wetu wengi sana. Kwa nini Serikali inalifumbia macho suala hili na ni hatua gani zinazochukuliwa kujirekebisha?

Mheshimiwa Spika, la pili, linahusu miundombinu katika baadhi ya maeneo. Katika miaka ya 1970 maeneo kama Makurumla, Mburahati, Magomeni na kadhalika yalikuwa na barabara za lami. Sasa hivi barabara ni za udongo, wananchi wanahamia kwenye makazi wanayojipimia wenyewe Makuburi, Kimara, Goba na kadhalika hakuna miundombinu yoyote. Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba maeneo haya yanaandaliwa na kwamba mafanikio tumeshapata yanadumishwa. Nashukuru Mheshimiwa Spika.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ujenzi holela unaoendelea katika miji. Ni kweli kabisa kwamba katika miji yetu na hasa katika Jiji la Dar es Salaam watu wanaoishi kwenye makazi ambayo hayajawa *planned* ni zaidi ya asilimia 75. Lakini kama

nilivyoeleza katika jibu langu la msingi kwamba Wizara pamoja na Serikali kwa ujumla imekwishaanza kuchukua hatua za kuhakikisha kwamba watu wasiendelee kujenga kwenye makazi holela.

Lakini pia imeanza kuchukua hatua ya kutambua katika maeneo mbalimbali ambayo wananchi wamejenga kiholela ili kuyafanya yatambuliwe kwa mujibu wa kisheria. Kwa Dar es Salaam kwa mfano milki ambazo zimetambuliwa katika Wilaya ya Ilala ni zaidi ya 58,605, Kinondoni ambazo zimetambuliwa ni zaidi ya 63,146 na Temeke ni zaidi ya 98,380. Kwa hiyo, tunafanya hivi katika kuhakikisha kwamba hawa wananchi wanatambuliwa katika hali halisi ya kisasa. Lakini pia kwa Dar es Salaam kuna mradi ambao unaihusisha pia Benki ya Dunia ambao unagharimu karibu shilingi bilioni 37 wa kurasimisha katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutengeneza miundomsingi ikiwa ni pamoja na barabara.

Kuhusu sehemu yake ya pili, ameeleza kwamba kuna baadhi ya sehemu ambazo zilikuwa ni barabara za lami lakini sasa hivi ni za changarawe. Mimi ningependa kumshauri Mheshimiwa Keenja kwamba ahakikishe sasa anazungumza na Halmashauri yake ya Wilaya ili waweze kutumia fedha za *Road Fun*d ambapo katika Bajeti ya mwaka huu wanakaribu shilingi bilioni 23 katika nchi nzima waweze kuzitumia katika kukarabati baadhi ya maeneo. Lakini pia Bajeti za Halmashauri zetu zina wajibu wa kutengeneza barabara zinazohusika katika kuhakikisha kwamba barabara zinakuwa nzuri katika maeneo yetu.

Katika mradi wa viwanja 20,000 Wizara ya Ardhi imetumia zaidi ya shilingi bilioni 6 katika kuhakikisha kwamba inatengeneza barabara kwenye maeneo ambapo viwanja vinatengwa. Zaidi ya kilomita 677 zimekwishatengenezwa hadi sasa.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii.

Kwa kuwa hivi sasa ujenzi holela unazidi kila kukicha na hasa katika baadhi ya mito iliyokuwa inatiririsha maji kutoka juu kuelekea Pwani kama Mto Kizingo, Msimbazi na mingine watu wanachukua vifusi,uchafu wanakwenda kumimina na baadaye panakalika na huwa wanajenga majumba na Manispaa zipo, uongozi upo wa Dar es Salaam unaona lakini inaelekea umechemsha. Je, Serikali Kuu inasema nini juu ya jambo hili?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**: Mheshimiwa Spika, katika mpango wa kutambua makazi ambayo yamejengwa kiholela haina maana kwamba tutatambua maeneo yaliyomo kwenye mabonde na ndiyo suala la msingi langu lilivyokuwa likijibu. Kwa hiyo, katika maeneo ambayo yako mabondeni kama *Msimbazi Valley* na kadhalika haya hayawezi yakatambuliwa na wala hayawezi yakahusika katika mpango huu kwa sababu haya-*qualify* katika mpango huu. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba Sheria za Ardhi zinazingatiwa ikiwa ni pamoja na Sheria Na. 4, 5 ya Mwaka 1999 ili suala la makazi liweze kuleta manufaa kwa Watanzania wote.

Lakini ningependa kutoa wito kwa Halmashauri za Wilaya na Maofisa Ardhi waliopo katika Halmashauri zetu wahakikishe kwamba Sheria zinazingatiwa na wasiendelee kutoa viwanja kwenye mabonde na kwenye maeneo ambayo hayafai kuwa makazi ya wananchi.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa imedhirika wazi kwamba tatizo la upimaji wa viwanja sasa ni kwa nchi nzima na hasa katika miji na Manispaa zote zilizopo nchini. Je, Waziri atakubaliana nami sasa kwamba inafaa tujielekeze wote huko ili miji yetu isije ikawa ya ovyo na gharama zote hizi zinaonekana zinalipiwa na wananchi baada ya kupimwa. Kwa hiyo , ungekuwa ni mpango maalum kwa nchi nzima?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba tatizo la viwanja si la Dar es Salaam tu liko katika miji yote na hasa kwa kuzingatia kwamba sasa karibu asilimia 2 ya maeneo tuliyonayo ndiyo yame-*cover* eneo la miji katika nchi hii. Kwa hiyo, kuna wajibu wa kila Mamlaka inayohusika kuhakikisha kwamba inapima viwanja kwa ajili ya makazi yake.

Mheshimiwa Spika, katika kutambua suala hili ndiyo maana Wizara ya Ardhi ilianza na Mpango Kabambe wa Kuanza kupima viwanja. Tulianza na mkopo wa shilingi bilioni 8.9 lakini katika mkopo huo umeweza kuzaa hadi shilingi bilioni 21 na hadi sasa hivi vimeshapimwa na vinaendelea kupimwa karibu viwanja 50,000 kwa Dar es Salaam ni viwanja 31,000, Mwanza 9,500, Morogoro viwanja 4,000, Manispaa ya Mbeya viwanja 5,000 na kadhalika.

Napenda kutoa wito katika fedha ambazo zinapatikana ambazo zinatokana na *land rents* katika Halmashauri zetu za Wilaya hizo fedha zitumike katika kupima viwanja katika maeneo yao na viwanja hivyo viweze kuuzwa kwa wananchi kama *revolving fund* ili kusudi suala la viwanja lisiwe tena tatizo katika sehemu zetu za nchi na miji yetu iweze kupimwa kulingana na hali halisi ya makazi.

**SPIKA:** Ahsante tunaendelea. Lakini kabla sijaendelea napenda niseme kwamba uwezo wa Waziri Magufuli kuwa na takwimu kichwani haukuhusu barabara peke yake sasa hata viwanja pia. (*Makofi/kicheko)*

Na. 361

***Youth Employment Network***

**MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza:-

Kwa kuwa, tatizo la ajira kwa vijana nchini ni tatizo sugu hawa ikizingatiwa kuwa vijana wengi wa Kitanzania hawana elimu:

(a) Je, Serikali ina habari juu ya mtandao wa ajira kwa vijana "*Youth Employment Network"* uliozinduliwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Bwana Koffi Annani mnamo mwezi Septemba, 2000?

(b) Kwa kuwa, Tanzania ni mwanachama wa Umoja wa Mataifa na Shirika la Kazi Duniani. Je, ni kwa kiasi gani Serikali imetumia fursa hiyo inayodhaminiwa na washirika husika pamoja na Benki Kuu ya Dunia?

(c) Je, Serikali haioni kwamba, sasa ni wakati muafaka wa kuungana na nchi za Afrika za Mali, Rwanda, Misri na Senegal kuitumia fursa hiyo ipasavyo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO)** alijibu:- Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi, Ajira, Maendeleo ya Kazi, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge Viti Maalum lenye sehemu (a), (b) na (c), napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mtandao wa Ajira kwa Vijana (*Youth Employment Network*) kwa kifupi *YEN* ulianzishwa Desemba 2000 kwa kuzingatia Azimo Na. 57/165 lililopitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa. Lengo kuu la kuanzisha *YEN* lilikuwa kuzihimiza nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa kulipa kipaumbele suala la kukuza nafasi za ajira kwa vijana duniani kote.

Mheshimiwa Spika, wadau wakuu wa mtandao wa *YEN* ni Benki ya Dunia *(WB)*, Shirika la Kazi Duniani *(ILO), UNICEF* na Umoja wa Mataifa *(UN)*. Aidha, mtandao huu hujumuisha jopo la wataalamu 13 wa masuala ya Ajira kwa vijana ambao huwakilisha katika Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mapendekezo ya mbinu za kukuza nafasi za ajira kwa vijana duniani.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo mafupi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge (Viti Maaluum) kama ifuatavyo:-

(a) Ndiyo Serikali inazo habari kuhusu Mtandao wa Ajira kwa Vijana Duniani *(YEN).*

(b) Kwa kushirikiana na viongozi pamoja na Mashirika ya Umoja wa Mataifa, Tanzania:-

· Imetumia fursa hii katika mambo mengi ikiwa ni pamoja na kuhamasisha vijana na makundi mbalimbali ya kijamii katika kuunda mtandao wa Kampeni ya miaka 10 ya kukuza Ajira Duniani – *Youth Employment Summit (YES) – 2002 – 2012)* mpango ambao ulizinduliwa rasmi hapa Tanzania mwaka 2002 na Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa ambaye ni Rais Mstaafu.

· Kubadilishana vijana katika ziara za mafunzo kati ya vijana wa Tanzania na Canada mpango ambao mpaka sasa unaendelea.

· Kwenye kituo chetu cha vijana cha Ilonga mkoani Morogoro tumeanzisha mafunzo maalum ya teknolojia ya habari *(ITC)* na vijana wengi wa mijini na vijijini wananufaika.

· Kwa kushirikiana na *UNICEF,* tumeendelea na kuwa na Mikutano mbalimbali ya kuhamasisha ajira kwa vijana nchini kote.

· Tanzania, kama zilivyo nchi za Afrika hususan Mali, Rwanda na Senegal ambazo pia ni nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa zimeungana kwa kupitia mtandao huo na zinashirikiana katika kubadilishana uzoefu na ujuzi kupitia mikutano mbalimbali inayoitishwa na *YEN* pamoja *YES* chini ya udhamini wa Umoja wa Mataifa.

Na. 362

**Nishati Inayotumika Migodini**

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE** aliuliza:-

Kwa kuwa, ipo migodi inayotumia umeme wa gridi ya Taifa kama Bulyanhulu na mingine hutumia umeme utokanao na mafuta:-

Je, Serikali imefanya utafiti wowote ili kujua ni njia ipi iliyo bora na rahisi ya kuipatia migodi nishati na kuwashauri wenye migodi ili watumie njia hiyo kwa lengo la kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza faida na mapato ya Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge wa Msalala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, migodi ya uchimbaji madini hutumia umeme mwingi kwa sababu ya ukubwa na wingi wa mitambo inayotumika katika shughuli ya uchimbaji. Kama alivyobainisha Mheshimiwa Mbunge, umeme wa mafuta unaozalishwa na migodi una gharama kubwa ukilinganisha na umeme wa gridi. Aidha, iwapo migodi hiyo itatumia umeme wa gridi mapato ya *TANESCO* yataongezeka kwa kuiuzia umeme migodi.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha azma ya migodi kutumia umeme wa gridi, *TANESCO* imekuwa na mazungumzo na wamiliki wa migodi kwa lengo la kuangalia uwezekano wa kujenga njia za umeme wa gridi hadi kwenye migodi ili migodi hiyo iweze kutumia umeme wa gridi. Mazungumzo yanaendelea na wamiliki wa Migodi ya Geita, Tuluwaka, Buzwagi, *North Mara* na Mgodi wa Bati wa Kyerwa (Kabanga) kwa lengo la kufikia maelewano na hatimaye kusaini mikataba husika.

Mheshimiwa Spika, kwa migodi mipya inayotegemewa kufunguliwa siku za usoni, Serikali inayataka Makampuni yanayotegemea kufungua migodi kuwasilisha

mahitaji yao ya umeme mapema ili mipango ya kupeleka umeme wa gridi katika migodi hiyo iweze kufanyika.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri hata hivyo nilikuwa na maswali madogo mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa mafuta yanayotumika katika migodi kwa kawaida yamesamehewa ushuru wa *VAT* yaani *0 Vated*. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba mafuta hayo hayatumiki au hayauzwi kwenye soko na hivyo ikiwa ni chanzo cha ukopaji wa ushuru;

(b) Kwa kuwa mgodi wa Bulyankulu ulilipa wenyewe gharama za kupeleka umeme katika mgodi huo ambazo kwa mujibu wa takwimu za mgodi huo ni kama dola milioni 7. Je, Serikali imenufaikaje na upungufu au punguzo la gharama za uzalishaji katika mgodi huo katika makubaliano hayo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri wa Fedha alipowasilisha hotuba yake ya Bajeti mbele ya Bunge lako Tukufu. Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* inaunda Kitengo Maalum cha kushughulia masuala ya Makampuni makubwa ya Madini, migodi mikubwa. Ningependa kumhakikishia kwamba Mamlaka ya Mapato itafanya kila linaloweza kuhakikisha kwamba mafuta ambayo yamesamehewa *VAT* hayatoingia kwenye soko la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, swali la pili la Mheshimiwa Mbunge limehusu suala la mapato ambayo yanapatikana kutokana na Kampuni ya Bulyankulu yaani *Kahama Mining* kujenga njia yake ya umeme yenyewe na faida gani ambayo Serikali inapata kutokana na kwamba Kampuni hiyo imejenga njia ya umeme yenyewe.

Ningependa kumfahamisha kwamba kitendo cha Kampuni kujenga laini ya umeme yenyewe imeiwezesha *TANESCO* na Serikali kutumia fedha ili kujenga laini za umeme katika maeneo mengine mbalimbali.

Pia imeiwezesha Serikali kuwafikishia umeme wananchi ambao wanaishi katika njia hiyo ambayo laini hiyo ya umeme imepita. Tungependa kuendelea kuwahimiza wenye Makampuni ya migodi kuisaidia Serikali katika kuweka njia za umeme katika maeneo mbalimbali ili Serikali na wananchi wa Tanzania waendelee kufaidika na umeme huo.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza.

Nchi nyingi zenye migodi zimefaidika sana kutokana na kwamba zinatangulia kuweka miundombinu halafu wawekezaji wakileta migodi wanalipa fedha na nchi zinafaidika. Kwa kuwa kuna maeneo mengi ambayo yanatarajiwa kupata migodi kwa mfano Nyarugusu. Je, Serikali haioni kwamba ni vyema sasa hivi ipeleke miundombinu kwa mfano umeme ili migodi ikija tuweze kutoza kodi kubwa na sehemu zingine?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi Serikali kwa kupitia *TANESCO* inawasiliana na Makampuni yote mikubwa ya migodi kuhakikisha kwamba pale ambapo wana mpango wa kufungua mgodi katika eneo fulani Serikali iweze kupeleka umeme ili wananchi pamoja mgodi ifaidike katika eneo hilo.

Ningependa kumhakikishia kwamba tunaendelea kufanya vile na pili ningependa kumhakikishia anavyofahamu katika kipindi hiki Serikali iko katika majadiliano na Makampuni makubwa ya migodi hapa nchini na masuala hayo yanaongelewa.

Na. 363

**Ubinafsishaji wa Shamba la NAFCO – Magamba**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa, shamba Na. 208 lenye ukubwa wa hekta 4,879 sawa na ekari 12,051 lililokuwa linamilikiwa na *NAFCO* – Magamba liko kwenye mpango wa kubinafsishwa; na kwa kuwa, vijiji vinavyolizunguka shamba hilo vya Magamba, Itaka, Iwalanje, Msanyila, Lwati na Iporoto hawana mashamba ya kutosha kwa kilimo hivyo hulazimika kukodi shamba hilo:-

(a) Je, isingekuwa busara kwa Serikali inayowajali wananchi wake ifute hati ya umiliki wa shamba hilo, ili wananchi hao wauziwe kwa bei nafuu, hivyo kuwajengea nafasi nzuri kujiongezea kipato na kuondokana na umaskini kama inavyosisitizwa kwenye Ilani ya CCM ya 2005 – 2010?

(b) Je, fedha ambazo Meneja wa shamba hilo hulipwa kutokana na kukodisha sehemu ya shamba kwa wananchi kwa Tshs. 10,000/= kwa ekari moja, zinafanya kazi gani? Je, ni utaratibu unaofaa kuwakodisha wananchi mashamba kwa kiasi hicho cha fedha?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kufuatana na Sera ya Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma, Shamba la Mahindi la Mbozi liliwekwa chini ya *PSRC* (*Specified*) kwa ajili ya kuuzwa mwaka 1996. Shamba lilitangazwa mara tatu kuanzia mwaka 2004 kabla ya kupata mwekezaji mwaka 2005. Tarehe 28 Julai, 2005 Serikali iliamua tathmini ya hali halisi ya shamba ifanyike kwanza ili kuiwezesha kutoa uamuzi mzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Zambi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye utangulizi, shamba hili limekwishatangazwa na kupata mwekezaji kwa utaratibu wa tenda. Kwa hiyo, kutokana na hatua iliyofikiwa ni vigumu kwa Serikali kurudi nyuma kutokana na athari ambazo zinaweza kujitokeza.

Kwa takwimu tulizonazo hakuna tatizo la ardhi kwenye maeneo ya Mbozi, bali ni kawaida tu wananchi kupenda kupata mashamba ambayo tayari yamekwishaendelezwa na yenye miundombinu. Lakini inabidi kuzingatia kuwa shamba hili lilikusudiwa kwa kilimo cha shamba kubwa la kibiashara.

Uamuzi wa Serikali unaendana na Kifungu 31 (m) cha Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 kinachosomeka hivi nanukuu: “CCM itazitaka Serikali kuongeza msukumo katika kuvutia wawekezaji katika mashamba makubwa ya kilimo cha biashara”. Kwa hiyo, wananchi kwenye maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge wanashauriwa kuchagua sehemu nyingine na kuanzisha mashamba yao.

Aidha, kwa kumwuzia shamba hilo mwekezaji mwenye uwezo wa kuliendeleza kutaibua ajira, kuongeza pato la Serikali kutokana na kodi na chakula kitakachozalishwa kwa wingi kitachangia katika kuondoa tatizo la upungufu wa chakula nchini.

(b) Mheshimiwa Spika, Meneja aliyeko kwenye Shamba la Mahindi Mbozi amewekwa na *PSRC* kama mtunzaji wa shamba hilo kabla ya kupata mnunuzi. Huu ni utaratibu wa kawaida unaotumika kwenye mashamba na mali nyingine zinazobinafsishwa ili kuhakikisha kwamba mali ya umma inabaki bila kuharibiwa au kuibwa mpaka mnunuzi apatikane.

Aidha, kitendo cha kuwaruhusu wananchi kulima mazao ya msimu shambani kwa kukodisha au bure huwa kinafanyika kwa kusudi hilo hilo la kuhakikisha kwamba mashamba ambayo hayajapata wanunuzi hayageuki kuwa mapori. Kiwango cha kukodisha mashamba ni mapatano kati ya mkulima na Meneja. Fedha zinazopatikana zinapelekwa Serikalini kupitia *PSRC* na kutumika kwa matumizi ya kawaida kama vile kutunza shamba hilo na kulipa mishahara.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Lakini naomba tu niseme kwamba nasikitika na majibu ya Waziri kwamba wananchi wa Mbozi hawana shida ya ardhi. Nina hakika hilo halijafanyiwa tathmini Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, baada ya hilo naomba niulize maswali mawili kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa tarehe 4 Julai, 2006 nilimwandikia Mheshimiwa Waziri Mkuu nikimwomba sana sana Serikali ifikirie uamuzi wake wa kuyauza mashamba hayo.Na kwa kuwa tarehe 24 Julai, 2006 Waziri Mkuu aliwaandikia Mawaziri wa Kilimo pamoja na Mipango kwamba wakae ili waeleze *status* ya shamba hilo.

Je, majibu hayo ya Waziri yamezingatia agizo hilo la Mheshimiwa Waziri Mkuu? (*Makofi)*

La pili, kwa kuwa tarehe 29 Julai, 2006 Waziri Mkuu alipokuwa anazindua Semina ya Uzinduzi wa Programmu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo *(ASDP)* alisema vijana ni nguvukazi ya Taifa na itabidi wawezeshwe sana huko vijijini ili waweze kulisaidia Taifa kwenye shughuli za kilimo.

Je, kama Serikali itaendelea na uamuzi wake wa kuliuza hili shamba la Magamba Mbozi ambalo zaidi ya asilimia 70 wanaolima shamba hili ni vijana si Serikali itakuwa inakwenda kinyume na agizo lake kama lilivyotolewa na Waziri Mkuu?

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa maelezo hapa Bungeni kwamba kweli kulikuwa na agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Mawaziri hawa wawili.

Jibu la msingi limezingatia maagizo haya ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Waziri Mkuu alituagiza tuangalie *status* ya ubinafsishaji wa shamba lile la Mbozi. Na jibu limesema hivyo kwamba tumepiga hatua kubwa, mwekezaji amepatikana kwa hivyo tuendelee na ile *process*. Na hii ni Sera ya Chama chetu ya kuwa na mashamba makubwa ambayo yatazalisha zaidi na hivyo kuweza kukabili tatizo la umaskini hapa nchini.

Lakini vilevile agizo la pili la Mheshimiwa Waziri Mkuu la kutaka kuwawezesha wananchi na hasa vijana vijijini linazingatiwa. Kwanza Serikali imetamka hapa Bungeni itatenga kwa wastani kwa kila Mkoa shilingi milioni mia tano (500,000,000/=) fedha hizi zitatumika kuibua shughuli za maendeleo vijijini.

Vilevile katika Wizara yangu tutaanzisha mfuko wa kuwezesha wananchi kiuchumi hilo nalo pia litasaidia maendeleo ya wananchi huko vijijini na hata mijini. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nimepata ombi maalum kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii kwa sababu anauguliwa na ameniomba ikiwezekana ajibu haya maswali ili aende Dar es Salaam. Naomba niongeze dakika kidogo ili tuweze kuyapitia haya maswali. Swali linalofuata Dr. Mahenge.

Na. 364

**Maeneo ya Kuishi Wananchi Kikondo**

**MHE. BINILITH S. MAHENGE** aliuliza:-

Kwa kuwa, Muswada wa kuifanya Hifadhi ya Kitulo iliyoko Wilayani Makete kuwa Hifadhi ya Taifa umekwishapitishwa na kwa kuwa eneo hilo kuna kijiji cha

Kikondo chenye shule ya msingi na familia zinazoishi kwa kutegemea kilimo na kwamba, wananchi hawa wameishi katika maeneo hayo kwa muda mrefu.

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuwapa maeneo mengine wananchi hawa wa Kikondo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Mahenge Mbunge wa Makete kama ifuatavyo:-

Eneo la Hifadhi ya Taifa ya Kitulo lilikuwa ni Ranchi ya Taifa iliyoanzishwa mwaka 1965. Wakati Ranchi hii inaanzishwa eneo la Kikondo lilikuwa wazi. Wananchi walioko kwenye kijiji hicho walianza shughuli za kulima vianzi katika eneo hilo wakati wa msimu wa kilimo na kuondoka mara msimu unapokwisha. Shughuli za kilimo hicho zilikuwa zikiendeshwa ndani ya Ranchi hiyo isivyohalali hivyo kilimo hicho kilikomaa na kuwa cha kudumu kikaambatana na ustawi wa makazi ya watu. Hifadhi ya Taifa ya Kitulo ilianzishwa rasmi kwa tangazo la Serikali namba 279 la tarehe 16/9/2005. Hifadhi hiyo ina umuhimu kitaifa kama moja ya maeneo makuu ambapo vijito vinavyounda Mto Ruaha vinaanzia.

Baada ya kutolewa rasmi kwa tangazo la kuanzisha Kitulo Wizara yangu kwa kupitia shirika la Hifadha za Taifa ilikutana na Uongozi wa Wilaya ya Makete chini ya Uongozi wa Mkuu wa Wilaya kupanga namna ya kahamisha wananchi waishio katika kijiji cha Kikondo. Maamuzi yalifikiwa kwamba Halmshauri ya Wilaya ya Makete itafute eneo ambalo wananchi hao watahamishiwa na isimamie zoezi lote la uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Makete tayari imepata eneo kwenye kitongoji cha Kigosi kijiji cha Kinyika katika Tarafa ya Matamba Wilayani Makete. Shirika la Hifadhi za Taifa kwa kupitia mpango wake wa ujirani mwema litaendelea kuchangia miradi ya maendeleo ya wananchi hao sehemu wanakohamishiwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumwaarifu Mheshimiwa Mbunge kuwa manufaa yatakayopatikana baada ya Kitulo kuwa Hifadhi ya Taifa ni mengi. Baadhi ya manufaa hayo wananchi hao wameanza kuyapata, ni pamoja na uchangaiji wa gharama za uchangiaji wa gharaza za miradi ya kijamii. Katika kipindi cha mwaka 2006, Shirika la Hifadhi za Taifa ilitoa kiasi cha shilingi 6,890,000/- kusaidia ujenzi wa darasa na ofisi ya Walimu, shule ya sekondari Matamba Wilayani Makete. Mchango mwingine uliotolewa ni wa kiasi cha shilingi milioni 3,340,000/- kwa ajili ya shughuli za uhifadhi wa kikundi cha Mangano kilichoko kwenye Kijiji cha Mpangala Wilayani Makete.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa Fedha, 2006/2007, *TANAPA* imechangia kiasi cha shilingi 11,762,763/- kwa ajili ya huduma ya watoto na walimu wa shule ya msingi ya Kikondo ikiwa ni gharama zitakazohusika katika kuwatafutia mahali wanafunzi wa darasa la nne na saba ili waweze kufanya mitihani yao kama wenzao wote kitaifa wakati mikakati mingine ya kuhama ikiwa inaendelea. Maombi haya yalifikiwa

baada ya Halmashauri ya Wilaya ya Makete kuongea na uongozi wa shamba la Kitulo na kuafikiana kwamba baadhi ya majengo yake yatumike kusomea pamoja na malazi kwa wanafunzi walimu wanne.*(Makofi)*

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpe pole Mheshimiwa Waziri na nimtakie safari njema kwenda kumwona mgonjwa wake Dar es Salaam na pili naomba nimshukuru sana kwa majibu yake mazuri lakini nilikuwa na swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa kijiji cha Kikondo kilisajiliwa mwaka 1978 kwa usajili Namba *IR/VC/64* wakati huo tukiwa Njombe na kikasajiliwa tena mwaka 1979 kwa usajili namba *IR/VC/562*, wakati ikiwa ni Wilaya ya Makete, na kwa usajili huu ilipelekea wananchi kujenga makazi ya kudumu na vilevile kujenga shule ya msingi ambayo mpaka sasa hivi tunapoongea ina watoto 425 wakiwemo wakike 216. Je Serikali itakuwa tayari kuwasaidia hawa wananchi kama alivyoainisha kuwajengea shule mpya kwenye sehemu wanayohamishiwa huko Kinyika?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Dr. Mahenge kwa jinsi ambavyo anafuatilia kwa karibu sana kuhusu uhamisho wa wanakijiji wa Kikondo. Lakini vile vile kutokana na kuhamishwa kwao Hifadhi ya Taifa inachofanya ni kupokea maombi kutoka kwa wananchi na kuwasaidia kutegemea na hali ya Bajeti iliyopo kwa wakati maalum. Sasa naomba nimshauri Mheshimiwa Mbunge awasiliane na Halmashauri ya Makete kuhusu shule na pia wanaweza kutuma maombi yao *TANAPA* na tutaona jinsi gani tunavyoweza kuwasaidia hasa tukizingatia ujirani mwema. *(Makofi)*

Na. 365

**Eneo la Kisiwa cha Maisome**

**MHE. SAMUEL M. CHITALILO** aliuliza:-

Kwa kuwa Kisiwa cha Maisome ni sehemu ya makazi pamoja na Hifadhi ya Taifa na kwa kuwa maeneo ya makazi waliyopewa watu kwa sasa hayatoshi kutokana na kuzalisha kwa wingi:-

Je, Serikali ipo tayari kuwaongezea ardhi wananchi hao kwa ajili ya kilimo kwa sababu eneo walilonalo kwa sasa halitoshi?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Chitalilo, Mbunge wa Buchosa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, msitu wa Hifadhi wa Maisome katika Wilaya Sengerema Mkoani Mwanza ulihifadhiwa mwaka 1942, ukiwa na eneo la jumla ya hekta 12,190.

Msitu huo ulianzishwa kwa madhumuni ya kuhifadhi viumbe hai, ardhi na vyanzo vya maji na kuzuia mmomonyoko wa udongo. Mnamo mwaka 1966, jumla ya hekta 1,600 za msitu huo zilitolewa kwa wananchi kwa ajili ya makazi na kilimo. Hivi sasa eneo la msitu limebaki hekta 10,590. Kuna uharibifu katika msitu wa Maisome unaotokana na uvunaji haramu wa mazao ya misitu. Hali hiyo inasababishwa pamoja na mambo mengine ongezeko la watu katika kisiwa hicho.

Mheshimiwa Spika, sababu za msingi za kuhifadhiwa kwa msitu wa Maisome zilizotajwa hapo awali bado zipo na kwa hakika mahitaji ya mazao ya msitu katika maeneo yanayozunguka kisiwa hicho Wilaya ya Sengerema na jiji la Mwanza kwa ujumla yanazidi kuongezeka siku hadi siku. Kama wanakijiji wanahitaji maeneo zaidi kwa ajili ya shughuli mbalimbali kama kupanua makazi yao ya kilimo basi inatakiwa iwe nje ya kisiwa hicho kwani sehemu iliyobaki ni msitu wa hifadi wa Serikali. Msitu huo umehifadhiwa kwa ajili ya kulinda viumbe hai pamoja na kuzuia mmomonyoko wa udongo unaweza kuathiri hata kingo za kisiwa hicho ndani ya Ziwa Victoria na kusababisha uharibifu wa mazalia ya samaki na viumbe vingine.

Mheshimiwa Spika Wizara yangu kwa kweli haiko tayari kumega tena ardhi na kuwaongezea wananchi wa kisiwa cha Maisome.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha ninayo matangazo yafuatayo:-

Kwanza kuhusu wageni, kwenye *Public Gallery* upande wa kushoto wapo wanafunzi na walimu wa shule ya sekondari ya Miuji ya hapa Dodoma Mjini, ningewaomba wasimame. Karibuni sana vijana pamoja na walimu wenu tunapenda sana hasa ninyi mlio karibu hapa Dodoma Mjini kuweza kuja kushuhudia wenyewe kwa macho yenu na kusikia jinsi demokrasia inavyoendeshwa nchini kwetu. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Katika *Gallery* ya Spika, tunaye Mheshimiwa Profesa. Mbilinyi, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Taifa la Maendeleo, karibu sana Profesa Mbilinyi. Profesa Mbilinyi anakofia nyingi na mtakumbuka kwamba alikuwa Mbunge katika Bunge lililopita. Leo amekuja akiwa ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Taifa la Maendeleo yaani *NDC*. Hapo hapo kwenye *Speaker's Gallery* kuna Ndugu yetu. Ndugu Reginald Mengi.(*Makofi*)

Yeye naye anakofia nyingi lakini leo amekuja kama Mwenyekiti wa *CTI*, yaani Shirikisho la wenye viwanda hapa Tanzania. Kwa sababu leo ndiyo hotuba yao basi amekuja kusikiliza mambo ya Waziri. Karibu sana Mheshimiwa Mengi.

Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, ameniomba niwatambue wageni wake ambaye ni mdogo wake anaitwa Rehema Adam Kimwanga, siyo tu kwa kuwa ni mdogo wake lakini ndiye msaidizi mkuu wa kisiasa na ndiye aliyemshawishi kuingia katika siasa. Yule pale anapunga mkono ni kweli anafanana naye. Pia amekuja na mwanae Mheshimiwa Mbunge anaitwa Kheri Abdul. Karibuni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Said Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, ameniomba niwatambue wageni wake wawili ambao ni Mheshimiwa Seif Said Spear, Mwenyekiti wa CHADEMA Wilaya ya Mpanda na Bwana Suleiman Mohamed Tumaini, Mwakilishi wa wachimbaji wadogo wa madini Ruhemba, kule kule. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa George Malima Lubeleje, ana wageni Madiwani wawili wa Halmashauri ya Mpwapwa. Kwanza ni Diwani George Mbuti na Diwani Mdagile. Wale pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Shah, Mbunge wa Mafia anaomba tutambue familia yake, mkewe Bi. Samila Mohamed na wanawe. Mama Samila na vijana wale pale. Lakini pia kwa ujirani mwema anaomba tutambue familia ya Mheshimiwa Sinani: Bi Asma Sinani huyu ni mke wa Mheshimiwa Sinani jirani yao hawa yule pale ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa John Lwanji, ameomba niwatambue wageni kutoka Manyoni Magharibi, mmoja ni Sheikh Shaban Mkoma, Mwalimu Mkuu wa shule ya msingi pale Itigi na Ndugu Wilson Lwanji Mwalimu Mkuu wa shule ya msingi Sanjaranja. Karibuni sana.(*Makofi*)

Waziri wa Biashara na Masoko Mheshimiwa Nazir Karamagi, ameomba niwatambue wageni wake, kwanza ni Bwana Peter Machunde Mkurugenzi wa Shirika linaitwa *Vatex Financial Services,* Bwana Deusdedit Dancan, ambaye yeye ni mwanasheria kutoka *FK Law Chambers* wanafanyakazi kwa karibu na ile *Vatex*. Yupo pia Ndugu Omary Abdallah Kabaka, kutoka kutoka Jimbo la Bukoba Vijijini huyu ni mpiga kura wake wale pale. Inasemekana huyu ni mmoja wa watu mashuhuri sana anabeba kura kama 2,000. *(Makofi/ Kicheko)*

Mwisho lakini si kwa kipaumbele ni kijana, Emil Karamagi ni mtoto wa Mheshimiwa Waziri na kwa cheo yeye ni Rais wa *International School of Tanganyika.* Karibu sana. Mheshimiwa Lucy Owenya anaomba niwatambulishe wanae Rachel Fidelis Owenya na Yohanne Fidelis Owenya. Wamekuja kushuhudia mama yao Mheshimiwa Lucy Owenya akitoa mantiki kama Msemaji Mkuu wa Upinzani kwenye Sekta ya Viwanda na Biashara na mambo haya si madogo kusimama hapa na kutoa hotuba kwa niaba ya wenzako, si jambo dogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Owenya aliongezea hapa nadhani anajaribu kujibu lile nililosema kwamba Mawaziri na Manaibu Mawaziri wanawake hawatambulishi hata kidogo waume zao hapa, ni wachache sana wanaofanya hivyo. Sasa hata Wabunge ni mtindo huo huo, Mheshimiwa Owenya ameleta wanae lakini anasema mume ni Daktari Bingwa basi anashughuli nyingi huko nyumbani. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa nije kwa watani zangu, rafiki zangu, wazee wangu wa *Club* ya Yanga wamekuja Dodoma, kumkabidhi Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo muafaka wa makundi ndani ya *Club* ya Yanga. Viongozi wa Yanga simameni. Viongozi hawa wanaongozwa na Mzee Jabir Katundu, ambaye ndiye kiongozi wa msafara, wapo Ibrahim Akilimali, Silima Jaffa, Hashimu Mhita, Seif Mpita, Masoud Abdallah na Yusuf

Mzimba. Mzee Yusuf Mzimba, hebu punga mkono. Mheshimiwa Yusuf Mzimba hatimaye amesalimu amri naye amechukua hisa. *(Makofi/Kicheko)*

Wengine ni Ismail Idrisa, Mohamed Omary, Thabit Madenge, Hilary Chakupewa, Mikidadi Jagalaga na Hamis Ramadhan. Kwa kuwa hii ndiyo *Club* kubwa ya mpira hapa nchini tunawapongeza sana kwa kuleta amani katika *Club* ya Yanga. Karibuni sana Bungeni. Nimeanza na wengine na mimi nitambulishe wageni wangu. Nafurahi kuwatambulisha Binti yangu Agnes na mumewe Kefa. Wote wawili ni wa-*Pharmacia* wanafanyakazi Dar es Salaam karibuni sana. Taarifa ya Kikao, Mheshimiwa Mwenyekiti, John Cheyo wa Kamati ya Hesabu za Serikali anatangaza kwamba kesho tarehe 8 kuanzia saa nne asubuhi watakuwa na Kikao muhimu sana kinachopanga ratiba ya shughuli zao. Kikao hicho kitafanyika Ukumbi namba 432.

Kama nilivyotangaza siku ya Ijumaa, leo saa tano Spika pamoja na Tume ya Huduma za Bunge, tutawapokea Wajumbe wa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mishahara. Baada ya hapo Kamati ya Fedha na Uchumi na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala pamoja na wanatume baada ya kunisalimia wanatume hapa *Speaker's Lounge* wataenda sasa kwenye Kikao cha Kazi kwa pamoja chumba Namba 231 saa tano na nusu. Ningewaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati zile mbili Fedha na Uchumi, Katiba, Sheria na Utawala watangulie kiasi cha saa tano na robo pale kwenye chumba Namba 231 kwa Kikao cha Kazi pamoja na hiyo Tume ya Rais kuhusu mishahara katika sekta ya Umma.

Mwisho, kutona na Kikao cha dharura cha Serikali, ule Mkutano tuliopanga kuwa nao na Mheshimiwa Waziri Mkuu saa saba na nusu umeahirishwa. Kuna kikao cha dharura kwa hiyo Mkutano wa Tume pamoja na Kamati ya Uongozi kuzungumza na Mheshimiwa Waziri Mkuu tumeahirisha tutawafahamisheni baadaye. Sasa kwa kuzingita kwamba Spika inabidi akakutane na hii Tume kwa niaba yenu kwa sasa ningemwomba Mheshimiwa Job Ndugai anipokee kiti. Hapa kuna Mheshimiwa amesahau ufunguo wa gari basi amwone Kaimu Katibu. Ahsanteni sana.(*Makofi*)

*Hapa Mwenyekiti (Job Y. Ndugai) alikalia Kiti.*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea kuna matangazo mawili ya nyongeza. La kwanza ni kuijulisha Kamati ya Muafaka ya Yanga kwamba Simba nao wamo kwenye Bunge hili. (*Makofi*)

La pili, ni kwamba kuna wawakilishi wetu Waheshimiwa Wabunge ambao walikwenda kwenye uchaguzi kama sehemu ya usimamizi wa Kimataifa katika uchaguzi wa Congo baadhi tunawaona hapa kidogo tu na ningeomba tuwasalimie kidogo. Namwona Mheshimiwa Zitto na Mheshimiwa Eng. Manyanya, karibuni sana. (*Makofi*)

Baada ya hapo tunaendelea na hatua inayofuata, Katibu. *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2006/2007 Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko**

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti**,** kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara iliyochambua bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete pamoja na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa kwao kwa ushindi mkubwa wa kishindo.

Aidha, nampongeza kwa namna ya kipekee Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Kitaifa. Napenda pia, kumpongeza Mhe. Amani Abeid Karume kwa kuchaguliwa kwake kwa kipindi cha pili kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Vile vile, nampongeza Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mbunge na hatimaye kuteuliwa na kuthibitishwa na Bunge kwa kura nyingi kuwa Waziri Mkuu katika Serikali ya Awamu ya Nne ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti aidha, napenda kukupongeza wewe mwenyewe Mheshimiwa kwa kuchaguliwa kwako kwa kura nyingi kuwa Spika na pia kumpongeza Mhe. Anna Makinda kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika katika Bunge la Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawapongeza pia Mawaziri wenzangu wote pamoja na Manaibu Waziri, kwanza kwa kuchaguliwa kuwa Wabunge na pili kwa kuteuliwa kwao na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa kwenye Baraza la Mawaziri. Vile vile, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Uwekezaji na Biashara ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa William Shellukindo, kwa kutupatia ushauri na maelekezo wakati wa kujadili muhtasari wa hotuba hii.

Aidha, ninawashukuru wale wote tulioshirikiana nao katika maandalizi ya Hotuba hii ninayowasilisha leo. Mwisho napenda niwapongeze Wabunge wote kwa kuchaguliwa au kuteuliwa kwao kuingia katika Bunge hili Tukufu. Mimi pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. David Mathayo David, tunawashukuru kipekee wapiga kura wa Majimbo yetu waliotuwezesha kuwa miongoni mwa Wabunge katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti napenda kuchukua nafasi hii kuwapa pole Waheshimiwa Wabunge waliopata mikasa ya kufiwa na jamaa zao. Mwenyezi Tunaomba Mungu awape faraja na azilaze roho za marehemu mahali pema peponi – Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti Majukumu na Muundo wa Wizara. Majukumu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko yamezingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa *(National Development Vision 2025)* ambayo imeweka bayana kwamba Sekta za

Viwanda, Biashara na Masoko ndiyo ziwe mihimili mikuu ya kuuwezesha uchumi wa nchi yetu kukua na kufikia kiwango cha kati cha maendeleo ya uchumi wa viwanda. Majukumu ya msingi ya Wizara ni pamoja na:-

(a) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera za kuendeleza Sekta za Viwanda, Biashara na Masoko;

(b) Kuandaa mipango na mikakati ya kushirikisha na kuimarisha Sekta Binafsi katika kuchangia maendeleo ya uchumi wa Taifa kupitia uendelezaji wa uwekezaji katika Sekta za Viwanda, Biashara na Masoko;

(c) Kusimamia utekelezaji wa sheria mbalimbali chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko;

(d) Kusimamia utekelezaji wa mikakati mahsusi ya uendelezaji wa mauzo ya mazao na bidhaa za Tanzania katika masoko ya nje;

(e) Kubaini na kutekeleza mikakati ya kuendeleza ushirikiano wa kiuchumi na nchi nyingine ili kuhakikisha kwamba Taifa linapata manufaa kwa kiwango cha juu hususan kupitia Sekta ya Viwanda, Biashara na Masoko; na

(f) Kuimarisha uwezo wa Wizara na Asasi zilizo chini yake ili kutekeleza majukumu yake kwa kiwango cha ufanisi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Muundo kufuatia kuundwa kwa Serikali ya Awamu ya Nne, Sekta ya Masoko imeunganishwa na Sekta za Viwanda na Biashara na kuunda Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Kwa hiyo, muundo mpya wa Wizara sasa una Idara nne zenye majukumu muhimu ya kisekta na Idara mbili za huduma na uratibu. Idara za majukumu kisekta ni Idara ya Viwanda, Idara ya Biashara ya Kimataifa, Idara ya Maendeleo ya Masoko na Idara ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo. Idara za huduma na uratibu ni Idara ya Utawala na Utumishi na Idara ya Sera na Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirikiano na Sekta Binafsi.Wizara inashirikiana kikamilifu na Sekta Binafsi kwa kuzingatia azma ya Serikali kwamba Sekta Binafsi ndio mdau mkuu katika kutekeleza majukumu yake mbalimbali ya uwekezaji na biashara katika mkakati mzima wa kukuza uchumi na kuondoa umaskini. Baadhi ya taasisi zinazoshirikiana na wizara yangu ni *"Tanzania Private Sector Foundation (TPSF)", "Tanzania Chamber of Commerce, Industry and Agriculture – TCCIA" "Confederation of Tanzania Industries – CTI"* pamoja na Asasi Zisizo za Kiserikali *(AZISE).*

Aidha, Taasisi za Sekta Binafsi hushiriki katika mikutano ya kila mwaka inayoshirikisha Sekta ya Umma na Sekta Binafsi na kupata michango yao kuhusu mikakati mbalimbali ya kuendeleza viwanda, biashara na masoko. Mkutano huu wa pamoja hufanyika chini ya uratibu wa Baraza la Taifa la Biashara ambalo Mwenyekiti wake ni Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile, Serikali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo ya viwanda, huandaa maadhimisho ya siku ya

kumbukumbu ya maendeleo ya viwanda barani Afrika kila mwaka tarehe 20 Novemba, ambapo hujumuika na Sekta binafsi kutafakari mikakati ya kuharakisha maendeleo ya viwanda nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala katika kipindi cha miezi sita wakati tukiendelea kutekeleza mpango wa MKUKUTA, uongozi wa Serikali ya awamu ya nne ulipoingia madarakani, Wizara yangu ilizingatia mpango wa MKUKUTA pamoja na utekelezaji wa ahadi za Chama Tawala (CCM) zilizobainishwa katika Ilani yake ya uchaguzi ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Chama Tawala imebainisha wazi kinachotakiwa kufanyika katika sekta zinazosimamiwa na Wizara yangu ili kuleta maendeleo katika nchi yetu. Katika sekta ya Viwanda, Ilani imeelekeza kuwa ifikapo mwaka 2010 kiwango cha ukuaji wa sekta kififikie asilimia 15 kwa mwaka. Hii ni changamoto na hatua muhimu katika mikakati ya kuwezesha kufikia kiwango cha Maendeleo ya kati ya Uchumi wa Viwanda ifikapo mwaka 2025 kama ilivyoelekezwa kwenye Dira ya Maendeleo ya Taifa.

Aidha, katika Sekta za Biashara na Masoko, Ilani imeelekeza kuandaa mikakati itakayouwezesha uchumi wa Taifa kuhimili ushindani na kulifanya Taifa letu liwe na uwezo madhubuti wa kushiriki na kufaidika katika mfumo wa biashara kwenye masoko ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa katika mazingira ya utandawazi. Hii inatarajiwa kuwa kichocheo cha kuongeza uwezo wa uwekezaji kwenye sekta za uzalishaji katika uchumi wa ndani kwa kuzingatia fursa zilizopo za rasilimali na masoko.

Aidha, Ilani imesisitiza kipaumbele kiwekwe katika shughuli za kupanua ajira kwa kuendeleza ujasiriamali katika viwanda vidogo na biashara ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi ambacho uongozi wa awamu ya nne umekuwa madarakani, Wizara yangu imeweza kutekeleza yafuatayo kama sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi:-

(a) Zoezi la kumpata mwekezaji wa Mradi wa Kuzalisha Magadi wa Ziwa Natron limekamilika. Uzalishaji wa magadi kwa ajili ya matumizi ya mbolea, vioo, madawa na vigae unatarajiwa kuanza mwaka 2008. Aidha, Mradi unatarajiwa kutoa ajira kwa watu wasiopungua 500;

(b) Maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa makaa ya mawe ya Mchuchuma na mradi wa chuma wa Liganga yamefikia hatua ya kuanza kubainisha wawekezaji

(c) Teknolojia mbalimbali zinazofaa kutumika vijijini na mijini kwa kurahisisha kazi, kuendeleza viwanda vidogo mijini na vijijini, kuhifadhi na kusindika mazao, pamoja na kuchangia hifadhi ya mazingira zimeendelezwa na taasisi zilizo chini ya Wizara. Teknolojia hizo zinajumuisha yafuatayo:-

· Ukamilishaji wa maandalizi ya mradi wa wachimbaji wadogo wa madini hadi hatua ya ufungaji wa mitambo Igunga, Tabora;

· Majembe ya kukokotwa na ng'ombe yapatayo 5,352 katika Mikoa tisa inayojumuisha Mwanza, Kagera, Arusha, Rukwa, Iringa, Dodoma, Singida, Mbeya na Shinyanga yalitengenezwa;

· Viwanda Vidogo 199 ambavyo vimeajiri watu 406 vilianzishwa;

· Mafunzo mbali mbali ya ufundi yamefanyika katika kozi 59 kwa washiriki 2,254; kozi nane za usindikaji wa vyakula kwa wajasiriamali 160; utengenezaji wa zana za kilimo na za uchukuzi vijijini kwa wajasiriamali 23 pamoja na utumiaji wa udongo-saruji katika ujenzi wa nyumba bora zenye gharama nafuu vijijini kwa wajasiriamali 10;

· Mashine ndogo 101 kwa ajili ya shughuli mbali mbali zilitengenezwa katika karakana za Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo *(SIDO);* na

· Jumla ya mikopo 831 yenye thamani ya shilingi milioni 556 ilitolewa katika Mikoa 11 na kutoa nafasi za ajira kwa watu 4,100.

(d) Chama cha Hakimiliki (*Copyright Society of Tanzania - COSOTA*) cha kulinda maslahi ya wasanii kimejisajili katika taasisi ya kulinda maslahi ya wasanii duniani *(International Confederation of Authors and Composers - CISAC).* Kwa kujiandikisha huko, muziki wa Tanzania utalindwa katika nchi mbalimbali ambazo ni wanachama wa *CISAC*;

(e) Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (*BRELA*) wameanza kutumia sheria mpya (*New Company Act No. 12 of 2002)* tangu tarehe 1 Machi 2006.

(f) Kituo cha kutoa taarifa za kibiashara kwa wananchi na wadau mbali mbali kuhusu haki za ubunifu kimeanzishwa ndani ya *BRELA*;

(g) Ujenzi wa tembe bora 5 za ukaushaji wa tumbaku huko Mkoani Ruvuma umekamilika na tayari zinatumiwa na wakulima;

(h) Viwango vya Ubora vya Taifa 38 vimekamilishwa kwa bidhaa za huduma zikijumuisha nne katika nyanja mbalimbali za uhandisi, 32 za vyakula, kemikali na nguo na viwili vya ufungashaji; na

(i)Leseni za ubora wa bidhaa saba zenye alama ya *"TBS"* zikijumuisha saba kwa viwanda vidogo, 21 kwa viwanda vikubwa na 163 kwa bidhaa zinazoingizwa kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Malengo ya Bajeti ya Mwaka 2005/06. Sehemu kubwa ya bajeti ya mwaka 2005/2006 ililenga katika kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania maarufu kwa jina la MKUKUTA.

Wizara yangu ilielekeza nguvu katika kuwaongezea uwezo wanaviwanda na wafanyabiashara wadogo kushiriki katika juhudi za kukuza uchumi na kuondoa umaskini wa kipato. Msisitizo uliwekwa katika kuendeleza wajasiriamali kwa kuwawezesha katika

nyanja za kiufundi, masoko, mawasiliano na huduma za kifedha hususan vyanzo vya mtaji. Ili kufikia malengo hayo, Wizara yangu ilishirikiana na Taasisi zilizo chini yake na Sekta Binafsi katika kuboresha mazingira wezeshaji katika Sekta za Viwanda, Biashara na Masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Viwanda katika kipindi cha mwaka 2005/06, sekta ya viwanda ililenga kufanya yafuatayo: -

(a)Kutekeleza sera na mikakati ya kuendeleza sekta ya viwanda ili kukuza mchango wa sekta katika pato la Taifa;

(b)Kuimarisha Taasisi za Utafiti zilizo chini ya Wizara (*CAMARTEC*, *TEMDO*, *TIRDO*, *TBS* na *NDC*) katika kuendeleza sekta ya viwanda chini ya bajeti ya MKUKUTA; na

(c)Kushirikiana kwa karibu na wenye viwanda ili kujua matatizo yao na kuyatafutia ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda Wizara iliendelea na utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda (1996 – 2020) kwa kutekeleza programu mbali mbali ikiwa ni pamoja na awamu ya pili ya Mpango wa Maendeleo ya Viwanda. Mpango huu unalenga katika kuhamasisha, kuwezesha na kuelekeza wawekezaji binafsi katika kujenga viwanda vya usindikaji wa mazao na bidhaa za kilimo ili kuongeza thamani, nafasi za ajira na kupunguza uharibifu baada ya mavuno. Mradi wa majaribio wa kusindika matunda ulioanzishwa huko Muheza, Tanga ni mmojawapo ya baadhi ya miradi katika lengo hilo. Kazi nyingine iliyotekelezwa chini ya mpango huu wa awamu ya pili ni kutoa mafunzo ya utengenezaji wa bidhaa za ngozi kwa watu wenye ulemavu ambapo vijana 10 walipatiwa mafunzo hayo yaliyoendeshwa na *Leather Association of Tanzania* (*LAT)*, kwa ushirikiano kati ya Wizara na *UNIDO* kwa lengo la kuwawezesha kuanzisha miradi ya kujiajiri wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha 2005/06, yamekuwepo maendeleo ya kutia moyo katika sekta ya viwanda vya kuyeyusha chuma baada ya Serikali kuzuia uuzaji nchi za nje chuma chakavu kinachoweza kuyeyushwa na viwanda vya hapa nchini. Kutokana na hatua hiyo, viwanda sita vipya vimeanzishwa na kutoa nafasi mpya za ajira kwa wananchi wasiopungua 1,000 na hivyo kuwaongezea kipato na kupunguza umaskini. Aidha, Wizara imewakutanisha wadau wa sekta ya chuma chakavu kwa lengo la kupata maoni yao na mapendekezo yatakayosaidia katika kukamilisha mkakati wa kudumu wa biashara ya chuma chakavu.

Mkakati huu unalenga kuhakikisha upatikanaji wa malighafi ya kutosha kwa viwanda vya kuyeyusha chuma na kuuza tu nje aina ya chuma chakavu ambacho uwezo wa kuyeyusha haupo nchini. Vile vile, tathmini ya sekta ya viwanda vya mkonge ilifanyika na mapendekezo kutolewa na wataalam yenye lengo la kukwamua sekta hiyo ambapo yanajadiliwa na Serikali kubainisha hatua za kuchukua.Wizara pia iliandaa semina za kuhamasisha wamiliki wa viwanda kuhusu masuala ya kuhifadhi na kulinda

mazingira katika uzalishaji viwandani ambapo watendaji wakuu viwandani wapatao 30 waliohudhuria semina hiyo walijifunza mengi yenye manufaa ikiwa ni pamoja na Sera ya Mazingira, Sheria ya Mazingira, *"Cleaner Production Technology", "Environmental Impact Assessment" na "Environmental Audit".* Aidha, walitoa ushauri wao yatakayozingatiwa katika kuandaa miongozo ya kisekta kuhusu mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya marekebisho ya Sheria ya Maeneo Huru ya Uzalishaji wa Bidhaa za Kuuza Nje *(Export Processing Zone (EPZ)* kukamilika na kupitishwa na Bunge tarehe 15 Februari 2006, Wizara imeunda Mamlaka ya *EPZ* kwa kuongozwa na matakwa ya Sheria hiyo. Kuhusu upatikanaji wa wawekezaji katika programu ya *EPZ* katika kipindi cha 2005/2006, wawekezaji watano walipewa leseni za uzalishaji (*EPZ Operators' Licence)* ambao wanajumuisha: *Tsubasa Renew Car (EA) Ltd, Dar es Salaam; Net Health Ltd, Arusha; Vector Health International Ltd, Arusha; African Packaging International Ltd*, Dar es Salaam; pamoja na *Metrec International Ltd, Dar es Salaam*. Aidha, wawekezaji watatu*, Fruit Kin Concentrates Ltd*, Kibaha; *Net Health Ltd*, Arusha na *Vector Health Ltd*, Arusha walipewa leseni ya ujenzi wa miundombinu ya *EPZ* (*EPZ Developers' Licence)*. Jumla ya mtaji uliowekezwa katika *EPZ* hadi sasa ni Dola za Kimarekani milioni 121.98.

Mheshimiwa Mwenyekiti ili kubaini hali ya maendeleo ya viwanda nchini, katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Wizara ilifanya ziara ya kutembelea viwanda katika kanda tatu ambazo ni Kanda ya Ziwa, Kanda ya Kaskazini na Kanda ya Mashariki ambayo ilisaidia katika kudumisha ushirikiano na kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya viwanda. Aidha, ziara hizo zilisaidia kutathmini mafanikio na changamoto zinazokabili viwanda na kuwezesha Serikali kubuni mikakati ya kutatua matatizo na kuboresha mazingira ya uwekezaji katika sekta ya viwanda**.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla uwekezaji katika viwanda unaendelea kuongezeka na kutoa nafasi za ajira. Kati ya viwanda vipya vilivyoanzishwa ni pamoja na *China Paper Corporation* cha Kilimanjaro (ajira 60), Kahama *Ginnery* and *Oil Mill Ltd* cha Shinyanga (ajira 120) na *Merchandise Products Group* cha Kibaha (ajira 20) pamoja na viwanda vingine vya kusindika samaki katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa. Aidha, kati ya viwanda vya zamani vilivyokarabatiwa na kufanyiwa upanuzi ni pamoja na Kiwanda cha Zana za Kilimo *(UFI)* ambacho sasa kinaitwa Tanzania *Steel Pipes* (*TSP*), Dar es Salaam; Kiwanda cha Nyuzi Tabora (*TABOTEX*); Tanzania *Dairy Ltd*, Tanga; Tanganyika *Instant Coffee (TANICA),* Kagera na Tanzania *Pharmaceutical Industries Ltd (TPI),* Arusha.

Kutokana na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Wizara kama nilivyoeleza hapo awali, mchango wa sekta ya viwanda katika uchumi wa Taifa katika mwaka 2005/2006 uliongezeka. Katika kipindi cha mwaka 2005, sekta ya viwanda ilikua kwa asilimia 9 ikilinganishwa na asilimia 8.6 mwaka wa 2004. Mchango wa sekta ya viwanda kwa pato la Taifa kwa mwaka 2005 ulikuwa asilimia 9 ikilinganishwa na asilimia 8.8 mwaka 2004. Aidha, mauzo ya bidhaa za viwanda nchi za nje yalikuwa na thamani ya Dola za Kimarekani milioni 156.1 mwaka 2005 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 110.1 mwaka 2004, sawa na ongezeko la asilimia 41.8. Ajira katika sekta ya viwanda iliongezeka kufikia watu 88,713 mwaka 2005 kutoka 83,712 mwaka 2004, sawa na

ongezeko la asilimia 6 kama ilivyonyeshwa katika Jedwali Na. 2. Ukiondoa uzalishaji wa nguo, rangi na chuma, uzalishaji wa bidhaa nyingine kama vile nyuzi za katani, "*aluminium*", mabati, saruji, unga, biskuti, sigara na vinywaji baridi na vikali uliongezeka katika kipindi cha mwaka 2005 ukilinganisha na mwaka 2004. Katika kipindi cha mwaka 2005, sekta ya viwanda ilikabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo upatikanaji wa umeme usio na uhakika na gharama kubwa ya nishati; miundombinu duni hususan barabara za vijijini zinakotoka malighafi; kuporomoka kwa thamani ya shilingi kulikochangia kuongezeka kwa gharama za malighafi na vipuri kutoka nje pamoja na gharama kubwa za usafirishaji kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta na bidhaa za petroli. Kama yasingekuwepo hayo matatizo, mchango wa sekta ya viwanda ungekuwa mkubwa zaidi katika pato la Taifa kuliko ulivyokuwa. Aidha, matatizo haya yanachangia kwa kiwango kikubwa kupanda kwa gharama za uzalishaji na bei za bidhaa hizo kwa mlaji na hivyo kuvifanya viwanda vingi vishindwe kuhimili ushindani katika soko la ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti Sekta ya Biashara, Utekelezaji Sera ya Taifa ya Biashara iliyozinduliwa rasmi mwezi Agosti 2003, ina madhumuni ya kujenga uwezo wa Sekta Binafsi, Asasi na Taasisi za Umma katika ushindani wa biashara. Aidha, Sera ya Taifa ya Biashara inabainisha nyenzo zitakazotumika katika kupanua na kukuza biashara kwa kuzingatia misingi ya kuongeza tija na ushindani katika sekta za uzalishaji mali pamoja na utoaji huduma. Sera imetafsiriwa katika lugha ya Kiswahili na vile vile maandalizi yamefanyika ya kuchapisha nakala katika lugha rahisi inayotumia viponzo (*Cartoons*) ili kutoa ujumbe kwa urahisi na kuwafikia wananchi wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Sera ya Taifa ya Biashara imeendelea kutekelezwa kwa kuendesha mafunzo kwa wadau mbalimbali kutoka Wizara, Idara za Serikali, Taasisi na Sekta Binafsi katika jitihada za kuwajengea uwezo wa kuchambua na kushiriki kwa manufaa katika majadiliano ya Kimataifa. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Kitengo cha Usimamizi wa Miradi *(Project Management Unit – PMU)* iliendesha mafunzo maalum ya wiki sita kwa kutumia wataalam kutoka Taasisi ya Biashara Duniani *(World Trade Institute).*

Mafunzo hayo maalum yalilenga kuboresha uwezo wa kushiriki majadiliano katika Shirika la Biashara la Dunia (*WTO*), kwenye maeneo ya kilimo, bidhaa za viwandani, biashara ya huduma, hakimiliki, biashara na uwekezaji na utatuzi wa migogoro ya kibiashara. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Denmark (*DANIDA*) kwa mwaka wa fedha 2005/2006 imefadhili watumishi 24 wa Wizara, Idara za Serikali, Sekta Binafsi na Asasi nyingine kusomea Shahada ya Uzamili ya Biashara ya Kimataifa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Lengo la mafunzo hayo ni kujenga uwezo wa wataalam kushiriki katika masuala ya biashara ya Kimataifa ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo mahiri katika ujuzi wa mbinu za kushiriki katika majadiliano ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti Dunia ya sasa ya utandawazi imeegemea sana kwenye Biashara ya Kimataifa. Kwa kutambua hili, Sera ya Biashara ya Taifa imeweka msukumo madhubuti katika kukuza mauzo ya bidhaa zetu katika soko la nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mauzo ya Nje, kutokana na utekelezaji wa msukumo huu, mauzo nje ya nchi yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka. Mauzo ya nje yaliongezeka toka Dola za Kimarekani milioni 682.9 mwaka 1995 hadi Dola za Kimarekani milioni 1,549.3 mwaka 2005. Aidha, kiwango cha ukuaji wa sekta ya biashara kiliongezeka toka asilimia 3.1 mwaka 1995 hadi asilimia 16.5 mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** katika jitihada za kukuza biashara ya nje, Wizara imewezesha Halmashauri ya Biashara ya Nje (*BET*) chini ya mpango wa MKUKUTA kuchangia zoezi la kuongeza msukumo wa mauzo ya nje kwa kubuni mikakati mbalimbali. *BET* ikishirikiana na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (*SIDO*) iliviunganisha vikundi mbalimbali vya Sanaa za Mikono na kuunda Chama cha Kitaifa cha Sanaa za Mikono (*Tanzania Handcraft Association – TanCraft).* Katika mchakato huu, yaliandaliwa maonesho ya bidhaa hizo na kuhudhuriwa na wanunuzi wa bidhaa kutoka Marekani, Canada na Ulaya. Wanunuzi hawa walipata fursa ya kubainisha mahitaji ya masoko yao na kufanya mazungumzo ya ana kwa ana na wajasiriamali wa Tanzania.

Aidha, katika jitihada za kuendeleza na kuongeza uzalishaji wa mazao ya viungo kwa ajili ya soko la nje, *BET* ikishirikiana na Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine imeanzisha mpango wa kuendeleza zao la iliki katika Tarafa ya Turiani Wilaya ya Mvomero na mazao ya mdalasini na pilipili manga katika Tarafa ya Mkuyuni Wilaya ya Morogoro Vijijini. Dhana ya utekelezaji ni ile ya kuwa na *Export Production Villages* ambayo inahimiza aina moja ya zao kuzalishwa katika eneo moja kwa lengo la kuongeza uzalishaji. Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine, kinatoa mafunzo na pia kusambaza mbegu bora kwa wakulima wa mfano walioteuliwa ili hatimaye ujuzi huo uigwe na wakulima wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** *BET* imefanikiwa kupata wakufunzi washauri 11 katika mpango wa pamoja wa Taasisi za Afrika Mashariki zinazokuza Biashara ya Nje kwa ushirikiano na Kituo cha Kukuza Uagizaji Bidhaa kutoka Nchi Zinazoendelea *(Centre for Promotion of Imports from Developing Countries)* cha Uholanzi. Wakufunzi washauri watatumiwa na *BET* katika programu zake za mafunzo kwa wajasiriamali na makundi mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** *BET* iliratibu ushiriki wa Tanzania katika maonesho mbalimbali ya Kimataifa, kama vile *Nairobi International Trade Fair"*, 9th China *Investment and Trade Fair*, *Rwanda EXPO, Cairo International Trade Fair* na *Zimbabwe International Trade Fair* ambapo *BET* iliwadhamini wajasiriamali 30 kushiriki maonesho hayo kwa kuwalipia gharama za pango la mabanda pamoja na usafirishaji wa bidhaa zao. Fursa hii inawapa nafasi ya kujua mwenendo wa masoko na mahitaji yake na kujua namna ya kuongeza mauzo katika masoko ya nje. Katika mwaka wa fedha 2005/2006, *BET* ilikiongezea uwezo kituo chake cha Zanzibar kwa kuwapa vifaa na vitendea kazi kama vile mashine ya *photocopier* , kompyuta, *scanner,* viyoyozi, samani, majarida na kuunganisha mtandao wa mawasiliano katika ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** katika mkakati wa kutafuta masoko kwa bidhaa zetu, *BET* ilifanya utafiti wa soko la asali na nta ya Tanzania katika nchi za Oman na Muungano wa Nchi za Falme za Kiarabu. Utafiti umetoa matokeo mazuri kwa asali hiyo kukubaliwa katika soko hilo na tumepata oda ya tani 30 zenye thamani ya Dola za Kimarekani 45,000. Taarifa za utafiti huu zimesambazwa katika vijiji vya Mikoa ya Singida na Tabora kwa lengo la kuhamasisha uundaji wa vikundi vya wafugaji nyuki ili waweze kutumia fursa za soko hilo la Uarabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Urari wa Biashara: Manunuzi ya bidhaa kutoka nje yaliongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 1,340.5 mwaka 1995 hadi kufikia Dola za Kimarekani milioni 2,677.8 mwaka 2005. Kadhalika, manunuzi ya bidhaa kutoka nje yaliongezeka toka asilimia 2.38 mwaka 1995 hadi kufikia asilimia 7.2 mwaka 2005. Katika mwaka 2005, urari wa biashara ya bidhaa ulikuwa na nakisi ya Dola za Kimarekani milioni 985.5, ikilinganishwa na nakisi za Dola za Kimarekani milioni 866.6 mwaka 2004 sawa na asilimia 13.7. Kuongezeka kwa nakisi katika urari wa biashara ya bidhaa kulichangiwa zaidi na ongezeko la thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje ikilinganishwa na mauzo ya bidhaa nje. Aidha, urari wa biashara ya huduma ulikuwa na ziada ya Dola za Kimarekani milioni 35.2 mwaka 2005 ikilinganishwa na ziada ya Dola za Kimarekani milioni 151.9 mwaka 2004. Kupungua huko kulichangiwa na ongezeko kubwa la malipo ya huduma, hasa malipo ya gharama za uingizaji mizigo pamoja na safari za nje ikilinganishwa na ongezeko la mapato yaliyotokana na biashara ya huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fursa za Masoko ya Masharti Nafuu kwa Nchi Zinazoendelea: Kuwepo kwa fursa nyingi za masoko kutawawezesha wafanyabiashara wa Tanzania kwa ujumla kuuza bidhaa nyingi na bora. Ili kukuza na kupanua wigo wa biashara baina ya Tanzania na nchi mbalimbali, Wizara yangu ikishirikiana na Sekta Binafsi ilifanya makongamano ya biashara na uwekezaji katika nchi za Falme za Kiarabu, China, Jamhuri ya Korea Kusini, Japan, Vietnam na Urusi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ilifanikiwa kuingia katika mpango maalum wa *African Growth and Opportunity Act (AGOA)* Februari 2002. Mpango huu umewezesha kuvutia wawekezaji hususan, katika uzalishaji wa nguo na mavazi. Kwa sasa waliofanikiwa kushiriki katika mpango huu wanajumuisha *Sunflag (T) Ltd; Tanzania - China Friendship Textile Mills Ltd; A to Z Textile Mill Ltd; Footlose Ltd na Marvelous Batik. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa Dola za Kimarekani milioni 12.4 zimepatikana kutokana na mpango wa *AGOA*. Aidha, fursa nyingine za masoko yenye masharti nafuu ni mfumo unaoruhusu nchi maskini kuuza bidhaa mbali mbali kwenye soko la Ulaya isipokuwa silaha unaojulikana kama *Everything But Arms (EBA)*. Vile vile, China, Japan na Canada wanatoa masharti nafuu kwa nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2005/2006 kupitia bajeti ya MKUKUTA, *BET* ilifanya semina katika Mikoa ya Mwanza, Tanga, Morogoro na Arusha ambazo zililenga kuwaelimisha wafanyabiashara katika Mikoa husika juu ya fursa za masoko nafuu yakiwemo ya *EAC, SADC*, China, *AGOA* na *EBA*.

Wafanyabiashara 300 waliweza kunufaika na mafunzo haya muhimu na baadhi wameanza kufanya mawasiliano na wanunuzi ili kuweza kufanya biashara.

Vile vile, *BET* imefanikiwa kutoa mafunzo kwa wajasiriamali 15 katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2005/2006 ambayo yanafadhiliwa na taasisi ya Ujerumani iitwayo *INWENT*. Mafunzo haya yanalenga kuwafundisha wajasiriamali wa Kitanzania (ambao wameonyesha uwezo wa kuuza bidhaa nje) juu ya mbinu za kushiriki katika Biashara ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirikiano Kikanda; *EAC* na *SADC*. Mwenendo wa biashara kati ya Tanzania na nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* umekuwa wa kuridhisha kiasi. Mauzo ya Tanzania yameongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 24.4 mwaka 1997 na kufikia Dola za Kimarekani milioni 96.4 mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya kimuundo katika *SADC* yamewezesha kuanzishwa kwa mpango kamambe wa kimkakati ujulikanao kama *Regional Indicative Strategic Development Plan – RISDP* kwa ajili ya kufikia azma yake ya kuwa chombo cha muungano, kupunguza umaskini na kuleta maendeleo endelevu. Masuala muhimu yanayoshughulikiwa na nchi zote kwa sasa ni yale ya taratibu za kulinda Afya ya Wanyama, Binadamu na Mimea *(Sanitary and Phytosanitary Measures – SPS)* na yale ya vizuizi vya kiufundi vya kibiashara *Technical Barriers to Trade - TBT* ili bidhaa katika soko zifikie kiwango cha Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirikiano na nchi za *ACP* na *EU*: Majadiliano ya utaratibu mpya wa kudumu wa ushirikiano *(Economic Partnership Agreements (EPAs)* baina ya nchi za Afrika, *Carribean* na *Pacific (ACP)* na Jumuiya ya Ulaya *(EU)* yanaendelea. Mpango huu ni wa kubadilishana fursa za biashara yaani "nipe nikupe" *(reciprocity)* na unatarajiwa kuanza kutumika ifikapo Januari 2008, kwa misingi ya Mkataba mama wa *Cotonuo*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Majadiliano ya kibiashara kati ya *SADC* na Jumuiya ya Ulaya yanaendelea. Kwa upande wa *SADC*, katika majadiliano ya *SADC/EPA* na *EU*, Tanzania imepewa jukumu la kuratibu majadiliano hayo katika Biashara ya Huduma na Sera ya Uwekezaji na Ushindani. Maandalizi haya yanaendeshwa na Serikali ikishirikiana na wadau katika kuweka misimamo ya Kitaifa na Kikanda kuhusu maeneo yote yanayohusika katika majadiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utandawazi: Serikali iliazimia kushiriki kikamilifu katika michakato ya Kimataifa inayoratibiwa chini ya mfumo wa *WTO* kwa lengo la kuboresha mazingira ya Biashara ya Kimataifa na utandawazi kwa ujumla hususan majadiliano ya Doha. Masuala muhimu yaliyopewa kipaumbele katika mkutano wa Mawaziri Hong Kong ni upatikanaji wa misaada inayolenga kuinua biashara, masuala ya uwezeshaji wa biashara, huduma na hakimiliki. Katika utekelezaji wa makubaliano hayo, hatuna budi kwenda sambamba na matakwa ya wanachama wengine wa Shirika la Biashara la Dunia. Tanzania ikiwa mojawapo ya nchi maskini za kundi la *LDC* ilifanikiwa kutetea maslahi yake katika maeneo mawili: la kwanza, ni lile la kusamehewa

majukumu ya kulegeza masharti ya soko la biashara ya huduma; na la pili, ni lile la kusamehewa kutumia kanuni ya kupunguza ushuru wa forodha kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mchango wa Taasisi za Uwezeshaji katika Sekta ya Biashara: Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* kinatoa mafunzo ya taaluma za Uhasibu, Masoko, Ununuzi na Ugavi, ambayo yanawezesha watu mbalimbali kupata utaalamu wa kushiriki nyanja mbalimbali za kuanzisha na kuendeleza biashara. Aidha, Chuo kina mpango wa kupanua mtandao wa mafunzo ya elimu ya biashara kwa kuanzisha tawi jingine Kanda ya Ziwa jijini Mwanza kwa lengo la kusogeza huduma zake karibu na wananchi. Vile vile, Chuo kinaendesha mafunzo kwa mfumo wa masomo ya jioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uboreshaji wa mitaala katika Chuo cha Elimu ya Biashara kulingana na mahitaji ya soko unazingatiwa hasa katika michepuo ya masoko, uhasibu, ununuzi na ugavi. Aidha, uenezaji wa elimu ya biashara ya ujasiriamali, uendeshaji na usimamizi bora wa biashara ndogo na za kati unatolewa na Chuo. Pia, mafunzo ya ushauri na utafiti ya ujasiriamali yanatolewa kwa wafanyabiashara katika stadi za uhasibu, fedha, utunzaji kumbukumbu za biashara na ukuzaji wa masoko na mauzo.*(Makofi)*

Vile vile, Chuo kinatoa mafunzo ya ushauri wa kitaalamu na utafiti vijijini kupitia Kitengo cha Ujasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Kibiashara cha Tanzania kilichoko London kwa kushirikiana na Ubalozi wetu nchini Uingereza, kiliendelea kuitangaza Tanzania katika nchi za Ulaya. Katika kipindi cha mwaka 2005/2006, kituo kilikusanya na kutoa taarifa za fursa za biashara na uwekezaji, kuhudumia misafara ya kibiashara, kutangaza vivutio vya utalii katika maonesho yaliyofanyika katika miji ya London, Manchester na Glasgow. Aidha, kituo kilishiriki mikutano mbalimbali ya mashirika na taasisi ambazo Tanzania ni mwanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zinazoikabili Sekta ya Biashara ni pamoja na:-

(a) Gharama kubwa za uzalishaji;

(b) Ufungashaji wa bidhaa usiofikia viwango vya ubora wa Kimataifa;

(c) Ukosefu wa taarifa za masoko na taaluma ya utumiaji wa teknolojia ya mawasiliano;

(d) Mwitikio mdogo wa wawekezaji;

(e) Ukosefu wa teknolojia zinazoinua ufanisi wa uzalishaji wa bidhaa nyingi na za viwango vya ubora unaokidhi mahitaji ya soko la Kimataifa;

(f) Kutokuwepo Maafisa Biashara Waambata katika Balozi zetu nje ambao wangetafiti na kutoa taarifa za *Market Intelligence* na kuwa kiungo kati ya Serikali na wafanyabiashara;

(g) Mfumo wa ushindani wa Biashara ya Kimataifa usio wa haki;

(h) Kushindwa kuongeza thamani katika bidhaa zetu

(i) Kushindwa kupanua wigo wa bidhaa na masoko na

(j) Miundombinu hafifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zifuatazo zimechukuliwa ili kukabili changamoto hizo:

(a)Wizara imewezesha wadau kushiriki kikamilifu katika majadiliano ya biashara ya Kikanda na Kimataifa

(b) Sheria ya *EPZ* ilipitishwa mwanzoni mwa mwaka 2002 pamoja na marekebisho ya mwaka 2006 kuwawezesha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuzalisha bidhaa bora kwa ajili ya soko la nje

(c) Katika kutatua tatizo la ukosefu wa taarifa za masoko, tayari Kituo cha Taarifa za Masoko *(Trade Portal)* kimeanzishwa *BET*, ikiwa ni pamoja na vituo vya kupokea na kutoa taarifa za biashara *(Reference Centres)* vilivyoko *CBE*, *TCCIA*, *TBS*, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na Wizara ya Kilimo, ambapo wafanyabiashara wanaweza kupata taarifa mbalimbali za masoko

(d)Mchakato wa kuboresha maabara za Tanzania na kuzifanya zikubalike *(Accredited)* na asasi za Kimataifa za viwango unaendelea

(e) Katika kuimarisha Ofisi ya Geneva, Wizara imeongeza mtaalamu wa biashara katika ubalozi wa Tanzania Geneva, ikiwa ni pamoja na mtaalamu mmoja kupata mafunzo kazini katika ubalozi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera na Mkakati wa Kuendeleza Masoko, kwa kuwa maendeleo ya sekta ya kilimo hutegemea kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa masoko ya uhakika kwa mazao yanayozalishwa, Serikali imekuwa ikifanya mabadiliko ya kisera na kimkakati ili kukuza masoko ya mazao ya kilimo tangu mwanzoni mwa miaka ya tisini.

Baadhi ya matokeo ya mabadiliko haya yanajumuisha kuimarika kwa bei za mazao; kuongezeka kwa uzalishaji na mauzo ya nje kwa baadhi ya mazao; kuongezeka kwa vyanzo vya mikopo pamoja na kuboreshwa kwa miundombinu ya masoko na mfumo wa upatikanaji wa taarifa za masoko. Aidha, mafanikio mengine yanajumuisha yafuatayo:-

(a) Wizara kwa kushirikiana na Programu ya Kuendeleza Mifumo ya Masoko ya Mazao imeviunganisha vikundi vya wakulima na masoko maalum ikiwa ni pamoja na kuanzisha kilimo cha mkataba kwa mazao ya mboga mboga kati ya wakulima wadogo na Kampuni zinazouza mboga mboga katika soko la Jumuiya ya Ulaya

(b) Kufanya utafiti wa zao la Vitunguu Wilayani Kilosa; utafiti kuhusu biashara ya zao la Kahawa Mkoani Kagera ili kuainisha chanzo cha kuwepo kwa biashara isiyo rasmi

kati ya Mkoa huo na nchi za jirani unaoendelea na uchunguzi wa vipimo vinavyotumika kununulia mazao kutoka kwa wakulima

(c) Mafunzo ya ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa za masoko yalitolewa kwa wakusanyaji wa taarifa za masoko kutoka Wilaya 75. Vile vile, wakusanyaji wa taarifa hizo katika ngazi ya Mkoa walipatiwa vitendea kazi zikiwemo kompyuta sita

(d) Wizara imepanua wigo wa usambazaji wa taarifa za bei za mazao kwa kupitia ujumbe mfupi wa maneno katika simu za mikononi za Kampuni ya *Vodacom Tanzania Limited* ;na

(e) Wizara imeboresha mfumo wa kuhifadhi na kuchambua taarifa za masoko kwa kutumia kompyuta na programu maalum kwa taarifa za masoko ya mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pamoja na mafanikio hayo, bado kumekuwepo na changamoto zinazowakabili wazalishaji, wasindikaji na wafanyabiashara wa mazao. Ili kuweka mwongozo wa kisera na kimkakati katika kushughulikia changamoto za masoko ya mazao na bidhaa za kilimo, Serikali iko katika hatua za mwisho za maandalizi ya Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ununuzi wa Mazao Asilia: Mazao ambayo ununuzi wake uliongezeka katika msimu wa mwaka 2005/2006 ikilinganishwa na msimu wa mwaka 2004/2005, yanajumuisha pamba mbegu, tumbaku ya mvuke, korosho, mkonge, maua ya pareto na miwa. Vinatoa takwimu za ongezeko kwa kila zao. Kuongezeka kwa ununuzi wa mazao hayo kulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji. Aidha, ununuzi wa mazao ya tumbaku ya moshi, kahawa na chai ulipungua. Kushuka kwa ununuzi wa kahawa na chai kulisababishwa na kushuka kwa uzalishaji ambao kwa kiasi kikubwa kulisababishwa na ukame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bei ya Mkulima *(Producer Price)* bei ya mkulima iliongezeka kwa mazao ya kahawa ya *robusta*, kahawa ya *arabica*, chai pamoja na zao la miwa kwa mkataba *(outgrowers)* kama. Kuongezeka kwa bei ya mkulima kwa mazao ya kahawa na chai kulisababishwa na kuimarika kwa bei ya mazao hayo katika soko la dunia na kuongezeka kwa ubora wa mazao. Kwa mfano, bei ya kuuzia nje kahawa aina ya *arabica* iliongezeka kwa asilimia 13 na bei ya chai iliongezeka kwa asilimia 2. Aidha, bei ya mkulima kwa zao la pamba ilishuka kutoka wastani wa Shilingi 250 kwa kilo msimu wa 2004/2005 hadi Shilingi 220 kwa kilo msimu wa 2005/2006 ikiwa ni anguko la asilimia 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bei ya Kuuzia Nje Mazao bei ya kuuzia nje kahawa aina ya arabica iliongezeka kwa asilimia 13, pamba asilimia 10, tumbaku ya moshi asilimia 25, chai asilimia 2 na mkonge asilimia 7. Bei ya kuuzia nje korosho ghafi na tumbaku ya mvuke ilipungua kwa asilimia 17 na 20 sawia. Bei ya kuuzia nje korosho ghafi ilishuka kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa zao hilo duniani. Uzalishaji wa korosho duniani umeongezeka maradufu kutoka tani milioni 0.8 mwaka 1995 hadi tani

milioni 1.6 mwaka 2005. Zao jingine lililoonyesha kushuka kwa bei ya kuuzia nje ni kahawa aina ya robusta ambayo ilishuka kwa asilimia 1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mauzo ya Mazao Ndani ya Nchi: Mauzo ya korosho kwa wabanguaji wa ndani yaliongezeka kutoka tani 7,070 msimu wa 2004/2005 hadi tani 20,000 msimu wa 2005/2006. Aidha, jumla ya tani 381 za kahawa safi ziliuzwa kwa wasindikaji wa ndani msimu wa 2005/2006 ikilinganishwa na tani 229 msimu wa 2004/2005. Jumla ya tani 363 za kahawa zilisindikwa katika viwanda vya ndani msimu wa 2005/2006 ikilinganishwa na tani 214 msimu wa 2004/2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya tani 3,000 za chai zenye thamani ya Shilingi bilioni 3.6 zinatarajiwa kuuzwa katika soko la ndani msimu 2005/2006 ikilinganishwa na tani 4,329 zilizouzwa msimu wa 2004/2005 zilizokuwa na thamani ya Shilingi bilioni 4.3. Aidha, mauzo ya pamba kwa viwanda vya ndani msimu wa 2005/2006 yamefikia tani 25,100 ikilinganishwa na tani 30,475 zilizouzwa msimu wa 2004/2005. Msimu wa mauzo wa 2005/2006 bado unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mauzo ya Mazao Nje ya Nchi: Katika msimu wa 2005/2006 mauzo ya nje kwa mazao makuu ya biashara yalipungua kwa mazao mengi isipokuwa zao la tumbaku na pareto. Aidha, mauzo ya mkonge yalilingana na mauzo ya msimu uliotangulia ambapo tani 11,693 ziliuzwa. Hata hivyo, thamani ya mauzo hayo iliongezeka kwa asilimia 8 kutoka Dola za Kimarekani 8,214,505 hadi Dola za Kimarekani 8,899,694. Aidha, mauzo ya korosho ghafi nje yalishuka kutokana na kuongezeka kwa wasindikaji wa ndani. Jumla ya tani 20,000 ziliuzwa kwa wasindikaji wa ndani msimu wa 2005/06 ikilinganishwa na tani 7,070 msimu 2004/2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Mei 2006, mauzo ya kahawa safi *(green coffee)* nje ya nchi yalikuwa tani 31,356 na kuliingizia Taifa Dola za Kimarekani 59,406,628. Msimu wa mauzo ya kahawa bado unaendelea. Jumla ya tani 42,517 za kahawa safi zenye thamani ya Dola za Kimarekani 74,792,907 ziliuzwa nje ya nchi msimu wa 2004/2005. Wanunuzi wakuu wa kahawa ya Tanzania msimu wa 2005/06 walikuwa ni Japan (33%), Ujerumani (22%), Italia (19%), Marekani (6%), Uswisi (4%), Ubeligiji (4%), Uholanzi (4%) na nchi nyingine (8%).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauzo ya nje kwa zao la pamba msimu wa 2005/06 hadi Aprili 2006 yalifikia tani 83,362 ikilinganishwa na tani 84,021 zilizouzwa msimu wa 2004/05. Msimu wa mauzo unaendelea na hivyo kuna uwezekano wa kuzidi kiwango cha mauzo yaliyopatikana msimu wa 2004/2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mauzo ya Nje kwa Mazao ya Biashara Yasiyokuwa Asilia: Thamani ya mauzo ya maua na mboga nchi za nje yaliongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 14.3 kipindi cha msimu wa 2004/2005 na kufikia Dola za Kimarekani milioni 18.3 msimu wa 2005/06. Ongezeko hili ni asilimia 28 na kwa kiasi kikubwa limetokana na kuongezeka kwa wastani wa bei na matumizi katika soko la dunia pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bei ya Mazao Makuu ya Chakula: Wastani wa bei ya mazao makuu ya chakula hususan mahindi, mchele na maharage ulipanda mwishoni mwa mwaka 2005 na mwanzoni mwa mwaka 2006 kutokana na kupungua kwa ugavi wa mazao hayo, kulikosababishwa na kuchelewa kwa msimu wa mvua za vuli na masika. Kwa mfano, bei ya jumla ya gunia la mahindi la kilo 100 katika jiji la Dar es Salaam ilipanda kutoka wastani wa Shilingi 15,438 mwezi Septemba 2005 hadi Shilingi 20,700 mwezi Desemba 2005 na kuendelea kupanda hadi kufikia wastani wa Shilingi 30,000 mwezi Machi 2006. Katika Jiji la Mbeya bei ya jumla ya mahindi iliongezeka kutoka Shilingi 12,041 mwezi Septemba 2005 na kufikia Shilingi 29,916 mwezi Machi 2006. Bei ya mchele Jijini Dar es Salaam iliongezeka kutoka Shilingi 52,958 mwezi Septemba 2005 na kufikia Shilingi 82,500 mwezi Machi 2006. Jijini Mbeya, bei ya jumla ya mchele iliongezeka kutoka Shilingi 44,833 mwezi Septemba 2005 na kufikia Shilingi 64,166 mwezi Machi 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti kubwa ya bei ya mazao makuu ya chakula kati ya masoko mbalimbali nchini ni kiashirio cha kuendelea kuwepo kwa matatizo ya miundombinu duni ya masoko kama barabara za vijijini, magulio au vituo vya kuuzia na kununulia mazao. Gharama kubwa za kusafirisha mazao kutoka maeneo yanakozalishwa kwenda kwa walaji husabisha kushuka kwa bei anayopata mzalishaji. Aidha, soko la mazao ya chakula bado linakabiliwa na matatizo ya kiwango cha chini cha usindikaji wa mazao hayo, kukosekana kwa mitaji kwa wafanyabiashara wadogo na udhaifu katika usimamizi wa uuzaji wa mazao kulingana na madaraja, ubora na vipimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifugo na Bidhaa Zake: Sekta ya Mifugo imeendelea kutegemea soko la ndani kwa maendeleo yake. Sababu kubwa ya mifugo na bidhaa zake kuendelea kutegemea soko la ndani ni pamoja na kuwepo kwa magonjwa ya mifugo na ubora usiokidhi mahitaji na masharti katika masoko ya nchi za nje. Serikali imeendelea kuweka mazingira mazuri yatakayowezesha bidhaa hizo ziweze kuuzwa katika masoko ya Kimataifa. Tanzania huuza mifugo katika nchi za Ghuba na Visiwa vya Comoro ingawaje biashara hii siyo kubwa. Aidha, biashara ya mifugo isiyo rasmi hufanyika kati ya nchi yetu na nchi za jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ununuzi wa ngozi za ng'ombe, mbuzi na kondoo katika msimu wa 2005/2006 uliongezeka kwa asilimia 4 ikilinganishwa na msimu wa 2004/2005. Mapato ya wafugaji kutokana na mauzo hayo yaliongezeka kwa asilimia 24 kutoka Shilingi bilioni 5.5 hadi Shilingi bilioni 6.2 msimu wa 2005/2006. Aidha, mauzo ya ngozi nje ya nchi katika kipindi hicho yaliongezeka kwa asilimia 8 kutoka vipande milioni 3.2 hadi vipande milioni 3.7 na mapato kutokana na mauzo hayo yaliongezeka kwa asilimia 86.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwepo kwa fursa mbalimbali za masoko ndani na nje ya nchi, Tanzania haijazitumia fursa hizo kikamilifu kutokana na matatizo ambayo bado yanaukabili mfumo wa masoko ya mazao ya kilimo nchini. Matatizo hayo ni pamoja na:-

(a) Gharama kubwa za kufanya biashara ya mazao kutokana na uduni wa miundombinu ya kusafirisha, kuhifadhi na kusindika mazao ya kilimo

(b) Uduni wa ubora na uchache wa mazao yanayozalishwa na hivyo kushindwa kushindana na bidhaa kutoka nchi nyingine hasa katika soko la dunia

(c)Upungufu wa taarifa sahihi za masoko kwa wazalishaji, wasindikaji na wafanyabiashara

(d)Uwezo mdogo wa kuyaongezea thamani mazao ambao pamoja na sababu zingine unatokana na ukosefu wa mtaji(e) Udhaifu katika kusimamia sheria, kanuni na taratibu za ununuzi wa mazao na hasa yale yasiyosimamiwa na Bodi za Mazao na

(f) Kuongezeka kwa ushindani usiokuwa wa haki wa mazao na bidhaa za kilimo zinazoingizwa kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na matatizo yanayokwamisha Sekta ya Masoko ya mazao na bidhaa za kilimo, Wizara ilichukua hatua zifuatazo:-

(a) Kuandaa, kusimamia, kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Sera, Sheria na kanuni zinazohusu masoko ya mazao na bidhaa za kilimo kwa kutekeleza yafuatayo:-

· Kukamilisha Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo

· Kukamilisha Kanuni za Utekelezaji wa Sheria ya Stakabadhi za Mazao Ghalani ya mwaka 2005 na

· Kuhamasisha wadau mbalimbali (wakulima, wafanyabiashara, taasisi za fedha) kuhusu matumizi ya Mfumo huo.

(b) Kuanzisha na kuendeleza mikakati ya kukuza masoko ya mazao na bidhaa za kilimo ndani na nje ya nchi. Utekelezaji wa jukumu hili ulihusisha yafuatayo:-

· Kuhimiza wakulima na wasindikaji kuzalisha kulingana na mahitaji ya soko ili kuifanya shughuli ya kilimo kuwa na manufaa

· Kuhamasisha uwekezaji katika miundombinu ya masoko na uongezaji thamani wa mazao na bidhaa za kilimo

· Kuendeleza matumizi ya mbinu mbalimbali za kukinga athari zinazojitokeza katika masoko

· Kuendeleza soko la ndani kwa mazao na bidhaa za kilimo zinazozalishwa nchini

· Kuhamasisha wakulima na wafanyabiashara kutumia fursa zilizopo za masoko ya kikanda na Kimataifa na

· Kufanya tafiti mbalimbali za masoko ili kuainisha matatizo kwa lengo la kuyatafutia ufumbuzi

(c) Kuboresha upatikanaji na usambazaji wa taarifa za masoko ya mazao na bidhaa za kilimo. Utekelezaji wa hatua hii ulihusisha:

· Kuandaa Kitabu cha Orodha ya Wanunuzi na Wasindikaji wa Mazao ya Kilimo *(Agribusiness Directory*

· Kuimarisha na kuendeleza mfumo wa ukusanyaji, uchambuzi, hifadhi na usambazaji wa taarifa za masoko ikiwa ni pamoja na kuwezesha Halmashauri kutekeleza jukumu hilo.

(d)Kusimamia utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Mifumo ya Masoko. Utekelezaji wa jukumu hili unahusisha Wilaya 38 katika Mikoa nane kwa kutekeleza yafuatayo:-

·Kuwezesha maandalizi ya Sera ya Masoko ya Mazao kwa kugharamia wataalam, washauri waelekezi na mafunzo.

·Programu ilitoa mafunzo kwa Wahandisi na Mafundi kutoka Wilaya 18 na kukamilisha ujenzi wa masoko ya kisasa katika maeneo ya Kikatiti (Arumeru), Matai (Sumbawanga) na Kwasadala (Hai). Pia ujenzi wa ghala la kuhifadhia mazao katika mji mdogo wa Magugu (Babati) umekamilika na ukarabati wa maghala katika vijiji vya Qash (Babati), Chimala (Mbarali) na Iwindi (Mbeya) umefanyika.

Aidha, jumla ya kilomita 210 za barabara za vijijini zilijengwa katika Wilaya nane (Arumeru, Hai, Babati, Muheza, Mufindi, Mbeya, Sumbawanga na Songea).

·Mafunzo ya matumizi ya mfumo wa stakabadhi za mazao ghalani yalitolewa kwa wanachama wa vyama vya kuweka na kukopa *(SACCOS),* pamoja na kuunganisha vyama hivyo na mabenki yanayotoa mikopo kwa ajili ya mfumo wa stakabadhi za mazao; benki za *CRDB* na *Exim* ndizo zilizokubali kutoa mikopo chini ya Mfumo wa Stakabadhi za Mazao. Mfumo huu umeonyesha mafanikio makubwa kwa wakulima kupata bei nzuri za mazao yaliyojaribiwa katika mfumo huo.

·Kuboresha upatikanaji wa mitaji na mbinu za kujikinga na maanguko ya bei za mazao kwa kutumia Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani; na

·Kujasirisha wakulima na wafanyabiashara wa mazao na bidhaa za kilimo na kuwaunganisha na masoko.

(h) Kusimamia Mradi wa Kuendeleza na Kuboresha Biashara ya Pamba na Kahawa kwa kufanya kazi zifuatazo katika mwaka 2005/06: -

· Kujadili na kupokea maoni ya wadau kuhusu Rasimu ya Kanuni za Sheria ya Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalan.

·Kushiriki katika mikutano ya wadau wa mazao ya pamba na kahawa kwa lengo la kuboresha masoko ya mazao hayo na kufuatilia utekelezaji wa mradi; na

·Kuandaa stakabadhi zitakazotumika katika Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani na kuendeelea kuhamasisha matumizi ya mfumo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo. Utekelezaji wa Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo: Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo imeendelea kutoa mchango muhimu katika ukuaji wa uchumi. Maendeleo ya sekta hii ni muhimu hasa kwa vile pamoja na kuongeza ajira, inasaidia kutoa msingi wa ujuzi na uzoefu kwa wanaviwanda na wafanyabiashara wadogo. Katika kuchochea maendeleo ya sekta hii, Serikali ilipitisha Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo katika mwaka 2003. Sera hii inalenga kuweka mazingira mazuri yatakayowezesha uanzishaji wa miradi mipya na wakati huo huo kuwezesha miradi iliyopo kuimarika na kuongeza mchango wa sekta hii katika pato la Taifa. Mikakati iliyoainishwa katika sera ni pamoja na kuboresha mfumo wa sheria na taratibu; kuimarisha miundombinu; kuboresha huduma za masoko, ujasiriamali, upatikanaji wa taarifa na teknolojia na pia kuboresha upatikanaji wa huduma za kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, semina za kikanda zilifanyika ili kuendelea kuelimisha wananchi juu ya Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo na kuwafahamisha juu ya fursa zilizopo. Aidha, nakala ya sera katika lugha rahisi inaandaliwa. Wizara imekwishaanza kuchukua hatua mbali mbali za utekelezaji wa sera, hii ikiwa ni pamoja na maandalizi yaliyofanyika kwa kushirikiana na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo *(IFAD)* ya kuanzisha programu ya kuendeleza viwanda vidogo na biashara ndogo vijijini. Kwa kuanzia, programu hii itatekelezwa katika Mikoa ya Pwani, Tanga, Manyara, Mwanza, Iringa na Ruvuma. Vile vile, Mfuko maalum wa kuchochea ukuaji wa viwanda vidogo na biashara ndogo *(SME competitiveness Facility)* umeanzishwa kwa msaada wa Shirika la Maendeleo la Denmark *(DANIDA).* Madhumuni ya mfuko huu ni kuwezesha wajasiriamali wadogo kuimarisha ubora wa bidhaa zao ili kuweza kuyafikia masoko ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kufuatilia utekelezaji wa mfuko wa kudhamini miradi ya viwanda vidogo na biashara ndogo. Pia, Wizara inashirikiana na Shirika la Kazi Duniani *(ILO)* kutekeleza mradi wa kuendeleza wajasiriamali wanawake kwa kuwapatia mafunzo yanayochochea ujasiriamali, uimarishaji wa vikundi vya uzalishaji na utafutaji wa masoko.

Aidha, Wizara imeendelea kuimarisha taasisi zinazohudumia sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo, hii ikiwa ni pamoja na *SIDO* ili taasisi hizi ziimarishe utoaji wa huduma kwa wajasiriamali wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha 2005/06, Wizara kupitia *SIDO* iliendelea kutoa huduma za kiufundi kwa wajasiriamali wadogo ambapo, jumla ya mashine 383 zilitengenezwa na wanaviwanda 540 walipatiwa mafunzo ya kiufundi. Pia, jumla ya wajasiriamali 4,926 walipatiwa mafunzo ya ujasiriamali na mbinu za biashara, wananchi 1,066 walipatiwa mafunzo ya usindikaji na uhifadhi wa vyakula na wananchi 4,200 walipatiwa ushauri. Aidha, wajasiriamali wadogo 968 walipata fursa ya kushiriki katika maonesho ya kikanda yanayoendeshwa na *SIDO* ambapo waliweza kufanya mauzo ya Shilingi milioni 120 na pia kupata oda za Shilingi milioni 160.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya kuendeleza ardhi na miundombinu kwa ajili ya viwanda vidogo na biashara ndogo inayotekelezwa ni pamoja na:- vituo vya biashara vya Songea na Moshi; uimarishaji wa kituo cha mafunzo na uzalishaji cha Njombe; ujenzi wa majengo ya wafanyabiashara wadogo katika miji ya Makambako na Babati; ujenzi na uimarishaji wa majengo kwa ajili ya viatamizi kwa ajili ya Dar es Salaam na Mbeya; na ujenzi wa vituo vya wajasiriamali kuoneshea bidhaa zao. Aidha, kwa kutumia utaratibu wa kushirikisha Sekta Binafsi kuendeleza maeneo, ujenzi wa majengo ya viwanda unaendelea katika mitaa ya viwanda iliyoko Mikoa ya Mwanza na Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliendelea kusambaza teknolojia mbalimbali zilizobuniwa, kuzalishwa na kujaribiwa ili ziwafikie walengwa na ziweze kuchangia katika kuongeza ufanisi wa uzalishaji mali, kuongeza ajira na kipato na hatimaye kupunguza umaskini. Mashine za kuwasaidia wakulima katika kilimo na usindikaji wa mazao ya kilimo zilitengenezwa na Taasisi za *TEMDO, CAMARTEC, TIRDO, Technology Development and Transfer Centre na SIDO.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Wafanyabiashara Wananchi – *NEDF* ulioanzishwa mwaka 1994 hadi kufikia mwezi Machi, 2006 ulikuwa umetoa mitaji yenye thamani ya Shilingi bilioni 8.34 kwa wajasiriamali 23,578 na kuwezesha upatikanaji wa ajira kwa wananchi 33,404. Mwaka 2005/2006, mfuko ulitoa mikopo ya thamani ya Shilingi milioni 285. Aidha, wajasiriamali wadogo 268 walipatiwa mikopo yenye thamani ya Shilingi milioni 481 kutoka Mifuko ya Mitaji ya Mikoa inayosimamiwa na *SIDO*. Wajasiriamali 44 walipatiwa mikopo yenye thamani ya Shilingi milioni 243 kutoka mfuko ulioanzishwa na *SIDO* kwa kutumia fedha za Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Viwanda Vidogo na biashara Ndogo nchini bado inakabiliwa na changamoto mbali mbali. Hii ni pamoja na mwamko mdogo wa wananchi kuzitumia fursa zilizopo, uwezo mdogo wa taasisi zinazoihudumia sekta, ukosefu wa taarifa muhimu hususan kuhusu masoko, matumizi ya teknolojia na miundombinu duni, pamoja na kushindwa kunufaika na mitaji inayotolewa na taasisi za fedha, ikijumuisha kushindwa kumudu masharti ya mikopo.

*Mheshimiwa Mwenyekiti,* Utafiti Na Maendeleo: *CAMARTEC* iliendelea kueneza teknolojia ya *biogas,* majiko sanifu na teknolojia ya udongo-saruji. Katika kipindi hicho, mafunzo na ujenzi wa mtambo wa *"biogas"* wenye mita za ujazo 16 vilifanyika jijini Dar es Salaam kwa mafundi waashi watano. Pia mtambo mmoja wenye ukubwa wa mita 50 za ujazo ulitengenezwa kituoni *CAMARTEC*. Mafunzo kuhusu Teknolojia ya majiko sanifu yalitolewa kwa wajasiriamali 20 waliofundishwa katika Wilaya za Rombo na Ulanga. Katika Wilaya ya Kondoa mafunzo ya teknolojia ya udongo–saruji yalitolewa kwa wajasiriamali sita kwa ajili ya ujenzi wa nyumba bora vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TEMDO* katika mwaka 2005 ilibuni teknolojia ambazo zililenga katika kuboresha hali ya maisha ya wananchi walio wengi pamoja na kuendeleza ujasiriamali na kuongeza ajira. *TEMDO* katika kipindi hicho iliendeleza teknolojia za kukamua mafuta ya alizeti, kusindika matunda na kupukuchua mahindi.

Lengo ni kueneza teknolojia hizo vijijini ili kurahisisha kazi na kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vidogo vya kusindika mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TIRDO* katika kipindi cha mwaka 2005 ilibuni teknolojia ambazo zililenga katika kuboresha hali ya maisha ya wananchi, kuendeleza ujasiriamali na kuongeza ajira. *TIRDO* katika kipindi hicho imetoa mafunzo ya uchomeleaji vyuma kwa wazalishaji wadogo na wajasiriamali 75 huko Morogoro, Dar es Salaam, Songea na Ulanga wanaotengeneza mashine za kusindika vyakula na matunda. Aidha, kwa mwaka 2005/2006 idadi ya watu waliofundishwa kusindika matunda na nyanya ni 35 katika maeneo ya Dar es Salaam, Njombe, Iringa na Tanga. Pia, jumla ya wakulima 58 wa Mikoa ya Pwani na Mtwara wamefundishwa juu ya utengenezaji wa unga wa mihogo usio na sumu na wanga katika kuongeza thamani ya mwani, *TIRDO* imefundisha wakulima 85 katika Wilaya za Mkinga na Pangani. Vile vile, *TIRDO* imetoa mafunzo kwa wajasiriamali 649 katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Ruvuma na Kagera kuhusu ufuatiliaji wa mazao toka shambani, viwandani hadi kwa mlaji kwa lengo la kuimarisha ubora na kuweka kumbukumbu. Mazao yaliyohusishwa katika mafunzo hayo ni kahawa, korosho, chai, samaki, maua na viungo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TIRDO* imeendelea kutoa mafunzo ya kilimo cha uyoga kwa wakulima 237 katika Mikoa ya Kilimanjaro, Morogoro na Dar es Salaam. Wazalishaji wadogo 20 wamefundishwa jinsi ya kutumia mtambo wa majaribio wa kutengeneza chumvi wenye uwezo wa kuzalisha tani nne kwa wiki katika Mkoa wa Singida. Kuhusu utengenezaji wa chaki, wajasiriamali 154 wamefundishwa katika Wilaya za Nzega, Ulanga (Mahenge) na Songea. Mafunzo hayo yanaendelea katika Mikoa ya Morogoro na Mtwara. Aidha, vikundi vinne vya wajasiriamali 82 vimefundishwa juu ya ukusanyaji, usafishaji na kurejeleza taka za plastiki na karatasi kwa lengo la kutunza mazingira na kuongeza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu ya utafiti, taasisi hizi zimekuwa zikikabiliwa na matatizo kama vile uwezo mdogo kifedha kwa ajili ya kufanya tafiti, uwezo mdogo wa wajasiriamali kuzalisha kibiashara kwa kutumia teknolojia zilizopasishwa kwa matumizi, uwezo mdogo wa kutangaza teknolojia zilizopasishwa, uwezo mdogo wa walengwa kununua na kutumia teknolojia zinazobuniwa, na kupanda kwa gharama za malighafi. Aidha, viwanda vinavyomilikiwa na Makampuni ya Kimataifa hupendelea kutumia kampuni mama katika utafiti na hivyo kutotumia huduma za taasisi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zilizochukuliwa ili kukwamua matatizo ya Taasisi hizo ni pamoja na Serikali kuzitengea fedha kutokana na bajeti ya MKUKUTA ili kuziwezesha kufanya tafiti mbalimbali na kutangaza teknolojia zilizopasishwa ziweze kufikia walengwa. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine imeendelea kufanya marekebisho ya sheria zilizoanzisha taasisi hizi ili ziendane na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usimamiaji wa Sheria za Udhibiti: Usajili; *BRELA* iliendelea kutekeleza majukumu yake ya usajili na kusimamia sheria ya makampuni, majina ya biashara, alama za biashara, hataza, na sheria ya leseni ya viwanda. Katika

mwaka 2005/06, ufanisi wa utendaji kazi wa Wakala ulikuwa wa mafanikio. Kwa mfano usajili wa kampuni na usajili wa majina ya biashara haukuwa na muda maalum wa kukamilishwa hapo awali, hivi sasa unakamilika ndani ya siku tatu hadi tano. Kwa ujumla muda anaotumia mteja kupata huduma umepungua, kiwango cha kutii sheria kwenye makampuni na kufuata taratibu zake kiliongezeka na mapato ya wakala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *BRELA* imefanikiwa kupunguza kero za wateja na washitiri wake katika kusubiri muda mrefu kuandikisha kampuni, jina la biashara na kupata leseni ya viwanda kwa kuondoa masharti yasiyokuwa ya lazima. Mafanikio mengine ni pamoja na Sheria mpya ya Makampuni Na.12 ya mwaka 2002 kuanza kutekelezwa mwezi Machi 2006. Mafanikio hayo yamewezesha kuongezeka kwa majina ya biashara zinazosajiliwa kutoka 5,890 mwaka 2004/2005 hadi 7,409 mwaka 2005/2006 na makampuni yaliyoandikishwa kutoka 3,347 mwaka 2004/2005 hadi 3,791 mwaka 2005/2006. Ongezeko hilo pia limetokana na uelimishaji wa wadau kuhusu taratibu za usajili kwa njia ya vyombo vya habari, warsha na vipeperushi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hakimiliki: Jukumu mojawapo la Chama cha Hakimiliki cha Tanzania *(Copyright Society of Tanzania – COSOTA)* ni kulinda na kukuza kazi za utunzi na sanaa. *COSOTA* itaendelea kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria ya Hakimiliki Na. 7 ya mwaka 1999. Napenda kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa hadi kufikia mwezi Mei, 2006 *COSOTA* ilisajili wanamuziki binafsi 525, waigizaji 74, watunzi wa vitabu 106, wachapishaji 13 na vikundi 142 vinavyojishughulisha na sanaa.

Aidha, kazi zilizoandikishwa hadi sasa ni 4,875 zikijumuisha 4,467 za muziki, maigizo 110 na maandishi ya vitabu 298. Vile vile, *COSOTA* imeendesha semina za uhamasishaji na kuelimisha wadau kuhusu haki na wajibu chini ya Sheria ya Hakimiliki, katika mikoa ya Mtwara, Kilimanjaro, Tanga, Mara, Lindi, Ruvuma na Iringa. Uhamasishaji na uelimishaji umefanywa pia kwa njia ya Radio na Luninga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ilitayarisha na kuchapisha kanuni mbili zinazohusu Hakimiliki ambazo ni:-

(a) Kanuni ya Usajili wa Wanachama na Kazi Zao, za mwaka 2006 *(Copyright and Neighbouring Rights Registration of Members and Their Works Regulations- 2006)*, ambazo zinaruhusu kutoza ada za uanachama. Kanuni hizi zilichapishwa katika Gazeti la Serikali Na. 6 la tarehe 20/1/2006 na zimeanza kutekelezwa kikamilifu; na

(b) Kanuni ya Kupiga Vita Uharamia wa Kazi za Sanaa na Matumizi ya *Hakigram (The Copyright and Neighbouring Rights- Production and Distribution of Sound and Audiovisual Recordings Regulations 2006)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Vipimo *(Weights and Measures Agency (WMA)* uliendelea kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria na Kanuni ili kuhakikisha kuwa kuna biashara ya haki kati ya wadau.

Katika mwaka 2005/2006, Wakala ulichukua hatua madhubuti ya kuelimisha wananchi kuhusu matumizi sahihi ya vipimo. Kwa kuanzia, mafunzo hayo yalitolewa katika Mikoa ya nyanda za juu kusini. Vile vile, wafanyabiashara wameendelea kupewa ushauri kuhusu vipimo wanavyotakiwa kutumia. Elimu hiyo pia ilitolewa kupitia matangazo katika vyombo vya habari kama vile luninga, redio, magazeti na majarida; na kwenye maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ubora: Shirika la Viwango Tanzania *(Tanzania Bureau of Standards (TBS)* iliendelea na majukumu ya uwekaji viwango vya ubora wa bidhaa na usimamiaji wake. Hadi kufikia mwezi Machi 2006, Shirika lilikuwa limetayarisha Viwango vya Taifa 957 katika sekta mbalimbali zikiwemo za kilimo na chakula, nguo, kemikali, uhandisi na mazingira. Aidha, Shirika liliendelea kusimamia utekelezaji wa Viwango vya Taifa kwa kutumia mifumo iliyopo ya kuhakiki ubora *(certification scheme)*. Hadi kufikia mwezi Machi 2006, Shirika lilikuwa limetoa jumla ya leseni 706 za ubora wa bidhaa mbalimbali katika viwanda 433 vya humu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pamoja na mafanikio hayo, *TBS* inakabiliwa na uchakavu wa vifaa vya maabara na uhaba wa nyenzo nyingine zinazotumika kupima na kudhibiti viwango vya ubora wa bidhaa mbalimbali. Pia, uelewa mdogo wa umma na wafanyabiashara kuhusu umuhimu wa viwango vya ubora katika kulinda afya na usalama wa mlaji na kuzifanya bidhaa zikubalike katika soko la Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBS* kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za Kimataifa ikiwemo *DANIDA*, Sida, *UNIDO*, *UNFPA* na *FAO*, ilifanikisha upatikanaji wa vyombo na mahitaji mbalimbali ya maabara. Aidha, *TBS* kwa msaada wa *Sida* waliweza kutoa mafunzo kwa umma na jumuiya ya wafanyabiashara juu ya umuhimu wa viwango vya ubora wa bidhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushindani wa Haki: Katika kipindi cha mwaka 2005/2006, maandalizi ya utekelezaji wa Sheria mpya ya Ushindani 2003, yalifikia hatua ya kuteua Mwenyekiti, Mkurugenzi Mkuu, Makamishna wa Tume ya Ushindani pamoja na Mwenyekiti na Wajumbe wa Baraza la Ushindani mwezi Novemba 2005. Baada ya uteuzi huo, Makamishna wa Tume na Wajumbe wa Baraza la Ushindani walipata mafunzo ya awali mwezi Desemba 2005 kuhusu sheria na wajibu wao. Vyombo hivi sasa vinakamilisha ajira ili kuweza kutekeleza vyema majukumu yake. Aidha, Baraza la Taifa la Ushauri kwa Mlaji lilianzishwa mwezi Julai 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ya kuendeleza sekta za viwanda, biashara na masoko katika mwaka 2006/2007: Katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaendelea kutekeleza MKUKUTA na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya mwaka 2005. Kama nilivyokwishasema, Ilani hiyo, imebainisha wazi kwamba mwelekeo wa Sekta ya Viwanda iwe ni kukua kwa asilimia 15 ifikapo 2010 na kwamba Sekta za Biashara na Masoko zijenge uwezo wa kushiriki na kufaidika na mfumo wa Biashara ya Kikanda na Kimataifa katika mazingira ya utandawazi. Katika maelezo yafuatayo nimebainisha kwa muhtasari mipango tuliyojiwekea kutekeleza mwelekeo huo kwa kila sekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Viwanda: Katika mwaka 2006/2007, mkazo umewekwa katika juhudi za kuanzisha viwanda mama, kwa kutafuta wabia wa kuwekeza katika mradi wa makaa ya mawe ya Mchuchuma, mradi wa chuma wa Liganga na tafiti za miradi mingine iliyo katika Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara. Kipaumbele kingine ni kuendelea na utekelezaji wa programu inayolenga katika kuimarisha usindikaji wa mazao ya kilimo, mifugo na maliasili; kuendelea kuhamasisha uanzishaji wa maeneo ya uzalishaji kwa ajili ya uuzaji nje *(EPZ)* pamoja na uwekezaji katika viwanda ndani ya maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Changamoto kubwa ambazo zinaikabili sekta ya Viwanda ni pamoja na ukosefu wa vyanzo vya mikopo ya muda mrefu kwa ajili ya uwekezaji katika sekta ya Viwanda, ufinyu wa soko la ndani unaotokana na kasumba ya wananchi kuthamini na kupendelea kununua bidhaa kutoka nje badala ya zinazotengenezwa na viwanda vya hapa nchini hata kama zina ubora wa juu ikilinganishwa na bidhaa za aina hiyo toka nje. Vile vile, kutokana na wananchi wengi kuwa na kipato kidogo, uwezo wao wa kununua bidhaa za viwandani ni mdogo. Changamoto nyingine ni kushindwa kufikia viwango vya ubora wa bidhaa na mbinu za utafutaji masoko ya bidhaa ili kuweza kushindana vema katika soko la Kimataifa na la ndani.

Vile vile, kuna upungufu wa wataalamu hasa katika fani maalum, kwa mfano wataalam wa nguo *(textiles technologists)* na ngozi *(leather technologists)*. Tanzania haina vyuo vinavyotoa wataalamu wa fani hizo, hivyo viwanda vingi vinategemea wataalam kutoka nje. Changamoto nyingine ni ukosefu wa nishati nafuu na ya kuaminika. Ili kufikia malengo hayo na kukabili changamoto husika, kazi zifuatazo zimepangwa kutekelezwa katika kipindi cha mwaka 2006/2007: -

(a)Kuandaa taarifa kuhusu fursa za uwekezaji katika miradi ya maendeleo ya viwanda *(project profiles);*

(b)Kuendelea kutekeleza mkakati wa kuimarisha sekta ya ngozi na viwanda vya ngozi;

(c)Kuwezesha na kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vya kusindika mazao ya kilimo, mifugo, maliasili na viwanda vya msingi;

(d)Kutekeleza mkakati wa kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji na kufuatilia utekelezaji wa tamko la serikali la kupiga marufuku utengenezaji wa mifuko laini ya plastiki;

(e)Kuweka utaratibu wa kudumu wa upatikanaji wa biashara ya chuma chakavu;

(f)Kuimarisha taasisi za utafiti na maendeleo ya viwanda hususan, *CAMARTEC, TEMDO, TIRDO*;na

(g)Kushirikiana na Sekta Binafsi katika kubuni mikakati ya kuendeleza sekta ya viwanda kwa lengo la kukuza mchango wa sekta hiyo katika maendeleo ya uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii itaendelea kushirikiana na Wizara na Taasisi nyingine pamoja na Sekta Binafsi katika kubainisha na kutafuta ufumbuzi wa matatizo mbalimbali ikiwa ni pamoja na matatizo ya upatikanaji wa mikopo ya muda mrefu kwa wawekezaji. Aidha, Serikali itaendelea kuvutia na kuhamasisha wawekezaji wa nje na wa ndani kwa kubainisha fursa za uwekezaji katika sekta mbalimbali za viwanda na fursa za mitaji. Pia, Wizara itaendelea kuhamasisha wananchi kwa kufanya kampeni ya *Nunua Bidhaa za Tanzania Jenga Tanzania*. Aidha, wawekezaji watahamasishwa kuwekeza katika teknolojia mpya za kisasa ili kuzalisha bidhaa bora zinazoweza kuhimili ushindani. Vile vile, Serikali itaendelea na juhudi za kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi na nchi nyingine za kiafrika kupitia *EAC* na *SADC* ili kufungua masoko ya bidhaa za Tanzania katika nchi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Biashara: Katika mwaka 2006/07, Sekta ya Biashara inaandaa mikakati itakayouwezesha uchumi wa Taifa kuhimili ushindani na kuweza kushiriki kikamilifu na kufaidika na mfumo wa biashara katika mazingira ya utandawazi kama ilivyoelekezwa kwenye Ilani ya Uchaguzi. Vile vile, Wizara itaendelea na utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Biashara, katika kutekeleza malengo ya MKUKUTA. Aidha, masuala muhimu ni pamoja na kukuza na kuendeleza biashara na nchi mbalimbali, kuendeleza ushirikiano wa kibiashara na nchi za Mashariki ya Mbali na Mashariki ya Kati kwa lengo la kupanua wigo wa masoko badala ya kuendelea kutegemea masoko asilia ya nchi za Ulaya Magharibi. Pia, Wizara yangu itatoa elimu kwa wananchi juu ya kanuni za masoko na biashara nchi za nje hususan Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika *(SADC)*, Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki *(EAC Customs Union)* na nchi nyingine ambazo zinatoa upendeleo kwa bidhaa zinazozalishwa katika nchi zinazoendelea kwa lengo la kupanua soko la bidhaa zetu na kuvutia wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza biashara, changamoto zinazoikabili sekta ya biashara ni uwezo mdogo wa uzalishaji wa bidhaa kukidhi mahitaji ya soko, kupanua wigo wa bidhaa tunazozalisha, kuhakikisha Tanzania inafaidika na fursa zinazotokana na majadiliano ya *EPAs* pamoja na fursa za masoko kikanda. Vile vile, kujenga na kudumisha mshikamano kati ya nchi maskini na zinazoendelea kushikilia msimamo wa kupinga vitendo vinavyosababisha biashara isiyo ya usawa na haki. Changamoto nyingine ni kujenga na kudumisha mshikamano na nchi zilizoendelea kiviwanda ili zisaidie katika mchakato wa kutatua matatizo ya uzalishaji wa bidhaa na huduma zinazohimili ushindani wa soko. Kwa ujumla changamoto katika Sekta ya Biashara ni kuboresha urari kati ya mauzo na manunuzi nje nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuitangaza Tanzania nchi za nje, Kituo cha Biashara cha Tanzania kilichopo London kitaendelea kushirikiana na Makampuni Binafsi, Mashirika na Mamlaka mbalimbali ili kuongeza ufanisi wa mauzo ya bidhaa na mazao ya asili kwa lengo la kuliongezea Taifa mapato ya fedha za kigeni. Kituo cha

Biashara kitaendeleza mkakati wa kuitangaza Tanzania kiutalii katika vyombo vya habari nchini Uingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2006/2007, *BET* itaboresha Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam ambayo sasa yanatambulika na Chama Kinachosimamia Maonesho Duniani *(Union des Foires Internationale (UFI)*. Lengo ni kuendeleza viwanja vya maonesho vya Mwalimu J.K.Nyerere kufikia kiwango cha ubora wa Kimataifa.

Vile vile, *BET* itaendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali wapatao 100, kuhusu ubora wa bidhaa, utaalamu wa kuuza nje kwa ujumla na jinsi ya kuzitumia fursa za upendeleo zinazopatikana katika masoko kadhaa. Aidha, Wizara itaendeleza kampeni ya *"Nunua Bidhaa Za Tanzania Jenga Tanzania"*. Vile vile, nachukua fursa hii kuzipongeza Wizara zilizoshiriki kwenye Maonesho ya 30 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam na hasa Wizara ya Fedha na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ambazo zimeshiriki kwa mara ya kwanza. Natoa mwito kwa Wizara nyingine nazo kushiriki kwani hii ni fursa nzuri ya kuwaonyesha na kueleza umma wa Watanzania kuhusu fursa mbali mbali za shughuli za serikali kwa maendeleo ya wananchi. *BET* pia, itaendelea kufikisha huduma za kutoa habari za biashara kupitia *Tele-Centres* katika Mikoa ya Morogoro na Mbeya. Kwa upande wa Zanzibar *BET* itaimarisha na kuongeza wafanyakazi na vitendea kazi. Aidha, Serikali inakusudia kuiunda upya *BET* kuwa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (*Tanzania Trade Development Authority)* yenye jukumu la kuendeleza biashara na wafanyabiashara. Hatua hiyo inalenga kuiwezesha Mamlaka hiyo kusimamia maendeleo ya biashara vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Biashara katika kipindi cha mwaka 2006/07 itaendelea kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya Biashara

(b) Kuainisha na kuandaa mkakati wa utekelezaji wa fursa zitokanazo na makubaliano ya *WTO*

(c) Kuimarisha Mamlaka ya *EPZ* pamoja na *BET* ili kuongeza juhudi za kuongeza mauzo ya nje

(d) Kuendelea kufanya mashauriano na wadau kuhusu programu ya kuainisha matatizo yanayokwamisha biashara *(Diagnostic Trade Integration Study - DTIS)*

(e) Wizara kwa kushirikiana na *DANIDA* itafadhili watumishi 26 wa Wizara, Idara za Serikali, Sekta Binafsi na Asasi zingine kuchukua mafunzo ya Shahada ya Uzamili ya Biashara ya Kimataifa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

(f) Kuendeleza shughuli za vituo vya kupokelea na kutolea taarifa mbalimbali zilizoanzishwa na mpango wa pamoja *(UNCTAD/WTO/ITC)* wa kujenga uwezo wa kitaalamu katika muasuala ya biashara

(g) Kuendelea na majadiliano ya *EPAs* baina ya nchi zinazoendelea na Jumuiya ya Ulaya

(h) Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini ikiwa ni pamoja na kukamilisha utaratibu wa uandikishaji wa biashara badala ya utaratibu wa utoaji wa leseni

(i) Kuendeleza mkakati wa kurasimisha biashara

(j) Kamati ya Kitaifa ya kusimamia utekelezaji wa mpango wa *AGOA* itaimarishwa kwa madhumuni ya kutoa ushauri katika masuala ya utekelezaji na uenezaji wa taarifa za masoko kwa Sekta Binafsi ili waweze kuuza zaidi kupitia mpango wa *AGOA*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mkutano wa Mawaziri wa biashara wa nchi wanachama wa Shirika la Biashara Duniani uliofanyika Hong Kong, China mwezi Desemba 2005, ilitarajiwa kuwa majadiliano ya Doha yangekamilika ifikapo Desemba 2006. Hata hivyo, kutokana na kuahirishwa kwa majadiliano kuna uwezekano kwamba yanaweza yasikamilike kama ilivyotarajiwa. Wizara yangu, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inaratibu zoezi la kuainisha jinsi gani wote kwa pamoja tutatekeleza kwa manufaa ya Taifa makubaliano yatakayofikiwa. Tanzania itanufaika na kufanya biashara na nchi wanachama na kuendelea kupata misaada ya kiufundi na kisheria pale itakapohusika katika mgogoro wa kibiashara unaohitaji kutatuliwa katika bodi ya usuluhishi ya *WTO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Masoko: Malengo ya Sekta ya Maendeleo ya Masoko ya mazao na bidhaa za kilimo kwa mwaka 2006/2007 ni kuendelea na jitihada za kuwezesha mazao ya wakulima kuuzwa kwa bei ya kuridhisha kulingana na mahitaji ya ubora wa soko la ndani na nje. Vile vile, mwelekeo wa sekta ya masoko ya mazao ya kilimo ni kuendeleza usindikaji wa mazao yanayozalishwa hapa nchini ili kuongeza thamani na nafasi za ajira. Pia, kuhakikisha upatikanaji wa masoko kwa bidhaa zisizokuwa za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zinazoendelea kukabili masoko ya mazao na bidhaa za kilimo nchini ni pamoja na kuporomoka mara kwa mara kwa bei za mazao katika masoko ya Kimataifa; miundombinu duni ya masoko ya mazao; uzalishaji mdogo usiokidhi wingi na viwango vya ubora unaohitajika katika masoko ya Kimataifa; kuongezeka kwa ushindani wa Kimataifa usiokuwa wa haki; kuongezeka kwa matumizi ya mazao na bidhaa mbadala; na kuwepo kwa magonjwa ya mifugo na mimea yanayoathiri Biashara ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanikisha upatikanaji wa masoko ya uhakika, Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo katika kipindi cha mwaka 2006/2007:-

(a)Kukamilisha Sera na Mkakati wa Masoko ya Mazao ya Kilimo nchini

(b)Kuimarisha na kuendeleza mfumo wa ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa za masoko

(c) Kuwezesha mchakato wa ujenzi wa masoko ya Kimataifa ya mazao ya kilimo na bidhaa zake.

(d) Kufanya tathmini ya uboreshaji wa miundombinu ya masoko.

(e) Kukamilisha Kitabu cha Orodha ya Wanunuzi na wasindikaji wa mazao

(f)Kuelimisha wadau kuhusu maendeleo ya masoko ya mazao na bidhaa ndani ya nchi na katika Jumuiya za Ushirikiano wa Kibiashara *(EAC, SADC, EU)* na nchi nyingine

(g)Kuimarisha uwezo wa Halmashauri na Manispaa kukusanya na kusambaza taarifa za masoko

(h) Kuratibu na kusimamia Programu ya Kuendeleza Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilimo kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu na wadau wengine

(i) Kuendelea kutekeleza Mradi wa Kuendeleza na Kuboresha Biashara ya Pamba na Kahawa hususan utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani; na

(j) Kuendeleza soko la ndani kwa kukuza matumizi ya mazao na bidhaa mbali mbali zinazozalishwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo: Katika kutekeleza Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo kwa mwaka 2006/2007, msukumo utawekwa katika kuhamasisha uanzishaji na uimarishaji wa viwanda vidogo na biashara ndogo. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha utoaji wa huduma zinazolenga kuchochea uanzishaji na uimarishaji wa viwanda vidogo na biashara ndogo. Huduma hizi zitatolewa katika nyanja za ufundi, mafunzo, ushauri, masoko, habari na mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati mbalimbali italenga kutoa huduma kwa wajasiriamali wadogo hususan wanawake na vijana kwa lengo la kuongeza nafasi za ajira na kipato. Msukumo wa huduma za ufundi katika mwaka 2006/2007 utalenga kujenga uwezo wa wajasiriamali kuzalisha kwa tija kwa kutafuta na kusambaza teknolojia zilizotengenezwa na kujaribiwa na taasisi mbalimbali za hapa nchini. Aidha, *SIDO* itawawezesha wajasiriamali kuanzisha miradi ya usindikaji wa vyakula na kutoa huduma za ushauri wa kiufundi. Kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa, *SIDO* itatafuta maeneo na kuratibu ujenzi wa miundombinu na majengo kwa matumizi ya wajasiriamali wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itahamasisha zaidi huduma zitakazoweka msisitizo katika kusaidia maendeleo ya shughuli za uzalishaji na biashara vijijini hasa kujenga na kuimarisha uwezo wa wahunzi na makundi mengine. Aidha, huduma za kiatamizi

zitaendelea kutolewa pamoja na huduma kwa wachimbaji wadogo wa madini katika maeneo mbalimbali ya nchi. Uzalishaji wa bidhaa za ngozi utahamasishwa kwa kutoa mafunzo na huduma kwa wazalishaji. Wizara yangu kupitia *SIDO* itaendesha kozi za ujasiriamali na uongozi wa biashara na kutoa mafunzo kwa wasindikaji wa vyakula na matunda. Pia, *SIDO* itatumia mbinu ya kuwaendeleza wazalishaji wadogo kwa kuwatumia wazalishaji na wafanyabiashara waliofanikiwa *(mentorship program)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kupitia *SIDO* itaendelea kuilea mifuko ya mitaji iliyopo na kuhakikisha kuwa mitaji inatolewa na kutumika kwa ufanisi. Aidha, *SIDO* itaendelea kutoa mitaji kwa wajasiriamali wadogo na kutafuta vyanzo mbalimbali vya fedha kwa ajili ya mitaji ya wajasiriamali. Wizara itaendelea na juhudi zake za kuwawezesha wajasiriamali kushiriki katika masoko ya ndani na nje ya nchi na pia kongamano la Kitaifa litakalowakutanisha wadau mbali mbali wa sekta litaandaliwa. Madhumuni ya Kongamano hilo ni kuzungumzia maendeleo ya sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo, hii ikiwa ni pamoja na fursa zilizopo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utafiti na Maendeleo: Katika kipindi cha mwaka 2006/2007, taasisi za utafiti yaani *CAMARTEC*, *TEMDO* na *TIRDO*, zinalenga katika kubuni teknolojia zitakazokwamua matatizo yanayokabili sekta ya kilimo na viwanda hususan, viwanda vidogo na vya kati ambavyo havina uwezo wa kufanya utafiti vyenyewe. Hii ni pamoja na kuongeza uwezo wa taasisi hizi kwa kufundisha wataalamu wake. Lengo ni kuboresha na kuinua maendeleo ya sekta hizi muhimu. Taasisi hizi zinalenga katika kutangaza teknolojia zilizobuniwa na kuzitengeneza ili ziweze kufahamika na wengi na kupata wajasiriamali watakaozitengeneza na kuzisambaza kwa wananchi. Matumizi katika shughuli zao hususan, kilimo vijijini na kuanzisha viwanda vidogo huko vijijini vya kusindika mazao yanayozalishwa. Aidha, eneo lingine jipya litakaloshughulikiwa katika utafiti wa mashirika haya ni teknolojia ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuzitengea Taasisi hizi fedha za bajeti kupitia MKUKUTA na kutafuta wafadhili kwa lengo la kuziwezesha kuendelea na shughuli zao. Taasisi zenyewe zitaongeza nguvu katika kutangaza teknolojia walizobuni na kutengeneza ili kupata soko na kujipatia fedha. Aidha, zitazingatia kubuni teknolojia kulingana na mahitaji ya soko *(demand driven)* badala ya kuzitengeneza ndipo watafute soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usimamiaji wa Sheria za Udhibiti: Ubora: katika mwaka 2006/2007, *TBS* inalenga kukamilisha ununuzi wa vifaa muhimu vya Kituo cha Ufungashaji ili kuongeza ubora wa ufungashaji wa bidhaa zinazozalishwa hapa nchini na kuhakiki vifungashio kwa bidhaa zinazotoka nje ya nchi. Pia, *TBS* inatarajia kuanza utekelezaji wa kiwango cha mita za teksi na kukamilisha ujenzi wa maabara ya kemikali. Shirika la Viwango Tanzania litaendelea na hatua za kuthibitisha maabara za shirika na mifumo ya utendaji wa Shirika la Viwango la Kimataifa *(ISO certification)* pamoja na kuhakikisha kuwa maabara zake zinaboreshwa ili kuweza kutoa huduma nzuri zaidi kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushindani wa HakiTume ya Ushindani, baada ya zoezi la uteuzi wa wataalamu, katika kipindi cha mwaka 2006/2007, itaendelea kutoa mafunzo

kwa wataalam wake, kuelimisha umma na utekelezaji wa Sheria ya Ushindani ya mwaka 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vipimo Katika mwaka 2006/2007, Wakala wa Vipimo unategemea kutekeleza majukumu yake yakiwemo: -

(a) Kuhakiki vipimo vinavyotumika kwenye biashara

(b) Kutangaza majukumu ya Wakala ili wadau waweze kuelewa huduma zinazotolewa

(c) Kushirikiana na taasisi nyingine, hususan Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kuhakikisha wauzaji wa mazao ya kilimo wanatumia vipimo sahihi na

(d) Kuhakikisha mianya yote ya wizi na udanganyifu wa kutumia vipimo visivyokuwa sahihi na rasmi katika biashara inazibwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usajili: Katika mwaka 2006/2007, *BRELA* itatekeleza yafuatayo:- (a) Kuanza kutekeleza mpango wa awamu ya tatu wa mwaka 2006/2007-2008/2009. Katika kutekeleza mpango huu mambo ambayo yatazingatiwa ni kuboresha na kusimamia sheria, kuelimisha na kuhamasisha wadau wake kwa kutangaza huduma zake kupitia radio na luninga, kujenga uwezo wa ndani, kujenga na kutumia mbinu za kisasa za utekelezaji na kupanua wigo ili kupeleka huduma karibu na wananchi

(b) Kuboresha na kuzingatia mkataba wa huduma kwa wateja;

(c) Kupunguza kero za wadau kwa kuanzisha mtandao wa kuratibu matatizo yanayojitokeza wakati wa kuwahudumia ;na

(d) Kuendelea kujijengea uwezo wa utendaji kazi na ufanisi wa utekelezaji kwa msaada wa MKUMBITA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hakimiliki Katika kipindi cha mwaka 2006/2007 *COSOTA* itaendelea na kazi zake kama ifuatavyo:-

(a) Kukusanya mirabaha kupitia kwa wakala katika kila mkoa wa Tanzania na kuweza kuwagawia wasanii husika

(b)Kuendesha semina na elimu kwa umma katika mikoa kwa njia ya vyombo vya habari na

(c) Kuingia mikataba na Vyama vya Hakimiliki vya nchi mbalimbali vya kulinda Hakimiliki kwa lengo la kukusanya mirabaha kwa niaba ya *COSOTA* pale ambapo kazi za wasanii na watunzi wa Tanzania zimetumiwa nchini kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uendeshaji wa Wizara na Taasisi zilizo Chini yake Wizara yangu inaweka msisitizo katika kuzingatia misingi ya utawala bora na uwajibikaji. Wizara imeunda Kamati ya Uadilifu kufuatilia ukiukwaji wa maadili sehemu

za kazi. Aidha, Kamati ya Ukaguzi wa matumizi na mapato ya Serikali imeundwa ili kuhakikisha matumizi bora ya fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vita Dhidi ya Rushwa Katika juhudi za kupambana na rushwa, Wizara yangu imeendesha warsha nne za utawala bora na huduma kwa mteja kwa watumishi wake na watumishi wa wakala wa vipimo. Aidha, juhudi hizo zitaendelezwa katika mwaka wa fedha wa 2006/07 ikiwa ni mwendelezo wa utekelezaji wa Mkakati wa Wizara wa Vita dhidi ya Rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapambano Dhidi ya UKIMWI Wizara yangu iliendelea kutekeleza mpango mkakati wa kudhibiti UKIMWI sehemu za kazi, ikiwa ni pamoja na kuandaa vipeperushi na kuendesha semina sita juu ya mbinu za kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huu kwa watumishi wa Wizara na Taasisi zake. Vile vile, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI *(TACAIDS)* itaendeleza juhudi hizo kwa lengo la kupambana na kupunguza athari zitokanazo na ugonjwa huu hatari. Wizara itapitia na kuboresha Mkakati wake wa kupambana na UKIMWI, ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya hali halisi ya maambukizi kwa watumishi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Masuala ya Jinsia Katika mwaka wa fedha 2005/06, Wizara yangu ilianzisha Dawati la Jinsia na Kuunda Kamati ya Jinsia ya Wizara. Aidha, Wizara imeandaa mkakati wa kushughulikia masuala ya jinsia ambayo yanapaswa kuingizwa kwenye Sera, mipango, programu na katika utendaji wa kila siku.

Pia, Kamati za Jinsia zilianzishwa kwenye Mashirika, Taasisi na Wakala chini ya Wizara yangu, ili ziweze kuzingatia masuala ya jinsia katika utekelezaji wa majukumu yao. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu imepanga kuendesha semina za uhamasishaji kuhusu masuala ya jinsia ili wafanyakazi waweze kuwa na uelewa wa jinsi ya kuyahusisha katika kazi zao za kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza azma ya Serikali ya kuwa na utendaji kazi bora katika Utumishi wa Umma, Wizara yangu imeajiri jumla ya watumishi 20 kwa mwaka 2005/2006. Aidha, Wizara imewapatia watumishi 35 mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi kwa nia ya kuinua viwango vyao vya utendaji kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makadirio ya Bajeti ya 2006/2007: Napenda kutumia nafasi hii kuzishukuru nchi rafiki na Mashirika ya Kimataifa ambayo yamekuwa yakitoa misaada iliyoiongezea Wizara uwezo wa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na tija zaidi.

Napenda kuzishukuru nchi za Austria, Canada, China, Denmark, Finland, Ireland, Uswisi, India, Japan, Marekani, Sweden, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na nchi nyingine ambazo zimeendelea kuisaidia Wizara. Aidha, napenda kuyashukuru Mashirika ya Sida, *UNIDO, DANIDA, DFID, GTZ, ILO, IFAD, NORAD, WTO, UNCTAD, OECD, USAID, UNDP, OPEC Fund, JICA, WIPO, ARIPO, SECO* na *ITC*. Nazishukuru pia Taasisi za Kimataifa za Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika na Shirika la

*Common Fund for Commodities (CFC* kwa misaada na michango yao ya fedha na utaalamu katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii ni matokeo ya kazi nzuri na ushirikiano wa karibu nilioupata kutoka kwa wenzangu katika Wizara, Mashirika, Wakala, Asasi na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko Mhe. Dr. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, Bwana Wilfred L. Nyachia, Katibu Mkuu, Bwana Godfrey Mkocha aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara, Mashirika, Wakala, Asasi na Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa michango yao katika kufanikisha kazi za Wizara na kwa kuhusika na maandalizi ya Bajeti ninayoiwasilisha leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazishukuru pia Jumuiya na Taasisi za Sekta Binafsi, ikiwemo *CTI, TCCIA na TPSF*. Aidha, nazishukuru Taasisi za elimu ya juu na utafiti, hasa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine, Chuo Kikuu Mzumbe na *ESRF* kwa michango yao ya mawazo wakati wa mikutano, warsha, semina na makongamano mbalimbali kuhusu Sekta za Viwanda, Biashara na Masoko.

Ushirikiano huu ni muhimu katika kuendeleza na kuimarisha Sekta za Viwanda, Biashara na Masoko kwa maendeleo ya Taifa letu. Natoa pia shukrani za dhati kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa huduma muhimu ya kuchapa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maombi ya Fedha: Maombi ya Fedha kwa Matumizi ya Kawaida ili kutekeleza malengo na majukumu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko:-

Katika kipindi cha mwaka 2006/2007 ninaomba Shilingi 15,654,086,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizi, kiasi cha Shilingi 6,120,846,000/= ni matumizi ya Wizara yenyewe na Shilingi 9,533,240,000/= ni ruzuku kwa ajili ya mishahara na shughuli za kuondoa umaskini zinazofanywa na mashirika ya umma yanayosimamiwa na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maombi ya Fedha kwa Matumizi ya Maendeleo: Katika mwaka wa 2006/2007, Wizara inaomba Shilingi 3,002,000,000/= kwa ajili ya shughuli za miradi ya maendeleo ya Viwanda, Biashara na Masoko.

Kati ya fedha hizi, Shilingi 326,000,000/= ni fedha za ndani ambazo zitatumika katika shughuli za maendeleo ya Taasisi zilizo chini ya Wizara na Shilingi 2,676,000,000.00 ni fedha za nje kutoka kwa wahisani ambazo zitatumika kulipia tafiti za kitaalamu na vifaa kwa miradi mbalimbali itakayotekelezwa na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba hii, nimeambatisha majedwali na vielelezo mbalimbali ambavyo kwa pamoja vinatoa takwimu zitakazowezesha Waheshimiwa Wabunge kutafakari vizuri zaidi maendeleo na utendaji katika sekta za Viwanda, Biashara na Masoko. Ninaomba takwimu hizi zichukuliwe kama sehemu ya vielelezo vya hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwisho, lakini siyo mwisho kwa umuhimu, namshukuru Mke wangu Natalie pamoja na watoto wetu Paulina, Pila na Emily ambaye yuko pale kwa mapenzi yao kwangu na kuendelea kuniunga mkono na kunipa moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI (K.N Y MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni Na.81(1) ya Kanuni za Bunge Toleo la Mwaka 2004, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa mara nyingine tena kwa niaba ya Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa juu ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa Mwaka 2005/2006 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kusema kwamba naiunga mkono hoja ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko. Aidha, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara ambao ndio waliochambua Bajeti ya Wizara hii, nao ni kama wafuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wajumbe wenyewe ni Mheshimiwa William H. Shellukindo, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati na Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wajumbe wengine wa Kamati ni Mheshimiwa Mohammed A. Chomboh, Mheshimiwa Yahya K. Issa, Mheshimiwa Asha M. Jecha, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Mwajuma H. Khamis, Mheshimiwa Vuai A. Khamis na Mheshimiwa Fuya G. Kimbita.

Wejumbe wengine ni Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Mohammed H. Mnyaa, Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro, Mheshimiwa Saverina S. Mwijage, Mheshimiwa Dr. Lucy S. Nkya, Mheshimiwa Christopher O. Ole–Sendeka, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Ahmed A. Salum, Mheshimiwa Haji J. Sereweji, Mheshimiwa Ahmed M. Shabiby, Mheshimiwa Mohammed S. Sinani na Mheshimiwa Abdallah S. Sumry. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Kamati inachambua Bajeti ya Wizara hii ilizingatia vipengele muhimu vifuatavyo kuhusu fungu 44.

(i) Dira ya Wizara kwa kulinganisha na Dira ya Taifa kuhusiana na Sekta ya Viwanda,Biashara na Masoko.

(ii)Majukumu ya Wizara.

(iii)Taarifa kuhusu utekelezaji wa malengo ya Mwaka 2005/2006.

(iv)Taarifa ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati wakati wa kuchambua bajeti ya Mwaka 2005/2006.

(v)Maelezo kuhusu Mapato na Matumizi ya Kawaida pamoja na fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2005/2006.

(vi) Maelezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa majukumu na ushauri uliotolewa na kamati wakati wa kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara mwaka 2005/2006: Kwanza naomba niishukuru Serikali kwa kukubali kuipatia Wizara hii Ofisi yenye hadhi kulingana na majukumu yake. Kuwepo kwenye Ofisi nzuri kutaonyesha umakini wetu katika kuvutia wawekezaji.

Ofisi hizo zilizopo katika jengo la *NSSF* la *WATERFRONT* ni nzuri na zenye hadhi kulingana na uzito wa Wizara hii. Aidha, napenda nilipongeze Shirika la kuendeleza Viwanda Vidogo *(SIDO)* lililo chini ya Wizara hii kwa kuweza kupata ushindi wa kwanza kama Banda bora kuliko yote kwa mwaka 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ushindi wa kwanza kwa Taasisi zinazojishughulisha na mambo ya kihandisi *(Engineering Products Category)* kwenye Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yaliyofanyika mwaka huu 2006 katika Uwanja wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Dar es salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baada ya maelezo hayo naomba sasa nitoe maoni kuhusu utekelezaji wa ushauri uliotolewa na Kamati hii kwa Wizara. Ushauri uliotolewa na Kamati umetekelezwa. Hata hivyo kuna mapungufu yafuatayo:

(i) Mheshimiwa Mwenyekiti, Nafasi ya Taasisi za Utafiti: sisi kama Taifa ni vizuri kwa mara nyingine tena tuelewe kuwa hakuna mfadhili yeyote atakayefadhili Taasisi zetu kwa lengo la kujinasua kutoka kwenye mfumo wa dunia wa kuagiza bidhaa kutoka mataifa yaliyoendelea, kwa vile kufanya hivyo kutakuwa na maana ya kujitia kitanzi kiuchumi. Taasisi zetu zikitumika kikamilifu kwa mujibu wa majukumu ya kuzianzisha zitaleta msingi thabiti wa maendeleo ya Taifa hili na hatimaye kujitosheleza kwa chakula, teknolojia na kadhalika.

Taasisi hizi zitaweza kutoa majibu mengi ya maswali ya wakulima, wafugaji na wavuvi wa nchi hii kwa kutengeneza zana zinazolingana na mazingira yake.

Kutokana na umuhimu wa Taasisi hizi, Kamati hairidhiki na kiwango cha ruzuku kinachotolewa ili kuendeleza shughuli za utafiti ikiwa ni pamoja na jinsi fedha hizo zinavyotolewa.

Kamati inaishauri Serikali kuongeza kiwango cha ruzuku kwa Taasisi hizi ili ziweze kutekeleza ama kutoa michango katika maendeleo ya Taifa letu.

(ii) Kanda za Mchakato wa Mauzo Nje *(Export Processing Zones 9EPZ)*: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeridhika na juhudi zinazochukuliwa na Serikali katika kuhakikisha kuwa maeneo ya *EPZ* yanafanikiwa. Hii ikiwa ni pamoja na kuleta Bungeni Sheria ya Kuunda Mamlaka ya kusimamia maeneo hayo. Hatua nyingine ni kubaini maeneo mbalimbali nchini, hali ambayo itatoa chachu ya maendeleo kwa maeneo husika. *(Makofi)*

Kamati inashauri kuwa pamoja na kujenga maeneo yake, Serikali iendelee kuweka mazingira mazuri ambayo yatawavutia wawekezaji binafsi kuwekeza katika kujenga maeneo kwa ajili ya shughuli za *EPZ*. Utaratibu huu umewezekana katika baadhi ya nchi duniani na umefanikiwa katika hali kama hiyo. Jukumu la Serikali liwe ni kuweka miundombinu mizuri katika maeneo hayo pamoja na kuyatangaza maeneo na vivutio vyake. *(Makofi)*

(iii) Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kujenga Masoko ya Kimataifa kwa mazao mbalimbali katika maeneo mbalimbali nchini. Utaratibu huu utawahamasisha wakulima kuongeza bidii katika kilimo kwa vile watakuwa na uhakika wa soko na bei inayojali gharama za uzalishaji.

Pia utaratibu huu utaondoa matatizo yaliyopo sasa ambapo mazao mengi hasa matunda yanaharibika kwa kukosa soko; na hata mazao mengine kuuzwa kwa bei ambayo hailingani na gharama za uzalishaji. Hata hivyo; ujenzi wa masoko haya mapya ya Makambako na Segera uepuke matatizo yanayolikumba soko la Kibaigwa. Utaratibu wa uendeshaji wa soko la Kibaigwa hauridhishi hali ambayo inawafanya wakulima wasiuze mahindi yao hapo na kuamua kutumia soko lingine lililo karibu na soko hilo. *(Makofi)*

Hapa tungependa kumpongeza Rais wa Jaamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya M.Kikwete kwa ushauri wake alioutoa alipotembelea soko hilo hivi karibuni ambapo aliwataka Wafanyabiashara kuzingatia usafi na afya za Walaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali iangalie maeneo mengine zaidi kwa lengo la masoko hayo kuwa karibu na wazalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shamba la Mpira Kihuhwi, Muheza, Kamati katika ziara zake imegundua kwamba mashamba ya mpira Kihuhwi, Muheza na Zanzibar hayaendelezwi kama inavyostahili kwani madhumuni hasa ilikuwa ni kwa ajili ya malighafi kwa ajili ya kiwanda cha *General Tyre.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu wawekezaji katika mashamba hayo hupeleka na kuuza nje malighafi wanayozalisha katika nchi jirani. Malighafi hizo hazipelekwi katika kiwanda cha *General Tyre.* Kamati inashauri kwamba mashamba hayo yatumike kama yalivyokusudiwa. Aidha, Kamati inashauri kwamba *General Tyre East Africa Ltd.* ikabidhiwe jukumu la kumtafuta mwekezaji *(Strategic investor)* wa mashamba husika yakiwa ni pamoja na mashamba ya Kihuhwi, Kilombero na Zanzibar ili yaendelezwe kwa kuwashirikisha wananchi katika maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeweka hisa nyingi katika kiwanda cha *General Tyre,* lakini uendeshaji wake unakwama kutokana na upungufu wa malighafi na mtaji mdogo. Kiwanda hiki kinaweza kuchangia kwa kiwango kikubwa kwenye uchumi wa nchi hii kama hatua madhubuti zitachukuliwa. Kwa mfano, mahitaji ya matairi aina zote hapa nchini ni karibu milioni moja. Kwa sasa Kiwanda cha *General Tyre* kinachangia kwa asilimia 20 tu. Iwapo *General Tyre* watapewa mahitaji yao yote muhimu, upo uwezekano mkubwa kwamba kiwanda hicho kingeweza kuchangia kwa zaidi ya asilimia 30 ya mahitaji yake na hivyo kupunguza gharama za uzalishaji kwa zaidi ya asilimia kumi. Faida ambayo ingepatikana kwa uchumi wetu ni kubwa sana ikiwemo mahitaji ya fedha za kigeni pamoja na ajira katika Sekta hii ya Mpira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na madai kuwa tairi za *General Tyre* zinauzwa kwa bei ya juu kuliko tairi zinazoagizwa kutoka nje ya nchi. Hiyo ni kweli kwa kiasi fulani na hii inatokana na kuingizwa kwa wingi kwa matairi yanayotoka nje kwa njia za magendo bila kulipiwa kodi zinazositahili, pamoja na kuwa nyingi ya tairi hizo hazina ubora madhubuti. Kamati inashauri yafuatayo: -

(i) Serikali ifikirie maombi ya kiwanda hiki ya kuongezewa mtaji.

(ii) Kuboresha upatikanaji wa malighafi toka mashamba ya mpira ya Kihuhwi, Zanzibar na Kilombero na udhibiti wa viwango vya ubora.

(iii) Kudhibiti uingizaji wa matairi kutoka nje ya nchi bila kulipiwa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imepokea toka kwa wafanyabiashara malalamiko mengi kuhusu urasimu mkubwa na usumbufu wa kupitisha na kutoa shehena za bidhaa katika bandari zetu, hususan Dar es Salaam. Ucheleweshaji huo unaleta hasara kubwa kwa wafanyabiashara kwani hulazimika kulipa ada kubwa ya ucheleweshaji usiokuwa wa lazima. Zaidi ya hayo, upotevu wa mali zao na wizi kwa baadhi ya bidhaa zao ni hasara nyingine wanazozipata.

Aidha, hali hii imewafanya wafanyabiashara wengi kuhamia katika bandari za nchi jirani na hivyo nchi yetu kupoteza mapato mengi. Kamati inashauri kwamba Serikali kupitia *SUMATRA* iharakishe utaratibu wa kupitisha, kutoa na hatimaye kulinda shehena kutoka katika bandari zetu za Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa soko unahitaji washiriki wengi katika bidhaa au huduma mbalimbali au bidhaa ya aina moja. Washiriki wamefanikiwa wakijionyesha kutokana na ubora wa bidhaa au huduma pamoja na bei. Hivyo basi, hali

hiyo haimuachi muuzaji au mzalishaji mmoja kutumia njia za kiutawala kuhodhi soko. Kila mzalishaji au muuzaji afanye shughuli zake kwa kuzingatia sheria za nchi na sheria za ushindani wa biashara wa halali *(Fair Competition Trade).*

Kamati ilitembelea Kiwanda cha Kuzalisha Sigara cha *Mastermind Tobacco* kilichopo Jijini Dar es Salaam mapema mwezi Juni, 2006. Uongozi wa Kiwanda ulieleza matatizo mengi unayokumbana nayo kutoka kwenye Taasisi za Serikali na washindani wake. Matatizo hayo yanaathiri shughuli za uzalishaji kiwandani hapo na kudhoofisha ushindani wa kibiashara. Kamati imekwishamuandikia Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko kuhusu tatizo la kiwanda hicho na Kamati inaamini kuwa suala hilo litashughulikwa. Ni matumaini ya Kamati kuwa tutapata matokeo ya uchunguzi unaofanywa na Tume ya Ushindani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hali hiyo, Kamati inashauri kuwa wafanyabiashara waelimishwe kuhusu kuwepo kwa Tume ya Ushindani ambayo kazi zake ni kusuluhisha wafanyabiashara. Vile vile, tunaishauri Serikali kuiwezesha Tume hiyo kwa kuipatia nyenzo za kazi zinazohitajika kwa ajili ya utendaji na ufanisi wa kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Wizara hii ni mengi na mtambuka ambayo yakitekelezwa kikamilifu yatatuondoa katika hali ya umaskini na kuweka mazingira mazuri katika viwanda, biashara na masoko mbalimbali ambazo zitatumia malighafi zinazopatikana hapa nchini. Pia kwa kupitia Taasisi zake, Wizara inafanya tafiti mbalimbali kuhusu viwanda, biashara na masoko pamoja na ubora wa bidhaa. Aidha, Wizara ina jukumu kubwa la kuboresha na kusimamia Sera ya Biashara ili Tanzania iweze kunufaika katika biashara ya ndani, ya Kikanda na ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza majukumu hayo, Wizara pamoja na Taasisi zake inaomba fedha chini ya Fungu 44 kama ifuatavyo, Matumizi ya Kawaida shilingi 15,654,086,000/= na Matumizi ya Maendeleo shilingi 3,002,000,000/=. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inakubaliana na maombi hayo ya fedha na inatarajia kuwa Wizara pamoja na Taasisi zake, itatekeleza kwa ufanisi malengo yaliyowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitia Makadirio na Matumizi ya Bajeti ya Wizara, Kamati ina maoni yafuatayo: -

Kuhusu viwanda vilivyobinafsishwa, ukiacha vile vilivyofilisiwa na kuwekwa chini ya *LART* vilitarajiwa baada ya kuuzwa, viendeleze shughuli zilizokuwa zinafanywa hapo awali. Lakini hali halisi kwa sasa ni kuwa viwanda hivyo vingi havijafanya kazi tangu vinunuliwe yapata zaidi ya miaka mitano na vingine vimeachwa tu wakati vingine vimebadili hata shughuli zake za msingi. Pia katika viwanda hivi, hatma ya waliokuwa wafanyakazi wa hapo imeachwa mikononi mwa wanunuzi. Kwa upande mwingine baadhi ya viwanda vinavyofanya kazi, maslahi ya wafanyakazi hayatiliwi maanani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiit, mafanikio makubwa ya uwekezaji yanaonekana kwa baadhi tu ya viwanda wakati viwanda vingine hakuna kinachofanyika. Kwa mfano, kiwanda cha *Mkata Saw Mill* kilichopo Wilayani Handeni ambacho kina takriban miaka kumi na nne hakijafanya kazi na Kiwanda cha Chuma cha Tanga nacho kimetelekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali iweke utaratibu wa kufuatilia utekelezaji wa masharti yaliyowekwa wakati wa kuuziana viwanda hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Madini ya Chuma Liganga na Mkaa wa Mawe Mchuchuma, suala hili lilikwishatolewa ushauri na Kamati ya Uwekezaji na Biashara wakati wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Hata hivyo, tunaipongeza Serikali kwa jitihada inazofanya kupitia Shirika lale la Maendeleo *(NDC)* ili kufanikisha miradi hiyo miwili. Miradi hiyo ina umuhimu mkubwa kwa Taifa hili. Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua thabiti na kwa uwazi ili kuendeleza miradi hiyo muhimu kwa haraka iwezekanavyo hasa katika kuzingatia ubora, umahiri na umakini wa mikataba itakayowezesha taarifa kunufaika zaidi na raslimali zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ya kazi katika baadhi ya viwanda si ya kuridhisha na viwanda hivyo vinakiuka misingi ya afya na usalama. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko pamoja na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo Vijana kuweka utaratibu wa kuvitembelea viwanda hivyo mara kwa mara ili kuona kuwa masharti ya usalama kazini yanafuatwa na kutekelezwa. Pia Serikali ipitie upya Sheria ya Kazi ili iendane na wakati huu wa uchumi wa soko huria ili kuweza kuweka na kulinda maslahi ya wafanyakazi na wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya faida inayoweza kupatikana kutokana na uwekezaji katika viwanda nchini ni matumizi ya malighafi zinazopatikana nchini kwenye mchakato wa uzalishaji pamoja na ajira inayoweza kupatikana, vyakula na huduma nyingine. Kwa sasa hapa nchini tunayo gesi asilia ambayo inaweza kutumika badala ya mafuta mazito *(Heavy Fuel Oils)*. Pia tunao mkaa wa mawe unaopatikana Kiwira na unaopatikana Mchuchuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini tusitumie mkaa wa mawe unaozalishwa hapa nchini kwenye viwanda vyetu badala ya kuagiza kutoka nje ya nchi kama kinavyofanya Kiwanda cha Saruji Tanga? Kwa sasa kumekuwa na mahitaji makubwa ya shayiri, mbegu za michikichi, alizeti na kadhalika. Malighafi hizi kwa sasa zinaagizwa toka nje ya nchi. Serikali ihimize upatikanaji wa malighafi hizo hapa nchini kule zinakoweza kustawi ili pamoja na kupeleka huduma za ugani tuweze kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matumizi ya gesi asilia dhidi ya bei za bidhaa, kati ya tarehe 17 Julai, 2006 na 18 Julai, 2006 Shirika la Taifa la Maendeleo ya Petroli lilionyesha baadhi ya viwanda vya Dar es Salaam kwamba vinatumia gesi katika mchakato wao wa uzalishaji. Pia ilielezwa kuwa bei ya gesi asilia ni asilimia 50 chini ya bei ya mafuta ya kawaida. Hata hivyo, bei hizo hazijaonyesha unafuu wowote. Viwanda vifuatavyo ambavyo viko katika Jiji la Dar es Salaam vinatumia gesi asilia kwenye mchakato huo wa uzalishaji, Kiwanda cha Saruji *(Wazo Hill),* Kiwanda cha Bia,

Ilala, Kiwanda cha Kioo, Kiwanda cha Mabati *(ALAF), Tanzania China Textile Mills (*Urafiki), *Karibu Textile Mills, Nida Textiles,* Kiwanda cha Sigara *(TCC),* Kiwanda cha Bora, *Lakhani Textiles, Murzah Oil Mills I, Murzah Oil Mills II* na *Murzah Oil Mills III.* Viwanda vingine pia vinaendelea kuunganishwa. Kamati inaishauri Serikali iangalie hali hiyo ili manufaa ya upatikanaji wa gesi na mapunguzo ya bei za uzalishaji katika viwanda hivyo viweze pia kuwanufaisha walaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapenda kuishukuru Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa kuikaribisha Kamati kutembelea Maonyesho ya 30 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam kuanzia tarehe 3 hadi 7 Julai, 2006 ambapo Wajumbe walipata nafasi ya kutembelea mabanda mbalimbali ya maonyesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ina maoni yafuatayo baada ya kutembelea uwanja huo: -

(i) Uwanja huo ndio lango la Biashara ya Kimataifa kwa vile mahali hapo wanakuja wafanyabiashara kutoka sehemu mbalimbali duniani, lakini kwa kweli uwanja hauko katika hadhi inayostahili. Barabara ndani ya uwanja bado haziridhishi. *(Makofi)*

Pamoja na jitihada ambazo zimefanywa kuboresha barabara hizo, Kamati inashauri kwamba tuendelee kuziboresha. Pia ndani ya uwanja huo hivi karibuni kulikuwa na harufu kali toka katika shimo la taka (dampo) lililoko karibu na uwanja huo. Ni vizuri hatua za makusudi zikachukuliwa ili kumaliza tatizo la harufu hiyo ambalo limekuwa likiwafedhehesha wananchi pamoja na wageni waliokuwa wakihudhuria maonyesho ya Sabasaba.

(ii)Waonyeshaji bidhaa wa hapa nchini, hususan wafanyabiashara wadogo, wenyewe huonyesha bidhaa za aina moja na kwa kiasi kidogo. Kamati inashauri kuwa wazalishaji hawa waelimishwe ili waweze kujiunga katika vikundi ambapo wataweza kuzalisha bidhaa husika kwa idadi kubwa ambapo itakuwa rahisi kupewa alama za ubora na *(TBS)* kuliko ilivyo hivi sasa ambapo walikuwepo wazalishaji wengi na wote wakiwa na bidhaa ya aina hiyo moja tu. *(Makofi)*

(iii) Uwanja huu wa maonyesho haujatumika kikamilifu ipasavyo ambapo matumizi makubwa huwa ni takriban siku kumi tu kwa mwaka wakati wa Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ili kuutumia vema zaidi kwa vipindi mbalimbali vya mwaka na ili kuongeza mauzo nje ya nchi kwa bidha za sekta mbalimbali, Kamati inashauri kwamba Serikali kwa kupitia Mamlaka ya Biashara ya Nje *(BET)* na kwa ushirikiano na Vyama vya Wafanyabiashara *(Tanzania Chamber of Commerce, Industries and Agriculture (TCCIA)* na *Confederation of Tanzania Industries)* na kadhalika, ili iweze kuandaa Maonyesho ya Kisekta na matukio mengine kama vile mikutano kati ya wanunuzi na wauzaji. Baadhi ya bidhaa ambazo *BET* inaweza kuzionyesha kwenye maonyesho kama haya ni kama vile mavazi, nguo na bidhaa za ngozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vya mipakani kwa upande wa Tanzania viko katika hali mbaya sana kwa maana ya kuwa havijaandaliwa kwa ajili ya biashara za mipakani. Hali hiyo inasikitisha kwa vile upande wa pili wa majirani zetu miji yao

inapendeza. Hali hiyo mbaya kwa upande wetu iko katika miji yote ya mipakani ya Sirari, Namanga, Horohoro, Holili, Tarakea, Tunduma, Kasumulo, Mtukula, Rusumo na kadhalika. Kamati inashauri kuwa Serikali ijenge mazingira ya kuwezesha kujengwa miji mizuri ya kibiashara katika maeneo ya mipakani na kuboresha miundombinu inayohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka ya 1970 tulikuwa na sera nzuri sana ya viwanda. Tulikuwa na Sera ya Viwanda Mama *(Basic Industry Strategy),* Viwanda vya Kati na kadhalika. Sera hii ilituelekeza namna ya kujinasua katika hali tuliyonayo sasa hadi kufikia katika nchi yenye viwanda, lakini hivi sasa hatuna kitu kama hicho. Kamati inashauri kuwa kuwepo na mpango mahsusi *utakaotuwezesha* kufikia malengo na uboreshaji wa viwanda hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ilikuwa mwanachama wa soko la *Common Market for Eastern and Southern Africa(COMESA)* ambalo linajumuisha nchi za Afrika Mashariki *(Eastern Africa)* na Kusini mwa Afrika *(Southern Africa).* Tangu Tanzania imejitoa katika soko hilo, hakuna nchi nyingine tena iliyojitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii ilipotembelea baadhi ya viwanda iliambiwa kuwa Tanzania inashindwa kufaidika na soko la Zambia na Malawi kwa baadhi ya bidhaa, hasa ya mafuta ya kupikia kwa sababu tu sio mwanachama wa *COMESA.* Kamati inaiomba Serikali ieleze faida au hasara ambazo tulikuwa tunapata wakati tukiwa wanachama wa soko hilo na sasa ambapo sisi sio wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu soko la *The African Growth and Opportunity Act (AGOA),* hili ni soko ambalo liko wazi kwa baadhi ya bidhaa hasa katika nchi za Kiafrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania haijashiriki kikamilifu katika utekelezaji au uuzaji wa bidhaa katika soko hili. Nchi kadhaa zimefaidika na soko hili. Tanzania kwa upande wake haijafaidika kwa kiwango kipasacho kutokana na soko hili. Kamati imebaini na kwa masikitiko kwamba bidhaa nyingi haziingizwi na wananchi wengi hawajapewa ufahamu katika utekelezaji wa bidhaa na kuweza kuziingiza katika soko hili. Kushindwa kunufaika kwa Tanzania na soko hili pia kulielezwa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, hivi karibuni alipokuwa anafungua rasmi Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa pale Dar es Salaam mwaka 2006 ambapo aliwaambia wafanyabiashara wachangamkie soko hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashauri wafanyabiashara wa Kitanzania wajielekeze katika soko hilo kwa kuzalisha bidhaa bora hasa kwa kuzingatia uwekaji kwenye makasha *(packaging),* uwekaji wa nembo *(labeling)* na ujazo, ili kuweza kushindana na bidhaa za aina hiyo zinazozalishwa na nchi nyingine. Tunashauri Vyama vya Wafanyabiashara vitoe elimu kwa wafanyabiashara na kuweza kuwaandaa waweze kushiriki vizuri katika soko hili ili kuweza kuifanya Tanzania inufaike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Sera ya Uchumi wa Soko kwa nchi yetu umekuwa wa kasi mno bila kuwa na tahadhari zinazostahili. Hivi sasa kwenye soko hilo ziko bidhaa za ajabu ambazo zinanunuliwa nje kwa fedha za kigeni. Baadhi ya bidhaa hizo ni zile tunazozalisha hapa nchini na kutokana na bei kuwa chini, bidhaa nyingi zinaingizwa tena nchini bila ya kulipiwa ushuru, pamoja na misamaha ya kodi kwa upande wetu.

Pia misamaha ya kodi inayotolewa kwa baadhi ya malighafi inafanya bidhaa zinazozalishwa hapa nchini zisinunuliwe. Sera hii itaua viwanda vyetu. Kwa mfano, kiwanda cha Tabora kinachozalisha nyuzi za pamba kinakosa soko, kwa vile baadhi ya viwanda vinavyoweza kutumia nyuzi kutengeneza vifaa hupata vibali vya kuagiza kutoka nje ya nchi na bila kulipia kodi. Inatubidi tuangalie namna ya kulinda viwanda vyetu na ajira kwa watu wetu kwa kuongeza ushuru wa bidhaa zitokazo nje ya nchi ambazo zinaweza kudhuru viwanda vyetu kama vile maji ya kunywa ya chupa.

Mheshimiwa Spika, hali hii inakwenda sambamba na hali iliyopo sasa ambapo wafanyabiashara wanapata vibali vya kusafirisha malighafi nje ya nchi na kusababisha viwanda vyetu kukosa malighafi. Kiwanda cha *Lion Wattle Company* cha mjini Lushoto ni mfano wa kiwanda kinachokosa malighafi. Kiwanda hicho kinakosa Miwati kwa vile Miwati hiyo inapelekwa nchi jirani.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yaliyokuwa yametengwa kwa ajili ya viwanda *(Industrial areas)* na hasa katika Jiji la Dar es Salaam yamekwishajaa na hivyo yanahitajika maeneo mengine mapya. Tunaishukuru Serikali kwa kutenga maeneo katika miji mbalimbali nchini. Hata hivyo, mengi ya maeneo ya viwanda yaliyotengwa hayana huduma muhimu kama vile barabara, maji na miundombinu mingine. Ni muhimu sasa kwa maeneo mapya yanayotengwa huduma muhimu zikawekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuhitimisha kwa kukushukuru kwa mara nyingine tena kunipatia fursa hii ambayo imeniwezesha kutoa maoni na ushauri kwa niaba ya Kamati yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Mheshimiwa Nazir Karamagi, Naibu Waziri; Mheshimiwa Dr. David Mathayo David, Katibu Mkuu wa Wizara, Ndugu Wilfred Nyachia na watumishi wote wa Wizara hiyo kwa kuandaa taarifa nzuri na bajeti nzuri kwa kipindi cha mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Katibu wa Bunge, Ndugu Damian Foka, ambaye aliiwezesha Kamati hii kufanya kazi zake vizuri sana.

Aidha, nawashukuru Ndugu Aggrey Nzowa na Ndugu Abdallah Hancha, ambao ni Makatibu wa Kamati, hii kwa kuihudumia Kamati kwa ufanisi na umakini mkubwa katika kipindi chote cha bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha na ninarudia tena kwamba ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Herbert Mntangi. Kabla sijamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, niwaandae wachangiaji watakaofuata baada ya hotuba hiyo. Wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Mohammed Habib Mnyaa, atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mheshimiwa Mohammed Chomboh, ajiandae, naye atafuatiwa na Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro katika mpangilio huo. *(Makofi)*

Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Lucy Owenya. *(Makofi)*

**MHE. LUCY F. OWENYA – MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba yangu na kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba nitoe shukrani kwa kupata fursa hii kutoa maoni yetu kuhusu hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa mwaka wa Fedha 2006/2007, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43(5)(b)(c) na 81(1) Toleo la mwaka 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda naomba hotuba hii inukuliwe kwenye *Hansard* kama ilivyo, hata nisipomaliza kuisoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani zangu za dhati kwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Naibu wake, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, kwa kuniteua kuwa Msemaji Mkuu wa Wizara hii. Aidha, nakishukuru chama changu cha CHADEMA kwa kuniteua kuwa Mbunge. Imani waliyonayo kwangu naahidi kuitunza na ninamwomba Mwenyezi Mungu anipe uwezo wa kutimiza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Nazir Karamagi, Waziri na Mheshimiwa Dr. David Mathayo, Naibu Waziri, pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa juhudi wanazozifanya za kuboresha sekta hii ya Viwanda na Biashara iwe na maana halisi katika uchumi wa Mtanzania na Taifa kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Aidha, napenda kumshukuru mume wangu mpenzi, Dr. Fidelis John Owenya, wanangu wapendwa Rachel na Yohanne Fidelis Owenya na dada yao Agnes anayewaangalia wakati nikiwa katika shughuli za Kibunge. *(Makofi)*

Mwisho kabisa, napenda kuwashukuru wazazi wangu kwa kunisomesha na kunitunza mpaka leo hii naweza kusimama hapa mbele yenu na kuwasilisha Kambi ya Upinzani hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtazamo kuhusu Wizara kwa ujumla ni kwamba Taasisi zilizo chini ya Wizara hii ni nyeti na muhimu sana kwa maendeleo ya nchi hii. Hata hivyo tunaona kuna mwingiliano dhaifu kati ya Wizara hii na Wizara ya Kilimo

ukiachilia mbali Taasisi moja tu inayojihusisha na kuangalia bei za mazao ya kilimo katika masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TIRDO, SIDO, CAMARTEC* na *NDC* ni Taasisi ambazo zina uwezo mkubwa kufanya tafiti katika Sekta ya Kilimo na kutoa suluhisho la kudumu la njia rahisi na nyepesi zitakazosaidia kumwongezea mkulima uwezo wa kuzalisha mazao kwa ubora unaokubalika. Mwingiliano wa Taasisi hizi uimarishwe ili uweze kutoa changamoto kwa wale wenye mitaji kuwekeza katika Sekta ya Kilimo na hatimaye kukuza biashara ya mazao ya kilimo. Taasisi hizi hazipewi fedha za kutosha kwa utafiti, wataalam na nyenzo za kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa mbolea katika uchumi wetu kwa ujumla, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutumia Taasisi nilizozitaja na nyingine kufanya utafiti wa kina ili kufufua kiwanda cha kutengeneza mbolea kwa kutegemea malighafi zinazopatikana hapa nchini kwetu, ili bidhaa hiyo ipatikane kwa bei nafuu. Aidha, tafiti hizo zijikite pia katika utengenezaji mbolea hai *(organic)* katika viwanda ili kukuza kilimo hai *(organic farming)* na hatimaye kukuza soko letu. *(Makofi)*

Aidha, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe ufafanuzi kuhusu uchimbaji wa gesi ya Songosongo na ujenzi wa kiwanda cha mbolea hapa nchini ambacho tunaamini kingekuwa kichocheo kikubwa kwa kilimo na kuokoa fedha nyingi zitumikazo kuagiza mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitia maombi ya fedha kama yalivyoainishwa katika Kamati ya Bunge na kwa kuangalia majukumu ya Wizara hiyo hasa vitengo vyake vya maendeleo, mambo yafuatayo yamejitokeza:-

Kwanza pamoja na kufanya kazi nyingine za uwekezaji yaani kutafuta wabia, bado *NDC* inafanya kazi ya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya tafiti zinazofanywa na *NDC* ni jinsi ya kupata mafuta ya kuendeshea mitambo kutokana na zao la Alizeti. Utafiti huu upewe kipaumbele ikiwa ni pamoja na kupanua wigo kwa kuhusisha mazao yote yenye asili ya mafuta kama vile, nazi, mawese, pamba, korosho, karanga, mbono, muhogo na kadhalika, kama ambavyo Waziri wa Fedha Kivuli alivyoshauri katika hotuba yake ya fedha mwaka uliopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya kushindwa kwa viwanda vyetu kuzalisha bidhaa kwa bei ya ushindani katika soko ni gharama za umeme. Hivyo, utafiti huu unaweza kuwa ni mkombozi kwa viwanda na vile vile kwa kilimo kwani wakulima watakuwa na uhakika wa soko la mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la *NDC* limekuwa ni mwakilishi mkuu wa Serikali katika miradi mbalimbali, ikiwemo ya madini na kadhalika. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itueleze ubia wa *NDC* katika mashirika mbalimbali na mafanikio au hasara iliyopata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi kubwa inayofanywa na *TBS* ukilinganisha na fedha kidogo walizotengewa, bado kuna tatizo la kiutendaji ambalo wazalishaji wa bidhaa wanaona kuwa *TBS* inawakwamisha. Kwa mfano, kiwanda cha *General Tyre* licha ya kuzalisha matairi yake ili *TBS* itoe taarifa ya ubora wake, lakini mpaka sasa taarifa hiyo bado haijatolewa. Wakati huo huo tairi za nje zinazodhaniwa kuwa na ubora wa chini zimejaa na kutapakaa katika masoko yetu. Ni lazima sasa Serikali itoe tamko rasmi ndani ya Bunge hili kwani hali hiyo siyo tu inahatarisha uhai wa Kampuni ya *General Tyre,* bali pia uhai wa maisha ya Watanzania ambao unahatarishwa kwa ajali za mara kwa mara ambazo moja ya sababu zinazotolewa ni ubovu wa matairi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kupata ufafanuzi wa Serikali ni kuhusu madai kwamba Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* limeteua mashirika binafsi nchini Dubai kukagua magari yanayonunuliwa na Watanzania kwenye soko la magari Dubai kwa dola za Kimarekani 150 sawa na fedha za Tanzania shilingi 187,500/= kwa *rate* ya shilingi 1,250/= kwa dola moja kwa kila gari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama madai hayo ni ya kweli, basi naomba maelezo ya kina taratibu za Serikali zilizotumika na sababu zilizofanya uongozi wa *TBS* uruhusu uamuzi huo wa kuwatoza Watanzania fedha nyingi kiasi hicho kwa kila gari wakati nchi nyingine za Afrika Mashariki wao hawatozi kodi hiyo na je, utaratibu huo unaingiliana vipi na ule wa kisheria wa *Pre-Shipment Inspection?* Je, kampuni hii inayowatoza kodi Watanzania yenyewe inalipa kodi au ni kuwanyonya Watanzania tu kwa faida ya wachache? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi kama ni kweli *TBS* wanalipwa na mawakala hao dola 10 ambazo ni sawa na shilingi za Kitanzania 12,500 tu kwa kila gari na kuna utaratibu gani wa kupokelewa kwa hizo fedha Serikalini na uhakiki wake ukoje? Mpaka sasa ni kiasi gani kimekusanywa tangu mawakala hao wateuliwe na *TBS? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na *TBS* kupiga marufuku uagizaji wa nguo za ndani zilizotumika, Serikali inatuambia nini, kwani nguo hizo ambazo zinamdhalalisha Mtanzania bado zinauzwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba tuko kwenye biashara huria, kila siku ipitayo biashara hii imekuwa holela na kuifanya nchi yetu kuwa jalala la bidhaa duni kama vipuli vya magari, vifaa/nyaya za umeme, dawa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uduni wa bidhaa hizi, nyingine ni *fake*. Je, sisi Tanzania hatuna *standard* ya bidhaa zinazoruhusiwa nchini? Iweje unakwenda kununua *spare* na kuanza kuulizwa unataka *genuine* au *non-genuine?* Serikali haioni bidhaa kama hizi zinaua viwanda vyetu vichanga na zinadhoofisha uchumi wa nchi hasa katika matumizi ya fedha za kigeni? Tunaomba tamko rasmi kuhusu msimamo wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *SIDO*, lengo kuu la kuanzishwa kwa *SIDO* lilikuwa ni kuwawezesha Watanzania wazawa kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali kupitia viwanda vidogo vidogo kwa kutumia teknolojia rahisi na kuzalisha bidhaa zenye ubora mijini na vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, inasikitika kuona kuwa kwa sasa *SIDO* imejikita zaidi katika utoaji mikopo midogo midogo ya biashara tu badala ya kujishughulisha na uanzishaji na uendelezaji wa viwanda vidogo vidogo. Hili limeanza kuwa ni tatizo sugu la kuchanganya mambo na kupoteza mwelekeo wa lengo/msingi la kuanzisha viwanda vidogo vidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgawanyo wa kazi ni muhimu sana katika ufanisi wa kazi na maendeleo ya nchi kwa ujumla. Bila hivyo ni vurugu tupu *(Jack of all Trade Master of None)*. Serikali inabidi idhibiti tatizo la mgawanyo na mwingiliano *(distribution and coordination*) wa kazi. Kazi ya mikopo inaweza kufanywa vizuri zaidi na vyombo vingine vya fedha na *SIDO* ibakie na kazi yake ya msingi na kama mikopo inatolewa basi iwe ile inayoendeleza kazi za kukuza viwanda vidogo vidogo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Viwanda Vidogo Vidogo *(SIDO)* limetengewa shilingi 26,000,000/= kwa ajili ya kugharamia shughuli za Maendeleo za Shirika hilo. Lakini bado Serikali haijaweka bayana mpango mahsusi wa kuwawezesha *SIDO* kuwasaidia wazawa ili waweze kushindana na wageni kibiashara ambao wanaingilia kwa kasi kubwa katika sekta ya biashara ndogo ndogo ya uchumi kwa Tanzania, kwa kiasi kikubwa wana uzoefu wa viwanda na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka *SIDO* ijikite zaidi katika ubunifu,uelimishaji na uendelezaji wa viwanda vidogo vidogo vitakavyomsaidia mwananchi kule kule anakozalishia bidhaa zake na iwaendee wadau vijijini sio kuendesha semina na warsha tu mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shirika La Utafiti na Maendeleo ya Viwanda *(TIRDO)*. Dunia ya sasa haina maendeleo au uwekezaji ambao unaweza kufanyika na ukawa wa maana bila ya kufanya utafiti wa kina wa kisayansi kwa kile ulichokusudia kukifanya. Wizara yetu hii ina bahati ya kuwa na Taasisi mbili tofauti ambazo zinajihusisha na tafiti japokuwa mielekeo ya tafiti zao inatofautiana. Vyombo hivyo ni *NDC* na *TIRDO*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 6260, *Support to Institutions* la shilingi 276,000,000/= kati ya hizo *TIRDO* imetengewa shilingi 10,000,000/= kwa ajili ya shughuli za maendeleo katika ujenzi wa misingi na shughuli za maendeleo na nguzo za karakana ya uhandisi ya Taasisi hiyo. Kambi ya Upinzani inadhani Serikali bado haijaona umuhimu wa Taasisi hii, teknolojia rahisi na inayoweza kutumika hapa nchini kulingana na hali halisi ya mazingira ya Mtanzania wa kawaida na kwa kutumia malighafi inayopatikana hapa kwetu ibuniwe na Taasisi hiyo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa fedha kidogo hizo zinazotolewa na Wizara kwa Taasisi inayojihusisha na tafiti ni kupoteza hela za wananchi. Kwa kawaida *Research and Development Budget* kwa nchi zilizoendelea na zile zinazotaka kweli kuendelea inachukua karibu asilimia zaidi ya sitini ya bajeti ya Wizara husika. Lakini hapa kwetu ni kinyume chake na hii inatufanya hata kwa miaka mingi ijayo bado tutaendelea kuwa nyuma kimaendeleo kulingana na mataifa yaliyotuzunguka kama vile Rwanda. Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri atueleze fedha hizi hasa zinakusudia kufanya utafiti gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *CBE,* kwa kuwa Serikali imeshapitisha sera ya kuboresha elimu ya juu na kutokana na umuhimu wa biashara katika nchi yetu, Kambi ya Upinzani inaona huu ni muda muafaka kwa Serikali kuangalia uwezekano wa kukifanya Chuo cha Biashara *(CBE)* kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Mzumbe au Chuo Kikuu Kishiriki cha Dar es Salaam. Mabadiliko haya yatawasaidia Watanzania katika uendeshaji wa biashara na kutoa mbinu bora zaidi za biashara na ujarisiliamali kwa wakati huu wa utandawazi na soko huria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa bajeti ya 2005/2006. Naipongeza Serikali kwa kazi nzuri ya kukamilisha jengo la *TBS* la Maabara ya Ufungashaji *(Packaging Technology Centre).* Japokuwa jengo hilo limemalizika, Kambi ya Upinzani ina wasiwasi kama kiwango cha shilingi 150,000,000/= kinachoombwa katika bajeti hii kwa ajili ya kununulia vifaa vya maabara hiyo kitatosha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kukumbusha mara kwa mara umuhimu wa kufungasha bidhaa kwa ubora, bado Taifa liko nyuma katika *packaging technique.* Kambi ya Upinzani inaona *packaging technique* ni sanaa ya aina ya pekee ambayo maabara ya *TBS* inahitaji kuiwekea msukumo wa dhati ili kuweza kukuza biashara yetu ndani na nje ya nchi. Kwa mfano, sisi tunashindwa kuuza kwa wingi mazao yetu nchi za nje pamoja na sababu nyingine, uduni wa *packaging technique* ukituathiri kwa kiwango kikubwa.

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanya juhudi zote kuhakikisha Maabara hii ya *TBS* inaikomboa nchi yetu na bidhaa zinafungwa kwa ubora wa Kimataifa ili kuwa washindani katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na taarifa ya utekelezaji ya Wizara bado Kambi ya Upinzani, inaona Wizara haijakuwa na vipaumbele kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu, Viwanda na Biashara kwa ujumla wake. Taarifa ya Wizara inasema kuwa Serikali imebainisha maeneo mbalimbali kwa ajili ya mpango wa *EPZ* na kutaja maeneo hayo katika mikoa mbalimbali na kumalizia kuwa kwa miaka mitano ijayo Serikali itajenga Miundombinu katika *EPZ* za mikoa minne.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa haionyeshi katika kila kituo ni bidhaa gani hasa zitakuwa zinapatikana maalum kwa ajili ya soko la nje. Taarifa ya mapema ingesaidia wale wanaohitaji kuanza maandalizi ya uwekezaji katika mikoa husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya malengo muhimu ya bajeti ya mwaka 2005/2006 ilikuwa ni kutekeleza MKUKUTA ambayo imegawanyika katika mafungu matatu makuu. Nijielekeza katika fungu la ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili azma ya kufanikisha ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa kipato ni vema sasa kuongeza kwa makusudi fedha za maendeleo katika bajeti hii kuliko ilivyo sasa kwani fedha za matumizi ya kawaida ni nyingi kuliko fedha za bajeti ya maendeleo hivyo ni vigumu kupiga vita umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha kwa mwaka 2006/2007, Wizara imeomba kiasi cha shilingi 15,654,085,000/= kwa mwaka wa fedha 2006/2007 kati ya hizo shilingi 9,533,240,000/= ni kwa ajili ya taasisi zilizo chini ya Wizara na shilingi 6,120,846,000 kwa ajili ya Idara zilizo katika Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uchache wa fedha hizo ukilinganisha na majukumu ya Wizara hiyo, matumizi yake yanaonyesha matatizo makubwa ya kiuwiano. Kwa mfano, 17% ya fungu la Wizara yaani shilingi 1,040,496,000/= itatumika kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara, karibu 51% ya fungu la taasisi zilizo chini ya Wizara yaani shilingi 4,894,990,000/= itatumika kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa taasisi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitaalam unapokuwa na gharama za mishahara zinazolingana na gharama za uendeshaji, maana yake ni kwamba Taasisi husika inapiga hatua bila kwenda mbele *(mark time)* watumishi waliopo wengi hawana shughuli za kufanya, baada ya kuzalisha wanatumia tu, kuna tatizo la *over employment* kwa maana hiyo, Serikali inatoa mishahara na posho bila ya kazi kufanyika. Tunaomba ufafanuzi wa kina kwa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi zetu zinahitaji Watanzania watalaam *(Professionals)* na ambao wataweza kukidhi mahitaji (ku-*deliver)* katika taasisi husika na sio wingi wa wafanyakazi kwani tunaamini taasisi za taaluma kama hizi zinahitaji wanataaluma yaani *well educated and highy motivated staff* na matokeo yake yatakuwa wazi kwa Watanzania wote.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeomba kiasi cha shilingi 755,870,000/= kwa ajili ya malipo ya kazi za ziada *(Extra duty & Honorarium).* Wizara pia imeomba kiasi cha shilingi 1,040,496,000/= kama mishahara ya watumishi wake. Sasa ukifanya hesabu utaona kwamba malipo ya kazi za ziada ni 73% ya malipo ya mishahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Wizara isilipe malipo ya ziada na kila mfanyakazi afanye kazi kwa saa nane tu kwa siku, inahitaji kwa wastani kuongeza idadi ya watumishi wake kwa 73%. Kwa kuwa hivi sasa malipo ya kazi za ziada yanafanyika basi ina maana kuwa kwa kiwango hiki cha malipo kwa wastani kila mfanyakazi wa Wizara kila siku ya kazi anafanya kazi ya ziada kwa wastani wa saa sita.*(Makofi)*

Kambi ya Upinzani inauliza kweli kama tunataka kwenda mbele hali hii inaweza kuwa daraja la kuvukia au ni kutufanya na sisi Waheshimiwa tunaopitisha fedha hizi hatujui wajibu wetu kwa Watanzania? Tunaitaka Serikali itoe ufafanuzi wa kina kuhusiana na haya matumizi na kuna uwezekano mkubwa Wizara zote ndio mtindo ni kama huu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoelezea hapo mwanzo matumizi hayaendani na hali halisi. Kwa mfano, Idara ya Sera na Mipango imeomba shilingi 240,000,000/= kwa ajili ya gharama za mafunzo. Kwa mujibu wa mchanganuo wa matumizi ya fedha hizi, shilingi 90,000,000/= zitanunulia vitabu kwa ajili ya wanafunzi wa vyuo vikuu waliofadhiliwa na moja ya miradi inayosimamiwa na Idara hiyo na shilingi 150,000,000/= kwa ajili ya kulipia karo zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wastani gharama za vitabu kwa wanafunzi wetu wanaosoma vyuo vikuu nchini ni shilingi 120,000/= kwa mwaka kwa mwanafunzi mmoja, kwa mujibu wa mchanganuo wa bodi ya mikopo. Hii ina maana shilingi 90,000,000/= zilizoombwa na Wizara kwa ajili ya kununulia vitabu kwa wanafunzi wanaosoma vyuo vikuu ni kwa ajili ya wanafunzi 750. *(Makofi)*

Kambi ya Upinzani inaitaka Wizara itoe maelezo ni wanafunzi wangapi hasa wamedhaminiwa na Wizara hii ili na sisi pamoja na wananchi turidhike katika haya matumizi isiwe ni kutengeneza mwanya wa matumizi mabovu ya fedha za wavuja jasho ambao wengi wao ni maskini wa kutupwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wastani gharama ya karo kwa wanafunzi wanaosoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni shilingi 1,800,000/= kwa mwaka kwa mwanafunzi mmoja. Hii ina maana shilingi 150,000,000/= zilizoombwa na Wizara kwa ajili ya karo za wanafunzi chuoni kwa ufadhili wake kupitia Idara yake ya Sera na Mipango ni kwa ajili ya wanafunzi 83 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo juu inaonyesha vitabu ni kwa ajili ya wanafunzi 750 kwa gharama za bodi ya mikopo na karo kwa gharama ya chuoni kwa wanafunzi hao 83 tu. Serikali inaeleza nini kuhusu tofauti hii ya kitakwimu?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni kweli waliopata ufadhili na kupata fedha za vitabu ni 83 tu, je, hao waliobaki 667 wanasoma kwa ufadhili wa nani? Na je, idara ina watumishi wangapi inaowasomesha na kwa kiwango gani *Certificate, Diploma, Degree?* Tunaomba maelezo ya kina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda vya ngozi, Tanzania katika Bara la Afrika ni nchi ya tatu kwa kuwa na idadi kubwa ya mifugo yaani ng'ombe, mbuzi na kondoo. Kama kumbukumbu zetu zitakuwa sawa, miaka ya 1970 na 1980, Tanzania ilikuwa na Shirika mama lililokuwa linaangalia jinsi viwanda vya ngozi vinavyofanya shughuli zake, shirika hilo lilijulikana kama *Tanzania Leather Industries (TLI).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya ngozi vyote na viwanda vya viatu vilikuwa chini ya shirika hili. Moja kati ya majukumu ya hilo shirika ilikuwa kuweka sera za ngozi na viwanda vinavyotumia malighafi za ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuuzwa kwa viwanda vyetu vya viatu, mfano *Moro Shoes* na *Bora Shoes* na kiwanda cha ngozi cha Moshi, baadhi ya kazi za msingi za viwanda hivyo zimebadilika, kwa mfano, Kiwanda cha Bora badala ya kutengeneza viatu vya ngozi kinatengeneza kandambili na kuagiza matairi ya baiskeli toka nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imesababisha soko la ngozi kutokueleweka na kuliletea hasara kubwa sana Taifa. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze viwanda ambavyo vinafanya shughuli tofauti na ile ya awali na ni hatua gani zimechukuliwa na ni viwanda vingapi vimekwisha chukuliwa hatua kwa kukiuka Mkataba wa kuviendeleza viwanda hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tunaitaka Wizara itueleze hatma ya viwanda vya ngozi vilivyokuwepo na nini hatma ya soko la ngozi kwa ujumla Wizara ina mpango gani wa kuhakikisha viwanda vyetu vya bidhaa za ngozi vinafanya kazi kulingana na mkataba wa kubinafsisha? Pia kama kumbukumbu zetu ziko sahihi, *Livestock Development Fund Act* ya mwaka 2003 ilianzisha mfuko wa kuboresha zao la ngozi ikiwa ni pamoja na kuendeleza viwanda vya ngozi. Je, Serikali inaweza kutuambia mpaka leo huo mfuko umekusanya shilingi ngapi na sekta ya viwanda vya ngozi imenufaikaje na mfuko huo? *(Makofi)*

Kuhusu *COMESA,* Tanzania ilijitoa katika soko la pamoja kwa nchi za Kusini mwa Afrika *(COMESA)* mwaka 2000. Inawezekana kabisa kuwa uamuzi huo ulikuwa muafaka kwa wakati huo.

Hata hivyo tafiti mbalimbali zilizofanywa na wataalamu wa biashara ya Kimataifa na umoja wa wafanyabiashara kama *Confederation of Tanzania Industries (CTI)* zinaonesha kuwa Tanzania inapata hasara kwa kuwa nje ya *COMESA*. Makampuni makubwa ya Tanzania yanatumia makampuni dada ya nje *(Sister Companies)* kuuza bidhaa zao katika soko la *COMESA,* hivyo kuikosesha nchi yetu pesa nyingi za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itueleze ni kiasi gani tumepoteza kupitia makampuni yenye matawi nchi jirani kwa kutokuwa mwanachama wa *COMESA?* Kuna taarifa kuwa Tanzania imeendelea kulipia michango ya kila mwaka kwa *COMESA* kwa kiwango cha Dola za Marekani 400,000 kwa mwaka, je, ukweli ni nini na ni kwa misingi ipi wakati Tanzania imeshajitoa *COMESA*? Ni vema Serikali itoe tamko la wazi katika eneo hili.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengine inatubidi tutathmini kwa kina na kuweka mbele maslahi ya Taifa kwa ujumla katika maamuzi yetu tukizingatia kwamba katika miaka ijayo ambayo si mbali sana dunia nzima kwa taratibu za *WTO* itakuwa soko la pamoja. Je, itakapokuwa katika mazingira hayo mfumo wetu wa

ushirikiano wa *East Africa*, *SADC* au hata *COMESA* utachukua sera gani na sisi tunajiandaa vipi kwa hali hiyo inayokuja kwa uhakika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu majadiliano ya *Economic Partnerships Agreements,* Tanzania ni moja ya nchi za kundi linaloitwa *Africa, Caribean and Pacific (ACP).* Tanzania inae Mbunge katika Bunge la pamoja la nchi hizi na Jumuiya ya Ulaya ambae ni Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi za Kenya na Uganda zinajadili *EPA* kupitia kundi la *Estern Southern African (ESA)* ambalo ni wanachama wa *COMESA*. Kitendo cha nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kujadili *Economic Partnerships Agreements (EPA)* katika makundi tofauti ni kitendo kitakachoua ushuru wa forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwani kitaalamu nchi moja haiwezi kuwa mwanachama wa ushuru wa forodha mbili tofauti. *EPA* inapelekea makundi ya nchi kuwa na ushuru wa forodha. Sisi kama nchi, tukijua kabisa madhara, tumeamua kujiweka katika ushuru wa forodha na Afrika ya Kusini badala ya ushuru wetu wa forodha na Kenya na Uganda.

Kwa vile kwa maelekezo ya *WTO* mwisho wa kujadili mpango wa sasa ni mwaka 2008, je, Tanzania inaweza kulieleza Bunge hili Tukufu, hatua ya makusudi kuhakikisha kuwa nchi yetu haitaathirika na kutokuwa na maamuzi ya uhakika na imara katika mambo makubwa kama haya ya *EPA?(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Miradi ya Mchuchuma na Liganga, Kambi ya Upinzani imepokea taarifa nyingi juu ya miradi ya Mchuchuma na Liganga lakini uzoefu umeonesha kuwa Serikali haitoi maamuzi ambayo hatimaye huliingiza Taifa katika hasara kubwa na bila ya walioamua vibaya kuchukuliwa hatua. Hivyo Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali izingatie mambo manne muhimu katika mchakato wa kuipata Kampuni ya kuchimba chuma cha Liganga na Mchuchuma :-

(a) Uwazi katika kuitisha na kuteua mwekezaji/wawekezaji;

(b) Uwezo wa kitaalam wa kuweza kuchimba na kuchenjua madini aina mbalimbali yatakayochimbwa;

(c) Uwezo kifedha; na

(d) Uzoefu katika kufanya shughuli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kufuata misingi hiyo, tutalipeleka suala hili kwa wananchi kwa nguvu zetu zote kwani Watanzania wamechoshwa kubebeshwa gharama za mikataba potofu kama *IPTL, SONGAS, KIA*, Meremeta, *Mwananchi Gold,* TVT na migodi mingine ya dhahabu na almasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maeneo yenye kuhitaji maelezo ya kina, kwa vile Wizara hii ndiyo inayohusika na kuandikisha au kusimamia wakala anayeandikisha

Makampuni yaani *BRELA,* Kambi ya Upinzani inapenda kupata taarifa ya kina kuhusu yafuatayo:-

(a) Kampuni ya *Tanzania Container Terminal*, Kampuni hii ndiyo iliyokodishiwa *Container Terminal* iliyoko Bandarini. Kuna malalamiko kuwa Kampuni hii imeongezewa muda wake wa mkataba kwa miaka mingine 15 bila kufuata utaratibu wa kisheria uliowekwa na *Public Procurement Act* yaani *tender* hazikutangazwa kwa utaratibu uliowazi. Mkataba huo sasa unasemekana umeongezwa hadi mwaka 2025 yaani kwa miaka 15 zaidi, kipindi hiki ni kirefu sana.

Kambi ya Upinzani inataka majibu ya kina na ya uhakika ni kwa nini mkataba huu unakodishaji umeongezwa bila *tender* kutangazwa na kufanywa kinyemela? Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuliarifu Bunge hili Tukufu kuwa wamiliki na wakurugenzi wa Kampuni hii ni kina nani hasa ili kuondoa minong'ono ya *conflict of interest* ambayo sasa inatembea wazi mitaani. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iwasilishe kwa Kamati ya Uwekezaji na Biashara hati za usajili wa Kampuni hii na hatimaye Bunge liarifiwe rasmi. *(Makofi)*

(b) Kambi ya Upinzani inazidi kuomba tena, kwa mara nyingine tena kuwa suala Kampuni ya Meremeta liwekwe wazi. Kampuni ya Meremeta ilianzishwa kama Kampuni ya Umma yenye kumilikiwa na Jeshi la Wananchi kama *Corporation Sole*. Kampuni hii sasa inasemekana imehamishwa na kuandikishwa kama Kampuni na Jeshi la Wananchi si wamiliki tena. Kambi ya Upinzani inahitaji kujua imeuzwa kwa nani, kiasi gani kauziwa, kwa utaratibu gani na mamlaka gani iliyotoa amri ya kuuzwa, kama imefilisika wadai ni kina nani na wanadai kiasi gani hadi kampuni kufilisika? Mfilisi alichaguliwa kwa utaratibu gani?

(c) Serikali kuwajibika kwa Wananchi kwa kupita Bunge ndio wajibu wa Kikatiba, wala kudai hili si kuingilia mamlaka ya Serikali ni Wajibu wetu na Watanzania wana haki ya kufahamu. Serikali imeeleza kuwa sasa wako kwenye hatua ya *winding up* ndani ya Bunge hili, hii ikiwa na maana ya kuwa taratibu zote za ufilisi zimekamilika ambazo ndiyo hatua yenye usiri ndio maana tunaendelea kudai taarifa hizo. Kama ndiyo hivyo, je, wadaiwa ni akina nani na wanadai kiasi gani hadi kampuni kufilisika na mfilisi alichaguliwa kwa taratibu gani? *(Makofi)*

(d) Hivi karibuni kumekuwa na malumbano kuhusu Kampuni ya *Mwananchi Gold Mines Ltd.* Kambi ya Upinzani imehoji ndani ya Bunge hili lakini Serikali imepata kigugumizi kujibu hoja zetu. Kwa mara nyingine tena na kwa Wizara ambayo ndio mhusika Mkuu wa usajili tunaitaka Serikali ieleze Kampuni ya Mwananchi mmiliki wake kila mmoja ana hisa kiasi gani na fedha za uwekezaji zimetoka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania baada ya kuingia katika soko huria biashara nyingi nazo zimekuwa holela kama nilivyoshaeleza huko nyuma. Hii ina maana kuwa wageni wameruhusiwa kununua viwanda vyetu na kufanya biashara ndani na nje kwa nembo ya Tanzania. *(Makofi)*

Moja ya matarajio makubwa ya kuwakaribisha wageni ni kuleta *Foreign Direct Investment (FDI)* nchini. Ni jambo la kusikitisha kuona kuwa wawekezaji wachache wameleta *FDI,* walio wengi wamekuja mikono mitupu na kuja kukopa fedha za ndani na wazawa kuambiwa kuwa hawakopesheki. Mapato yatokanayo na mauzo mengi ya bidhaa nchi za nje yanabaki huko huko nje, hayangii hata kwenye *foreign reserve* ya nchi hii na wala hayarudishwi kuja kuongeza uwekezaji nchini. Nchi hii sasa itabakiwa na uharibifu mkubwa wa mazingira mara wageni hawa watakapotosheka na faida watakayoivuna hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa njia hii kwanza wanachukua pesa zetu za ndani kwa kufanya biashara na faida kuwa yao bila Watanzania kunufaika na biashara hiyo na pili biashara wanayofanya nje kwa jina letu faida inaenda kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho tunaomba maelezo ya kina ni kwa nini utaratibu wa uteuzi wa Mkurugenzi wa *BET* ulikiukwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo naomba Watanzania wajenge nchi yao kwa kununua, kuvaa, kula bidhaa zinazotengenezwa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kuwasilisha, ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia na nikawa mchangiaji wa mwanzo. Naomba nichangie au nijikite katika masuala manne na la kwanza litakuwa ni suala la viwanda vilivyobinafsishwa. Lakini Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko tunaelewa kwamba ni Wizara nyeti, ni uti wa mgongo wa uchumi wa nchi hii na majukumu yake ni mazito. Kwa haraka haraka Wizara hii ina majukumu yasiyopungua 14 makubwa sana. Lakini ningependelea kwa sababu ya uchangiaji wa viwanda vilivyobinafsishwa tutazame jukumu gani kubwa la Wizara hii katika Viwanda hivi vilivyobinafsishwa.

Naomba ninukuu: "Jukumu kubwa la Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Masoko kuhusu viwanda vilivyobinafsishwa ni kufuatilia kwa karibu viwanda vilivyobinafisishwa na kuchukua hatua zinazofaa kurekebisha pale penye matatizo ili kuhakikisha kuwa vinaongeza mchango wao katika Pato la Taifa, pia kuendeleza juhudi za kufufua viwanda vya nguo, viwanda vya ngozi na bidhaa za ngozi, ili sekta hizi zichukue nafasi yake katika kuchangia ukuaji wa uchumi."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, tumegundua kwamba moja katika jukumu kubwa katika Wizara hii, ni kufuatilia kwa karibu mno viwanda vyote vilivyobinafsishwa ili kuona kwamba vinachangia Pato la Taifa. Tuchukue mfano sasa viwanda vingapi vilivyobinafsishwa na mpaka leo havifanyi kazi. Tuna viwanda vingi mno vilivyobinafsishwa na mpaka leo havifanyakazi na hakuna mchango wowote tunaoupata kwa Taifa zaidi ya matatizo mazito.

Tuchukue mfano wa kiwanda cha *Mkata Saw Mill*, kiwanda hiki kina miaka mingi sana na ripoti ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara imesema ni miaka kama 14 na mpaka leo hakijafanya chochote. Kiwanda hiki wakati huo kilikuwa na matrekta mengi sana mazima, magari mengi sana mazima, matrela ya kubebea magogo mazima, mashine mbalimbali za upasuaji na ukataji wa magogo, jenereta na vitu vingi vingi. La kushangaza hivi leo ukienda ukiviona vile vifaa vilivyozagaa pale na vimeshakufa vimechakaa na kiwanda hakijafanyakazi, tumbo litakuuma hata kama kiwanda kile sikununua mimi lakini tumbo liliniunguruma. *(Makofi)*

Mheshimiwa mwenyekiti, kinachositikisha au cha kujiuliza hapa hivi huyu aliyenunua hiki kiwanda halafu akaacha mali yote pale ikafa mpaka hivi leo miaka yote iliyopita, kweli alitoa hela mfukoni? Hivi ni kitu gani kilichosababisha vile na kama ni migogoro ya wafanyakazi, je, kwa muda wa miaka yote hiyo, bado migogoro hiyo haijaisha?

Sasa Watanzania tungependa waelewe na namwomba Mheshimiwa Waziri, atufafanulie huu ubinafsishaji wa namna hii ni kweli mtu yule aliyenunua kiwanda hiki hana uchungu wa mali yake, ni kweli alitoa hela mfukoni au huu ubinafsishaji wa *PSRC* wakati mwingine kuna makubaliano? Ni vyema leo tuelezwe kilibinafsisha kwa kiasi gani kiwanda hiki? *(Makofi)*

Mheshimiwa mwenyekiti, viko viwanda vingi vya namna hii. Kuna kiwanda cha *Steel Rolling Mill* cha Tanga, ni kiwanda kingine cha mfano wa namna hiyo hiyo na bahati nzuri hawa wawekezaji ni wajanja mno maana yake ukifika pale unavyokaribishwa na matumaini unayopewa ya kushangaza, tulipotembelea kiwanda kile kama mwanakamati wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara taarifa tuliyopewa na mwekezaji ni kwamba kiwanda kile kitakuwa tayari kinafanyakazi kuanzia tarehe Mosi Juni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Waziri akifika hapa atatueleza labda sasa hivi kiwanda hicho ni kweli kinafanyakazi? Isitoshe mwekezaji alizungumzia kwamba tayari ameshatumia dola laki nane katika matengenezo ya kiwanda hiki. Lakini ukiingia ndani unaona ni *furnace* (tanuru) tu iliyorekebishwa na vitu vingine zaidi ya kung'olewa vikaenda vikatumika katika viwanda vingine na ahadi nzuri unapewa na maneno mazuri matamu na kila anayetembelea hapo kwa taarifa tulizonazo huwa anapewa maneno matamu lakini mpaka leo kiwanda hiki hakijafanya kazi.

Mheshimiwa Mwneyekiti, ni kiwanda muhimu kwa maendeleo ya nchi, kilichokuwa kinazalisha nondo muhimu mno na ambacho chuma ni kitu muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa lolote. Lakini mpaka leo kiwanda kile hakifanya kazi na ni miaka mingi mno. Hivi kweli Wizara hii ya biashara na viwanda inafuatilia kwa karibu katika viwanda walivyobinafsisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatia uchungu sana kuona mwekezaji katika kiwanda kuna vitu vinang'olewa au mpaka sasa hajafanya kitu. Hivi hii *PRSC* hii mikataba ambayo inalalamikiwa kila siku inakuwaje? Ngoja nitoe mfano mmoja katika hiki

kiwanda cha Mkata wakati wa kamati nilimwuliza Mheshimiwa Waziri, hivi Mheshimiwa Waziri kile kiwanda cha Mkata mpaka leo hakijafanyakazi inakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kweli jibu lake sikufurahia hata kidogo kwa sababu aliniambia ukishabinafsisha kitu, kitu umeshamuuzia mtu kwa hiyo, jukumu limeshaondoka. Ni mali yake yeye huwezi kumwingilia sana. Mimi nikashangaa na kwa kujua hiki kipengele jukumu la kazi ya biashara na viwanda nikashangaa. Leo watu wanapewa ardhi na ikiwa hajaiendeleza kwa muda mfupi tu ananyang'anywa, je, kiwanda kizima ni mali ya nchi, halafu mkataba wenyewe kwamba umeshamuuzia tena iwe basi tu haiwezekani hata kidogo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni viwanda vingi sana, lakini bora nitoe mfano wa vitatu hapa hapa Dodoma. Kuna kiwanda kiko Zuzu cha kutengeneza *tiles,* kiwanda hiki mwekezaji alihidiwa mambo mengi sana na yeye akaja akawekeza akatafuta sehemu kule akawekeza akaanza kuzalisha *tiles* punde si punde inaonekana kukawa na matatizo, leo kiwanda kile hakifanyi kazi, vijana wa hapa hapa Dodoma wangapi wa eneo la Zuzu waliokosa kazi na sehemu nyingine ni vyema Mheshimiwa Waziri, atufafanulie nini kilitendeka mpaka leo kiwanda kile hakifanya kazi ni kwa sababu gani? Mfano nilioutoa viwanda vyote vitatu, je, wananchi wetu wamekosa kazi kiasi gani? Serikali imekosa mapato kiasi gani na tuvinyamazie kimya, tufumbe macho tu wakati moja ya jukumu la Wizara hizi lazima ifuatilie na tujue kinachoendelea hii mikataba ikoje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatosha kwa kifupi tu kujikita katika suala hili la viwanda. Ningeomba niende katika viwango vya ubora vya taifa. Tuna *TBS* ipo hapa ina jukumu la kuweka viwango vya Taifa vya ubora kwa bidhaa kwa makundi mawili. Bidhaa zinazoingia nchini, bidhaa zinazotoka nje au bidhaa zinazozalishwa nchini zinafaa au kwa mujibu wa utaratibu zinatakiwa zihakikiwe ubora wake. Je, zinafikia viwango kwa bidhaa zote zinazotoka nje na zinazozalishwa hapa nchini ziko aina nyingi sana ambazo hazifikii viwango?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwananchi wa kawaida ukimwambia bidhaa hii imetimia kiwango labda umepima *tensile test* au umepima kwa kiwango cha milimita mwananchi wa kawaida hawezi kuelewa. Lakini ma-*contractor* na watu wengine wanaojua mambo wanafahamu. Lakini kiwango cha ubora mwananchi wa kawaida anakijuaje, anakijua kutokana na matumizi ya vitu vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano leo zipo nyaya nyingi za umeme zinazotumika za *fitting* za ndani, tunazo *bulb* tele ambazo zinatumika majumbani. Tunazo *switch socket* tele tunazotumia nyumbani, mwananchi wa kawaida atajua hiki hakikufikia ubora wakati kila wiki ananunua *bulb* inaungua. Vifaa hivyo tunavyo tele, vina matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukinunua bati kwa mfano vifaa vinavyozalishwa nchini, ukienda ukinunua bati *gauge 30* ya Tanzania ukienda ukanunua bati hiyo hiyo *gauge 30* ya Kenya, ukienda ukanunua bati *gauge 30* hiyo ya India utakuta udhaifu wa bati yetu au tuseme hawa Kenya na nchi nyingine *instead* ya *gauge 30* wanaifanya *gauge 28* iwe *stronger* zaidi kwa kupata soko zaidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna udhaifu fulani katika ufuatiliaji wa viwango. Mifano hii inaonekana mara nyingi sana hata hapa Bungeni kwako hivi karibuni Mheshimiwa Haroub Said Masoud alizungumza kuhusu ubora wa viwango hata magodoro hapa hapa Bungeni kwako. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mifano hiyo iko mingi na kila mtu anaelewa leo tuangalie hata hizi simu za mkononi tunazoletewa kuna vimeo vingapi, unanunua simu siku tatu, ya nne tayari haifanyi kazi tena. Je, zote zinapitia viwango? Nafikiri inaonekana kwa ujumla namna gani tunahitaji kurekebisha kwenye mambo ya viwango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya tatu ningeomba haraka haraka na nisipigiwe kengele ya pili, hizi taasisi za utafiti *TIRDO, TEMDO, CAMARTEC* na kadhalika. Inasikitisha kuona kwamba kwanza ile maana ya kuwa sekta hizi zifanye utafiti, ziwezeshwe vizuri suala hili halipo na ni kweli tunaziita sekta hizi kama sekta za utafiti tuchukue mfano mdogo *TEMDO* ina wafanyakazi 45 katika wafanyakazi 45 kuna *Engineers* kumi akiwemo Mkurugenzi Mkuu, kuna *techinician* au mafundi 15 lakini watu wa utawala na uhasibu wako 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitengo cha utafiti hicho jamani. Takriban ni nusu kwa nusu, ma-*Engineers, Technician,* Utawala na mambo ya Uhasibu wako 20. Sasa kweli hicho kitengo kitafanya kazi bajeti yake mwaka huu imeombewa shilingi 322,201,000. Lakini shilingo milioni 159 zinakwenda kwenye mishahara na haya mambo ya utafiti na kazi nyingine ni shilingi milioni 163, *are we really serious?* Kitengo kidogo cha Utafiti watu 45 lakini watu wa Utawala na Uhasibu watu 20 ma-*Engineer* kumi na mifano hiyo iko kwenye *CAMARTEC* na sehemu nyingine.

Ningeomba Mheshimiwa Waziri, hivi vitengo kama kweli unataka vifanye kazi ya utafiti mambo mawili yatazamwe. Viwezeshwe vizuri na halafu vitazamwe uwiano wake mambo ya kiufundi na mambo ya kiutawala. Hatuwezi kwenda kitengo cha watu sawasawa na utawala na watu wa ufundi wakati kitengo chenyewe cha kufanya utafiti.

Mwenyekiti, la mwisho jambo la nne. Kuna haya mashamba ya mipira. Mashamba ya mipira, kuna kiwanda chetu cha *General Tyre* lakini *raw material* tunaagiza kutoka Malaysia na Amerika ya Kusini. Mashamba ya mipira yaliyopo hapa Muheza ya Kihuhwi na mengine yapo Pemba, wawekezaji hao waliokodi wananunua mipira hiyo wanauza Nairobi kwa kutengeneza *chewing gum*. Kiwanda chetu leo *raw materials* kipate wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tuangalia bei ya mpira wa *General Tyre* ni kubwa, ndiyo lazima iwe kubwa, kwa sababu *raw materials* viwanda vyake inaagizwa kutoka Malaysia, viwanda vyetu sisi tutakuwa tukitengenezea *chewing gum* ndiyo masharti yetu hayo ya *PSRC* wakipewa watu, siyo kwamba yaani anapewa uhuru afanye anavyotaka. Sasa viwanda hivi vitakuwa hai kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mifano mingi ya aina hii. Kwa mifano mitatu hiyo, ningeomba Mheshimiwa Waziri labda anifafanulie hii *PSRC* wana uhuru wa namna gani tusioelezwa na ni vema hivi viwanda tueleze hizi bei halisi, kwa sababu ikiwa kweli mtu ana uchungu hawezi kukiacha kiwanda kikatelekezwa na kama tuna viwanda ambavyo vinasaidia mashamba au malighafi ya kusaidia viwanda vyetu ni kwa nini muwekezaji aruhusiwe kuuza nje kwanza bila kufidia soko letu la ndani tukaendeleza viwanda vyetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Mimi kwa upande wangu nitaanza na Masoko hasa soko la Kimataifa ambayo Wizara inaeneza katika nchi yetu na hasa ya Kibaigwa.

Kwa mfano, utakuta pamoja na nia nzuri ya Serikali kupitia Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ya kujaribu kuwawekea wananchi masoko ya Kimataifa kama alivyozungumza Msemaji wetu wa Kamati ya uwekezaji na Biashara kwa ajili afya na kurahisisha kupata bei nzuri zaidi ya mazao. Lakini masoko haya hayana udhibiti wa aina yoyote na wala hayalindwi. Kwa hiyo, badala ya kuwa na maslahi kwa wananchi yamekuwa sasa hivi ni kero kwa wananchi.

Kwa mfano, katika soko la Kibaigwa, lile soko ni zuri, limewekwa lami, lina mizani, lina barabara nzuri ya lami, kuingia katika barabara kuu, lakini baada ya kujengwa lile soko, kuna soko lingine tena limetengenezwa mita 100 tu kutoka soko lile la Kimataifa. Lakini Wizara kupitia vyombo vyake mbalimbali vya biashara vimekaa kimya. Pale Kibaigwa sasa hivi kuna soko lingine tena limejitokeza na ni kubwa kuliko lile soko la Kimataifa na watu wengi hawalifahamu, lakini lipo mita 100 tu kutoka lile soko. Sasa tunapozungumza masuala ya afya kwamba watu wamewekewa lami, ili waanike mahindi yao kama alivyozungumza Mheshimiwa Rais alipofika pale kwamba hataki watu waweke mahindi kwenye vumbi, waweke mahali pazuri. Lakini watu wamekimbia pale wameweka tena kwenye sehemu nyingine ya vumbi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado tunakaa hapa tunajisifia kwamba tumeanzisha masoko ya Kimataifa. Sasa hii imekuwa kama baa za mjini. Maana yake baa za mjini, ukimwekea mtu kiti ndani hataki anataka umwekee viti nje yanapopita maji machafu yeye ndiyo anaona safi. Hakuna udhibiti wa aina yoyote. Sasa itakuwa haina maana yoyote, kama masoko haya ya Kimataifa yataendelea kujengwa wakati hakuna udhibiti wa kuyaondoa yale masoko ya pembeni ambayo yanaanzishwa. *(Makofi)*

Sasa hivi mkulima akipeleka katika masoko ya Kimataifa anapimiwa mazao yake kwa mizani, ina maana anauza kwa kilo na akipeleka katika lile soko la pembeni anauza kwa debe. Nyumbani kwake labda amepima gunia lina debe saba akifika pale madebe yale yameshapashwa moto linatoka debe sita. Kwa hiyo, tayari ameshaibiwa debe moja ambalo lina kilo 18 na bado pale watu hawaendi tena kwa kutishwa tishwa tu kwamba mkienda pale soko la Kimataifa sijui hakuna hiki, wanakwenda kwenye yale masoko ya wahuni ya pembeni yale. Lakini bado Wizara pamoja na Serikali imekaa kimya na bado

hapa tutaongeza masoko mengine sasa kama masoko haya yanazidi kuongezwa na haya maslahi kwa wananchi yana faida gani? La kwanza. *(Makofi)*

La pili, sasa hivi katika nchi hii pamejitokeza vituo vya mafuta ambavyo havina idadi na vimo ndani ya makazi ya wananchi. Sasa tulitaka kufahamu wanapata leseni kwa mtindo gani au ninavyofahamu mimi, katika miji yoyote au katika sehemu yote kuna ramani maalum zinazoonyesha kwamba hapa panatakiwa iwepo stesheni ya mafuta, hapa panatakiwa iwemo hospitali. Lakini kwa mfano ukienda Dar es Salaam barabara ya Shekilango, ukiwa na tenki tu la mafuta unaweka chini tayari, una gereji nyuma, mbele pana *petrol station*. Ukienda mitaa ya Tandika vituo vya mafuta kati kati ya nyumba, sasa hii inaweza kuleta majanga ya moto au nchi hii kama tulivyozoea mpaka utokee mlipuko ndiyo aende bwana mkubwa mmoja pale ndiyo akaseme kwamba kuanzia leo tunaunda Tume ya Uchunguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake lazima leseni ziwe zinatolewa kwa kuangalia mazingira na sheria. Halafu cha ajabu hata watu wanapewa hata leseni za kuweka *petrol station* ambaye hana hata tenki ya *under the ground* na sheria ni kuwa huwezi kuanzisha *petrol station* mtu ana mapipa saba, nane anapewa leseni.

Huwezi kufanyia biashara ya mafuta. Hii nii hatari na wewe ni shahidi katika jimbo lako, katika kijiji cha Pandambili watu wameshawaka moto pale kwa ajili ya mapipa wakufa. Wengine mpaka leo wana alama za maisha na vile vile sasa hivi imetokea milipuko mingi sana kwa ajili ya mafuta ya taa. Watu wamekufa kwa ajili ya milipuko hiyo, lakini watu hawaelewi, tunaibana tu Wizara ya Nishati na Madini lakini lazima tuangalie na huko nako kunatolewa leseni Wizara ya Biashara, lazima iangalie. Hii yote ni sababu ya kutoa leseni kwa watu ambao hawana vyombo maalum ya kuhifadhia mafuta ambayo ni kama vile *under ground tanks.*

Kwa hiyo, chombo hicho cha kuwekea petroli kesho ataweka mafuta ya taa atayauza kwa mteja ataenda kutumia nyumba kwenye koroboi au kwenye chemli au kwenye *stove* au kwenye kitu chochote, mwishowe inaleta mlipuko. Kwa hiyo, tuangalie namna ya utoaji wa leseni. Sio watu wamekaa tu hakuna chochote kinachofanyika, tutawapoteza wananchi wengi hapa kwa mtindo huu.

Suala langu la mwisho ni kuhusu habari ya viwanda, hasa vile vinavyotengeneza vifaa vya ujenzi, *cement* na mabati. Kwa mfano msemaji aliyenitangulia hapa amezungumzia ubora wa bati toka Kenya na mabati mengine, ni bora zaidi kuliko bati ya hapa Tanzania. Sasa hivi bati *gauge* 30 ni sh.10,000 kwa bei ya kiwandani, wakati mshahara wa mwalimu ambaye hana marupurupu mengine ya ziada labda 70,000 au 80,000 ana watoto tisa hivi unategemea atajenga huyu si mpaka mwisho wa dunia atakuwa anakaa kwenye nyumba za porini porini huko. *(Makofi)*

Mimi nasema kama tunaamua kulinda viwanda vya ndani, basi tulinde vile ambavyo tuna maslahi kwa wananchi maana yake unapozungumzia habari ya vifaa vya ujenzi inamgusa kuanzia mtu wa juu hadi mtu wa chini kabisa, mtu maskini wa mwisho. Sasa Serikali iwe na utaratibu tu kwamba iruhusu vifaa vya nje viingie kama mabati toka

nje, *cement* toka nje, hivi sasa ukichukua *cement* iliyobanwa mpaka kuileta hapa saa nyingine ukiilipia na kodi kama unatakiwa kodi ya kawaida kama ya viwanda vyetu ya kawaida ita-*cost* shilingi 7,500/= au 6,500/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunang'ang'ania kuvilinda viwanda ambavyo viko vichache na vinaweza vikakaa na tukapanga bei. Kwa mfano viwanda vya bati, viko viwili, kuna *ALAF* na kuna Kiboko. Lakini tunapozungumzia habari ya kuweka kodi kubwa kwenye bidhaa ya nje kama ya mabati au *cement* wakati vyenyewe vya kwetu havina uwezo wa kuzalisha kwa wingi na hazina uzalendo wa kuweka bei ya wastani basi haina maana yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bora tuwe tunapata tu bidhaa kutoka nje ambayo wananchi wa kawaida watafaidika nayo. Hivi viwanda hata vikifa havina faida yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wananchi hawawezi kufaidika navyo, sasa vya nini sasa, haina maana yoyote, kama kodi tutapata kwa bidhaa zinazotoka nje, Serikali itaendelea kupata kodi. Lakini tusing'ang'anie tu kwa sababu tuna viwanda Tanzania sasa ni nchi ya viwanda. Wakati viwanda havina manufaa yoyote kwa wananchi. Sasa tunalinda nini hapa, ooh! Tunalinda maslahi ya watu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, lazima tuangalie kuna viwanda ambavyo vinalindika na kuna viwanda vingine havilindiki. Hamuwezi mkalinda kitu ambacho chenyewe kinaweza kikakaa na kikapanga bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kusema hayo, tuko katika Awamu ya Nne na watu wengi ni wapya, naunga hoja mkono. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMMED AMOUR CHOMBOH:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie kidogo katika Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Masoko. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu yake kwa kuandaa hotuba yao nzuri ya Bajeti ambayo kidogo naona ina matumaini. *(Makofi)*

Lakini mimi kidogo nilitaka kuchangia kwenye sehemu ya mambo ya masoko kwa sababu biashara yoyote bila kuwa na soko la uhakika itakuwa haina maana na viwanda bila kuwa na soko itakuwa haina maana na roho ya biashara ni soko. Mimi nilitaka kugusia mpango mzuri wa Serikali wa kujenga masoko katika Mikoa mbalimbali kwa ajili ya kuwanufaisha wakulima wetu na wazalishaji wa mazao hasa ya vijijini.

Nimefurahi kuona kwamba Serikali ilifanya utafiti wa bidhaa ya asali na nta nje ya Tanzania. Lakini pia nilikuwa naomba nishauri kwa kupitia mpango huo huo au njia hizo hizo walizopata masoko ya asali na nta katika nchi ya *Gulf* kama Oman na Jumuiya ya Falme za Kiarabu. Kule kuna soko zuri sana ya bidhaa hizi za matunda. Matunda kama ndizi, embe, ndimu, chenza hata mboga mboga yakiwa *fresh. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema hayo kwa uzoefu kwa sababu mimi mwenyewe binafsi nimeshawahi kufanya kazi hiyo. Kwa kuwa sasa hivi kuna Ubalozi wetu pale Oman na Falme za Kiarabu, ni vizuri sana na kwa uzoefu tuliokuwa nao kuna Watanzania wengi sana kule na wanavikosa sana vitu hasa kutoka Tanzania na wanatamani sana. Kwa hiyo, kwa kupitia Idara ya Masoko ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na kwa kuwa wamekwishaanza kutafuta soko la nta na asali basi ni vizuri kujikita pia katika matunda haya ili katika masoko yetu yale ambayo yanakuwa yanajengwa sasa hivi katika mikoa mbalimbali wakulima wetu watakuwa na uhakika pia kusafirisha bidhaa baada ya kuuza ndani lakini pia tuweze kuuza nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna habari ambazo ni za uhakika kabisa, kuna baadhi ya wafanyabiashara wa nchi za jirani huwa wananunua matunda kutoka kwetu hapa na wakasafirisha nje ya nchi kwa kupitia nchini kwao wakasema hivyo ni matunda kutoka nchini kwao.

Kwa hiyo, nafikiri pia jambo hili nafikiri Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko italifuatilia vizuri kuna soko zuri na la kuweza kuwanufaisha wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kugusia tu kidogo kuhusu wazalishaji wetu wadogo wadogo hapa nchini wale wasindikaji wa matunda. Nimejaribu kupitia sehemu mbalimbali nikaona hasa katika mabanda ya biashara ya maonyesho pale Sabasaba, wasindikaji wa matunda walio wengi sana walikuwa wanakosa kitu kimoja ambacho ni muhimu sana. Wanapokuwa wanafanya *packaging* baadhi ya *container* wanazotumia kuna *container* ambazo sisi au watu wa Tanzania zimezoeleka kuwekwa vitu tofauti na kitu chakula.

Kwa mfano, kuna baadhi ya wafanyabiashara pale walikuwa wame-*pack* asali ndani ya *container* ambayo huwa kwa kawaida inawekewa *distilled water* au dawa ya choo au *oil* au *engine oil.* Sasa kwa mtazamo wa ghafla mtu akienda akiambiwa hii ni asali inamtoka imani kwamba labda haipo katika ubora unaohitajika. Halafu kuna bidhaa fulani ambazo huwa wanazi-*pack* wanapoweka hiyo *label* utaiona hiyo *label* huku imeshuka na kupanda.

Mimi nafikiri wenzetu wa *SIDO* wawaelimishe wale watu wa watu wanaofanya hii biashara hii ya usindikaji wa bidhaa namna ya kuweza kuiweka ile *label* kwa mpango mzuri. Kwa sababu kwa kawaida mtumiaji au mlaji kinachomvutia kwanza ni ile *label,* hajui ndani kitu kilichopo.

Sasa ikiwa kuna kitu cha kumvutia ndiyo inamvuta mpaka kilichopo ndani. Akiona kitu chenyewe kinachofanana, kinafanana ovyo basi na kilichokuwepo ndani chote anakidharau. Kumbe vile ni tofauti, basi ndugu zetu wa *SIDO* nafikiri mngewaelimisha zaidi hawa hasa wasindikaji wadogo wa bidhaa hizi wapate vipi *label* ambazo zinamvutia mteja kwa makusudi ya kuweza kuuza biashara zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napenda kuchangia sehemu hii ya viwanda vyetu ambavyo vinazalisha, ambao ndugu zangu waliotangulia pia na wao walizungumzia suala hili. Hasa hasa hivi viwanda vya *cement.* Viwanda vyetu vya *cement* kwa kiasi kikubwa sasa hivi hasa kiwanda cha Twiga na kile cha Tanga kinatumia nishati mbadala badala hii ya *TANESCO,* maana hiyo kuna habari za kuaminika kwamba kwa kiasi kikubwa sana hupunguza gharama za uzalishaji. *(Makofi)*

Lakini kila siku *cement* inapanda badala ya kuteremka na kama alivyoeleza mchangiaji aliyetangulia ni kweli kuna ushahidi wa kutosha kabisa kwamba *cement* ambayo unaweza ukaiagiza toka nje na ukailipia ushuru mkubwa tu ambao kwa sababu ushuru umewekwa kwa sababu ya kuvilinda viwanda vyetu hivi, lakini bado utaiuza kwa bei nafuu kuliko *cement* ya Tanzania na halafu inakuwa ina ubora zaidi kuliko hiyo ya Tanzania. Hivi viwanda nafikiri vingeangaliwa vizuri tukaona ni namna gani tunaweza tukavisaidia.

Suala lingine ilikuwa nataka kuzungumzia suala hili la usumbufu wa bidhaa za wafanyabiashara bandarini. Ukweli matatizo hayo yapo na yanakuwepo hapa kwa sababu ya urasimu uliokuwepo bandarini sijui ni kwa sababu gani na kwa maana hiyo, ndiyo maana wafanyabiashara wengi hutumia njia hizi bandari nyingine kwa kutolea mizigo yao kwa ajili ya kupitia mizigo yao kwa ajili ya kupitishia soko kuu ambalo soko lenyewe liko Dar es Salaam na moja ya bandari hiyo ni Zanzibar. Wafanyabiashara wengi hutumia bandari ya Zanzibar pia kwa kuteremshia mizigo yao kwa sababu ya usumbufu huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kinachokera zaidi nimeshawahi kuchangia wakati wa hotuba ya Waziri wa Fedha, lakini kwa sababu Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko mambo yake mengi ni mtambuka na Wizara ya Fedha kwa kiasi fulani huwa inahusika, imefika wakati sasa hili soko liweze tulitumie sote. Hata wale wafanyabiashara wanaoteremsha mizigo yao Zanzibar kuleta sokoni hapa Dar es Salaam waondolewe ule usumbufu wa bandarini pale Dar es Salaam na kuna bidhaa ambazo hasa ukiziangalia ni bidhaa muhimu sana kwa sababu sasa hivi bidhaa kama *television, music system, radio,* ni vitu ambavyo ni vya muhimu siyo *luxery* tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa inashangaza wakati tunatoka kule Zanzibar tukapata usumbufu *just* ni *TV, TV* ni kitu cha lazima sasa hivi kwa kila mtu. Sisi kule Zanzibar mwaka 1973 tulilazimishwa *not* kulazimishwa lakini tulilazimishwa kila mmoja awe na *television* kwa sababu ni kitu ambacho kinatoa elimu. Ilikuja *television* Zanzibar kama ni chombo cha kutoa elimu kwa wananchi na ilikuwa mpaka vijijini. Namshukuru Rais wetu wa Kwanza Mheshimiwa Abeid Amani Karume, aliliona hilo na ilikuwa kule vijijini ilikuwa hata hakuna umeme lakini Serikali ilichukua hatua ya kupeleka mpaka betri za magari lakini *television* iweze kuonekana kwa ajili ya kutoa elimu.

Kwa hiyo, sasa hivi *television* isichukulikuwe kwamba ni kitu cha anasa, ni kitu cha lazima kabisa au redio, friji ni kitu cha lazima kabisa, lakini bado ndugu zetu wanaosimamia bandarini pale hasa *Malindi Warf* wanawapa usumbufu sana jambo ambalo linatia uchungu sana na hasa wakiona vitu vya upande wa pili kule ambao ni

Tanzania Visiwani vile vile vimelipiwa kodi kama kawaida na tarehe. Kwa hiyo, mimi nashauri kupitia Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ambayo ndiyo *controller* wa soko hili, soko hili tulitumie sote wa kule na huku kama vile ilivyokuwa hapa wakipeleka bidhaa kule Zanzibar kwa sababu kule Zanzibar kitu chochote kinachotoka huku Tanzania Bara hakichajiwi wala hakiulizwi, kinajulikana kwamba hicho kiko safi. Cha ajabu kutoka kule kuja hivi kinaonekana kwamba kina kasoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyikiti, namwomba Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko kwa kupitia mchango wangu huu ajaribu azungumze na Wizara ya Fedha tuone ni namna gani tunaweza tukatumia soko letu kwa pamoja. Ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi ningependa kushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia. Awali ya yote ningependa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wao kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya kwa jumla na hotuba nzuri ambayo wametoa hapa leo. *(Makofi)*

Mimi ningependa kujikita katika kuelezea au kufafanua umuhimu wa sekta ya viwanda, biashara na masoko pamoja na umuhimu mkubwa wa hatua maalum za kuboresha sera, mikakati, mafunzo na vitu vingine ambavyo vinaambatana na hivi likiwemo na suala la utafiti na umuhimu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningependa kuzungumzia suala ambalo linafahamika na sisi sote. Sote tunafahamu kwamba leo ukizungumza habari ya nchi zilizoendelea, ukizungumza habari ya nchi kubwa, tunazungumzia nchi za viwanda. Ukizungumza habari ya *Super Powers, G8,* ukizungumza sijui *Tigers,* hizi ni nchi ambazo zimepata maendeleo makubwa, sehemu kubwa ya uchumi wa nchi hizi unatokana na viwanda. Mimi nafikiri hili ndilo suala la msingi ambalo ni lazima lijikite katika vitu vyetu na tuwe tayari kuvibadilisha kwa huko. Wengi wetu tunaamini kwamba kuna nchi maalum ambazo ndizo nchi zilizojaliwa na zitaendelea kuwa ni nchi za viwanda na sisi wengine tutakuwa ni nchi za kuzalisha malighafi na kuendelea kuuza malighafi kwa hao wengine ili waendelee. *(Makofi)*

Nashukuru kwamba hili kwa kulitambua kwani Dira yetu ya Taifa na mipango yetu mbalimbali kama vile mpango wa *min Tiger2020,* kama vile Ilani ya CCM na mengineyo yameweka mkazo huo. Nashukuru mpaka tarehe hii Serikali ya Awamu ya Nne imetambua umuhimu huo na imeipa Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Masoko umuhimu unaostahili, kitu ambacho tulikuwa tunalilia muda mrefu sana, angalau wamepata Ofisi nzuri yenye hadhi inayostahili, angalau wamepata fungu la fedha zaidi, lakini bado kwa Wizara hii ambayo ni muhimu na nyeti. Sasa pamoja na kuleta uhai bado, kunahitajika kazi hii ifanyike kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kimoja ambacho tulikuwa bado tunatazama ni kwamba je, viwanda ni sekta kiongozi au siyo sekta kiongozi. Mimi nafikiri kwamba

tukubaliane juu ya dhana hiyo. Viwanda ni sekta kiongozi kwa maana kwamba viwanda au mazao ya viwanda ndiyo yanahitajika

**MWENYEKITI:** Ongeza sauti kidogo Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, kusudi usikike katika kikundi kizima. *(Makofi)*

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda au bidhaa za viwanda, ndizo zinachochea maendeleo katika sekta hii. Kilimo kwa mfano, pembejeo, zana mbalimbali za kulimia, zinahitaji mazao kutoka viwandani. Uvunaji wa mazao, usindikaji wa mazao, usafirishaji wa mazao, uhifadhi wa mazao, unahitaji vitu hivyo. Hivyo hivyo madini, vinahitaji mchango mkubwa wa sekta ya viwanda wafanye hivyo. Kadri ya mazao ya viwandani yanavyoongezwa katika shughuli nyingine ya uzalishaji ndivyo kadri uzalishaji na tija inavyoongezeka.

Kwa msingi huo hizi sekta nyingine ambazo nchi zilizoendelea au za viwanda vingi zimeweza kupata maendeleo makubwa, imeendelea kutumia vizuri sekta ya viwanda na kuendeleza sekta ya viwanda. Sasa sisi tumelitambua hilo na tumekuwa na Sera mbalimbali, nyakati mbalimbali za kuweza kufikia huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali tulikuwa na Sera ya *Import Substution* ambapo tulijenga viwanda vingi sana ili sisi wenyewe tujitegemee kwa bidhaa zetu humu ndani, badala ya kuviagiza toka nchi za nje. Hatimaye tukaja katika Sera ya *Basic Industries Strategy* katika miaka ya 1970. Hatimaye tukaja katika *Sustainable Industries Development Strategy* na pia tukawa tunazungumza zungumza kitu kinaitwa *Export Development Strategy.* Kwa bahati mbaya hapana ufafanuzi ulio wazi. Je, Sera moja inayohusiana na nyingine vipi kwa mfano, hii *Sustainable Industrial Development Strategy* inahusiana vipi na *Import Subsitution Strategy* inahusiana vipi na *Basic Industry Strategy* je ni sehemu yake au imeachwa? *Export Development Strategy* na *Basic Industry* na *Export Develop Strategy* zinahusiana vipi?

Sasa haya ni masuala ambayo ni lazima yawe wazi vinginevyo tutakuwa tunakanganyika. Kwa mfano tumetoa fedha kwa ajili ya shughuli za maendeleo mbalimbali, kitu ambacho Waziri ameeleza humu ndani lakini kwa masikitiko ambacho hakionyeshi wazi, ni kujaribu kutekeleza ilani ya kuweka misingi ya viwanda vya msingi, viwanda mama, *basic industries*. Mchuchuma na Liganga, zimeelezwa kwamba matayarisho, yanafanywa ili kwamba tuanze kufanya shughuli hizo, lakini hamna fedha ambazo zimewekwa.

Kwa hiyo, sasa hii kwa kiasi fulani, inaonyesha jinsi ambavyo pengine hatuna uwazi sana au uhusiano wa karibu sana na busara zetu na sera zetu na jinsi tunavyopanga mipango thabiti na utekelezaji wake kuweza kufikia huko. Tumesema mwishoni mwa mwaka Dira yetu 2025 tunatakiwa tuwe na uchumi wa viwanda vya kati na viwe vinakua kwa asilimia 15, sawa ni vizuri tumeweka malengo hayo lakini haya malengo hayana budi kuhusishwa kwa mikakati na mipango rasmi ambayo itawezesha hatua kwa hatua kuweza kufikia huko.

Sasa hili ni suala ambalo nataka liwe wazi, Wizara inaweza kuwa ina nia njema ya kutekeleza haya kama inavyotakiwa, lakini haina uwezo wa kutekeleze kwa sababu Serikali kwa jumla au Wabunge au Chama kwa jumla pengine hakijaona uzito wa sekta hii. Kwa mfano tunatoa uzito mkubwa kwa kilimo ni sawa, tumesema kwamba kilimo wengine wanasema ni sekta kiongozi, wengine wanasema kilimo ni uti wa mgongo, wengine wanasema kilimo ni roho ya Taifa, sawa sawa hatukatai lakini sasa tukisema hayo na tukiwa tuna sera hii na mipango hii na mikakati hii ni vizuri vilevile kuwa na fedha ambayo itasaidia kwa kweli. Sasa kwa nini umuhimu huu ni lazima uendane na mahitaji mengi ya fedha, ili kuweza kuendeleza viwanda, ili kuweza kuendeleza biashara, ili kuweza kuendeleza masoko, utafiti ni kitu muhimu sana. Utafiti na maendeleo yanayotokana na utafiti ni muhimu.

Sasa Wizara yenyewe au Serikali zinashughulika na *policy research,* bahati nzuri Wizara na Serikali zimeweza kutengeneza uwezo huu kwa kiasi kikubwa hii *policy research* wanafanya wenyewe utafiti wa sera, mara ingine wanasaidia na wataalam kama *UNCTAD* na wengine lakini umefanyika vizuri.

Lakini maendeleo ya viwanda, maendeleo ya masoko yanahitaji utafiti wa sehemu mbalimbali kuweza kujua mahitaji halisi ya bidhaa mbalimbali, kwa sehemu mbalimbali, kwa misimu mbalimbali. Hayo yanahitaji fedha nyingi sana za utafiti. Ni bahati mbaya kama Waheshimiwa Wabunge waliopita walivyosema kwamba kwa Wizara hii hatuoni umuhimu wa utafiti inayofanya. Ni vizuri ukaona hivyo kama tunataka ipige hatua hiyo inayotakiwa, lakini zile taasisi basi tunazipa mishahara tu, mishahara tu jamani ya wafanyakazi bila fedha ndio tufanye utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke hao wenzetu ambao tunasema wameendelea wameweza kuendelea katika sekta mbalimbali za viwanda, tazama ushindani mkubwa ulioko kwenye sekta ya magari, sekta ya anga, sekta mbalimbali, sekta ya *electronics,* haya yameweza kufanyika kwa sababu ya utafiti mwingi ambao unagharimu fedha nyingi na sisi huku kwetu kama tunataka kweli kuendeleza sekta ya viwanda hatuna budi kuwekeza sekta ya viwanda, hatuna budi kuwekeza katika uwekezaji na utafiti, ili kuweza kuona namna gani bidhaa zetu tutaziboresha, namna gani bidhaa zetu zitaweza kushindana na ushindani huu, tunasema kuhimili ushindina, sasa kuhimili ushindani, huwezi kufanya bila utafiti wa masoko, utafiti wa bidhaa wenyewe, na hizi taasisi mbalimbali zinatufanyia kazi utafiti unaotakiwa ili kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda pengine huko ninakosema ni mbali sana pengine hatutafika huko na nchi zilizoendelea zinauwezo, mashirika yenyewe yanafanya shughuli hizo, kampuni zenyewe zinafanya hivyo. Lakini hapa kwetu tunasema tunataka kumsaidia mkulima, tunataka kumsaidia mchimbaji mdogo mdogo, tunataka kumsaidia mfanyabiashara mdogo mdogo. Mfanyabishara mdogo mdogo, mkulima hana uwezo wa kufanya utafiti huo. Ni lazima taasisi hizi ziweze kumsaidia kufanya hivyo na ili kufanya hivyo fedha inahitajika.

La pili, sasa haya yakishafanyika yanahitaji kusambazwa kwa mafunzo, nashukuru kwamba jitihada zimefanywa kufundisha ujasiriamali na hilo tumelikubali. Lakini mafunzo ya ujasiliamali, mafunzo ya utaalam, mafunzo ya taarifa za biashara,

mafunzo ya matangazo ni muhimu sana, kwa hiyo, taasisi hizi zipewe fedha za utafiti, zipewe fedha ya kueneza utafiti wake usikae tu kwenye mafaili, wapewe fedha za kuweza ku-*commercialize prototype* zao wanazoweza kutengeneza, vinginevyo hatutafika huko. La muhimu zaidi baadaye ni suala la kutokusambaza taarifa ya habari, hapa tumelalamika kwamba kuna nafasi nyingi sana za masoko zinatokea katika dunia. Ulitolewa mfano *EPA,* viko vitu vinaitwa *General Systems of Preferences* viko vitu vinaitwa *General Schemes of Trade Preferences (GSTPs), AGOA. AGOA* ndio iliyotumika pale, haya na mengineyo yapo baadhi ya sisi wananchi tunashindwa au Tanzania tunashindwa kuyatumia haya, kwa sababu ni Wizara na maofisa na taasisi chache ambazo zinalewa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Chamber of Commerce* inajitahidi, *CTI* inajitahidi lakini bado wao hawana uwezo wa kutosha wa kuweza kutoa taarifa hizi kwa wafanyabiashara, wacha wakulima wadogo wadogo wale wa vijijini wacha wafanyabiashara ndogo ndogo walio vijijini. Hapa basi kuna umuhimu mkubwa sana wa Serikali napo kuweza kuipa uwezo Wizara hii, kuzipa uwezo taasisi zake kuweza kufanya hivyo. Vinginevyo itakuwa vigumu kuyatekeleza hayo malengo makubwa tunayoweka haya kusema kweli itakuwa ndogo na yatakuja kupotea njia hivi hivi tu, bila hayo kufanyika inavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suala lingine, ni suala la masoko, utafiti wa masoko ni suala pana sababu kuna vitu vingi sana maonyesho ya biashara ni kitu kimoja, kwenda katika misafara ya biashara ni vitu vimojawapo. Bahati mbaya sisi tunapozungumza *Export Development Strategy*, tunafikiria tu au tumeji-*confine* bahati mbaya sasa hivi kwamba *Export Development Strategy* ni *Export Processing Zones* peke yake. Bila masuala mengine haya ambayo yanaambatana na ukuzaji, utafiti kwanza wa masoko, ukuzaji wa masoko ili kuweza kuyahudumia yanavyostahili kwa utashi wa walalaji kwa utashi wa matumizi katika viwanda mbalimbali ili kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa niaba ya wananchi wote wa Mkoa wa Singida, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa ajili ya siku hii ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wasanii wote nchini Tanzania napenda nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuwawakilisha hapa kwa kuchangia hotuba hii ya Waziri hasa kwa kulenga mfumo mzima wa haki za wasanii Tanzania. *(Makofi)*

Napenda kumshukuru na kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, na Watendaji wote wa Wizara hii ya Viwanda na Biashara, hasa kwa kutambua umuhimu wa kazi za wasanii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza kabisa nijitambuishe mimi mwenyewe binafsi, mimi ni msanii na mwimbaji wa nyimbo za injili Tanzania, pia ni mjumbe wa bodi ya *COSOTA,* Tanzania yaani Chama cha Haki Miliki. Chama hiki

ilianzishwa chini ya Kifungu 46 cha sheria Na. 7 ya mwaka 1999 iliyotungwan na Bunge lako Tukufu yaani sheria ya haki miliki na haki shiriki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Chama cha Mapinduzi imetangaza kuongeza ajira kwa vijana, tunatambua kabisa kwamba vijana walio wengi ni wasanii hapa nchini Tanzania lakini bado tunaishukuru kwamba iliweza kujua umuhimu wa kazi za wasanii. Nikisema kazi za wasanii, ni pamoja na watunzi, wachapishaji na shughuli zingine za ubunifu, si maana ya usanii kuimba peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo napenda kuzungumzia hasa chama cha haki miliki Tanzania yaani *COSOTA.* Chama hiki baada ya kuanzishwa kimekuwa kikifanya kazi kwa nguvu zote lakini katika mazingira magumu sana, labda kwa ridhaa yako niweze kunukuu baadhi ya kazi na haki inazopaswa kufanya *COSOTA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ni kukunza na kulinda haki za wasanii na watunzi. Pili, pia kulinda haki za wachapishaji.

Tatu, ni kukusanya na kugawa mirahaba kutoka kwa watumiaji wa kazi za wasanii. Kusajili kazi za wasanii, pia kutayarisha na kutambua na kutetea kazi za wasanii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia *COSOTA* imekuwa ikielimisha wadau mbalimbali hasa maafisa foroza, mahakimu pamoja na watumiaji wenyewe wa kazi za sanaa. *COSOTA* imekuwa ikifanya kazi katika mazingira magumu sana, ninapenda kuzungumzia kwa sababu sisi wasanii, tuna maslahi na *COSOTA. COSOTA* ina wafanyakazi watatu, (maafisa), sekretari mmoja dereva pamoja na mhasibu. Lakini wanatakiwa kufanya kazi nchi nzima, mikao yote 26 katika baadhi ya kazi hizi ambazo nimezitaja hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ufinyu wa wafanyakazi hawa imekuwa ni vigumu sana kuweza kufanya kazi hasa kufika katika ngazi za Wilaya pamoja na Tarafa na Kata. Napenda kuieleza Wizara, kwanza naishukuru kwamba imekuwa ikitenga fungu kwa ajili ya shughuli za *COSOTA.* Fungu hili mwaka 2005/2006 zilitengwa shilingi milioni 200, lakini hazikutoka zote, zilitoka shilingi milioni 110 tu, sasa napenda kuieleza Wizara inapotenga fungu kwa ajili ya *COSOTA,* naomba isitoe nusu na zingine zikabaki, kwa sababu inairudisha nyuma *COSOTA,* kwa ajili ya kufanya kazi yake hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia suala hasa la uharamia kwa kazi za wasanii, kumekuwa na uharamia mkubwa sana kwa kazi za wasanii. Napenda nizungumzie hasa mikataba inayofanywa kati ya wasambazaji wa kazi za wasanii, pamoja na wasanii wenyewe. Mikataba hii inapofanywa, inakuwa ni kati ya msanii na msambazaji, lakini msaani, kwa sababu yeye ni mhitaji anakuwa akikandamizwa na msambazaji, bado hata hivyo, mkataba unapowekwa, msambazaji anakuwa akisambaza kazi za wasanii, zaidi ya ule mkataba waliowekeana na msanii huyu.

Lakini bado msanii anapokuja kukamata kazi zake na kuzifikisha mahakamani, *COSOTA* imekuwa ikisaidia sana, katika kusuluhisha haya matatizo ya uharamia huu.

Wakati mwingine wanayamalizia palepale *COSOTA,* lakini suala linapokuja kufika mahakamani, mahakama zetu zinakuwa hazitendi haki kwa wasanii. Ninao mfano mmoja au miwili, kuna kesi ya msanii mmoja ambaye alikana kazi zake Morogoro, zikiuzwa bila ridhaa yake, msanii alipofika *COSOTA,* akaelekezwa aende polisi kesi ikafikishwa mahakamani, mara alipofika msambazaji akaihamishia kesi Dar es Salaam. Msanii alipoenda kuuliza na kudai, kwa nini kesi ihamishiwe Dar es Salaam, badala ibaki Morogoro, akakamatwa akawekwa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, ijaribu kuweka utaratibu ambao utaendelea kulinda na kutetea haki za hawa wasanii kwa kushirikisha na mahakama zetu na kesi hiyo bado inaendelea. Naiomba Wizara isimamie ili haki iweze kutendeka kwa msanii huyu. Lakini ninao mfano mwingine tena, tunaye mwimbaji wetu maarufu Saida Kaloli, alikama kazi zake kule Bukoba, kanda 500, kanda 200, kesi ilipofika Mahakamani, Sheria inasema milioni kulipa, lakini ilikuja kutoka hukumu ya faini ya 40,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Wizara, izidishe nguvu kwa *COSOTA,* ili *COSOTA* iweze kusimamia barabara haki za wasanii. Lakini pia nilikuwa naomba, mkataba uliowekwa na Serikali kwamba *COSOTA* itakapofikia Juni, 2007 Serikali itajitoa kutoa ruzuku *COSOTA,* naiomba Serikali, Wizara iendelee kutoa ruzuku mpaka pale *COSOTA,* itakapokuwa imesimama ili kuweza kutetea haki za wasanii. Kwa sababu tunayo ofisi moja tu Dar es Salaam, lakini hakuna mikoani, wasanii wengi wako mikoani, hawaweza wote kuweza kufika Dar es Salaam, naiomba Wizara isimamie ili ofisi za *COSOTA* ziweze kufunguliwa kwenye mikoa, pia iongezwe ruzuku na iongeze wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimwia Mwenyekiti, napenda kuwapongeza wafanyakazi wa *COSOTA* wachache, Mtetewaunga Stephen ambaye ni Afisa Mtendaji, Yustasi Boymanda Mkinga, ambaye ni Afisa Leseni na Justine Kimario ambaye ni Afisa Kumbukumbu, hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, Wizara naiomba muipe nguvu *COSOTA* ili sisi wasanii tuweze kuelimishwa tupate kujua haki zetu zaidi na tuweze kufaidi. Pia *COSOTA* imeweza kukusanya mrabaha shilingi milioni 11 ambazo zitagawanywa kwa wasanii hivyo nawaomba wasanii wote, waweze kujiunga na bodi ya *COSOTA,* maana nyimbo zetu zinatumika kwenye matangazo, kwenye *television,* watu wote wapate kujua kwamba wanatakiwa kutulipa, kulipa zile nyimbo zote ambazo wanazitumia, kwa kupitia *COSOTA,* wasanii wote wajiuge ili waweze kufaidi kazi zao na haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge wote, wasanii wote walioko kwenye majimbo yenu wahimizeni wapate kujiunga na bodi ya *COSOTA,* huku watapata elimu zaidi, watafahamishwa nini cha kufanya, ili waweze kufaidi matunda ya kazi zao. Kwa kuongea hayo naishukuru sana Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, kwa kuitilia maanani kazi ya sanaa hatimaye kuunda bodi ya *COSOTA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na nitajitahidi nitumie hizi dakika zilizopo kwa ajili ya kuzungumza masuala kadhaa, ambayo nadhani ni ya muhimu sana katika kuhakikisha kwamba Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Masoko, inafanya kazi zake vizuri, kama jinsi ambavyo Mheshimiwa Spika, alitangaza asubuhi, mimi pamoja na wenzangu tulikuwa *DRC* kuangalia uchaguzi na tunashukuru kwamba wananchi wa *DRC* walifanya uchaguzi wao kwa amani kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zaidi ya uchaguzi *DRC* ni nchi ambayo *very strategic* na karibia kila nchi duniani sasa hivi inaangalia *DRC,* wengine wanaingalia kama eneo la kwenda kuchuma, lakini wengine wanaiangalia kama soko na hii ni kitu ambacho kwa kweli ningependa nikiongee cha kwanza kabisa kwa sababu nimezungumza na maafisa wetu katika ubalozi wetu Kishansa, Balozi Maharage Juma, pamoja na msaidizi wake bwana Sam Shellukindo pamoja na wafanyakazi wengine wote wa Ubalozi na wametueleza baadhi ya vitu kwa kweli vingeweza kuifanya nchi yetu ifaidike na soko hili. *(Makofi)*

Sasa hivi vijana wengi sana wa Kitanzania na Watanzania wengine wapo Lubumbashi wanafanya biashara, lakini katika mji huu wa pili kwa ukubwa, hakuna *consulate* yetu na kwa hiyo, vijana wetu wanapata shida sana katika shughuli zao za kibishara, kwa sababu hakuna maafisa ambao wanawasaidia na zaidi ya yote sasa hivi tunaenda tunafuata kitu ambacho kinaitwa *economic diplomacy. Economic diplomacy* maana yake ni kwamba sasa hivi diplomasia yetu haiangalii siasa, inaangalia masuala ya kiuchumi, inaangalia biashara na katika Wizara ambayo inapaswa kutekeleza sera hii ya diplomasia kiuchumi, ni Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, licha ya kuwapongeza kwa juhudi za kuigeuza *BET* kuwa *Tanzania Trade Development Authority*, waweze kuangalia uwezekano wa kupeleka ma-*commercial attache* katika kila balozi ambayo tunadhani ni *strategic* kwa nchi yetu. Hili ni jambo la msingi sana kuweza kuangalia ili kuwafanya Watanzania waweze kufanya biashara na kwa hili nilikuwa naomba nimwombe Waziri aliangalie suala la *DRC* kwa mapana yake, tuna nchi nyingine wameiangalia *DRC very strategically*, wa *South Africa* wamejaa *DRC,* wanaangalia jinsi gani baada ya *stability* kurudi kwenye nchi, jinsi gani watakavyoweza kufaidika. Tanzania tuna mpaka mrefu sana na *DRC,* tusilale tukaangalia siasa tukashindwa kuweka mazingira ya kufanya nchi yetu kufaidika na soko hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufunguzi wa *consulate* ya Lumbumbashi, upelekaji wa *commercial attache* pale Lubumbashi ni muhimu sana ili kuweza kuunga mkono juhudi za balozi wetu pale na maafisa wengi katika kuhakikisha kwamba Tanzania inafaidika na uchumi ambao unakuja kwa *stable* wa nchi ya *Democratic Republic of Congo.(Makofi)*

Suala la pili ambalo nilikuwa napenda kulizungumzia ni suala zima hili la *COMESA,* nimeshtuka kidogo baada ya kuona kwamba katika hotuba ya Waziri hakugusia kabisa suala la uanachama wa Watanzania *COMESA.* Nimestuka kwa sababu tayari *stake holders,* wameshatoa ripoti ya kuonyesha ni jinsi gani ambavyo nchi yetu inapata hasara kwa kutokuwa uanachama wa *COMESA,* tayari na bahati nzuri, nimekuwa

*very consistency* toka mara ya kwanza nazungumza hapa Bungeni, kuchangia hotuba ya Rais na maswali yangu ndani ya Bunge, nimekuwa nikiomba na kusisitiza Serikali iangalie upya suala zima la Tanzania kujiunga na *COMESA.*

Wakati sipo, wakati nipo *DRC* swali langu liliulizwa hapa na Waziri akawa amejibu na sababu aliyoisema, kwamba naomba ni ninukuu: "Madhumuni, matarajio na viwango vya ushirikiano wa jumuiya hizi, akiwa na maana ya *COMESA, SADC, East Africa Community* na ile ya Ulaya, tofauti kutegemeana na sababu za kihistori." *(Makofi)*

Hatuwezi kuendelea kuwa watumwa wa historia, mambo yanabadilika, siasa sasa hivi haiendishi dunia na bahati mbaya sana, tulikuwa tuna nguvu sana ya kisiasa katika *SADC,* sisi ndio tulikuwa kimsingi *political power base*, tumenyang'anywa na *South Africa,* hatuna nguvu tena. Ni lazima tuangalie namna gani ambalo sisi tutaweza kuhakikisha kwamba tunaiweka ile nguvu yetu, vinginevyo Taifa letu litaendelea kuwa nyuma na kushindwa kupata faida ambazo zinatokana na jumuiya hizi.

Nilikuwa naiomba Serikali, *CTI* wametoa taarifa yao nzuri kabisa, kitabu kikubwa wame-*analyze* na kuonyesha ni viwanda gani ambavyo vinapata hasara kwa kuwa nje ya *COMESA.* Tumezungumza haya na Serikali imekaa kimya, haijatoa tamko lolote, nilikuwa naomba Serikali itueleze na kama hawajaipitia ripoti ya *CTI* sasa hivi baada ya mapumziko haya kabla ya jioni kuingia kwenye Kamati waipitie, waangalie ili waweze kutoa maelezo mahususi na mazuri kuhusiana na suala zima la nafasi ya nchi yetu katika *COMESA* ni lazima tulindwe, tujiangalie *our economic interest* zipo namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nilikuwa napenda kulizungumzia ni suala zima la majadiliano ya *EPA,* suala hili nalo pia bahati nzuri, nimekuwa *very consistency* katika hili toka tumeingia Bungeni, toka kuchangia hotuba ya Rais mpaka sasa. Nashukuru kwamba leo Waziri ameligusia, lakini ameligusia kwa uzito mdogo sana, amezungumzia *paragraph* moja tu kuhusu *EPA, paragraph* yenye mistari 19.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *EPA* sio suala dogo tunaenda kuzungumzia masuala ya *reciprocity* katika biashara, *reciprocity* maana yake ni kwamba sasa tunazungumzia *Everything But Arms(EBA)* kwamba tunapeleka bidhaa zetu Ulaya, bila ya kulipa kodi lakini kuanzia Januari 2008, watu wa Ulaya nao wanataka waingie wanataka waingize bidhaa zao nchi kwetu bila kulipa kodi, ndio maana ya *reciprocity*. Ni lazima hili jambo tuliangalie kwa sababu tafiti zote zinaonyesha kwamba tutapoteza asilimia ya 39 ya *customes duty* kutokana na kuingia kwenye *EPA,* wataalam wanasema hii ni *short term, in long term* nchi itafaidika zaida kwa hiyo *a decision* unakwenda kujali *EPA* kwenye kodi, ni *very* very *important decision*. *(Makofi)*

Lakini Serikali hili hailiangalii, katika jibu ambalo Waziri alilizungumza tarehe 14 Julai, 2006 alisema moja ya sababu ya sisi kuto *negotiate EPA* kupitia kundi muafaka ni hii hapa na nanukuu anasema: "Lakini Kenya na Uganda walijiunga na kundi la *ESA, EPA* na Tanzania ikaamua kujiunga na kundi la *SADC, EPA,* hivyo tu, kwa kuwa Kenya walienda *ESA* na Uganda basi na sisi tuliamua kwenda *SADC,* hakuna uchambuzi

wowote ambao umefanywa kuweza kuona ni wapi ambao tunafaidika na tafiti zinaonyesha na wataalamu wanatuambia na sijui ni kwa nini Serikali inapata kigugumizi, ni mambo mawili, aidha, tuka-*negotiate EPA,* kupitia *EAC,* tuwaombe wenzetu wa Kenya na Uganda watoke *ESA* tujadili kupitia *EAC* na bahati nzuri Burundi na Rwanda zinaingia *East African Community* au twenda tuka-*negotiate EPA* kupitia *ESA,* kwa sababu ndio eneo ambalo soko ni kubwa.

Sisi huku katika eneo la *SADC* kimsingi wanaojadili *EPA* ni nchi moja na nililieleza hili, kwa sababu nchi za *SADC* zinazojadili *EPA* ni saba, kati ya hizo nchi saba, nchi nne, ni wanachama wa *Southern African Customers Union (SACU)* ambayo iko *highly dominated* na *South Africa. South Africa* tayari inayo mkataba wa biashara huru na jumuiya ya Ulaya, kwa maana hiyo ni kwamba tunapoingia katika kundi hili, tunaenda kutekeleza mkataba wa soko huru ambao *TDCA* kati ya *South Africa* na Jumuiya ya Ulaya tunaenda kuwa soko la *South Africa,* tunaenda kujiuza kirahisi kwa *South Africa,* hili nashindwa kuelewa kwa nini wataalam wa Wizara hawalioni wakaishauri Serikali jinsi ambavyo inapaswa.

Mheshimiwa mwenyekiti, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri unipe majibu ya kina sana kuhusu hili leo jioni kwenye Kamati ya Matumizi, kwa sababu ni suala ambalo linahusu maslahi ya Taifa na ni lazima tulipe kipaumbele kinachotakiwa, sio suala la siasa tu hili, ni suala la maslahi ya Taifa letu kuanzia mwaka 2008 tunafanyaje biashara na *a giant like European Union*, tunawasaidiaje wafanyabiashara wetu na maamuzi mengi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, sio maamuzi ya Serikali haifanyi biashara, ni maamuzi ambayo tunayachukua kwa ajili ya wafanyabiashara, kwa kauli ya wafanyabiashara, lazima ni lazima isikike kuhakikisha kwamba mazingira yao ya kibiashara yanakuwa mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kwa hizi dakika mbili zilizobakia, kumekuwa na mazungumzo mengi sana kuhusiana na suala zima la Mchuchuma na Liganga, mazungumzo mengine ambayo yanaleta wasiwasi mkubwa katika nchi, mazungumzo ambayo kwa kweli unakuwa ni mjadala ambao unakuwa hauna mwelekeo ambao unatakiwa.

Jambo la msingi hapa ni kuweka maslahi ya nchi yetu mbele, kuna wawekezaji wengi ambao wanaomba kuwekeza katika eneo hili, lakini ni lazima tuangalie, teknolojia inayotakiwa sasa katika hii hatua inayoitwa hatua *at up stream* kule katika mradi wa Liganga inawezwa ikatekelezwa na *investor* yupi, hakuna sababu yoyote ya kuweza kung'ang'ania *investors* labda kwa sababu tu kuna mahusiano fulani yaliyopo, ni lazima tuangalie, tuweke maslahi ya nchi yetu mbele, tuweze kuona ni jinsi gani ambavyo *investor* ambaye anapewa pale, ataweza kuifaidisha nchi ili tuweze kuepukana na matatizo mbalimbali tuliyapata, huko nyuma. *(Makofi)*

Sasa mimi naomba niifungue macho Serikali, anaweza akaja *investor* ambaye hana uwezo wa teknolojia, hana uwezo wa fedha, hana uwezo wa kitaalam, tukasema huyu ni Mtanzania, tumpe Liganga, ukishampa tu na Tanzania ni mwanachama wa wanaita *MIGA,* ya kutatua matatizo ya wawekezaji, ukishampa tu anauza ule mgodi kwa

mtu mwingine wa nje, sisi tunampa kwa sababu tunataka aendeleze, hatumpi hata kwa gharama kubwa, yeye anaweza akamua kuuza kwa gharama kubwa na wala huwezi kumkataza kwa sababu inakuwa ni uhuru wake na tumeona biashara nyingi sana zina-*change hands* toka tulivyoanza shughuli za uwekezaji nchini. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba tuwe makini sana, tunao watu ambao tunaona kwamba wanaweza wakawekeza katika maeneo mbalimbali. Lakini kuna hatua ambazo wanaweza wakawekeza, tuwashauri wakawekeze katika hizo hatua muafaka, hatua hizi ambazo zinahitaji fedha nyingi, zinahitaji utalaam mkubwa, ni hatua ambazo zitumike kwa ajili ya faida ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa hii nafasi ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Kabwe Zitto.*(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kwa mchana wa leo tutaishia hapo, wazungumzaji wa jioni ya leo watakuwa ni Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya na muda ukiruhusu Mheshimiwa Aloyce Kimaro, atafuatiwa na Naibu Waziri dakika kumi na tano na Mheshimiwa Waziri atakuwa na saa moja kama kawaida. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi leo saa 11 jioni.

*(Saa 07.02 Bunge liliahirishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea pale tulipoachia saa za asubuhi, kuna wachangiaji watatu walioruhusiwa na Mwenyekiti nao ni Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, CHADEMA, Mheshimiwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, CCM na Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro, Mbunge wa Vunjo, CCM. Sasa nitamwita Mheshimwia Philemon Ndesamburo.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika hoja hii ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza ningependa kwanza niwarudishe nyuma kidogo Wabunge waelewe historia na Sera ya Biashara katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati tukipata Uhuru tulikuwa na wawekezaji katika nchi hii ambao tuliwaita ni mabepari. Mwalimu alitufundisha akasema walikuwa wana mirija mikubwa, walikuwa wananyonya nchi yetu na walikuwa siyo watu wanaofaa kukaa katika nchi hii na tukasema ubepari ni unyama. Tukaamua tukataifisha mali zao zote tukasema tutaanza upya na tukaanza kuwa na Vyama vya Ushirika ambavyo viliendesha biashara yetu na Mashirika ya Umma. Tukaendelea hivyo lakini mzawa wa nchi hii

Mtanzania hakupata nafasi ya kujenga biashara katika nchi hii, Mfanyabiashara wa nchi ilifika mahali mali zao zikataifishwa, majumba yao yakataifishwa ikawa kwamba ukifanya biashara wewe unakuwa ni mnyama na ni mnyonyaji. Ndiyo ilikuwa sera ya Serikali. *(Makofi)*

Tukafika mahali tukasema hatuwezi tukaendelea hivyo, tukasema sasa tutaleta sera ya Uwekezaji na Ubinafsishaji. Tulipoleta sera hii siyo ya kumkomboa Mtanzania tumejenga bomba kubwa ambalo linavyonza nchi hii linapeleka nje ya nchi. Ile mirija tuliyokata wakati ule wale tuliokuwa tunawaita ni mabepari na wanyonyaji tumewarudisha kwa njia ya nyuma sasa tukawajengea bomba kubwa na sisi tukiwa ndiyo tunawasaidia kujenga, wakaendelea kuinyonya nchi na mpaka sasa wanainyonya.

Mheshimiwa Spika, tukasahau kumsaidia Mtanzania mzawa, Mtanzania mzawa akabakia ni mtu anahangalia hajui nini kinachoendelea katika nchi yake hana zana, uwezo, hajui afanyaje biashara lakini biashara ikabaki katika mikono ya wageni na kila kitu kinachopatikana maana yake tusisahau mwekezaji wa nje anapowekeza hapa maana yake tunamjenga mtu wa nje ambaye ni mwenyeji labda wa Ulaya, Marekani, Canada na sehemu nyingine za nje na ananyonya anapeleka kwao sisi tunabakia hatuna kitu. Tukasahau kumjenga Mtanzania ambaye hana mrija wa kunyonya na hata akinyonya yatabaki humuhumu hakuna kitakachotoka nje utajiri wake utabaki hapahapa na ndiyo kitu nataka wakati Waziri akijibu atueleze Sera ya Biashara ya Tanzania inamuweka wapi mzawa wa Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaendesha biashara sielewi kwa misingi ya namna gani. Unazungumzia hapa shilingi milioni 500 ambazo tunataka kupeleka Mikoani za kwenda kuwapa wajasiriamali au kuondoa umaskini. Mimi nadhani tuna hisia mbaya za kuondoa umaskini, kuondoa umaskini siyo kujenga *machingas* katika nchi hii kila mahali, kuwajenga machinga katika barabara zetu siyo kuondoa umaskini, kuondoa umaskini katika nchi hii na watu wapate mlo ili waweze kuwa ni binadamu wa Tanzania tunataka wawe na kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tu-*create employment,* watu wapate kazi waweze kupata mlo, tu-*create employment* watu wapate chakula, unapogawa pesa kama njugu kwa vijana kupitia *SACCOS* ambazo tumesema zitaanza kukopesha, *SACCOS* kwanza hazina ujuzi, *SACCOS* hazina uwezo, *SACCOS* ni Vyama, Vikundi vya Kisiasa na pesa tutakazopeleka katika *SACCOS* zitapotea hakuna hata senti tano itakayorudi. Hivi ni vikundi vya Siasa vilivyopo na sasa hivi baada ya kutamka hapa Bungeni huko Mikoani watu wanajikusanya vikundi vikundi kungojea hizo pesa midomo iko wazi.

Sasa hii siyo sera ya kujenga na kuleta utajiri katika nchi hii kama pesa tunataka kuzitupa tuseme kweli tunakwenda kusaidia wapiga kura ili waweze kusema ahsante Seriakali yetu imetupa pesa. Lakini kama tulitaka kweli kuwawezesha watu ambao wanaweza kufanya biashara kwa nini hatutumii *Micro Finance Bank* yetu ambayo inajua *Micro Finance* wanajua *Micro Finance* lakini *SACCOS* hazijui *Micro Finance, SACCOS* hazina uwezo wa kufanya kazi ile.

Kwanza chimbuko la *SACCOS* ni vikundi vya mahali wanapofanya kazi watu pamoja kusaidiana kwenye mazishi na mambo mengine. Sasa unapokuja kuwachukua watu hawa na kuwaambia waanze kukopeshana pesa wafanye biashara, nani atafanya biashara kwa shilingi 50,000/= tuna matatizo tayari na *Machingas* katika Miji yetu tunasema *Machingas* wanaharibu barabara zetu, tunataka ku-*create* machinga wengi zaidi.

Kuna tatizo gani la Serikali kuwa na mkakati maalumu kwa kujenga matajiri ambao wanaweza kuanzisha viwanda na ku-*employ* watu katika nchi hii? Kwa nini hatujengi watu wenye uwezo kama tukiwa na watu kama Mengi kumi kila Mkoa, kama tukiwa na watu kama Mengi kumi au 15 kila Mkoa matatizo ya ajira nchi hii yatakwisha siku ile ile. Nasema kwa uhakika matatizo ya ajira yatakwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini huyu mzawa tunamwonaje? Kwa nini tunaogopa kum-*promote* mzawa? Kwa nini tunaweza kum-*promote* Mjerumani akija hapa anakuja na Kampuni yake lakini ni *individual* nchini kwao, yeye tunampa *facilities* zote, tunampa pesa, *tax relief,* tunampa kila kitu tunamsaidia. Kwa nini mzawa wa nchi hii tunakataa kumsaidia ili aweze kuwa na yeye ni mwekezaji mkubwa aweze kusaidia *unemployment* ya nchi hii ambaye hatatoa pesa zetu nje zile pesa zitabaki hapa na zitatusaidia. *(Makofi)*

Mimi naomba Waziri atakasimama atuambie Sera ya nchi hii ya Biashara itakayomsaidia Mtanzania kwa sababu tumepita kwenye mawimbi mabaya mpaka sasa sijaona mbele kama kuna mwanga kwa mfanyabiashara wa Tanzania. Kama kujenga Machinga ndiyo mwanga bila ku-*support* watu wenye uwezo ambao wanaweza ku-*employ* watu ambao ndiyo njia sahihi ya kuondoa umaskini. Tunadanganyana kwa kusema tuwape vikundi vidogo shilingi 20,000/= au 30,000/= halafu ndiyo wataondoa umaskini watauondoaje? Watauondoaje baada ya siku mbili ile pesa watakula watamaliza hakuna kitu huwezi kwenda hata kumdai kwa sababu palikuwa hakuna *collateral* katika kupata ule mkopo. Ni lazima tufikirie haya mambo kwa uzito zaidi na tuone je tunataka kweli kujenga nchi hii? Kama tutawajenga watu wa nje tukaacha kuwajengwa watu humu ndani tukasahau watu wa humu ndani tukajenga tu watu wa nje tunafika mahali pabaya.

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge nilisoma kwenye Magazeti, magazeti wakati mwingine yanatusaidia sana yanatusaidia kutuelimisha na kutuambia mambo ambayo hatuyajui. Nilishtuka niliposikia kuna Kampuni ya Mwananchi inafanya biashara ya dhahabu iko kimya kimya hatujui halafu Benki Kuu inakuwa ni mshiriki na hii Kampuni ni ya Siasa, Kampuni ya Mwananchi ni ya CCM. Je, sisi CHADEMA tukitaka *share* tutapewa? Kwa nini tunavuruga utaratibu wa biashara? Hii ni *scandal* mbaya kuliko hata *ile Gold Sera* ya Kenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika,tungeomba Waziri atuambie wakati atakapo *sum up* atumbie hii *Mwananchi Gold Mine* na wanaotajwatajwa maana yake magazeti yakizungumza yana ukweli tuweze kuelewa tujue kuna nini ndani kitu hiki lakini ni dhambi kubwa. Ni dhambi kubwa kama Chama cha Siasa kitakuwa *supported* na *Central Bank* ambayo ni ya Watanzania wote hii itakukwa siyo biashara itakuwa ni matani tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa labda nirudi kidogo kule Moshi kwenye Jimbo langu ninakotoka. Wakati wa kampeni wananchi wa Moshi wote waliambiwa na wakubwa wa nchi hii ya kuwa tarehe 1 Januari viwanda vyote vilivyokuwa vimefungwa kuna kiwanda cha Magunia, Karatasi, Mbao na kuna viwanda vingine chungu mbovu pale Moshi, wakaambiwa siku hiyo tarehe 1 kama mtamchagua Mbunge wa CCM viwanda vyote vitafunguliwa, sasa bahati mbaya nimechaguliwa mimi nataka Waziri aniambie kauli ile ilikuwa na maana gani? *(Makofi)*

Je, vile viwanda sasa vitafufuliwa au vitaachwa kwa sababu Mbunge ni Mpinzani? Tungetaka Waziri naye a-*elaborate,* ilikuwa na maana gani mazungumzo yale ambayo yalisemwa kwenye Kampeni, kwa sababu watu wa Moshi kwa sasa wanakusikiliza na wanataka kujua hatma ya biashara zao viwanda vyao vya Moshi ambavyo vimefungwa.

Mheshimiwa Spika, kuna viwanda siyo hivyo tu kuna kiwanda cha Magunia ambacho kilinunuliwa na *Mohammed Enterprises*. *Mohammed Enterprises* niliwahi kuzungumza nao wakasema kwamba kweli wako tayari kuanza kile kiwanda lakini tatizo ni kwamba hawezi kuuza magunia kwa sababu magunia yanayoruhusiwa kutoka nje yanauzwa kwa bei ya kutupa. Tutamsaidiaje mwekezaji huyu ambaye ana nia nzuri? Lakini akitengeneza magunia hawezi kuuza na viwanda vingine vingi vya namna hiyo vipo kwa sababu Sera ya Biashara haiko wazi kuonyesha tunalinda nini. Tunalinda maslahi ya watu wa nje au tunalinda maslahi ya Watanzania? Ni lazima tuwe wazi sera iwe wazi tujue tunamlinda nani katika biashara zetu za hapa Tanzania, *otherwise* tutakuja kukuta siku moja mali ya nchi hii yote tumeweka kwenye mabomba yanakwenda nje. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, bado naendelea msiwe na wasiwasi, bado naendelea.

Mheshimiwa Spika, mimi nimekuwa mstari wa mbele kila siku nikisema tuache hisia za kusema Watanzania ni maskini, nchi hii ni tajiri kuliko nchi nyingi sana katika Afrika. Tunawapakazia kila siku Watanzania ni maskini tena maskini tunawaondoa umaskini kwa nini hatuzungumzii utajiri wa Tanzania? Watanzania nchi yetu ni tajiri sana kama sera ni mbaya tufikirie upya tujue tufanye nini ili sera iweze kuwasaidia Watanzania hivi hatujatembea nje tukaona maskini? Wabunge wengi mmetembea, mmeona maskini katika dunia hii? Hivi Mtanzania naye mnamweka katika kundi la maskini? Mimi sidhani, kama tuna maskini ni wachache sana na kama tuna maskini ambao ni maskini ni ujinga wake kwa sababu hataki kufanya kazi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania mtu yeyote akitaka kupata atapata tu yapo maziwa na ardhi kila kitu kitu, sera yetu nzuri nchi ni imara, utawala mzuri, mtu unaogopa nini kufanya biashara? Unaogopa nini kufanya kazi? Nasema Sera ya Biashara inatufanya tuendelee kuwa maskini na mimi nataka Waziri leo atuhakikishie hizi Sera za danadana ziachane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kumalizia kwa hilo.*(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, sasa ni zamu ya Mheshimiwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya. *(Makofi)*

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu kuhusu Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda kabla sijasema ni vizuri kwa hili njitambulishe kwamba mimi nilishawahi kufanya kazi katika Wizara hii kama Naibu Waziri kwa muda wa miaka tisa, kwa hiyo, siwezi kusema maneno ya kubabaisha. *(Makofi)*

La pili ningependa kusema furaha yangu nina imani kwamba Waziri mwenyewe Mheshimiwa Nazir Mustafa Karamagi na Naibu Waziri wake wanaonyesha kama watasaidia sana kuleta mapinduzi katika Wizara hii na mimi nawatakia kila la kheri. *(Makofi)*

Sasa tulipopata Uhuru jambo la kwanza ambalo tulilikuta ilikuwa ni nchi zote za Kiafrika pamoja na Tanzania, tulikuwa tunawalimia wazungu mazao ili yakasindikwe kwao. Kwa hiyo, kwa leo hakuna kisingizio cha kuendelea kusema wazungu ni wanyonyaji kwa sababu ni juu yetu kujiondoa wenyewe maana ni nchi huru hatuna mtu wa kulaumu. Duniani unatakiwa mtu uanze na kitu rahisi usianze na mambo ambayo ni magumu.

Katika maendeleo ya nchi yetu kitu cha kwanza ambacho nitasema na ningependa ndiyo tukipe umuhimu wa kwanza ni usindikaji wa mazao ya kilimo na mifugo, haya ndiyo mambo tunayaweza kwa urahisi lakini yote haya hatujafanya na nitaeleza kwa nini hatujafanya.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, tumekubali unyonyaji wa biashara ambao si sahihi. Kwa mfano, nitatoa mifano kwa vitendo kama nilivyosema mimi nilishakaa katika Wizara ya Viwanda kwa hiyo najua. Usindikaji wa Matunda, Tanzania ina *climate* mbili yaani ina hali ya hewa mbili. Ina hali ya joto inaitwa *Tropical* na ina hali ya Nyanda za Juu. Kwa hiyo, ukitaka matunda yote yanayostawi katika hii dunia aliyoiumba Mwenyezi Mungu yanastawi Tanzania yote. Kama kuna mtu Wizarani anasema nimesema uongo, nikae, yeye asimame aseme Mheshimiwa Mzindakaya umesema uongo, matunda yote yanalimwa Tanzania. *(Makofi)*

Lakini kosa ambalo tumelifanya ni kwamba tumekubali kuwa nchi ya dampo kila kinachosindikwa nje kiletwe Tanzania na sisi tumeridhika. Kwa hiyo, kilimo chetu hakina tija kwa sababu tunalimia watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitatoa mifano hapo. Hapa nataka kuwaonyesheni hii ni *Orange juice* nzuri kweli lakini imetoka Kenya lakini machungwa yenyewe yametoka Tanzania. Kwa hiyo, sisi tunalima machungwa, tunalima *mango* kwa ajili ya Kenya kutengeneza *juice* waje kutuuzia sisi, sasa hii itaendelea mpaka lini? Ningeweza kuleta

makapu na makapu hapa kuonyesha tunavyoumia wenyewe na tunavyojiumiza wenyewe. *(Makofi)*

Hii ni *Tomato Sauce* inaitwa *Tropicana* hii ni ya Tanzania, ni nyanya za Iringa hizi na za Morogoro hii ni hongera. Lakini hawa hawajasaidiwa vyuo vingi ni hawa *Tropicana* na *Dabaga* Iringa. Kwa hiyo, hatujafanya hesabu ya mahitaji ya nchi hii ili tuweze kuwapa na kusema kutoka sasa hakuna kuagiza *Tomato Sauce* kutoka nje. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kabisa!

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Hivi inawezekanaje nchi hii huru miaka 40 tunaagiza *Tomato Sauce?* Ni aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninayo *Tomato Sauce* hapa, *Chilli Sauce* kutoka *Tropicana* Tanzania nzuri lakini pia ninayo *Chilli Sauce* kutoka Kenya, hii hapa. Nimeona nije kuonyesha hapa ili tuweze kuapa kutokana na aibu hii. Nimeshindwa tu kule nilikotoa vitu hivi kuna *Tomato Sauce* ya kutoka Canada, kuna mafuta ya kupikia kutoka Spain na nchi ya Spain mimi nimefika karibu nusu ni jangwa. Sasa Tanzania tunaagiza *Orange juice*, tunaagiza aina zote za *orange* iliyotengenezwa kama hii kutoka *South Africa.* Siyo hiyo tu ukienda madukani matunda kutoka nje kama *apples* zinatoka *South Africa* hivi hatuoni aibu? *South Africa* ni jangwa huwezi kulinganisha na ardhi ya Tanzania. Sasa mambo haya tusipoyakataa hayawezi kwisha kwa sababu sisi tunaoagiza tunaridhika na hii si bure ni pesa za kigeni.

Mbaya zaidi Waheshimiwa mnaona madukani, Arusha Tanzania wanalima maua na kuyauza nje, lakini bado Tanzania kuna maua bandia ya karatasi na tunatumia fedha za kigeni. Sasa ni sawa? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Si sawa!

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, vitu kama hivi mimi natoa ahadi mwezi Oktoba kutegemeana na majibu ya Waziri ikiwa tutaendelea kuruhusu maua Tanzania mimi nitaleta hoja mwezi wa Oktoba, 2006 kuzuia fedha ya wananchi ya kigeni kutumika kuleta maua kutoka nje, ni lazima tukatae baadhi ya vitu tunaweza tukasema hivi ni *priority* kwa nchi yetu bila kuagiza *Tomato Sauce* hii nchi itakufa? Tuulize hapa nchi itasimama? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Haisimami!

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, haiwezi kusimama! Bila kuagiza maua nchi itakufa? Haiwezi kufa.

La pili, kitabu cha Waziri kimeonyesha picha ya kiwanda kinachofanya *spinning* ya nyuzi za pamba katika hili hongera. Na ninaomba niseme mimi mwenyewe binafsi ndiye niliyesaini mkataba kule Japan na Kampuni ya *TOMEKA TOYOBO* kujenga kiwanda cha nyuzi cha Tabora, lakini tuulize tunahitaji viwanda vingapi? Tunahitaji vingi

kwa sababu sisi tumeshindwa kuingia *AGOA* kwa sababu bado tumekubali kupeleka pamba yetu nje.

Lakini leo hii kuna watu wanaagiza kitu kinachoitwa *Gray Cloth, Gray Clothing* ni nguo nyeupe iliyotengenezwa kwa pamba inakuwa haijamalizika yanakuja ni majora. Sasa yakija hapa wenye viwanda tunawasamehe kodi wanakwenda viwandani wanachapa khanga, wanapiga mihuri, *printing*. Kwa hiyo, vitenge na khanga tunazovaa ni *printed* kutokana na *cloth* au *Gray Cloth* kutoka nje, sisi ndiyo tungeuza nje ya nchi *Gray Cloth* na nyuzi.

Sasa mimi kwa kuwa nina imani kubwa sana na Serikali naomba tuletewe mpango hapa kwamba katika miaka mitano ijayo tutatengeneza tani ngapi za pamba kwa nyuzi na *Gray Cloth* tuachane na mambo haya ambayo ni ya zamani sana.

**MBUNGE FULANI:** Yamepitwa na wakati!

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Yamepitwa na wakati na mambo haya tunayaweza nani anasema hatuwezi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nisema tatizo, zamani Wizara ya Viwanda ilikuwa inamiliki viwanda, leo wamepunguziwa mzigo wa kumiliki wao wanasimamia Sera, sasa inatakiwa Serikali yenyewe tuseme wewe *Investor* ukija hapa itabidi uingie mkataba na wakulima wa pamba ili wewe utengeneze nyuzi. Wa mafuta vile vile.

Mheshimiwa Spika, juzi nimeona ajabu moja kuna gazeti nimesoma ninayo *cutting* hapa na ninafurahi Waziri Mkuu yupo hapa. Kuna wafanyabiashara wa Mafuta wanasema wanakwenda kumshitaki Waziri wa Fedha kwenye Bunge la Jumuiya, ni wajinga sana hawa, kweli. Kwa sababu mimi naweza kuwa-*scandalise* kwa sababu kuna watu wameingiza mafuta yasiyo *good oil* na hawakulipa kodi tukiweka *probe commit* kuna watu wataumia hapa itabidi walipe kodi ambayo hawakulipa.

Sasa mimi naomba wasiichokoze Serikali, mimi ni mwindaji na kwetu wawindaji wanasema hivi, ukimpiga nyati risasi ukamuumiza usimfuate, atakuumiza. Sasa unaweza kumpeleka Waziri wa Serikali hii nchi ni yetu hii na hao wanaotubabaisha wako watatu tu na wote *original* ni wafanyabiashara wa Kenya ndiyo wameng'any'ania *issue* ya mafuta. Mimi nikifanya utafiti hawa wataumia kwa sababu hawajalipa kodi, hawajalipa kodi na tunawaonea haya bure tu lakini naomba wanyamaze wasiponyamaza mwezi wa Oktoba, 2006 moto utawaka hapa, waache kabisa jambo hili. *(Makofi/Kicheko)*

Mimi ninao ushahidi kuna watu ninayo makaratasi wameagiza mafuta kutoka Singapore. Singapore hailimi mawese lakini yamekuja Tanzania wameya-*clear* kama ni *good oil* makaratasi mimi ninayo, wanataka niwaumize hapa? Waache kabisa mchezo huu, waache Mawaziri wetu wafanye kazi za maana na kodi ilipwe. Mimi katika hili ni kufa na kupona. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Sawa sawa! *(Makofi)*

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Kwa hiyo, mimi naomba Serikali iwaagize hawa kwenye viwanda vyote vya mafuta hivi ni *refine,* wana *refine* mafuta waagizwe waingie mikataba na Mikoa ya kulima *Oil Seeds*, Mawese Kigoma, *Sunflower* au Alizeti nchi nzima inalima.

Mheshimiwa Spika, leo mimi nazungumza Waheshimiwa Wabunge nafurahi kuwajulisha Sumbawanga peke yake Mkoa wa Rukwa tuna viwanda vidogo zaidi ya 30 vinavyosindika alizeti. Sasa waje tutawauzia ile *good oil* ya alizeti kutoka kwetu waje watengeneze katika Viwanda, kwa hiyo nimeona niseme hilo.

Mheshimiwa Spika, halafu vile vile nataka nirudie tena *juice* 90% ambayo Watanzania wanakunywa zinatokana na maji yaliyochemshwa, sukari, rangi, *citric acid* na *syrup* ndiyo *juice* mnazoziona huko madukani tunazokunywa.

Sasa ni lazima tunajiuliza hivi kwanini tutawanyweshaji wenye nchi nzuri na ardhi ya kutosha ma-*syrup* haya? Na pia ma-*chemicals* yanayochanganywa ile rangi siyo *orange* ni rangi tu mtu ni mtu wa viwanda najua. Wanaweka rangi halafu watu wanasema tunakunywa *juice*, siyo *juice* ile ni maji ya kuchemsha na sukari na rangi na vitamin. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumbe matunda yenyewe ya asili kwa kawaida chungwa lenyewe na mango yenyewe ina sukari na ina vitamin zote kuliko hata hata hii vitamini moja inayowekwa kwa madawa sasa watu wazima hatujajua hilo? Mimi nimeona niseme hili bila kuona haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu vile vile Tanzania ndiyo yenye chumvi Uvinza kuna chumvi na maji yote haya ya *Indian Ocean* yote ni chumvi lakini chumvi inatoka Arabuni inakuja inapita kwenda Kongo na Burundi na Rwanda ambao hawa chumvi.

Kwa hiyo, sisi ni wabebaji badala ya kutengeneza chumvi kutoka baharini na ile ya Uvinza tuuze sisi ni wabebaji wa kupeleka chimvi inayopita kutoka Arabuni kwenda nchi jirani, Mungu ametupendelea kweli.

Mheshimiwa Spika, nchi kama Zambia hawana chumvi, Congo yote ile wana dhahabu lakini chumvi hawana na huwezi kula bila chumvi, Burundi hawa chumvi na hata Uganda rafiki zetu hawana lakini sisi tunayo chumvi. Sasa mimi nasema tunangoja nini? Hilo nalo napenda niliseme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bidhaa za ngozi kwa mfano, tukazane. Mimi ningependa kuwapongeza wenzetu pamoja na Mheshimiwa Rostam Abdulrasul Azizi kile kiwanda cha Morogoro nilikuwa Mkuu wa Mkoa pale sasa hivi kinafanya kazi vizuri kweli, nzuri sana na mimi naomba niwapongeze kwa namna walivyokazana sasa wanaweza kutuondoa katika aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kwamba…

**SPIKA:** Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, kuna neno unalolitumia ambalo linaleta matatizo nadhani utalikumbuka. *(Makofi)*

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Tutajitahidi tutaongeza juhudi *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ningeomba *NDC* ibadilishe mwelekeo, *NDC* iwe ndiyo chombo chetu cha kusaidia katika uwekezaji hata wa ubia, ndiyo chombo tumebakia nacho cha Umma hiki. Miradi hii mikubwa mikubwa ya chuma hata mambo ya dhahabu na mengine *NDC* wao kwa niaba ya Serikali kwa sababu angalau *NDC* ipo na mimi ningependa tuwaunge mkono tuwasaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa naomba Mheshimiwa Waziri utamke neno hapa kuhusu suala la Mchuchuma maana yake ubishi ni mwingi juu ya jambo hili na wizara yako ndiyo inasimamia hebu tuelezee msimamo yaani tupeni msimamo ni nini?

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Dr. Mzindakaya kama kawaida mchango wako huwa daima ni wakusisimua ndani ya Bunge. Ahsante sana kwa hilo. *(Makofi)*

Msemaji wetu wa mwisho sasa ni Mheshimiwa Mbunge wa Vunjo Mheshimiwa Aloyce Kimaro. *(Makofi)*

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii angalau na mimi niweze kuchangia machache kwenye hoja hii ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko pamoja na Naibu Waziri wake pamoja na Watendaji wakiongozwa na Katibu Mkuu, Bwana Nyachia namfahamu ni mchapa kazi na ni mtu wa viwango na *standards* tangu zamani, haachi *file* likalala Ofisini kwake. Kwa hiyo, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nianze kwa maneno yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni kukuza uchumi na hatimaye kila Mtanzania awe na maisha bora. Hiyo ndiyo nia ya Serikali. Lengo hili linaweza kufikiwa kama tunaleta mapinduzi ya kilimo na baadaye mapinduzi ya viwanda na biashara. Hakuna nchi yoyote duniani ambayo imeendelea kama haina viwanda na haifanyi biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kufikia katika malengo, lazima tuandae vijana wetu, tuwasomeshe, tuwape malengo na baadaye waje kuajiriwa kwenye viwanda wakalete mapinduzi ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kufikia lengo hilo, ni lazima kuwe na mkakati wa kuwawezesha hawa Watanzania baada ya kusoma, leseni za biashara zitolewe kwa utaratibu unaoeleweka ambapo viwanda na biashara vitakavyoanzishwa lazima Watanzania wawe wabia. Tuwe na mikakati ya makusudi ya kutoa leseni kwenye biashara ambazo Watanzania wapo ndani, angalau kwa *percent one third.* Tutachukuaje hizi biashara kama hatutawapeleka Watanzania huko moja kwa moja kwa njia ya kuwawezesha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninasema hatuhitaji. Kule Kariakoo Wachina wamejaa, hawa Watanzania watafanya kazi gani kama tunaleta Wachina kuja kufanya biashara za maduka? Ukienda kwenye mbuga zetu za wanyama, mahoteli yaliyoko kule ni Wazungu watupu. Hivi wasomi tulionao wakiwezeshwa hawawezi kuanzisha hayo mahoteli! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiendelea na mtindo huu, Watanzania hawawezi kujikomboa na kujenga uchumi wao. Hata siku moja hatutafikia huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali inieleweshe viwanda ambavyo vilitaifishwa, baadaye tukatoka kwenye sera hiyo, tukaamua kuuza. Ni viwanda vingapi ambavyo vimenunuliwa na wageni moja kwa moja na viwanda vingapi vimenunuliwa na Watanzania moja kwa moja na viwanda vingapi vimenunuliwa kwa ubia kati ya Watanzania na watu wa nje? Je, viwanda hivyo vinafanyakazi? Mpaka sasa hivi ni viwanda vingapi vinafanya kazi?

Mheshimiwa Spika, walioajiriwa kwenye viwanda hivyo, tunasema tunatafuta ajira kwa Watanzania ili Mtanzania aweze kuwa na maisha bora. Akiajiriwa lazima apate mshahara mzuri wa kumwezesha kujikimu, kumpeleka mtoto wake Shule, kununua chakula na kumwezesha kidogo hata jioni anywe bia, haya ndiyo maisha bora. Utakuta nao njiani kila mtu anacheka, maana anaweza kumudu maisha yake. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, badala yake unakutana na Watanzania wanahangaika, mishahara midogo, lakini viwanda vipo. Hawa wawekezaji watakuja kuchuma hapa, wanalipa mishahara midogo, lakini fedha kama alivyosema Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, tumeweka bomba linanyonya, bomba linapeleka tu, lakini tunabakia hatuna kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu maonesho ya biashara, ni kazi ya Serikali kuhakikisha kwamba wazalishaji wa hapa nchini wanatangazwa. Kuna Maonyesho ya Dar es Salaam *International Trade Fair*. Yale maonyesho mara nyingi unakuta wengi ni wageni, lakini biashara inayofanyika pale inakuwa kama gulio, kununua na kuuza, hakuna mikataba inayowekwa pale, mikataba endelevu ya miaka mingi. Hata bidhaa zetu za Tanzania hakuna mikataba inayoingiwa pale ambayo itatuwezesha sisi kuuza bidhaa zetu nje. Sasa naomba Wizara isaidie sana katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, yako maonesha yanafanyika, nilikwenda katika maonesho ya Ujerumani, Hanover, nimekwenda maonesho Japan Osaka, nimekwenda maonesho makubwa sana China, unakutana na Maofisa wa Serikali kama wamekwenda kutembea, wanaacha kuwapeleka wafanyabiashara na wazalishaji, wanakwenda wao kutembea.

Nimekutana na akina mama wanaouza vinyago na batiki, ndiyo nimekutana nao Japan, nimekutana nao *Hanover*, wamebeba vinyago na batiki, bila msaada wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba Serikali iweze kuonesha sera yake katika hilo ni nini? China kuna maonesho ya mwezi mzima, bidhaa zote za China, nilikutana na vijana kutoka kule Kariakoo, wanahangaika wenyewe kule, lakini Serikali haiwasaidii katika hilo ambao ndiyo ungekuta wanasaidiwa, wanawekewa sera ambazo zitawawezesha hawa vijana wakienda kule baadaye watakuja kuanzisha viwanda vyao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la viwanda vidogo vidogo *SIDO*, sioni tena kupewa kipaumbele mpaka sasa hivi. Hata ukiangalia kwenye Bajeti wametengewa fedha kidogo sana na huwezi kuanzisha viwanda vikubwa kama hujaanza na viwanda vidogo na utundu unaanzia kwenye viwanda vidogo. Sasa naiomba Serikali, hilo lipewe kipaumbele, maana ndiyo linaleta ajira *direct*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni biashara ya Afrika Mashariki. Walisema hapa kwamba angalau tumejitahidi kuuza bidhaa Kenya, tunauza kidogo sana, Kenya ndiyo wanafanya Tanzania ndiyo soko lao.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wakitaka kupeleka vifaa Kenya, kule mipakani gari linaweza kukaa kwa muda wa wiki mbili, wanazunguka zunguka tu ili usirudie tena. Hizo zinaitwa *non tariff barriers* ambayo ni uchafu wa biashara. Lakini Serikali inatusaidia nini katika hilo? Ningeomba Wizara itoe jibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wako wanaotaka kuleta bia, kuna mikataba ya siri siri kwamba ee bwana, kwa sababu tumenunua kiwanda kilichokuwa pale Moshi, sasa nyie mtazalisha bia ya Kenya hapa Tanzania, lakini msiilete huku Kenya hata ile ya Tanzania msiilete, mkitaka kuileta mtuambie sisi, tutakuja kununua sisi. Maana yake ni *quota system.*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kwa sababu tumesharidhia makubaliano ya *East African Community*, naomba Serikali itoe tamko, hiyo mikataba ya chini chini ifutwe mara moja, watu wawe huru kufanya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine nitazungumzia suala la ukaguzi wa magari yanayotoka nje ambapo *TBS* ndiyo inateua Wakaguzi. Dubai kuna mkaguzi, Hong Kong kuna mkaguzi, Japan kuna Mkaguzi, Singapore kuna Mkaguzi.

Mheshimiwa Spika, hawa Wakaguzi wanapoteuliwa, kuna dalili *hundred percent* ya rushwa. Kwa sababu hakuna matangazo, hakuna *transparency,* unasikia anayekagua ni fulani. Huwezi ukawa mkaguzi mpaka labda umjue Mkurugenzi Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, nataka sasa Serikali iseme Mkaguzi kwenda Dubai alipatikana kwa tangazo gani na kikao gani kilimchagua na walikuwa wangapi na vigezo gani vilitumika?

La pili, aliyeteuliwa Mkaguzi wa Hong Kong, ni vigezo gani vilitumika? Mwaka 2004 aliteuliwa mmoja, akaenda enda akafutwa; mwaka 2005 akateuliwa Mkaguzi mwingine, akafutwa na mwaka huu wa 2006 sijui mwezi uliopita Julai, ameteuliwa Mkaguzi mwingine.

Mheshimiwa Spika, haya matangazo yanakuwa wapi ili na Watanzania nao waombe? Kwa nini fedha yetu inakwenda kubaki huko nje? Serikali itoke tamko. Kama hao Wakaguzi waliteuliwa nje ya utaratibu, uteuzi wao ni batili. Tuanze upya. Hiyo ndiyo *transparency* na ndiyo utawala bora. Kila mtu aelewe nini kinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, utoaji wa leseni. Leseni zingekuwa *centralized* zitolewe na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kama ilivyo *BRELA,* inaandikisha Makampuni yote Tanzania nzima, sasa unakuta Wizara ya Miundombinu inatoa leseni, Wizara ya Maliasili na Utalii inatoa leseni na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko inatoa leseni.

Mheshimiwa Spika, naomba ili kuwe na udhibiti, leseni zote zitolewe na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Wizara nyingine zitoe ushauri, ziseme huyu kufuatana na mipangilio yake ndiyo anafaa kupewa leseni.

Kwa hiyo, aende na maandishi tu kule. Sasa kuwe na *central pool* pale Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ya kutoa leseni na kudhibiti leseni zote za biashara Tanzania nzima. Isipokuwa zile leseni ndogo ndogo zinazotolewa na Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii. Lakini hayo masuala niliyoyasema ninataka yajibiwe. Bila hivyo, nitakwenda kwenye vifungu wakati wa Kamati ya Matumizi. Ahsanteni sana. *(Makofi/Kicheko)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. GEORGE M. LUBEJELE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri, yenye ufafanuzi mzuri kuhusu Sekta ya Viwanda, Biashara na Masoko.

Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayofanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ujenzi wa masoko, kwa kuwa Wilaya ya Mpwapwa inazalisha sana zao na karanga, alizeti na ufuta: Je, ni lini Serikali itawajengea soko la uhakika la kuuza mazao yao wateuliwe wa Wilaya ya Mpwapwa? Kujengwa kwa

soko hilo kutawahamasisha zaidi wakulima wa Wilaya ya Mpwapwa, kuzalisha zaidi mazao haya. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga viwanda vidogo vidogo vya kukamulia mafuta ya karanga, alizeti na ufuta.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Watanzania wengi na wakiwemo wa Wilaya ya Mpwapwa Mkoa wa Dodoma, kwa ujumla wangependa kujenga nyumba bora, lakini kwa kuwa bei ya mabati na saruji ni kubwa sana: Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza bei ya mabati na saruji ili watu wengi na hata wale wa kipato cha chini waweze kujenga nyumba bora? Je, viwanda vinavyobinafsishwa hapa nchini, vimeongeza ajira asilimia ngapi ikilinganishwa na hali ilivyokuwa mwanzo kabla ya kubinafsishwa na Serikali imeweka mikakati gani ya kuviendeleza viwanda hivyo ili kuleta tija kwa Taifa letu? Ukaguzi wa viwanda ufanyike mara kwa mara ili kuhakikisha kwamba waajiri wanalipa wafanyakazi wao ujira unaolingana na kazi wanazofanya, pia huduma za afya zidumishwe na kuboreshwa viwandani.

Baada ya mchango wangu huo, natamka kwamba, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niungane na wenzangu kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii kwa mashirikiano yao mazuri yaliyoiwezesha Wizara yao kuwasilisha hotuba na Bajeti katika Bunge hili Tufuku kwa majadiliano.

Mheshimiwa Spika, bei ya saruji na bati iko juu sana hapa nchini ukilinganisha na nchi nyingine. Kwa kuwa bidhaa hizi mbili ni muhimu sana katika ujenzi wa nyumba bora kwa wananchi wetu na kwa kuwa kauli mbiu yetu ni maisha bora kwa Mtanzania, kuna sababu zipi za msingi zinazozuia kuwaruhusu wafanyabiashara kuingiza saruji na bati nchini ili wauziwe wananchi wetu kwa bei nafuu kuliko ilivyo sasa? Licha ya kuwa na viwanda kadhaa vya bidhaa hizo hapa nchini, lakini bei zake ni za juu sana. Wakati umefika kwa Serikali kuwaruhusu wafanyabiashara kuingiza bidhaa hizo (saruji na bati) nchini badala ya kuendelea kulinda bidhaa zinazotengenezwa hapa nchini ambazo ni ghali sana na zinarejesha nyuma kauli mbiu ya maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, saruji na bati kutoka nje ni bora na bei yake itakuwa nafuu ukilinganisha na zile za bidhaa za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kupongeza Wizara kwa Bajeti nzuri kwenye baadhi ya maeneo inayosimamia. Maeneo mengine, baadhi nitayaelezea hapa chini, yanahitaji maelezo ya ziada. Kwa kipindi kirefu Serikali imelichukulia Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC)* kama chombo cha kuendeleza na kusimamia viwanda vya msingi. Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 inatamka kwamba Serikali, pamoja na mambo mengine, itaongeza uwezo wa *NDC* katika kuongeza juhudi za uanzishaji wa viwanda mama.

Hivyo basi, *NDC* ni chombo nyeti katika azma ya Taifa ya kujenga viwanda mama kama msingi wa mabadiliko ya mfumo wa uchumi. Lakini Bajeti ya Wizara haionyeshi umuhimu wa shirika hilo ambalo linaachwa kuwa tegemezi wa misaada ya wafadhili. Katika makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2006/2007. *NDC* haionekani kabisa kuongezewa nguvu na Serikali, licha ya kwamba inasimamia utekelezaji wa miradi mikubwa mingi kama Mchuchuma, Liganga, *Lake Natron* (Magadi), utekelezaji wa Kanda ya Maendeleo ya Mtwara na kadhalika.

Pili, katika taarifa yake kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini, kwa mwaka wa fedha 2006/2007, Kamati ya Uwekezaji na Biashara ilisisitiza kuwa mchakato wa kumpata mwekezaji au wawekezaji kwenye miradi mikubwa ya Mchuchuma na Liganga uzingatie mambo manne.

(a) Uwazi katika kuitisha na kuteua mwekezaji/wawekezaji;

(b) Uwezo wa kitaalam wa kuchimba na kuchenjua madini aina mbalimbali yatakayochimbwa;

(c) Uwezo kifedha; na

(d) Uzoefu katika kufanya shughuli hizo.

Mheshimiwa Spika, masuala hayo manne na mengine yamesisitizwa katika ripoti ya Kamati ya tarehe 12 Aprili, 2004 kuhusu ziara yake Wilayani Ludewa iliyofanyika tarehe 9 na 10 Aprili, 2006. Wabunge tunavunjwa imani tunaposikia tetesi za upendeleo bayana katika mchakato wa kumpata mwekezaji/wawekezaji. Tetesi za namna hiyo, hata kama sio za kweli, zinavunja imani ya wananchi kwa Serikali yao na kwa Bunge ikiwa Wizara haitoi na tamko la wazi na bayana kuhusu mchakato huo na tahadhari zinazochukuliwa kuhakikisha kuwa hakuna upendeleo wa aina yoyote.

Wajumbe wa Kamati wa Uwekezaji na Biashara, tunaunga mkono juhudi za Wizara, lakini suala la Liganga na Mchuchuma lisituweke njia panda. Dawa ni uwazi na kutenda haki inayoonekana. Wanasheria wanao msemo: *"Justice should not only be done, but should also be seen to be done*." Haki itendeke, lakini vile vile ionekane kuwa inatendeka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja na nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara na Mashirika yaliyo chini ya Wizara. Nampongeza kwa kazi nzuri inayofanywa na *SIDO* nchini. Naomba *SIDO* ianzishe Kituo cha Viwanda Makambako kutokana mahali Makambako ilipo na kasi ya ongezeko la wakazi pale Makambako.

Mheshimiwa Spika, katika ujenzi wa soko la Makambako, Wilaya imetenga ekari 300 Makambako na huu ni mwaka, tangu eneo litengwe. Umeme wa *grid* unashushwa Makambako, ni njia panda kuu na lango kuu.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ioneshe ratiba ya ujenzi na soko na nani atahusika na uchoraji wa ramani ya soko hilo. Watalaamu wa Wizara watembelee Makambako *site* mapema. Kama jibu la swali lilivyoeleza kuwa Shilingi milioni 120 zimetengwa kwa ajili ya Masoko ya Segera.

Mheshimiwa Spika, mbona habari za Segera na Makambako zimezimwa wakati uamuzi ulikwishatolewa? Tuelewe vipi? Hotuba haisemi lolote. Tafadhali naomba jibu la swali langu kuhusu soko la Makambako lilikuwa wazi. Vipi suala hili linasahauliwa au kupuuzwa? Wananchi watuelewe vipi? Ekari 300 zimetengwa, Waziri Kahama alitamka katika hotuba yake na kufika Makambako. Je, hizo zitafanya kazi gani? Ipo haja ya kujenga soko hilo kwa *Phases* ili wananchi waone vitendo. Halmashauri ya Wilaya ifanye nini zaidi katika suala hili ili kuwe na vuguvugu katika ujenzi? Napendekeza Wizara licha ya kujenga soko la Kimataifa Makambako, iwe na mkakati rasmi wa kuwa na *Zonal Agro-processing Centres* ili kuhakikisha ujenzi wa viwanda nchini.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie. Kabla, sijaanza, naomba kuwarudisha Waheshimiwa nyuma kidogo, ili wafahamu tulikotoka na tunakokwenda, kufuata sera ya biashara katika nchi yetu. Tulipopata uhuru, palikuwepo na Wawekezaji wakubwa tuliowaita mabepari. Waliweka mirija yao hapa na kunyonya wakiwa mbali, uchumi wetu na tukakataa, kunyonywa tukataifisha miradi yao yote na kukata mirija yote ya unyonyaji. Tanzania nzima tuliimba ubepari ni unyama na utajiri ni ujamaa.

Mheshimiwa Spika, baada ya muda siyo mrefu. Tukataifisha majumba na kuwafilisi karibu wafanyabiashara wote kwa kuwa tuliamini mfanyabiashara yoyote yule ni mnyonyaji. Misingi ya biashara ikawa imefutwa yote na kila biashara ikawa inaendeshwa na vyombo vya Umma.

Mheshimiwa Spika, tukaanza na Vyama vya Ushirika na Mashirika ya Umma, lakini hayakuchukua muda, Mashirika yakalegalega na Vyama vya Ushirika vikafa. Serikali ya Awamu ya Pili, itaanzisha biashara ya uwekezaji na ubinafsishaji. Kule nyuma, tulikata mirija, sana tukaanza kujenga mabomba makubwa ya kuimaliza nchi kupitia uwekezaji na ubinafsishaji. Badala ya mirija, sasa tuna mabomba yanayonyonga kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, mzawa wa nchi hii bado yuko kama mtazamaji, ubavu wa kujiingiza kwenye biashara hana. Kwanza ameshajazwa hisia za ubepari ni unyama. Mtaji hana, nyenzo hana.

Mheshimiwa Spika, tunavyo vyombo vya fedha vyenye uzoefu wa kukopesha; *NMB* ilianzishwa kwa ajili ya kutoa mikopo midogo midogo kwa wazawa. Lakini, hii Banki haitoi huduma ya *Macro financing*. Badala yake inafanya *High Steel Banking*.

Badala ya kuitumia hii benki, tumeanza kutumia *SACCOS* ambazo hazina uzoefu wala ujuzi. Tunazungumzia Shilingi milioni 500 zitakazotolewa Mikoani, hizi zitapitishwa kwenye *SACCOS* na kwa hakika, ni sawa na kusambaza njugu na kwa hakika, zitaleta uhasama au vurugu nchi nzima. Nasema hivyo kwa kuwa hizi *SACCOS* zote zina itikadi. Kwanza chimbuko la *SACCOS* ni vyama vya kukopeshana na ni vya wafanyakazi wa sehemu moja moja.

Mheshimiwa Spika, kuna hili jambo la kiwanda cha kusafisha dhahabu. Cha kutisha *Company* hii ni mali ya Chama cha Siasa, CCM. Iweje Benki Kuu ya Watanzania wote iwekeze kwenye *Company* hii? Ni kashfa kubwa kupita hata ile ya *Goldberg* ya Kenya. Watanzania wanataka wajue ukweli wa jambo hili. Mwandishi maarufu Makwaiya wa Kuhenga katika kipindi cha "Je, tutafika?"

Mheshimiwa Spika, tunapokaribisha Wawekezaji moja kwa moja, tunajenga matajiri. Hawa ni watu wa nje, tunazidi kupanua bomba la kuinyonya nchi yetu. Sasa Mheshimiwa Waziri, umefika wakati, tuwe na mtazamo mpya wa kuwajenga wazawa wa nchi hii. Tukimjenga mzawa mmoja ni bomba linalovujia humu humu ndani, halivuji nje. Hii sera ya kujenga mabomba yanayovujia nje ya nchi yetu ni hatari sana kwa uchumi wetu. Mheshimiwa Waziri angebuni mkakati maalum wa kujenga matajiri wazawa, angalau kumi kila mwaka na kama tunaweza kuwa na akina Mengi angalau watano kila Mkoa, hali ya uchumi wa nchi yetu ingegeuka vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, wakati wa Kampeni za mwaka 2005, Mheshimiwa Sumaye, Waziri Mkuu Mstaafu, alisema kwenye kampeni: "Mkimpa Mbunge wa CCM mwezi wa Januari 2006, Viwanda vyote hapa Moshi vitafufuliwa." Je, sera ya biashara ina ubaguzi wa itikadi? Mbona mpaka sasa hivyo viwanda havijafufuliwa? Ni kwa kuwa Mbunge wa Moshi Mjini sio wa CCM? Wakazi wa Moshi wanamwona na kumsikiliza Mheshimiwa Waziri atawaambia nini juu ya hivyo viwanda walivyovifunga.

Mheshimiwa Spika, moja ya viwanda vya Moshi vilivyofungwa ni kile cha Magunia. Lakini kufugwa kwa kiwanda hiki ni ubovu wa sera ya ubinafsishaji. Hapa *Mohamed Enterprises* anapewa kiwanda, azalishe magunia kwa malighafi ya hapa hapa kwetu na wakati ule ule wanaruhusu uingizaji wa magunia kutoka nje kwa bei ya kutupa, unatazamiaje huyu mwekezaji azalishe? Haiwezekani, iko kila sababu ya kuiangalia upya sera ya kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004 nilitumwa na wafanyakazi wa Kiwanda cha Madawa Moshi, kuwaulizia, mafao yao baada ya kiwanda kubinafsishwa. Nilijibiwa na Naibu Waziri wa Viwanda kuwa watalipwa haki zote. Mpaka hivi leo, hawa ndugu zangu, bado hawajalipwa na wamemwandikia Waziri Mkuu juu ya haki zao na *copy* nikampatia Mheshimiwa Waziri, lakini hadi sasa sijapata majibu la kuwapa, hawana wafanyakazi. Tafadhali, wakati wa majumuisho nipatiwe jibu sahihi la kuwapa.

Mheshimiwa Spika, kila siku tunahubiri kuwapa wananchi mikopo midogo midogo. Hivi kweli unaanza vipi biashara na Sh. 50,000/=? Mbona sera hii itajenga Machinga kila pembe ya hii nchi? Hata hivyo, Machinga wanafanyabiashara zao

pembezoni mwa barabara na kutembeza biashara zao kwa mikono. Je, huku ndio kujenga biashara? Hapana. Tujenge matajiri wachache waweze kutoa ajira kwa wengi.

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa tena nafasi hii.

**MHE. MGENI J. KADIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwa na afya njema na kuniwezesha kuchangia hotuba ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa umahiri wake na utendaji wake wa kazi pamoja na Naibu wake na Wenyeviti wake wote nao, wanastahili kupongezwa. Nampongeza Waziri pamoja na Naibu Waziri na timu yake kwa kuweza kuchangia hotuba hii na kuifanya iwe nzuri na iliyo na mwelekeo mzuri na upana. Naipongeza Kamati pia kwa kazi yao nzuri na wote walioshiriki katika kuchambua hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, sasa naanza hoja hii ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa mashamba ya mpira yaliyoko Kihuhwi, Muheza pamoja na Zanzibar. Mashamba haya hayaendelezwi inavyostahili kutokana na upungufu wa malighafi kwa ajili ya kiwanda cha *General Tyre.* Kwa hiyo, kiwanda hiki kinataka kiongezewe mtaji ili kiboreshwe.

Pia, kupatikane malighafi ili viwanda vipate viwango bora vya biashara na ili vipunguze uingizaji wa mpira kutoka nje. Vile vile, wale waajiriwa wapate tija na maslahi yao mazuri katika maisha yao, kwani inaonekana kama ni biashara iliyokuwa haina soko la uhakika mfano kama Pemba, zao hili ni kubwa sana, lakini kutokana na waajiri kutolipa kipaumbele, mpira mwingi hupotea kwa kusafirishwa nje ya nchi kwa njia ya magendo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa kupitia Wizara hii, nashauri Serikali iongeze viwanda na malighafi ipatikane kwa kiwango kikubwa na Zanzibar nayo wawekeze katika viwanda ili Watanzania nao waendeleze biashara hii.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali itoe ufafanuzi kuhusu uchimbaji wa gesi ya Songosongo na ujenzi wa kiwanda cha mbolea, kwani tukijengewa kiwanda hicho cha mbolea kitafanya wakulima kupata faraja kwa kupata mazao mengi ya biashara na mazao ya chakula cha kutosha kwa kutumia wataalam wetu tulionao na kupunguza ongezeko la bei ya kununulia mbolea kutoka nje au kutegemea kiwanda kimoja tu kilichopo Tanga.

Mheshimiwa Spika, naitakia mafanikio mema Wizara hii. Kila la kheri.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, naleta maandishi haya kwa lengo la kuunga mkono hoja. Hata hivyo, ninahitaji Serikali inipe majibu ama ufafanuzi kwa yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, buni ni zao la muda mrefu katika Mkoa wa Kagera. Zao hili ni maarufu kwa jina la Kahawa (Kahawa ni *product* siyo mti).

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mingi sasa Chama cha Ushirika cha *KNCU* kimeshindwa kukidhi haja ya kuwalipa bei nzuri ya zao la Kahawa. Vyama vya Msingi vinawahi kufungua msimu wa kununua Kahawa, lakini bado wanawakopa wakulima. Je, ni lini Serikali itaviwezesha Vyama vya Msingi ili viache mazoea ya kukopa mazao ya wakulima?

Mheshimiwa Spika, hii izingatie ukweli kwamba wanunuzi binafsi wanayo ruhusa ya kununua mazao ya wakulima kwa kuwafuata majumbani na kuwalipa fedha taslim papo kwa papo. Tena wanaongeza kidogo bei kulinganisha na bei ya Vyama vya Msingi. Katika hali hii, Serikali inategemea kweli wananchi wataacha kuwauzia wanunuzi binafsi ikisubiri kupanga foleni na kukopwa na Vyama vya Msingi vya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, je, sio wakati muafaka sasa kuwaruhusu wananchi waanzishe *SACCOS* za kununua mazao yao washindanishe Vyama vya Msingi katika wanunuzi binafsi? Aidha, Serikali inieleze ni lini itawakomboa wakulima wa zao la Kahawa wa Mkoa wa Kagera? Usindikaji wa buni, kuwa Kahawa nayo ni hatua ambayo haijawa na nguvu kwa kiwango cha kuongeza bei ya wakulima. Serikali isaidie sasa Kahawa isindikwe na izalishwe kwa wingi ili kumpa mkulima bei nzuri na kwa wakati, asikopwe.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali inieleze wanavyofaidika wananchi wanaozunguka Ziwa Victoria upande wa Tanzania, kwani sasa Ziwa Victoria linatoa samaki kwa wingi na kwa msingi huo, linaongeza Pato la Taifa. Ukienda visiwa vya ndani ya Ziwa Victoria katika upande wa Muleba, kuna wavuvi wakubwa, lakini hawana Shule, hawana Zahanati na hawana huduma nzuri ya mama na mtoto. Je, ni lini Serikali itahakikisha nao wanapata huduma hizi muhimu?

Mheshimiwa Spika, naiomba pia Serikali isaidie kueneza huduma ya viwanda vidogo vidogo kwa wakulima wa mazao madogo madogo ya matunda ili kusindika na kuuza. Hii itawasaidia hata kuendelea kuwa na kipato wakati ambao sio wa msimu mfano nanasi, nyanya, machungwa, ndizi mbivu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu kufa kwa kiwanda cha Zana za Kilimo (*ZZK* – Mbeya). Tangu kufa kwa kiwanda hiki mwishoni mwa miaka ya 1990, kunafanya zana nyingi za kilimo zilizokuwa zinazalishwa kiwandani hapo kuwa na bei kubwa sana. Baadhi ya zana hizo ni kama vile majembe ya kukokotwa na maksai, mejembe ya mkono, matoroli, mafyekeo, mikokoteni ya kisasa kabisa na kadhalika. Hivi ni sababu gani hasa zilizosababisha kufa kwa kiwanda hicho muhimu kwa wakulima hasa wale wa Kanda za Nyanda za Juu Kusini na je, Serikali kupitia Wizara hii ina mpango gani wa kuanzisha kiwanda cha aina hii kupitia kwa wawekezaji?

Mheshimiwa Spika, bei ya saruji ni kubwa sana nchini. Bei hiyo haimpi Mtanzania wa kawaida nafasi ya kujenga nyumba bora ya kuishi. Kwa wastani, bei ya saruji nchini kwa sasa ni kati ya Sh.10,000/= na Sh.15,000/= kwa mfuko mmoja. Ni Watanzania wangapi wataweza kununua saruji kwa bei hiyo?

Mheshimiwa Spika, kinachosikitisha zaidi ni kwamba, bei ya saruji inayozalishwa Mbeya ni ghali sana na kwa kweli wananchi wa Mbeya na wale wa jirani hawaoni maana na faida ya kiwanda hicho. Inakuwaje bei ya saruji inayotengenezwa Tanga au Dar es Salaam iwe na bei sawa na saruji ya Mbeya katika soko huko Mbeya? Pili, kwa nini bei ya saruji Mbeya iuzwe kwa bei ndogo Mikoa mingine kuliko Mbeya inakozalishwa?

Mheshimiwa Spika, ili kuwapa wananchi uchaguzi zaidi wa saruji na ili kuleta ushindani katika eneo hili, ni vizuri Serikali iruhusu watu binafsi waagize saruji nje ya nchi. Nina hakika ushindani huu unaweza kusaidia kupunguza bei ya saruji nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kiwanda cha saruji na uchimbaji wa udongo (malighafi) Mbozi, kiwanda cha saruji hutumia aina fulani ya udongo unaotumika kama malighafi katika uzalishaji wa saruji. Udongo huo huchimbwa katika eneo la Kijiji cha Mahenge, Kata ya Myorizi – Mbozi. Ninachopenda kujua hapa ni: Je, wananchi au Serikali ya Kijiji hicho au Halmashauri ya Wilaya Mbozi inafaidikaje na uchimbaji wa udongo huo?

Mheshimiwa Spika, bei ya bati katika nchi hii ni kubwa sana na inakatisha tamaa. Kama ilivyo kwa saruji, bei ya bati haimpi Mtanzania wa kawaida nafasi ya kujenga nyumba bora. Hivi maisha bora kwa kila Mtanzania yanayozungumzwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi (2005 – 2010) yatapatikana kwa wananchi kuendelea kuishi kwenye nyumba za udongo na nyasi? Ni nini mkakati wa Serikali na Wizara kudhibiti bei ya bati?

Mheshimiwa Spika, kuhusu soko la zao la Kahawa, hivi karibuni Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward N. Lowassa, alikutana na wadau wa zao la Kahawa. Ili kumpa mkulima wa zao hilo uwezo zaidi wa kuzalisha, Waziri Mkuu aliagiza kwamba mkulima asilipwe chini ya asilimia 75 ya bei katika Soko la Dunia. Ili kwenda sanjari na maelekezo ya Waziri Mkuu: Je, Wizara hii imejiandaa namna gani ili kuhakikisha kwamba mkulima hauzi Kahawa au zao lingine lolote la biashara chini ya asilimia 75 ya bei katika Soko la Dunia? Ningependa pia kujua Wizara inadhibiti namna gani ununuzi holela wa zao la Kahawa hasa katika Wilaya ya Mbozi?

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alizindua kiwanda cha utengenezaji wa mbolea cha Minjingu Mkoani Arusha. Ninachotaka kujua ni kwamba, ni mbolea gani zitakazozalishwa katika kiwanda hicho? Je, mbolea zitakazozalishwa kiwandani hapo zitakidhi mahitaji ya mbolea muhimu? Kama jibu siyo, Serikali ina mpango gani wa kuita wawekezaji wengine katika eneo hilo?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja. Pia, napongeza kwa Bajeti nzuri inayoeleweka. Pamoja na kuunga mkono, ninatoa maombi yafuatayo: -

- Serikali iangalie uwezekano wa kusaidia wafanyabiashara wadogo nao wapewe msamaha wa kodi na leseni. Wakati wanapoanza kufungua biashara, *TRA* huwa haiwapi nafasi yoyote ya kujiimarisha. Wapewe msamaha angalau wa miezi sita ili wazalishe ndipo waanze kulipa kodi. Wawekezaji wakubwa huwa wanapewa misamaha hiyo, kwa nini wafanyabiashara nao wasifikiriwe ili wawe na uwezo?

- Katika Wilaya ya Geita, kuna hazina kubwa ya matunda ya nanasi, embe na machungwa. Mara nyingi matunda hayo huozea mashambani kwa kukosa soko. Naomba kama kuna uwezekano, wapatiwe kiwanda kidogo cha kuweza kusindika matunda hayo na kupata juisi.

Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyo, naomba mikakati ifanywe ili matunda ya Geita yasipotee. Kama haiwezekani, tuwaite wawekezaji toka Uganda wawekeze kiwanda kama inavyofanyika kwao. Naomba pia suala la nyama ya ng'ombe litafutiwe soko. Ni vyema tukafufua viwanda vya nyama kwani ng'ombe wanaonekana hawana maana. Naomba sana viwanda vya kusindika nyama vianzishwe.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi, naomba kuwe na *tax relief* kwa wafanyabiashara wanaoanza (miezi 6 – 12), Kiwanda cha Kusindika Matunda ya Geita na Kiwanda cha Soko la Nyama ya Ng'ombe.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kutoa mchango wangu kwa maandishi. Kwanza, nampongeza sana Waziri na Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kushika nyadhifa hizo muhimu katika Serikali yetu. Pia, nawapongeza kwa hotuba nzuri ambayo imejieleza vizuri.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu unahusu ongezeko la bei ya zao la miwa kama ilivyo katika Hotuba ya Waziri, ibara ya 43, ukurasa wa 35.

Mheshimiwa Spika, jedwali namba 10(a) katika kitabu cha Hotuba ya Waziri wa Viwanda haijaonyesha mtiririko wa ongezeko la bei ya Zao la Miwa kwa miaka mbalimbali kama Mheshimiwa Waziri alivyoeleza. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri alijulishe Bunge lako Tukufu jedwali inayohusika na ongezeko la bei kwa zao la miwa kama ilivyotayarishwa kwa mazao mengine katika jedwali namba 10(a).

Mheshimiwa Spika, pamoja na tamko la Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, kuwa bei ya Zao la Miwa imeongezeka, jambo linalokiri kuwa ni la kweli, taarifa zilizopo na za kuaminika ni kwamba, kipato halisi cha mkulima wa miwa kimekuwa kinashuka hadi hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, sababu muhimu za kushuka kwa kipato ni zifuatazo: -

(i) *TRA* wameanza mpango wa ku-*charge VAT* asilimia 20 kwa kila tani ya miwa ya mkulina inapokatwa shambani;

(ii) *TRA* wana-*charge VAT* asilimia 20 kwa kila tani ya miwa ya mkulima inapopakiwa kwenye gari linalosomba miwa mpaka kiwandani;

(iii) *TRA* wana-*charge VAT* asilimia 20 kwa kila tani ya miwa ya mkulima inayosafishwa hadi kiwandani; na

(iv) *TRA* inawa-*charge withholding tax* asilimia mbili kwenye thamani ghafi *(gross earnings)* ya miwa iliyovunwa na mkulima na badala ya kum-*charge* baada ya kuondoa gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kwa mifano hii, napenda kushauri kuwa, kila mara ni vizuri zaidi kwa Serikali kutoa taarifa za ongezeko la bei za mazao kwa wakulima pamoja na makadirio ya wastani wa ongezeko la kipato halisi cha mkulima baada ya kuondoa gharama za makato mbalimbali ya mazao husika. Takwimu za aina hii zitawatia moyo wakulima kuongeza ufanisi na uzalishaji wa mazao. Ushahidi wa wazi unaonekana wa kuongezeka kwa kipato halisi baada ya gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, licha ya makato ya kodi zinazokatwa na *TRA,* ongezeko la bei ya mafuta, dawa ya magugu na ukosefu wa mbolea ya ruzuku kwa wakulima wa miwa, nako pia kulichangia kupunguzwa pato halisi la mkulima wa miwa.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla napenda kuishauri Serikali iimarishe *coordination* na *interaction* iwe ya karibu zaidi baina ya wataalam/wachumi kutoka Wizara ya Viwanda, Wizara ya Fedha na Wizara ya Kilimo ili takwimu za *economics* za kilimo cha mazao mbalimbali ziweze kuwa zimezingatia masuala (*factors*) mbalimbali zinazohusiana na kuongeza au kupunguza gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huu, naomba Serikali iyachunguze kwa maelezo yote niliyoyatoa na kuchukua hatua zitakazoboresha kipato halisi cha mkulima wa miwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko - Mheshimiwa Nazir Mustafa Karamagi, Naibu Waziri, Mheshimiwa David Mathayo, Katibu Mkuu na Watendaji wote walioshiriki kuandaa Bajeti hii ambayo ni nzuri na imewasilishwa kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile niendelee kuwapongeza kwani Waziri na Naibu wake tangu walipoteuliwa kushika Wizara hii, kweli wamekwenda sambamba na kauli mbiu ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania. Hivyo nawatakia kheri sana waendelee na mwendo huo huo wa kasi mpya, nguvu mpya na ari mpya ili waweze kutekeleza Bajeti hii barabara. Mwenyezi Mungu awe nao.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi, sasa nianze kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa zao la alizeti wakulima wa Mkoa wa Singida sasa wanazalisha zaidi na mashine zilizopo Singida zinakamua mafuta ya alizeti polepole sana na wakulima wanapata taabu sana na hukesha siku tatu au zaidi kusimamia ukamuaji wa alizeti zao: Je, ni lini sasa Serikali italeta mashine kubwa ambayo itawarahisishia kazi hii? naomba nipewe jibu.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika hoja namba (a), kuwa uzalishaji wa alizeti umekua sana na kwa kuwa hadi sasa wakulima wa zao hili hawajapata soko la kuaminika la mafuta ya alizeti: Je, Serikali pamoja na kuwa na soko huria, inawasaidiaje wakulima wa zao hili kuwatafutia soko la uhakika na lenye bei nzuri mafuta ya alizeti na mashudu ili wananchi waweze kunufaika na zao hili?

Mheshimiwa Spika, ni kweli usiofichika kuwa wanawake wa mkoa wa Singida wako sambamba na wanawake wa nchi nzima katika kubuni miradi ya uzalishaji mali kwa lengo la kuondokana na umaskini (MKUKUTA). Hivyo basi wanasuka mapambo mengi sana ya ukindu, yaani visonzo, lakini visonzo hivyo bado havina soko la uhakika zaidi ya mteja mmoja mmoja na kwenye maonyesho ya Saba Saba Dar es Salaam yanayofanyika mara moja kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, ni bora sasa Serikali ibebe mzigo huu wa kununua biashara hii ya visonzo kupitia *SIDO* ili wananchi ama akinamama wasipate taabu ya kusafiri mbali kwa kutafuta soko la visonzo. Nina hakika Serikali ikifanya hivyo, wanawake watazalisha zaidi kwa lengo la kutekeleza azma ya Serikali ya MKUKUTA.

Mheshimiwa Spika, napenda kuijulisha Serikali kuwa, uzalishaji wa zao la pamba Mkoani Singida unapungua sana kwa ajili ya kufungwa kiwanda chake Singida Mjini na vilevile kukosa soko la uhakika. Naiomba sana Serikali sasa itafute mwekezaji wa uhakika wa kufufua kiwanda hicho na wa kununua pamba hiyo. Matumaini yangu, zao hili litazalishwa zaidi Singida.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana wananchi wa Singida kwa kuzalisha mazao ya nafaka Mkoani Singida. Vilevile, naipongeza Serikali kwa kusaidia suala la njaa nchini. Kwa kuwa sasa ni soko huria kwa kuuza nafaka zetu, naiomba Serikali, ili kuwa na tahadhari ya janga la njaa, sasa Serikali inunue nafaka, yasitoke nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuikumbusha Serikali kuwa kati ya Mikoa inayofuga ng'ombe au mifugo, ni pamoja na Mkoa wa Singida. Hivyo, ninaiomba Serikali, sasa ni

wakati muafaka Serikali kuwatafutia wafugaji soko la uhakika la ngozi kuliko ilivyo sasa wanaonufaika ni wachache wenye uwezo wa kusafirisha mbali, yaani nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, sasa niitumie nafasi hii kwa njia ya maandishi kuunga mkono Bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, vilevile nizungumzie juu ya wachimbaji wadogo wadogo wa madini. Ni kweli wananchi wanajitahidi sana kuondokana na umaskini hususan akina mama, kwani hata kwenye uchimbaji wa madini, akina mama wapo. Lakini tatizo kubwa, wachimbaji wadogo wanapata taabu kupata soko la madini ili waweze kuuza kwa bei yenye faida. Naomba Serikali ilipatie ufumbuzi kupitia Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kupunguza bei ya mafuta ya taa, dizeli na petroli, lakini hadi leo hii bei bado iko juu kwa kisingizio kuwa bado wanayo *stock* ya zamani wakati sio kweli. Naomba Serikali ifuatilie kero hii ili hali hii isiendelee.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie juu ya Kiwanda cha Magodoro ya Dodoma. Ninafahamu Kiwanda hiki kilihamishiwa Dar es Salaam baada ya tatizo lililotokea, kwa kuwa kiwanda hicho cha Magodoro ya Dodoma kilikuwa kimeleta sifa na ustawi wa Mkoa wa Dodoma na Kanda ya Kati kwa ujumla. Naiomba Sasa Serikali ione umuhimu wa kiwanda hiki kurudisha huduma zake Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa kuna soko la machinjio ya kisasa Dodoma, naiomba Serikali sasa ichukue jukumu la kununua ng'ombe katika minada yetu ili wafugaji wapate soko la mifugo yao kwa bei yenye faida.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa *cement* na bati kwa ujenzi wa nyumba kwa wananchi. Bei ya *cement* na bati bado iko juu. Hivyo basi, naiomba Serikali itazame upya bei hii kwani Watanzania wetu hawana uwezo wa kumudu bei hizo na umuhimu wa *cement* na bati uko pale pale.

Mheshimiwa Spika, naendelea kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, suala la saruji ni mojawapo ya kuondokana na umaskini hasa kwa wananchi wa Vijijini, lakini saruji hii humfikia mwananchi wa Kijijini kwa bei kubwa zaidi. Kutokana na usafiri, hata saruji yenyewe kupanda kwa bei kila wakati: Je, Suala nzima la nchi kuondokana na nyumba ambazo sio za kudumu na kujenga za kudumu itawezekana kweli?

Mheshimiwa Spika, pia kupanda kwa bei ya bati kila wakati, cha muhimu ni Wizara kuangalia wananchi wa Vijijini tutawaondoaje katika suala la nzima la nyumba duni. Nashindwa kuelewa! Kwa nini *T.B.L* inauza bidhaa zake kwa bei ile ile Mijini na Vijijini? Hili linawezaje kutekelezeka na vifaa vya ujenzi kama nilivyovitaja vimeshindikana?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wakala, naomba kufahamishwa kuna sheria gani ya kupata Wakala mmoja tu kwa kanda ili wananchi wa Tabora, Kigoma, Singida, wachukulie saruji hapa Dodoma? Kwani kutoka maeneo hayo na kununua Dodoma ni mojawapo ya kuwa na bei kubwa sana. Pia, kuhusu suala la Mawakala liangaliwe vizuri. Ninaomba kupata jibu, Wakala wa Saruji wananunua saruji hiyo Shilingi ngapi kiwandani? Nadhani jibu litazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, ushirikishwaji wa wafanyabiashara Mikoani na Wilayani, nadhani kuna dhana ya wafanyabiashara wale wanaoishi Dar es Salaam tu, lakini Serikali lazima ikubali kuwa kuna haja ya uongozi wa Wilaya na Serikali kuelewa wafanyabiashara ndani ya Wilaya zao na Mkoa na kufahamu matatizo yao na jinsi ya kuwasaidia, maana kama wafanyabiashara na Serikali watakuwa hawana mazungumzo ni mojawapo ya mfumuko wa bei na wafanyabiashara kutopata mahali pa kutoa shida zao.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia sehemu ya viwanda vilivyoko Mkoa wa Kagera ili nipate maelezo ya kunifahamisha niweze kujua zaidi vinavyofanyakazi, kwa sababu wananchi wengi wanalalamikia viwanda vifuatavyo: Kagera, Kiwanda cha Sukari. Kiwanda kiko kwenye Mkoa huo huo lakini tunapata sukari kwa bei kubwa. Naomba nielezwe ili niweze kujua.

Pili, kuhusu wafanyakazi. Wafanyakazi wanalalamika na mpaka sasa wafanyakazi zaidi ya 300 kesi zao ziko Mahakamani. Je, hivi huyo mwekezaji si anaangusha kiwanda hicho! Je, wananchi wanafaidikaje na hicho kiwanda kama kuwapa ajira wakazi wa pale au wa Mkoa mzima?

Mheshimiwa Spika, tuna Kiwanda cha Majani ya Chai, hata hakijulikani kinavyofanya kazi. Naomba nielezwe kwa sababu wananchi wengi wakulima walikuwa wanauza majani yao ili kujipatia riziki zao. Tangu kimepata mwekezaji, wafanyakazi wa karibu na pale walisimamishwa na haijulikani kama watalipwa fedha zao au hapana. Tuna viwanda vya samaki. Je, vinafanyaje kazi? Ajira ya viwanda hivyo sio vya kuwapa ajira wananchi wa pale, vinawanufaisha wao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, *SIDO* imetupwa kwa muda mrefu sana. Naomba nipatiwe majibu. Kuhusu masoko yaliyoandaliwa kufanya kazi na Serikali ikajenga, kwa mfano, masoko yaliyoandaliwa Kashai, Hamgembe: Je, kwa nini watu wasiyatumie kuuza bidhaa zetu hasa zinazonunuliwa na nchi za jirani zetu kama Uganda? Serikali haioni ajabu kwa nini tusiwe na soko ndogo angalau wananchi wakawa wana sehemu ya kuuza mazao yao hasa kahawa, maharage, ndizi, karanga, mahindi, kama sasa tuna *vanilla,* hivi Serikali haioni kuwa sasa ni wakati wa kuwa na soko hilo?

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, watu wanaouza kahawa iwaruhusu wauze Uganda bila kukatazwa ili wajipatie kipato chao. Naomba niishie hapo. Naomba majibu na ninaunga mkono hoja.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, napenda kwanza nikupongeze kwa kuliendesha Bunge kwa umahiri na busara ya hali ya juu.

Pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Naibu Waziri wake na timu nzima ya Wizara hiyo kwa kuandaa hoja nzuri sana ya Bajeti ambayo sasa tunaichangia.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu alitamka siku moja kwamba, nanukuu: "Agenda yetu namba moja ni Elimu, lakini agenda yetu namba mbili ni Kilimo."

Mheshimiwa Spika, mimi naamini kabisa kwamba kama Watanzania watazingatia kauli hii ya Waziri Mkuu wetu, basi hautapita muda mrefu wa kusema Agenda yetu Na.3 ni Viwanda, Biashara na Masoko.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu zifuatazo: Nikiangalia nchi zote zilizoendelea, hakuna nchi inayotegemea kilimo kwa uchumi wake. Nchi nyingi zilizoendelea zinategemea viwanda na biashara kwa kukuza uchumi wake. Tegemezi katika kilimo na katika kukuza uchumi ni kigezo kinachopima umaskini wa nchi. Hivyo, Tanzania bado ni nchi maskini kwani uchumi wake kwa sehemu kubwa unategemea kilimo. Ili nchi yetu itokane na uchumi duni, ni lazima tuelekee katika kujenga misingi imara ya kuweka mipango ya muda mrefu katika viwanda na biashara na hatimaye kuwa na masoko ya uhakika ya bidhaa ya viwanda vyetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imelivalia njuga suala zima la kuboresha kilimo, haitapita muda mrefu tutazalisha ziada na hivyo ni wakati muafaka pia jitihada hizo zikaenda sambamba na viwanda vya mazao ya kilimo na kuweza kugeuza mfumo wa uchumi wetu na kwa kushindana na masoko ya dunia kwa kutoa bidhaa bora.

Mheshimiwa Spika, tunalima Pareto, kwa mfano, lakini Wakenya wananunua yote na kwenda kutengeneza dawa ya mbu na kurudi kutuuzia kwa bei kubwa. Hii ni pamoja na mazao ya aina ya miti inayotumiwa kutengeneza *perfume*. Miti hii inaota porini na pengine Serikali haina habari wala taarifa zozote kwamba nchi za jirani zinaagiza wananchi wa Vijiji husika kuwauzia magogo hayo ambayo husafirishwa nje kwa madhumuni ya kutengeneza *perfumes.*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina *potential* kubwa ya ku-*transform* uchumi wake na kuacha kutegemea kilimo. Mtazamo wa Awamu hii na karne hii, ianze kuweka mipango maalum wa kuanzisha viwanda. Suala zima la utandawazi na biashara huria, inaweza pia kulazimisha mfumo wa kukuza uchumi ubadilike kutokana na ushindani katika masoko ya dunia. Utandawazi na teknolojia *(information – technology)* inarahisisha upatikanaji wa soko la uhakika ndani na nje ya nchi kwa kuwezesha kufanya biashara kwa kutumia mtandao.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, katika Bajeti zake za miaka inayofuata, iweze kutenga fungu maalum la Mipango

Madhubuti ya ku-*transform* au kuelekeza uchumi wa nchi yetu utokane zaidi na Viwanda na Biashara badala ya Kilimo kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru tena na naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake pamoja na wasaidizi wake kwa kubeba majukumu ya Wizara hiyo. Lakini nawapa pole kwa kazi ngumu. Mchango wangu unalenga kwenye zao la korosho. Ninayoyasema, yanagusa Wizara ya Kilimo na Chakula na Ushirika na pia Wizara ya Fedha. Lakini Serikali ni moja. Nategemea atashauriana na Mawaziri wenzake husika ili kuwaridhisha wakulima wa korosho.

Mheshimiwa Spika, zao la korosho limetelekezwa ingawa mchango wake kwenye uchumi wetu ni mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo. Uzalishaji umeshuka kutoka tani 145,000 mwaka 1973/1974 hadi tani 80,000 hivi sasa (2004). Sababu kuu ni hizi zifuatazo:-

(a) Wakulima hawapati pembejeo za kutosha na huduma za kutosha.

(b) Wakulima hawapati bei nzuri na masoko ya kuaminika tofauti na Serikali inavyosaidia mazao mengine kama korosho, pamba na kahawa.

(c) Serikali imeacha kusimamia ubanguaji wa korosho kwa miaka zaidi ya 25 sasa. Ingawa viwanda hivyo vimeshabinafsishwa kwa miaka miwili iliyopita, bado havijaanza kubangua kikamilifu kwa sababu ya kukosa "*support*" ya Serikali katika kupata wafadhili na kukosa dhamana ya mikopo. Natambua nia ya kudhamini nusu tu ya mikopo. Hii haisaidii kitu.

(d) Hali ya sasa ya kubangua tani 7,400 mwaka 2003/2004, tani 6,061, mwaka 2003/2004 na tani 5,000 mwaka 2004/2005. Kati ya tani 90,000 na 120,000 za korosho ghafi zinazozalishwa nchini, hairidhishi hata kidogo.

(e) Kwa mujibu wa barua ya Hazina Na.TYC/100/78 ya tarehe 12/7/2006, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, achukue madaraka ya kukusanya ushuru wa korosho zisizobanguliwa ambalo lilikuwa jukumu la Bodi ya Korosho. Ushuru ulikuwa asilimia 8.5 ya mauzo. Ushuru huo ulikuwa unagawiwa kama ifuatavyo:-

    (a) Halmashauri zinazozalisha korosho asilimia tano;

    (b) Uendelezaji wa zao la korosho asilimia 2.0; na

(c) Bodi ya Korosho kwa usimamizi asilimia 1.5

Lakini uamuzi mpya Serikali inaugawa ushuru huo kama ifuatavyo:-

(a) Halmashauri zinazozalisha korosho asilimia 5.0; na

(b) Hazina.

Mheshimiwa Spika, mimi na wakulima wa korosho tunaona kuwa uamuzi huu wa Serikali utaendelea kulididimiza zao la korosho. Kwani Hazina haina uwezo wa kusimamia wakulima moja kwa moja. Lakini imenyang'anywa uwezo wa kuendeleza biashara ya korosho.

Kwa upande mwingine, Hazina haiwezi kufaidika sana na asilimia 3.5 ya ushuru kutoka tani 90,000 ya korosho zisizobanguliwa. Isitoshe, ushuru huo siyo endelevu. Kwani azma yetu ya kubangua korosho zote hapa nchini, ushuru huo utakoma, kwani basi fedha hiyo isiachiwe Bodi ambayo itaitumia kuboresha zao hilo hivi sasa ili lilete matunda wakati ushuru huo utakapokoma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushauri, nashauri yafuatavyo:-

1. Serikali iongeze ruzuku ya pembejeo tena itolewe mapema wala usifuatwe utaratibu wa *cash budgeting*;
2. Fedha ya Serikali isitolewe kwa waagizaji wa pembejeo binafsi, bali jukumu hilo sasa lipewe Bodi ya Korosho;
3. Serikali isaidie wenye viwanda kwa kutoa dhamana ya mikopo ili viwanda vikarabatiwe na korosho ghafi zinunuliwe kutoka kwa wakulima; na
4. Utaratibu wa kukusanya ushuru wa korosho ghafi uliokuwepo kabla ya mwezi huu uruhusiwe kuendelea.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, *TBS* ni chombo chenye umuhimu wa pekee katika kulinda ubora wa bidhaa zinazozalishwa na kuingizwa ndani ya nchi. Lakini kwa mwono wangu, chombo hiki pia licha ya kuwa zipo Taasisi zinazokagua ubora wa bidhaa kwenye biashara, mfano kwenye maduka, ipo haja ya chombo hiki kuongezewa Watendaji ili ukubwa wa ukaguzi huo waweze nao kukagua bidhaa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna uharibifu mkubwa wa matunda kwa mfano machungwa. Kwa kupitia *SIDO* ingaliwezekana kuwa na viwanda vidogo vidogo ambavyo vingewezesha wananchi kusindika matunda hayo. Lakini kinachoonesha sasa, *SIDO* imejikita katika kuwasaidia wananchi katika suala zima la mikopo midogo midogo badala ya kufanya utafiti na kuwasaidia wananchi katika suala zima la viwanda vidogo vidogo.

Ni nchi chache duniani zinazoweza kuwa na jiografia nzuri kama nchi yetu. Nchi yetu ina ufukwe wa bahari upatao kilometa 1,424 na ndani yake kuna Bandari ya

Tanga, Dar es Salaam, Mtwara na Zanzibar. Nchi kama Uganda, Rwanda, Congo, Zambia na Malawi zinategemea au zilikuwa zikitegemea sana bandari zetu. Lakini kutokana na kero nyingi zilizomo kwenye bandari zetu, nchi nyingi zimeacha kutumia bandari hizo. Miongoni mwa kero hizo ni huduma mbovu bandarini, wizi na uzembe. Ipo haja Wizara kujidhatiti ili dosari hizo ziwe hazipo.

Mheshimiwa Spika, hakuna nchi iliyoendelea bila utafiti. Inavyoonekana, katika Wizara hii, suala la utafiti halikupewa uzito unaostahili pale unapoona kuna fedha kidogo zilizotengwa kwa ajili ya utafiti. Ipo haja Taasisi za tafiti hapo baadaye zitengewe fedha nyingi kwa hilo. Ahsante.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia machache katika Wizara hii.

Pia, napenda kumpongeza Waziri na Naibu wake, pia Katibu Mkuu na Watalaam wote wa Wizara hiyo kwa kuweza kuandaa hotuba hii na kuiwasilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii kama zilivyo Wizara nyingine, ni muhimu sana kuonyesha jitihada ya kumkomboa Mtanzania katika lindi hili la umaskini ambalo ni tatizo kubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa sana katika viwanda ambavyo vilibinafsishwa kwa kutokuendelea kufanya kazi. Ninaamini Serikali ilibinafsisha viwanda hivyo kutoa ajira kwa Watanzania. Kinyume na matarajio hayo, viwanda hivyo vimefungwa na havifanyi kazi.

Mheshimiwa Spika, mimi natoka Mkoa wa Kilimanjaro ambao kwa miaka ya nyuma, ni Mkoa ambao ulikuwa mbele kwa maendeleo makubwa ya elimu na uchumi. Lakini kwa sasa ni Mkoa ambao unarudi nyuma kwa kasi kubwa na hii inatokana na viwanda vilivyokuwa Mkoani kutokufanya kazi na wananchi wa Mkoa huo kutokufanya kazi katika Viwanda hivyo na hivyo kukosa pesa au mishahara ambayo ingewasaidia katika kuwasomesha watoto wao na hata kufanya biashara ndogo ndogo ambazo zingekuza uchumi wao.

Mheshimiwa Spika, tunataka Mheshimiwa Waziri awaambie wanakilimanjaro kwamba, hivyo vitaanza kufanya lini na ni kwanini hao waliochukua viwanda hivyo hawakuendeleza kazi zilizokuwa zinafanyika katika viwanda hivyo?

Jambo lingine ni kuhusu wafanyakazi waliokuwa katika viwanda hivyo. Kuna haki zao wanazodai, lakini mpaka sasa hawajalipwa. Je, ni nini hatma ya wafanyakazi wa viwanda hivyo ambao walifanya kazi kwa bidii, lakini wananyimwa haki zao katika nchi yao?

Mfano ni kiwanda cha madawa ya wadudu Moshi, wafanyakazi hao hawajalipwa pamoja na Waziri aliyekuwepo Bunge lililopita kuwapa matumaini ya kulipwa, lakini mpaka sasa hawajalipwa. Je, Wizara inasema nini katika hili? Tunaomba watoe jibu

kamili ili wananchi hao wanaodai waweze kujua kama watalipwa na kama hawatalipwa ni vizuri wakayajua mapema kuliko kukaa kwa matumaini ambayo hayapo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuandika hayo, nakushukuru tena kwa kupata nafasi hii.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nawapongeza sana kwa hotuba nzuri ya Waziri , Mheshimiwa Nazir Mustafa Karamagi kwa jinsi alivyosoma na uchambuzi kwa ufupi sana na kwa kueleweka.

Mheshimiwa Spik, katika Wilaya yetu ya Njombe, soko la Makambako hakulisoma na tunaomba aliangalie kwa jicho la huruma, kwani ni mkombozi kwa Mikoa ya Kusini, kwani hata makaa ya mawe na chuma cha Liganga na Mchuchuma litategemea soko hilo.

Mheshimiwa Spika, kuna kiwanda cha Ulembwe, kiko katika Jimbo langu. Kiwanda hiki cha Ulembe kimepooza sana, tunaomba atembelee ili vijana wetu wapate ajira. Pia, tunaomba viwanda vya *SIDO* katika Tarafa za Mdandu, Imalinyi na Wanging'ombe vianzishwe na viendelezwe kwani kuna mazao ya alizeti, karanga na mbao.

Mheshimiwa Spika, kiwanda cha pareto cha Mafinga nacho kipewe kipaumbele. Sisi ni wakulima wa pareto katika milima ya Kipengere (Imalilo)Wangama, hivyo kiwanda hicho ni muhimu kwa Taifa na Taifa litapata mapato makubwa.

Mheshimiwa Spika, ubinafsishaji wa viwanda uwe wa ushindani na uwazi zaidi. Hata kwenye Sekta ya Madini na uwazi zaidi na ushindani. Hii itasaidia Serikali kupata mapato makubwa.

Mwisho, nampongeza sana Dr. David Mathayo David, Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko kwa jinsi anavyochapa kazi vizuri sana kwa jinsi anavyojibu maswali vizuri Bungeni na jinsi anavyowasilisha hoja Bungeni, hongera sana.

Pamoja na pongezi hizo, ajaribu sana kutoa elimu ya vijana wenzetu katika kuanzisha viwanda, kuhamasisha biashara kwa vijana na kukuza masoko ya ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, nawatakia Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara, afya njema na ufanisi bora katika ujenzi wa Taifa letu ili tuweze kumuenzi Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Serikali yake.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, kabla ya yote naomba kuwapongeza kwa dhati Waziri, Mheshimiwa Nazir M. Karamagi na Naibu Waziri - Mheshimiwa Dr. David M. David, Ndugu Wilfred Nyachia - Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara hii ambayo imesukwa vizuri na rais wetu Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete. Taarifa hii ni nzuri na ina mwelekeo wa kuleta mapinduzi katika Sekta ya Viwanda na Biashara na Masoko. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, nimeamua kutumia maandishi kwa sababu nafasi ninaweza kuikosa kwa kuzungumza. Yapo maeneo kadhaa ambayo ningeshauri Wizara iyazingatie kwa undani zaidi na inipatie maelezo ya kina juu ya nini hatma ya mambo yafuatayo:

Mheshimiwa Spika, la kwanza ni suala zima la masoko kuwekwa kwenye Wizara hii wakati masoko ni kwa ajili ya Wizara nyingi ikiwemo Kilimo, Ushirika, Mifugo, Maliasili, Uvuvi, Misitu na kadhalika. Kwa nini Wizara isibakie ya Viwanda na Biashara na iwepo Wizara ya Masoko pekee kwa mazao ya aina zote? Huu ni ushauri wangu kama nilivyoomba mwaka 2005, Wizara ya Maji na Mifugo iweze kutenganishwa ili maji yabaki kwa Sekta zote.

Mheshimiwa Spika, nini hatma ya Kiwanda cha Zana za Kilimo Mbeya? Ndiyo kimekufa kabisa? Kiwanda hiki kilikuwa ukombizi mkuu kwa wakulima, maana kilizalisha zana nyingi na zilizo bora kuliko hizi za sasa zinazoletwa na baadhi ya viwanda vya nje ambavyo huwa na uhafifu wa ubora wake.

Nini pia hatma ya kuendelea kuruhusu Viwanda vya Chuma kutumia *scraps* na mataruma kwa kutengeneza nondo za kujengea nyumba? Mbona hali hii imeendelea kusababisha wizi mkubwa wa hata mifuniko ya mifereji ya maji na mifuniko ya barabarani? Nani anayedhibiti kuwa viwanda hivi havipokei vyuma kama hivyo? Tunaomba Wizara iwe macho kwenye *receiving end* na *TBS,* wasimamie ubora wa mali inayozalishwa huko.

Mheshimiwa Spika, *SIDO* ndiyo mkombozi wetu mkuu hata huko Vijijini, lakini kiasi cha fedha zinazotengwa hakilingani na majukumu yaliyowekwa kwa shughuli hizi. Wakati umefika wa *SIDO* na *TURDO* na *CARMATEC* kuwa chombo muhimu cha kuleta mapinduzi ya kweli ili kuimarisha viwanda vyetu na kuongeza ajira kwa watu wetu na hasa vijana na akina mama. Sambamba na malengo yaliyowekwa kwenye Ilani ya Uchaguzi na msingi ukiwa ni *MKUKUTA*: Je, Wizara imeanza kuandaa hatua kwa hatua taratibu za kutekeleza *MDGs*?

Mheshimiwa Spika, suala la uingizaji na uagizaji wa mbolea kwa mfanyabiashara mmoja mmoja na kwa kiasi kidogo kidogo ni gharama kubwa sana. Nikichukua mfano wa mbolea ya *UREA (46%N)* ambayo kitaifa hutumika zaidi kwa ajili ya matumizi yake, yanaweza kufikia tani 100,000. Ni gharama kuagiza kidogo kidogo. Nalisema hilo kwa kutoa mfano huu ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, ukiagiza *urea* kati ya tani 300,000 hadi 500,000 bei yake ni *USD 67.7* kwa tani. Ukiagiza tani 100,000 hadi 150,000 utapewa bei ya *USD 110* kwa tani, wakati ukiagiza tani 12,000 hadi 100,000 bei itakuwa *USD 125* kwa tani na ukiagiza chini ya hapo, bei inazidi kupanda hadi *USD 278* kwa tani. Hivyo, atakayebeba mzigo huo ni mkulima.

Mheshimiwa Spika, ninashauri suala hili tulijaribu kwa kina, ili bei ya mkulima isiwe chini ya Sh. 12,000/= kwa mfuko wa kilo 50. Hii inawezekana kama kiasi cha tani

100,000, kimeingizwa pamoja ambayo ni sawa na meli moja. Bei itashuka na siyo lazima kutoa ruzuku.

Mheshimiwa Spika, *Logistics* za kuisambaza kwa kutumia mawakala 639 na *SACCOS* linaweza kutatua tatizo la kulundikana mbolea. Nitamwandikia Mheshimiwa Waziri namna ya kuliendesha suala hili vizuri.

Mheshimiwa Spika, suala la viwanda vya ngozi na hatma yake ni budi ikawekwa sawa na pia hatma ya kuimarisha biashara za mipakani zipewe kipaumbele na hasa kule mpaka wa Zambia na Tanzania (kasesya) kuanzishwe vuguvugu kwa kushirikiana na *TCCIA, CTI* na *TPSF*.

Naunga mkono hoja hii. Naomba majibu.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake yenye kutia matumaini kwa uchumi wa nchi yetu kutoka kwenye sekta mbalimbali za Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inahitaji viwanda vikubwa zaidi ya hivi tulivyokuwa navyo hivi sasa ili kuongeza pato la Taifa na kuongeza ajira. Moja ya mikakati ya nchi ni kuendeleza eneo la Mchuchuma na Liganga, ambayo pia ilani yetu imezungumzia mradi huu. Lakini hotuba yake haikueleza maelezo yoyote ya kuridhisha kwenye miradi hii.

Mheshimiwa Spika, mfano, nchi ya Msumbuji ni hivi karibuni imemaliza migogoro ya vita ya wenyewe kwa wenyewe na hali yao kiuchumi ilikuwa mbaya sana. Wameanza kuendeleza mradi wa *Aluminium* na kwa mradi huo, Msumbiji uchumi wake hivi sasa unakuwa kwa asilimia 13. Sisi bado tuna suasua katika kuendeleza miradi kama hiyo ambayo tunayo.

Miradi ya Mchuchuma na Liganga inaweza kutuondoa hapa tulipo na kuiweka nchi yetu kwenye uchumi bora zaidi. Naomba Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge hili wakati wa kuhitimisha hoja yake, ameweka mikakati gani katika kufanikisha mradi wa Mchuchuma na Liganga, hasa katika kupata wawekezaji wenye sifa zakitaalam, uwezo wa kifedha na tekinolojia upya kufanikisha mradi huu? Hayo yakiwa ni moja ya mapendekezo ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara.

Mheshimiwa Spika, mimi pamoja na Wabunge wengine, tuna shauku kubwa kumsikia anazungumzia suala hili kuliko kusikia maneno ya uje na magazeti wakati wewe upo. Tafadhali tupe maelezo yako kama Waziri mwenye dhamana ndiyo kauli sahihi ya Wizara na Serikali kwa ujumla. Ahsante.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Nazir Mustafa Karamagi, Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko kwa hotuba nzuri ambayo ameitoa asubuhi ya leo.

Mimi naamini kuwa hotuba hii itasaidia sana katika kutoa dira na mwelekeo mzuri wa kuendeleza viwanda na biashara nchini. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kipekee ningependa kuikumbusha Wizara kuhusu Viwanda mbalimbali ambavyo vimekufa Mkoani Kilimanjaro.

Mheshimiwa spika, pamoja na suala la kuvitoa viwanda kwa sekta binafsi, nashindwa kuelewa ni kwanini ni vigumu kufufua viwanda hivyo ambavyo vingesaidia sana suala la ajira.

Mheshimiwa Spika, ningeomba kueleweshwa kuhusu mkakati wa kufufua viwanda hivi. Naunga mkono hoja.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniruhusu mimi niwe mmojawapo wa kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Wizara hii kwa hotuba yake nzuri sana ambayo kama itakuwa na utekelezaji sahihi, basi inaweza kuleta mafanikio. Kabla sijaanza kuchangia, basi nianze kuunga mkono Wizara hii kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Mwanakwerekwe. Naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, mimi nafsi yangu, naiomba Wizara hii iangalie vizuri sana, kwa vile viwanda vinaelekezwa kuhusu wafanyakazi ambao wanakuwemo kwenye viwanda hivyo. Wananchi hao huondolewa kazini bila mpango ambapo wanakosa haki zao. Jambo hili ni unyanyasaji wa raia wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, viwanda vingi ambavyo vimebinafsishwa lakini hadi leo havifanyi kazi na wafanyakazi waliopo kwenye viwanda hivyo wapo ambao hawajui mafao yao wala mshahara, Wizara isimamie vizuri ili viwanda hivyo vianze kazi na wananchi waendelee na ajira. Kiko kiwanda cha nondo na misumari kule Tanga hadi leo nadhani kiwanda hicho hakijaanza kazi. Sijui Waziri ataeleza nini kuhusu kiwanda hicho?

Pia, kiwanda cha mbao, *Mkata Saw Mill* hakifanyikazi kabisa. Mwekezaji kakaa nacho bila shirika kupata pato lolote na huku wafanyakazi hawajui la kufanya, hawana mshahara wala pato au mafao yao. Sijui Wizara inasema nini kuhusu kiwanda hiki cha mbao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu makaa ya mawe na chuma cha Liganga, Serikali itoe kipaumbele ili ikamilishe mradi huu kwa sababu sera ya Chama cha Mapinduzi ina wajibu kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, napongeza sana ushindani wa biashara uliopo na hasa sehemu za viwanda ambavyo vinafanya kazi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja hii.

**MHE. KHALIFA S. KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wake kwa kuleta hotuba nzuri. Pamoja na pongezi hizo nina ushauri ufuatayo:-

Mheshimiwa Spika, hoja za uwekezaji zimekumbwa na utata mwingi, hali ambayo inasababisha manung'uniko. Kwa msingi huo, nashauri Serikali iwe makini sana katika kutoa fursa kwa Wawekezaji. Kwa mfano Miradi ya Liganga na Michuchuma. Miradi hii miwili ni mkubwa na inahitaji fedha nyingi na tekinolojia iliyopevuka.

Hivyo basi, kati ya wale waliojitokeza kuomba kuwekeza kwenye miradi hii ni bora apewe yule mwenye uwezo wa kifedha na kiteknolojia na siyo mwekezaji ambaye ni dhaifu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada zinazochukuliwa na Wizara, hata hivyo ipo haja ya kuleta viwanda vidogo vya kukamua matunda kama machungwa, maembe, mabungo na mengine ili wakulima wetu wawezekupata soko zuri la ndani na baadaye soko la nje.

Mheshimiwa Spika, ninashauri elimu itolewe kwa wakulima wetu juu ya kuzalisha matunda yenye ubora unaokubalika katika masoko mbalimbali kama vile masoko ya Ulaya, Asia na Amerika.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia suala la masoko kwa mazao yetu. Tanzania kwa muda mrefu itaendelea kuzalisha mazao ya kilimo na kuyauza nje. Mazao haya kama korosho, kahawa, pamba na chai ni chanzo cha fedha na ajira kwa watu wengi nchini. Kwa kazi hii, ni vyema Serikali ijumuishe kikamilifu katika kutafuta masoko imara kibei ili utafiti huu na hatua zinazochukuliwa ziwe na hamasa kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu bei za pamba zimekuwa nzuri na hii inawezekana kwa kuzungumzia makato kwenye bei kama vile Shilingi tano za kuendesha Bodi na Shilingi tano za Mfuko wa Elimu. Tunaipongeza Serikali kwa ujasiri huu. Tunaishauri Serikali iangalie makato ya *CDF- Cotton Development Fund.* Wakati haya ni Shilingi tano za utafiti *cotton research* na Sh. 15/= manunuzi ya pembejeo, kati ya hizi ni asilimia 25 na kwa hiyo, wakulima wananunua madawa kwa bei ya juu.

Aidha, wakulima wananyimwa fursa ya kupata mafunzo ya wenye madawa ambayo zamani walikuwa wanapata kama enzi za makampuni ya *CIBA*,*GEIGY*, *Hoesth*, *ICC* na kadhalika. Sasa madawa hata haijulikani yanauzwa na nani na majina yake ni *EKA packs*, jina ambalo halionyeshi ni *chemical* gani. Aidha, Sh. 15/= kwa kilo zingechangiwa na Serikali kama mkulima wa mahindi anavyofaidika. Jambo hili

likifanyika, bei ya mkulima itaboreshwa kwa Sh. 15/= kwa kilo na hili litaleta hamasa ya kielemu zaidi msimu unaokuja na pia pamba itakuwa imeongeza mapato ya fedha za kigeni na kupunguza umaskini kwa hali ya juu. Makato haya yanahusu mazao mengine kama korosho.

Mheshimiwa Spika, *Guaranteed Price,* Masoko mengi ya mazao yana *future* mauzo ya miaka ya mbele. Bei ya pamba ya 2007/2008 inajulikana leo. Kwa msingi huu, inawezekana kabisa kuhamasisha wanunuzi wote kutoa bei yake kabla ya kulima.

Mnunuzi pia anaweza kuchukua *insurance* kwa bei aliyoahidi *(Guaranteed Price)*. Itahamasisha wakulima kuongeza tija ya mazao yao. Kwa kuwa Serikali itatoa leseni ya ununuzi wa pamba au korosho, mojawapo ya masharti ya leseni, iwe bei kabla ya kulima, *guaranteed price before cultivation*. Jambo hili Wizara ya masoko na Serikali kwa ujumla inaweza kufanya.

**MHE. VUAI ABDALLA KHAMISI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya M. Kikwete, pamoja na Makamu wake Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein pia Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Amani Abeid Amani kwa kuchaguliwa kwao.

Mheshimiwa Spika, ninaishukuru Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na ninaipongeza sana kwa kushughulikia shughuli zake pamoja na kusimamia vyema maonyesho ya mwaka huu 2006 yaliyofanyika Dar es Salaam na kufanikisha vizuri. Naomba iendelee zaidi na kufanikisha na kuweza kuelimisha Watanzania na kupata wawekezaji bora kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, viwanda vingi vilivyobinafsishwa, kwa sasa vingi au baadhi havizalishi na wakiulizwa, majibu yao sio mazuri na wafanyakazi wao huwanyanyasa sana na viwanda hivyo hubinafsishwa kwa watu kwa Serikali, tarajio lake kwa viwanda hivyo vifanye kazi na kuchukua ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa viwanda havitekelezi wajibu wa Serikali, naiomba Serikali Viwanda hivyo virudishwe au wapewe wawekezaji wanaomudu kuweza kuzalisha.

Mheshimiwa Spika, pia naomba Wizara itoe elimu (Semina) mbalimbali ili kuwezesha biashara ya ndani na nje ya nchi ili uchumi wetu ukue na kupata maendeleo mazuri. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magogoni. Naunga mkono hoja zote kwa asilimia mia.

**MHE. HAMAD R. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kutokana na takwimu zilizomo ndani ya kitabu chako cha hotuba, inaonesha uzalishaji wa redio umesimama. Ni sababu zipi zilizosababisha uzalishaji kusimama? Serikali inachukua hatua gani kurudisha uzalishaji wa redio?

Mheshimiwa Spika, ufanisi katika viwanda, mchango wa Sekta ya Viwanda katika mauzo ya nje umekuwa ukipungua kutoka asilimia 16 hadi asilimia 10.1 mwaka 2005 wakati ambapo ndio tunaingia katika ushindani wa kibiashara na wakati sasa ndio tuna uchumi wa kisasa (huria) tatizo nini? Je, kweli tutaweza kuingia kwenye biashara ya ushindani?

Mheshimiwa Spika, naomba kupata taarifa juu ya makampuni tanzu ya *Mwananchi Gold Company Limited.*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri na Naibu Waziri kwa maandalizi mazuri ya Bajeti ya mwaka huu 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Wizara kwa sheria yake mpya ya usajili wa biashara na leseni *(BRELA),* usajili Makampuni, Sheria Na. 12 ya mwaka 2002. Sheria ya sasa ya Msajili kwa sehemu moja Dar es Slaam inanyima haki Watanzania wengi wenye nia ya kusajili kupitia sheria hii. Nashauri Wizara kuanzisha sheria ya kuwa na mawakala wa usajili kwa baadhi ya kanda ili kuondoa urasimu.

Taasisi za utafiti zilizo chini ya Wizara nazo zifunguliwe Vituo vya Kanda, Taasisi hizi kama vile *TBS, CAMARTEC, TEMDO, TIRDO* na *NDC.* Vituo hivi vya Kanda viweze kutoa elimu kwa wajasiriamali ili kuendana na suala la *MKUKUTA*. Naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. IDRIS ALI MTULIA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Hotuba hii ni makini na inatia moyo na matumaini makubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inahitaji mabadiliko ya mtazamo. Naomba Wizara hii ihakikishe kuwa *Agro-industries* kama viwanda vya kusindika maembe, mananasi, machungwa na nyanya. Mazao hayo yanaharibika sana kila msimu na kwa vile yanalimwa kutumia mboji ya asili wala sio makemikali kama matunda yanayolimwa nchi zilizoendelea. Bei ya matunda ya kwetu itakuwa ya juu kutupatia faida kubwa.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ni biashara. Hakuna nchi inaweza kuendelea bila kuwa na biashara inayowashirikisha wananchi wengi. Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Waziri wa Uwezeshaji wahakikishe kuwa wapate elimu kwa wingi (*mass business education for all),* wapate mitaji mikubwa, kuhakikisha sio hotuba tu, kuwa wananchi wengi wanafanya biashara kwa wingi, sio wahindi tu.

Mheshimiwa Spika, mbinu za biashara za kimataifa inaweza kuwa bidhaa ya nchi yako ikawa ndio inayopatikana katika nchi yako tu. Mathalani, pamba ya *Long Step Cotton* inalimwa Bonde la Mto Rufiji hasa katika Jimbo la Rufiji ambalo ni Jimbo langu la uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kuhimiza kilimo cha pamba aina ya *Long Step Cotton* inalimwa kwa wingi Wilaya ya Rufiji.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kuweko na azma ya makusudi kwa Wizara, kupanua soko la ndani ya nchi. Hali ya masoko yetu ya ndani ni mabovu na chafu sana. Masoko hayo yalijengwa miaka mingi sana iliyopita.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwepo na Kitengo katika Wizara yako kitakachofanya kazi ya kuratibu masoko yote hasa ya Vijijini ambako wananchi na wazalishaji wengi asilimia 80 wanaishi na kufanya kazi zao. Kule Rufiji kwa mfano tunahitaji huduma ya kukarabati na kupanua masoko hayo hasa ya Vijiji. Kwa mfano soko la Utete, Mohoro, Kibiti, Mkongo na Ikwiriri. Vilevile kuweko na magulio ya kuuza mazao ya wananchi kama pamba.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko kwa hotuba nzuri. Vile vile, nimpongeze Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote walioshiriki katika kuandaa Bajeti hii. Nitoe maoni au mapendekezo kama ifuatavyo:-

Kwanza, usimamizi mbovu katika kudhibiti au kusimamia mapato yanayotokana na wafanyabiashara kwa kutotoa risiti kwa kisingizio cha *VAT*. Iwapo mteja hatahitaji risiti yenye *VAT* atapunguziwa bei ya bidhaa aliyoinunua, lakini hatapewa risiti. Hii iko Dar es Salaam na kwa asilimia 90 ya wafanyabiashara wenye maduka wanajihusisha na tabia hii.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara hii ikishirikiana na Wizara ya fedha , Wizara ya Usalama wa Raia na Halmashauri husika waweke utaratibu wa pamoja ili wananchi waelimishwe umuhimu wa kulipa kodi na pia umuhimu wa kuwa na stakabadhi ya malipo (risiti).

Mheshimiwa Spika, elimu kwa umma kuhusiana na malipo na utoaji wa risiti uendeshwe mara kwa mara na kuueleza umma athari zitakazotokana na ukwepaji wa kodi na kadhalika.

- Mazingira mazuri ya kazi katika viwanda yaende sambamba na maslahi ya wafanyakazi.

- Wizara iwe na utaratibu wa kutoa mafunzo ya biashara kwa wadau kupitia au kushirikiana na Halmashauri za Wilaya kwa idadi kubwa kuliko ilivyo hivi sasa, ni watu wachache mno ndio wanafaidi.

- Wizara ielimishe wananchi juu ya soko la *AGOA* na umuhimu wa ushirika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko pamoja na Naibu wake, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji Waandamizi wa Wizara kwa kuleta Hotuba ya Bajeti inayokidhi matakwa.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu katika hoja hii unahusu zaidi utekelezaji wa mpango wa maendeleo Kusini, yaani *Mtwara Development Corridor* ambapo Shirika la Wizara, *NDC* ndilo lililopewa jukumu la kuibua na kutekeleza mipango ya maendeleo ya ukanda huo.

Mheshimiwa Spika, siridhiki na hali ya utendaji katika kuibua miradi ya eneo hili la *Mtwara Development Corridor.* Katika hotuba ya Wizara ukurasa wa nane na 60, Waziri bado haonyeshi hatua aliyofikia katika kuendeleza miradi ya mkaa wa mawe Mchuchuma na Chuma cha Liganga katika Wilaya ya Ludewa.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona mpaka sasa Wizara haitumii fursa tulizonazo ili kukabili tatizo kubwa la umeme nchini licha ya kuwa machimbo haya yaligunduliwa toka enzi za Wajerumani, lakini hadi leo hakuna lolote la maana tulilolifanya. Miaka miwili iliyopita, hapa hapa Bungeni, Mkataba wa Maelewano kati ya *NDC* na Kampuni ya *Siemens* ulitiwa saini, lakini mpaka leo hakuna cha maana kinachoendelea. Kulikuwa na ahadi lukuki, sioni chochote cha kutia matumaini.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha pia kwamba hata Mkurugenzi Mtendajiwa *NDC* Col. Simbakalia ameondoka na sasa ni Mkuu wa Mkoa wa Kigoma. Licha ya kuwa nampongeza kwa mafanikio yake binafsi, lakini ameacha pengo kubwa katika utekelezaji wa Mtwara *Development Corridor.* Tusipoangalia, itakuwa sawa na mtoto yatima asiye na wazazi.

Mheshimiwa Spika, nimeshauri mara nyingi ndani ya Bunge hili kwamba, *Mtwara Development Corridor* iwekwe katika Ofisi ya Wizara Mtambuka *(cross cutting)* kwa mfano:- Wizara ya Mipango ama Ofisi ya Waziri Mkuu ama Ofisi ya Makamu wa Rais, ama Ofisi ya Rais.

Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa *Mtwara Development Corridor* ipo Wizara ya Viwanda na Mwenyekiti ni Wizara ya Miundombinu. Ili kuendeleza *Mtwara Development Corridor* ni sawasawa tunahitaji Ofisi ama sekretarieti inayojitegemea chini ya Wizara Mtambuka.

Mheshimiwa Spika, Wizara za Miundombinu na Viwanda zina kazi nyingi katika Wizara zao kiasi kwamba hazina nafasi kushughulikia ukanda huu wa maendeleo ambao pia unahitaji kuendeleza sio tu miundombinu, bali pia kilimo, utalii, elimu, afya na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tusipounda upya mfumo wa *Mtwara Development Corridor,* sio ajabu hatutaweza kupata mafanikio yaliyokuwa yametarajiwa na mpango wenyewe.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo naunga mkono hoja.

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaunga mkono hoja ya Wizara hii. Hata hivyo, nalaani sana kile ambacho kwangu kinaonekana kuwa *double standard.* Wakati tunakazania uwekezaji katika viwanda toka nje au ndani ya nchi, tunasaidia kuviua vile vilivyokwishaanzishwa, licha ya kwamba jukumu kubwa mojawapo la Wizara siyo kuhamasisha tu uanzishaji viwanda, bali kuvilinda vile vile.

Mheshimiwa Spika, nimemzungumza na Mheshimiwa Waziri hivi karibuni na mara kadhaa nimemzungumza na Naibu Waziri, Mheshimiwa Mathayo ambaye pia alikuwepo siku Waziri Mkuu alipotukutanisha viongozi wa maeneo ya tumbaku. Kwa kifupi ni kwamba, kiwanda pekee katika Wilaya ya Iringa cha kutengeneza sigara za "Nyati", mwaka juzi kiliachiwa kuuawa na *TCC* kwa mtindo wa *corporate takeover* bila Serikali Kuu au ya Mkoa kufanya kitu. *TCC* iliwaburuza kortini wawekezaji na kushindwa katika madai yao kwamba nembo ya "Nyati" ni sawa na nembo yao ya "Farasi". Mchakato wa Mahakama uliwasababishia wawekezaji hasara kubwa na kusababisha kushindwa kulipa deni lao, ndipo *TCC* ilipowaendea na kuwanunua. Hivi sasa mashine zote zimeng'olewa, yamebakia majengo tu. Lakini muhimu kuliko yote ni kwamba tumepoteza ajira 600 kinyume na Ilani yetu.

Mheshimiwa Spika, natambua kuwa makosa haya yametendeka kabla ya Wizara hii kuundwa upya na kwamba maziwa yaliyomwagika hayawezi kuzoleka. Lakini kwa kuwa kuna uwezekano wa wawekezaji hao ambao ni wa hapa hapa nchini, wanafikiria kuwekeza katika aina nyingine ya kiwanda, ninaomba kauli ya Waziri kwamba, kiwanda kipya kitalindwa na Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, papo hapo, naomba Wizara itusaidie kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vingine katika ukanda wetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, pamoja na *reservations* zangu, naunga mkono hoja hii. Natumaini kuwa katika majumuisho, Mheshimiwa Waziri atatoa kauli niliyoomba hapo juu, vinginevyo aniandikie.

Mheshimiwa Spika, namtakia Waziri kila la kheri.

**MHE. DR. AISHA O. KIGODA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu mkuu na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi na Mashirika.

Mheshimiwa Spika, nalipongeza sana Shirika la Viwanda Vidogo Vidogo *(SIDO)* kwa kufanya vizuri hasa katika Maonyesho na kupta zawadi ya kwanza. Hongereni sana.

Lakini kuhusu suala la mikopo ambayo wanapatiwa wajasiriamali wadogo toka Mfuko wa Mitaji ya Mikoa, bado imekuwa ni tatizo. Kwanza, haitoshelezi na pili mtindo unaotumiwa kule Handeni unaleta kero hasa kwa akina mama kwani inachukua muda mrefu na wanasumbuka sana. Nadhani tatizo ni utendaji.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Meneja wa SIDO Mkoa, lakini naomba afuatilie Wilaya ya Handeni hasa Maeneo ya Segera/Michungwani/Kabuku.

Mheshimiwa Spika, kwa nini akina mama hawa huchukua muda mrefu tangu kuchangia/kulipia fomu ya kupatiwa mkopo? Sio kweli kwmaba Watendaji/wanaohusika wanatumia mtindo wa kuchelewesha hivyo kuashiria kwa waombaji kuwa wanataka chochote na kuipa picha mbaya kazi nzuri ambayo inadhamiriwa na *SIDO!*

Ni vyema uongozi uliangalie hili kwani pamoja na kuitambua kazi nzuri sana ya kuwawezesha wafanyabiashara wadogo wadogo, bado kuna malalamiko ambayo hutuletea kero!

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupatiwa masoko kwa wafanyabiashara wadogo wadogo, *SIDO* na Mashirika mengine yanajitahidisana kuwawezesha kujitegemea kufanya shughuli mblaimbali. Serikali bado haijawawezesha wafanyabiashara kupata soko zuri la ndani na nje hasa ukizingatia mfumko wa bei.

Bado huduma za kuwawezesha hazijafika Vijijini kwa walengwa. wizara iongeze juhudi Maofisa Biashara walioko katika Halmashauri Wizar ainawawezeshaje kufany akazi zao vizuri wakati wao wenyewe hawajimudu?

Mheshimiwa Waziri ana mpango gani? Kwani biashara bila utaalamu ni sawa na kutwanga maji katika kinu. tutawapa uwezo kifedha lakini bila ujuzi wa biashara hatufiki popote. Wananchi watakopa, watakopa mwisho hasara tupu. Kila la kheri. Ahsante.

**MHE. ADAM K. A. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Nazir Karamagi - Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa David Mathayo David, kwa uongozi wao wa Wizara hii na usimamizi wa malengo ya kitaifa, sera husika na utekelezaji wa awali ya Ilani ya Uchaguzi wa CCM.

Mheshimiwa Spik,a ili kuridhika na hoja hii ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, naomba nipatiwe maelezo kuhusu yafuatayo:-

Kwanza ni urari wa biashara mwaka 2005, ulikuwa na nakisi ya Dola za Marekani milioni 985.5. naomba maelezo ya kina kuhusu matarajio ya wizara ya mwenendo wa mauzo na manunuzi ya nje *(Export and Import Trends).* Ni sehemu gani na kwa muda gani tunatarajia uchumi wetu utakuwa umefika hatua ya kupunguza nakisi hii na kwa kiasi gani hali hii itakuwa imechangiwa na kuongezeka kwa mauzo kwa nchi jirani?

Mheshimiwa Spika, Kituo cha kibiashara cha Tanzania kilichoko London kimeshafanya kazi kwa muda wa zaidi ya miaka 18. Wizara inaomba pesa za kuendeshea Kituo hiki. je, Kituo hiki kimetoa mchango gani kwa uchumi wa Tanzania kutoka miaka mitano iliyopita? Ni uwekezaji gani uliopatikana kwa juhudi za Kiuto hicho na Uwekezaji umekuwa na manufaa gani kwa uchumi wa Tanzania?

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Masoko ni Sekta muhimu mno katika kuchangia kuongezeka kwa uzalishaji wa kilimo ama kwa kufungua masoko ya nje *(Export Markets)* au kwa kujenga mazingira ya mazao hayo kupata wasindikaji wa ndani wakubwa na wadogo *(large, medium and small processors).* Juhudi hii pia itadhibiti bei ya mazao hayo ya biashara.

Naomba maelezo ya kina zaidi ni mikakati gani ambayo Wizara inafanya, na ni pesa gani inayoombwa ili kukabiliana na tatizo lililotajwa kwenye hotuba ya Waziri kipengele 55(c), (upungufu wa taarifa sahihi za masoko, kwa wazalishaji, wasindikaji na wafanyabiashara).

Mheshimiwa Spika, nimeshangazwa na wepesi wa maelezo ya miradi ya Mchuchuma na Liganga na yote yatakayotokana na Uwekezaji mzuri utakaofanywa katika maeneo hayo. Uwekezaji huo ni wa mabilioni ya Shilingi za Tanzania. Tukifanikiwa ni dhahiri uchumi utakuwa maradufu. Tayari kuna taarifa za uhakika kwamba Wawekezaji kadhaa wamekusudia kuwekeza huko. Hivi karibuni Wawekezaji kutoka Australia walikuja hapa Bungeni na wakaonana na Wabunge, wakawasilisha mipango yao kuhusu kuwekeza mchuchuma na Liganga.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya Serikali ya kwamba mwaka mzima na 2006/2007 utatumika kutafuta wabia wa kuwekeza. Ni kauli isiyotosheleza, finyu mno na hailingani na kasi na malengo ya Ilani na sera ya kutukwamua kiuchumi kwa kutumia raslimali zetu.

(a) Je, *NDC* ina uwezo wa kusimamia mradi huo wa mabilioni ya shilingi?

(b) Je, Serikali imewasiliana na Serikali ya China ambao wana uwezo wa siku nyingi wa miradi mikubwa namna hii na uzalishaji wa makaa ya mawe na chuma?

Mheshimiwa Spika, naomba maelezo.

**MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri kwa hotuba yake na kuunga mkono hoja asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, tatizo la soko ni kubwa nchini. Masoko ya bidhaa za kilimo kama Mahindi ni tatizo kubwa. Naomba Wizara ianzishe Mfumo wa Stakabadhi za mazao ghalani kwa Wilaya ya Songea, kwani wakulima wa mahindi wanakaribia kukata tamaa juu ya bei ndogo ya mahindi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uwingi wa mahindi katika Mkoa wa Ruvuma, naomba Serikali ianzishe eneo huru la uzalishaji wa Bidhaa za kuuza nje *(EPZ)*.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mkoa huu tungewahamasisha zaidi juu ya kilimo cha mahindi, kwani mazao yao yangeweza kusindikwa na hivyo kuongeza dhamana ya bidhaa zao.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa *SIDO* kwa kazi nzuri ya kufundisha wajasiriamali wadogo na kuwaendeleza. Naomba Wizara iongeze fungu kwa *SIDO* Mkoa kwani wana hali ngumu. Pia, wafanyakazi hawatoshi, hivyo ni vizuri wakaongeza wafanyakazi ili waendane na kazi na majukumu mengi waliyonayo.

Mheshimiwa Spika, *CARMATEC* ingesambaa Mikoa yote kama *SIDO* ingesaidia wananchi kwa kiwango kikubwa. Naunga mkono hoja.

**MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSMY:** Mheshimiwa Spika, ni vyema nimwombe Muumba aniwezeshe kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hayo, sasa naomba nianze kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nianze kwa masikitiko kwa Serikali yangu juuya viwanda vyetu hapa nchini kunasibishwa. Serikali imeamua kuvitoa viwanda vyetu ambavyo viliweza kumsaidia mwananchi wa nchi hii kujipatia mahitaji kwa bei nafuu, pia, kuuza bidhaa yake kwa njia rahisi.

Serikali hivi sasa inafahamu umuhimu wa mnyama kama vile ng'ombe. Pamoja na kupata maziwa, nyama, lakini hata ngozi ni mali. Biashara ya ngozi ni nzuri. Nchi yetu iliweza kuwa na kiwanda cha viatu, kiko wapi sasa? Tumekosa kiasi gani cha mahitaji hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bandari zetu, ni jambo gani linalosababisha kucheleweshwa kwa mizigo bandarini hali ya kuwa chombo kipo *TISCAN*? Usumbufu huu hupelekea kuharibika kwa vitu vya watu pamoja na kuibiwa kwa baadhi ya mali za watu. Vifaa vya magari mara nyingi huibiwa katika Bandari zetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bandari ya Zanzibar na Tanzania Bara, ni kwa nini kinacholipiwa Zanzibar ukija nacho Tanzania Bara kilipiwe tena? Serikali haioni ni tatizo? Ni vyema Serikali zetu zingeweza kukaa pamoja ili tatizo hili litafutiwe ufumbuzi. Dosari kama hizi zipo katika nchi zetu. Ukienda *TRA* Zanzibar na ukija *TRA* Tanzania Bara, utaona kuna mambo ambayo hata kuyaeleza ni vigumu. Gari yenye namba ya Zanzibar ni kosa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mazao ya wakulima katika nchi yetu. Serikali haioni umuhimu wake? Kuna utafiti wa mazao kwa wakulima wetu? Wakulima wa machungwa

ama mananasi, hayaonekani, wakulima wanapata hasara kwa kuuza kwa mazao yao. Serikali haioni ipo haja ya kuwa na viwanda vya kutosha ili mazao yao yasiharibike?

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa Mradi wa Makaa wa Mawe (Mchuchuma) na wa Chuma (Liganga), Waziri anasema katika mwaka 2005/2006 wamefanya maandalizi ya utekelezaji hadi kufikia hatua ya kubainisha wawekezaji (ukurasa wa nane, sehemu ya 10b).

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa 60, Waziri amesema katika mwaka 2006/2007, juhudi za Wizara ni kuanzisha viwanda mama, kwa kutafuta wabia wa kuwekeza katika Mradi wa Makaa ya Mawe (Mchuchuma) na wa Chuma (Liganga).

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa nane, Wizara inabainisha Wawekezaji katika ukurasa wa 60. Wizara inasema, inatafuta wabia wa kuanzisha viwanda mama. Je, Wawekezaji wanaobainishwa katika ukurasa wa nane ni katika shughuli gani? Viwanda mama vinavyohusika na Makaa ya Mawe na Chuma ni vipi hivyo?

Mheshimiwa Spika, mimi naamini miradi hii mikubwa miwili inaweza kutekelezwa kila moja peke yake, yaani:-

(i) Makaa ya mawe yanaweza kuchimbwa na kuuzwa nje na ndani ya nchi ili mradi miundombinu ipo.

(ii) Makaa ya mawe yanaweza kutumika katika kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Spika, katika haya mawili, hakuna cha kiwanda mama.

Mheshimiwa Spika, taarifa niliyonayo ni kwamba, eti Chuma cha Liganga kinahitaji utafiti zaidi ili kujua kipo kiasi gani na imesambaa vipi. Hapa ndipo tunaweza kuzungumzia viwanda mama kwa kutumia kitalu kimoja kuyeyusha chuma kwa kutumia mkaa nje ya Mchuchuma kuzalisha "*Sponge/pig iron*" kwa ajili ya viwanda vikubwa na vidogo bila kuathiri mradi mkubwa wa Liganga/Mchuchuma.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua ni mambo gani ya uhakika yanayotarajiwa kuanza kutekelezwa Ludewa na kwa utaratibu upi. Tumezungumza miradi hii kwa muda mrefu hadi wananchi wamekata tamaa. Tuanze kutekeleza ilani ya *CCM* na *MKUKUTA* kwa kuchagua shughuli za maendeleo zinazoweza kuanza kesho wakati tunaandaa mradi mkubwa ili Watanzania wa leo tufaidi matunda yanayotokana na rasilimali za Liganga na Mchuchuma.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, sasa hivi viwanda vipo vingi katika Mkoa wa Dar es Salaam, lakini maeneo mengine, hakuna viwanda. Je, Serikali sasa haioni kuna umuhimu wa kupeleka viwanda Lindi ambako hakuna viwanda, ukizingatia kuwa *gas* sasa inapatikana Lindi na Mtwara kwa ajili ya Nishati hasa Viwanda vya Mbolea?

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi katika viwanda vilivyobinafsishwa vya Taasisi za Umma, wengine hadi leo hawajapata viinua mgongo vyao. Tunakuomba Mheshimiwa Waziri ashirikiane na Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, kuwahimiza ili watumishi hawa walipwe ili kuweka heshima ya viwanda vilivyopo. Nilipokuwa ninatembelea Viwanda na mashamba ya Taasisi za Umma kama Mjumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara na Viwanda, nimepata malalamiko mengi kutoka katika viwanda na mashamba yaliyobinafsishwa kuwa, hawakulipwa mafao yao. Maeneo hayo ni: Mashamba ya Mbarali, watumishi 170 bado kulipwa; Mashamba ya *Hanang W. Complex,* watumishi 400; Kiwanda cha Mkate *Saw Mill;* Kiwanda cha Chuma Tanga; na Mashamba ya Mpira Muheza.

Mheshimiwa Spika, mashamba na viwanda hivyo bado kulipwa mafao yao hivyo. Heshima ya Viwanda inapotea. Tafadhali naomba Mheshimiwa Waziri afuatilie suala hilo.

Mheshimiwa Spika, suala la Biashara na nchi za nje, hasa nchi za *SADC* zinakuwa ngumu sana kutokana na kutowawekea mazingira mazuri ya biashara. Katika Kikao cha *SADC* cha mwaka 1997 na kurudiwa tarehe 2004, kiliamua kuwa na ufunguzi wa Biashara na nchi ya Tanzania, *Mozambique*, Malawi, Zambia na Afrika ya Kusini. Ili biashara hiyo ifanyike, basi kuwepo na kitu kinachoitwa *Mtwara Corridor.* Lakini hadi leo suala la Mtwara *Corridor* halijatetekelezwa, hivyo kufanya biashara Kusini kuwa ngumu. Tunaomba biashara iendelezwe kati ya Tanzania na nchi za *SADC*.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja iliyopo mbele yetu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Chuma cha Tanga ni Kiwanda ambacho kilisaidia kuongeza ajira kwa wakazi wa Tanga, pia kupata unafuu wa vyuma na misumari. Cha kusikitisha, Kiwanda hiki kimekufa kifo cha mende. Hata wafanyakazi waliofanya kazi hapo kabla Kiwanda kupewa wawekezaji toka nje hawajalipwa haki zao. Baya zaidi, hao wawekezaji wa sasa wanakiendesha kiwanda kile watakavyo wao hata ajira zao pia zimekuwa ni shida kupatikana.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Mbolea nacho kilikuwa ni Kiwanda ambacho kiliinua hali ya uchumi kwa Tanga na ni kiwanda ambacho kilijengwa katika eneo zuri na kilikuwa karibu na bahari ambayo ilikuwa ni wepesi kwa kushushia mali ghafi pindi zinapoletwa na meli. Cha kushangaza, kiwanda kimeuzwa na sasa hivi kimenunuliwa na Kampuni ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali itueleze ni sababu zipi zilizopelekea kufa kwa Kiwanda cha Mbolea?

Mheshimiwa Spika, vilikuwepo viwanda binafsi kama vile Kiwanda cha Sabuni cha Kiran kilichokuwa eneo la Gofu.

Kiwanda hiki kilisaidia pia kutoa ajira kwa vijana na kupunguza wimbi la vijana wazururaji. Cha kushangaza, kiwanda hiki kimefungwa na hata majengo yake yamebaki yanaharibika na isitoshe wezi wanaiba hata mabati yaliyoezekewa majengo ya kiwanda hicho na huenda hata baadhi ya mashine zimeibiwa katika muda huu ambao kiwanda hakifanyi kazi.

Mheshimiwa Spika, kiwanda kingine kilikuwa ni Kiwanda cha Plastiki Amboni. Kiwanda hiki kilisaidia kutoa bidhaa zilizotengenezwa kwa Plastiki kama ndoo, mabeseni na kadhalika. Kiwanda hiki kimekufa na hata mitambo, kuna taarifa isiyo rasmi kuwa imeuzwa Dar es Salaam kwa Kampuni ya Simba Plastiki. Hivi kulikuwa na sababu gani ya kuhamishia mitambo toka Amboni Tanga kupeleka Dar es Salaam? Je, Serikali haikuona kuwa inaua ajira hususan kwa vijana? Vijana wafanye nini ikiwa viwanda vyote kwa makusudi vimeuliwa?

Mheshimiwa Spika, pia hapo zamani kulikuwepo na Kiwanda cha Kusindika Mafuta ya nazi. Mafuta ya nazi ni mafuta ambayo hayana tatizo kwa mlaji ukilinganisha na mafuta kama *Korie, O.K.* na mengineyo ambayo yana matatizo kwa afya za binadamu.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda hicho cha Kusindika Mafuta ya Nazi kilijulikana kama *"Nooran Industries"*. Je, Serikali haioni huu ni wakati muafaka kwa kuanza kusindika mafuta ya nazi ambalo ndio zao kuu kwa Mwambao wa Tanga? Mafuta ya nazi yangeongezea ubora wa mafuta yetu kama tunavyotumia mafuta ya alizeti, karanga, pamba mazao yanayolimwa hapa hapa kwetu Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda kingine kilikuwa ni Kiwanda cha Mbao cha *"SIKH SAW MILLS",* Kiwanda ambacho kilipanua wigo wa ajira. Kiwanda hiki pia kiliweza kuzalisha bidhaa ambazo ziliuzwa katika masoko mbalimbali. Kiwanda hiki pia ni sawa na kufa kabisa. Uzalishaji wake ni mdogo sana kiasi cha kuingiza hasara badala ya faida. Naiomba Serikali ifanye utaratibu wa kuhakikisha Kiwanda hiki kinafufuliwa na kufanya kazi ili kukuza ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kuna Kiwanda cha Mafuta ya Kujipaka eneo la Duga kinaitwa "Podoa". Wamiliki wa Kiwanda hiki ni Wahindi. Wahindi hawa wanawadhalilisha sana wafanyakazi katika Kiwanda hicho. Kuna wafanyakazi ambao kwa muda mrefu ni vibarua tu hawajaajiriwa. Huu ni utaratibu wao kwamba, huajiri vibarua ili kuepuka kulipa haki zinazostahili iwapo wataajiriwa.

Mheshimiwa Spika, bila kusahau, Kiwanda cha Ngozi cha Mwanza *(Mwanza Tanneries):* Je, Serikali ina mpango gani wa kukifufua Kiwanda hiki ukizingatia Mwanza kuna wafugaji wengi ambao wangeuza ngozi zao Kiwandani hapo? Hii inapelekea pia wafugaji kuzitupa ngozi zao kwa vile wameona hawana mahali ambapo watauza na kuweza kuwaingizia kipato.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Spika, wakati mradi wa uchimbaji wa *gas* wa Songosongo unaanza, kulikuwepo pia na mpango wa kujenga kiwanda cha mbolea huko Kilwa Masoko.

Wananchi waliyaacha makazi yao na kutoa eneo kwa ujenzi wa kiwanda hicho. Eneo hilo lipo hadi leo, limetengwa kwa madhumuni hayo. Lakini cha kushangaza, hadi leo hii kiwanda hakijajengwa na hata ile fununu ya kwamba kitajengwa hakuna.

(1) Je ni lini kiwanda hicho kitajengwa huko Kilwa Masoko?

(2) Je, bado mpango huo wa ujenzi wa kiwanda hicho upo au hakuna? Ni zipi sababu za kutojengwa, kama jibu litakuwa haupo mpango huo?

(3) Kama Serikali iliamua kujenga sehemu nyingine, naomba nifahamishwe ni wapi? Pia, naomba nifahamishwe, nini maana au faida ya wananchi kuwa na maliasili au mradi katika eneo lao au Wilaya yao wakati wao wenyewe hawawezi kufaidika na rasilimali hizo? Mfano, Kiwanda cha kusafishia *gas* ambayo imepatikana Kilwa, kipo Dar es Salaam na ajira wamepelekewa wananchi wa Dar es Salaam. Kiwanda cha mbolea ni Mkoa gani watapelekewa ili wananchi nao waweze kupata ajira na isiwe Wilaya ya Kilwa?

Naunga mkono hoja na ninaomba majibu ya maswali yangu.

**MHE. USSI AMME PANDU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kuchaguliwa kwao na Mheshimiwa Rais kuwa ndio ambao watamsaidia katika kufanikisha majukumu ya Wizara hii. Kuchaguliwa kwenu ni ishara tosha juu ya uwezo mliokuwa nao.

Mheshimiwa Spika, pia nataka kuchukua nafasi hii kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Mtoni kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi na mimi nawaahidi kuwatumikia kwa nguvu zangu zote.

Mheshimiwa Spika, nataka kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara hii kwa jinsi inavyokuza maendeleo ya Taifa katika Sekta za Viwanda na Masoko pamoja na Biashara katika kukuza uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye hoja ya kuchangia Wizara hii ukurasa wa 58 nataka nilipongeze Shirika hili la Viwango Tanzania *(TBS)* kwa jinsi linavyoendelea na majukumu yake ya uwekaji wa viwango vya ubora wa bidhaa pamoja na usimamiaji wake.

Mheshimiwa Spika, najua kwamba lengo la Wizara hii ni kumsaidia mwananchi wa Tanzania kutumia vitu vilivyo bora kwa viwango kama chakula, nguo na kadhalika. Katika majukumu yake, Shirika hili baadhi ya wakati huwa linaingiliana na *TFDA*

(Taasisi ya Chakula na Madawa) jambo ambalo sio zuri. Hivyo, namuomba Mheshimiwa Waziri wakati wa kujibu hoja anieleze kupitia Bunge hili, ni lini atafanya marekebisho ya Sheria ili kuondoa mwingiliano katika Taasisi hizi mbili?

Mheshimiwa Spika, mwisho, naipongeza kwa mara nyingine Wizara hii na naunga mkono hoja kwa asilimia mia.

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko. Nampongeza pia Naibu Waziri wake na Katibu Mkuu na Wataalam wote bila kusahau Kamati husika za Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mpango wa MKUKUTA, kupunguza umaskini, aidha, ilani imesisitiza kipaumbele kiwekwe katika shughuli za kupunguza umaskini kwa kupanua ajira kwa wananchi wakiwemo vijana na wanawake. Mpaka hivi sasa Serikali bado haijaweza kuvitambua vikundi vya vijana na vikundi vya wanawake wanaotafuta ajira na kuwasaidia katika kujiajiri kibinafsi na kadhalika?

Kipaumbele cha pili ni katika eneo la kuendeleza ujasiriamali katika viwanda vidogo vidogo na biashara ndogo ndogo na muhimu zaidi katika masoko, ambalo ni eneo linalokera sana wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, elimu ya biashara kwa wafanyabiashara ndogo ndogo na hasa wanawake ni muhimu sana! Pamoja na kutegemea *NGO's* na Taasisi mbalimbali katika kutoa mafunzo ya biashara kwa mfano *Haus Seidel Foundation* na kadhalika! Serikali pia ni lazima iweke bidii katika kuwapatia mafunzo ya biashara kwa wananchi na hasa wanawake.

Suala la uwezo mdogo wa mitaji ni kwa wananchi wote, wakiwemo wanawake na vijana. Suala lingine muhimu ni lile la taarifa za masoko kutopatikana kwa urahisi, masoko ya nje na ya ndani pia, kwa wazalishaji na wafanyabiashara wadogo wadogo. Mauzo ya nje na hasa katika eneo la vifaa vya utamaduni *(handcrafts)* pamoja na vipodozi na vyakula vya kuandika, vinayozalishwa na wanawake havina soko.

Mheshimiwa Spika, pamoja na sababu za kuwa, vifaa hivyo bado havijafikia viwango vinavyotakiwa, bado hata vile vinavyokidhi viwango havipati soko la uhakika na la kudumu. Mauzo ya nje kuhusu mazao kama vile vanilla, michaichai, mitonge (mbegu) miarobaini, *Aloe Vera* na kadhalika, bado mafunzo na soko katika eneo hili hayajapatikana, kwa hiyo, kukosesha nchi yetu mapato zaidi. Dar es Salaam, ni Mkoa unaoweza kuzalisha zao la mhogo kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itahamasisha wanawake na vijana Mkoani katika ukulima wa mihogo na kuwapatia nyenzo na ardhi ili waweze kulima mihogo ili kupunguza umaskini na hasa Vijijini na Mijini. Aidha, Serikali ijitahidi sana kutoa mafunzo ya usafi kwa wafanyabiashara wakubwa na wadogo wote na hasa katika

viwanda, katika masoko ya kuuzia vyakula na pia kwa mama lishe Miji na maeneo mengine ili kupunguza maambukizi ya maradhi. Naunga mkono hoja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ili kukuza uchumi wa Taifa hili ambalo uti wa mgongo ni kilimo, ni muhimu sana kiwepo kwa viwanda vya kutosha kwa ajili ya kusindika mazao ya kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Spika, viwanda vyetu hapa nchini vimekuwa vikishindwa kufanya kazi kama ilivyotarajiwa na nchi yetu badala ya kuangalia jinsi ya kuboresha viwanda hivi. Serikali inaona jambo la kawaida kabisa viwanda vyetu kufa na kuendelea kuoza bila shughuli yoyote.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali itueleze, ina mpango gani na kiwanda cha *Tanganyika Packers* kilichopo Kawe ambacho kilisaidia sana kusindika mazao ya mifugo na kilimo na hivyo kuwapatia wananchi *quality packed foods* kwa bei nzuri na zaidi sana kilisaidia kutoa soko zuri kwa wakulima na wafugaji na hivyo kuleta tija kwa kazi yao. Kwenye majibu ningependa kujua yafuatayo:-

(1) Kwa kuwa wakulima na wafugaji wa Tanzania moja ya tatizo kubwa walilonalo ni kukosa *processing industries,* Serikali ina mpango gani wa kufufua kiwanda hiki cha *Tanganyika Packers* ili kusaidia wakulima na wafugaji?

(2) Serikali inaandaa utaratibu wa kujenga machinjio ya kisasa Jijini Dar es Salaam, sambamba na kuzalisha nyama kwa wingi kwenye machinjio hayo. Serikali imeandaa utaratibu gani wa kuwa na mpango endelevu wa kuhifadhi *products* kutoka kwenye machinjio haya?

(3) Ikiwa hakuna mpango wa kufufua kiwanda cha *Tanganyika Packers,* nini hatima ya majengo hayo na Serikali inapanga kubadili majengo hayo kwa kazi gani?

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima na afya na kuniwezesha kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko. Pia, nawashukuru wananchi wa jimbo la Fuoni kwa kukipa heshima Chama cha Mapinduzi kwa kukichangia kwa kura nyingi katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 ambapo heshima hiyo imeniwezesha kuwa Mbunge wa Jimbo hilo.

Nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa majukumu waliyonayo na kuweza kuyatekeleza kwa makini na kwa ufanisi kabisa. Pia niwapongeze Katibu Mkuu na Timu yake kwa kumshauri vizuri Mheshimiwa Waziri na kuweza kutengeneza hotuba hii yenye mvuto na maelekezo yenye kuleta matumaini katika kukuza uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, sasa niipongeze Wizara kwa kusimamia na kuandaa maonyesho ya Kitaifa ya Saba saba. Maonyesho yalikuwa mazuri na wananchi wa ndani na nje ya nchi walifurahika nayo japokuwa kulikuwa na kasoro ya harufu mbaya

iliyotokana na dampo lililo karibu na uwanja huo. Hali hiyo haikuzuwia wananchi kufanya shughuli zao japo kuwa ilikuwa ni kero kwa wengine.

Mheshimiwa Spika, maonesho yaliyofanyika yalikuwa ni kivutio kikubwa kwa kujua mambo mengi yanayofanywa na Taasisi zetu za kitaifa na za kibinafsi, lakini pia kulikuwa na biashara za aina kwa aina kutoka kila Mikoa ya Tanzania, lakini bei za bidhaa zilikuwa ghali sana, ukilinganisha na kiingilio cha milangoni pamoja na ukodishwaji wa majengo.

Mheshimiwa Spika, Vitu hivi vilichangia kwa kiasi kikubwa bidhaa zilizouzwa katika mabanda ya maonyesho kuonekana ni bei ghali sana na baadhi ya wananchi kulalamikia hali hiyo. Kwa hiyo, ili kufanikisha maonesho yetu, ninaishauri Serikali kupitia Wizara hii kupunguza bei za viingilio katika viwanja ili waweze kupunguza hali hii na kufarijika wanunuzi na watembeleaji wa mabanda hayo pamoja na wafanyabiashara kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, sina budi kuipongeza Serikai kwa nia nzuri ya kubninafsisha baadhi ya viwanda vyetu kwa wafanyabiashara kwa lengo la kuviendeleza ili kuongeza ajira, uzalishaji, pia kulipatia mapato Taifa. Lakini inaonesha kwa baadhi ya viwanda hivyo ni kinyume na matarajio ya Serikali. Kuna viwanda bado havijaanza kazi na vimechukuwa muda mrefu na kusababisha hasara kutokana na malengo ya Taifa.

Ili kunusuru malengo na matarajio yetu, ninaishauri Serikali ipitie tena mikataba ya makubaliano na ikionekana kuna kinyume, basi viwanda hivyo wapewe wawekezaji wengine au Serikali iviendeleze wenyewe.

Mheshimiwa Spika, pia ninashauri kuanzia sasa anayetaka kuwekeza au kununua viwanda vyetu, kuwe na mikakati ya kuangaliwa mwekezaji huyo uwezo wake na pia kuwe na masharti kutokana na malengo ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuna wafanya biashara hawaitakii mema nchi hii na hufanya biashara zao kwa kutumiliwa na maadui zetu. Kwa hivyo suala hili tuliangalie kwa vizuri sana. Kwa machache naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Nianze kwa kusema kuwa ninaiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu kabla sijachangia hoja hii, niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote waliochangia katika Bunge lako Tukufu, kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa ushindi wake alioupata katika Uchaguzi wa Urais na Uenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Nampongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa kwa kuteuliwa kwake na Mheshimiwa Rais na kuthibitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Waziri wetu Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikupongeze wewe mwenyewe kwa kuchaguliwa na Waheshimiwa Wabunge kuwa Spika wetu wa Bunge hili Tukufu. Aidha, nimpongeze Mheshimiwa Anne Makinda kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge hili Tukufu. Nawapongeza Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Job Ndugai, kwa kuchaguliwa kwao kuwa Wenyeviti wetu wa Bunge hili. Nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Waziri wote kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais katika nyadhifa zao.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe shukrani za pekee kwa wananchi wa Jimbo la Same Magharibi kwa kuwa na imani na mimi na kwa kunichagua kwa kura nyingi sana kuliongoza Jimbo lao. Aidha, napenda kuwaahidi kuwa nitawatumikia kwa uwezo wangu wote. Ninawaahidi ushirikiano wa dhati katika kuendeleza Jimbo la Same Magharibi na Wilaya ya Same kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa, sasa nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais kwamba nitakuwa mwaminifu na mwenye hekima na utiifu mkubwa katika kutekeleza majukumu ambayo amenipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shukrani zangu za pekee ninazitoa kwa Mheshimiwa Nazir Karamagi, Waziri wangu kwa kunitia moyo na kunisaidia katika kutekeleza kazi zangu.

Namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara yetu, Ndugu Wilfred Nyachia, Wakurugenzi pamoja na Wafanyakazi wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa ushirikiano mkubwa ambao wametuonyesha.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumshukuru mke wangu Pamela na mtoto wangu Lina kwa kunitia nguvu na kunipa moyo wakati wote wa kazi na majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda sasa niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii ama kwa kuongea au kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, nitajibu hoja chache za Kamati ya Uwekezaji na Biashara na pia nitajibu hoja moja ya Mheshimiwa Aloyce Kimaro.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara imetushauri kwamba, Wizara ijaribu kuweka vigezo vizuri kwa ajili ya uwezekaji wa maeneo ya *EPZ*. Ushauri huo tumeshaupokea na tulishaanza kuufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia imezungumzia suala la viwango vidogo vya ruzuku ambavyo Taasisi zetu zinapata. Ni kweli kabisa kwa miaka trakriban 20, Serikali haitoi fedha za matumizi ya kawaida, yaani *OC* kwa Taasisi hizi. Lakini mwaka 2005/2006 Wizara ilitoa Shilingi bilioni 5.1 kwa ajili ya Taasisi zetu hizi. Fedha hizi zilitolewa kulingana na makusanyo ya Serikali kwa kila mwezi. Hata hivyo, ushauri unapokelewa na utafanyiwa kazi kulingana na mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge vilevile imeshauri kwamba tuangalia masoko ya Makambako yasije yakawa sawa na lile soko la Kibaigwa. Ni kweli kabisa soko hili lilikuwa na matatizo ya kiutendaji ama matatizo ya kiuongozi yaliyosababishwa na kuwepo kwa soko moja linaitwa Kinangari mita 500 kutoka kwenye soko hilo la Kibaigwa. Soko hili la Kinangari limeshafungwa kwa agizo la Mkuu Mkoa mwanzo mwa mwezi Juni, 2006 na hivyo soko la Kibaigwa linaendelea vizuri na linakusanya ushuru vizuri.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati imetushauri kwamba, tuweze kuisaidia *General Tyre,* kusudi iweze kujaribu kutafuta mwekezaji ambaye anaweza kuongoza mashamba ya mpira yale ya Muheza, Kilombero na Zanzibar. Kwa kuwa suala hili la Kiwanda hiki cha matairi ni suala mtambuka, Wizara yangu itashirikiana na itawasiliana na *PSRC*, Wizara ya Fedha pamoja na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa ajili ya kutatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuzungumzia urasimu wa kutoa shehena bandarini. Ni kweli kabisa mimi nakubaliana na Kamati ya Uwekezaji na Biashara na suala hili pia ni mtambuka na linahusisha Wizara na Taasisi nyingi na Mashirika mbalimbali ikiwa ni pamoja na Wizara yangu yenye dhamana ya kuwawezesha wafanyabiashara kufanya biashara hizo. Wizara itawasiliana na wadau wote hao ili kuhakikisha kwamba utatuzi wa suala hili unafanyika mara moja.

Mheshimiwa Spika, Kamati vilevile imeshauri wafanyabiashara waelimishwe kuhusu kuwepo kwa Tume ya Taifa ya Ushindani ambayo kazi yake ni kusuluhisha wafanyabiashara ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yake. Ushauri huu tumeuchukua.

Mheshimiwa Spika, limetokea suala la harufu mbaya kutokana na dampo pale uwanja wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere wa maonyesho juzi wakati wa Saba Saba. Taarifa hizi tumeshazipeleka kwa Taasisi zinazohusika na shimo hili litafukiwa. Kwa hiyo, kwa maonyesho mengine yanayokuja mwaka kesho, kutakuwa hakuna tatizo hili tena.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la viwanda vinavyobinafsishwa halafu vinabadilisha matumizi yake. Naomba nitoe mfano mmoja. Kwanza niseme kwamba, unapomuuzia mwekezaji kiwanda na akalipa kwa asilimia mia moja, huwezi tena kumwekea masharti kwamba ufanye hivi.

Tunasisitiza kwamba kama umenunua kiwanda kinatengeneza nondo aendelee kutengeneza nondo ili bidhaa ile iwepo. Lakini hatuwezi tukamlazimisha kama hapati malighafi ama hapati soko, tukamlazimisha kuzalisha kitu ambacho hatauza. Kwa hiyo, kama ameshalipia hiyo, hatuwezi tukamwingilia, hata kwa kisheria atatushinda. Lakini viwanda vile ambavyo Serikali ina hisa, hapo tuna uwezo wa kumwambia mtu ama mwenye kiwanda kwamba wewe sasa usibadilishe matumizi ya kiwanda hiki, kwa sababu na sisi tuna hisa pale.

Mheshimiwa Spika hatima ya wafanayakazi ambao wanaachishwa kazi kutokana na kiwanda kuuzwa ama kufungwa, vilevile viwanda ambavyo vinaweza kuendelea kuwaajiri wafanyakazi wale wale na vinaweza kuwalipa baada ya kubinafsishwa, kama mtu anataka kutoka, basi atalipwa mkono wa kheri. Lakini kama kiwanda hicho kinafungwa na hakiwezi kikalipa mshahara wowote, mfanyakazi analipwa mshahara wa mwezi mmoja badala ya *notes,* analipwa mshahara wa mwezi moja badala ya likizo zote za malimbikizo, analipwa fedha za kusafirisha familia yake pamoja na mizigo. Hiyo inaitwa ni mafao ya kisheria. Lakini kama kiwanda kinaweza kikamlipa zaidi, basi tunaita mkono wa kheri.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Kiwanda cha Madawa Moshi, kile kiwanda kilikuwa hakizalishi mwaka 2003, stahili yao ilikuwa ni Shilingi milioni 19, kama kingekuwa kinazalisha stahili yao ilikuwa ni Shilingi milioni 77. Kwa hiyo, walishalipwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutumika kwa makaa ya mawe, Kamati ya Uwekezaji na Biashara imetushauri kwamba viwanda vitumie makaa ya mawe ya Tanzania badala ya kuagiza kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi, sehemu pekee inayozalisha makaa ya mawe na kuuza ni Kiwira. Uwezo wa Kiwira wa kuzalisha makaa ya mawe kwa mwezi ni tani 1,000 tu. Wanunuzi wakubwa wa makaa ya mawe ya Kiwira ni Mbeya *Cement.* Mbeya Cement inahitaji tani 3,000 na ndiyo maana kiwanda cha Tanga kinaagiza kutoka nje na pia kiwanda cha Mbeya nacho kinaagiza kutoka Malawi ili kuweza kuziba lile pengo ambalo linatokana na Kiwira kutozalisha makaa ya mawe ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya gesi, kwa nini viwanda vingi vinatumia gesi, lakini bei ya bidhaa hazishuki, kwanza, niseme kwamba, gesi ile haitumiki kuzalisha umeme. Ile gesi inatumika kwa ajili ya *heat energy,* yaani kutoa joto katika mchakato mzima wa kuzalisha viwandani. Sasa bei ya gesi ni asilimia 75 mpaka asilimia 80 ya *heavy finest oil,* ile *oil* iliyokuwa inatumika mwanzoni. Asilimia hiyo ni punguzo la asilimia 20 mpaka asilimia 25 ambazo hazitoshi kusababisha *impact product*, yaani *impact* ya vitu vinavyozalishwa kutoka viwandani, kwa sababu gesi ile ni sehemu ndogo sana ya gharama za uzalishaji

Mheshimiwa Spika, gesi ama matumizi ya gesi ni asilimia 10 tu hadi asilimia 15 ya gharama zote za uzalishaji. Kuna gharama za *raw material*, kuna gharama za

umeme, maji na *labour*. Kwa hiyo, sio kwamba eti ile gesi ndiyo inazalisha umeme, hapana. Umeme lazima utatumika.

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 2005 *Ginger jowl* moja ambayo ni sawa na lita 22 za hiyo *heavy oil* ilikuwa inauzwa kwa Sh. 5,000/=, sasa hivi ni Sh. 10,000/=. Maana imeshaongezeka mara mbili. Lakini *crate* moja ya bia ilikuwa inauzwa Sh. 15,500/= mwaka 2005, lakini sasa hivi *crate* moja ya bia inauzwa Sh. 16,500/=, imeongezeka kwa asilimia 10 tu.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, hata pamoja na kwamba bei ya mafuta inavyoongezeka na bei ya gesi inaongezeka, bei ya bidhaa bado hawakuongeza kwa uwiano ule wa kuongezeka kwa gesi. Kwa maana hiyo, ni kwamba, pamoja na kutumia gesi, bado gharama nyingine zinaongezeka na kwa hiyo, zinafunika ule unafuu wa kutumia gesi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lilikuwa ni uboreshaji wa *Board of External Trade (BET).* Sasa hivi Wizara yetu kwa kushirikiana na *BET, BET* inaboreshwa. Hatua hizo za kuboresha *BET* ni pamoja na zifuatazo:-

- Kuandaa Mpango Mkuu wa kuendeleza *BET;*
- Kuandaa Mpango Mkuu wa kuendeleza uwanja, yaani *Master Plan* katika mwaka huu wa fedha;
- Kujenga *hall* jipya la mita za mraba 1,600;
- Kuboresha mazingira ya kuwekeza katika kuendeleza miundombinu ya uwanja, zikiwemo barabara pamoja na majengo; na
- Kujenga jengo kubwa la Mikutano na maeneo ya kufanyia biashara.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda kumjibu Mheshimiwa Aloyce Kimaro, moja ya hoja yake ya ukaguzi wa magari Japan.

Mheshimiwa Spika, kule Japan, Dubai pamoja na Hong Kong, labda niseme kwamba, *TBS* mwaka 2001 ilianzisha kiwango cha magari yaliyotumika. Kiwango hicho ni namba 698 cha mwaka 2001.

Nilitoa tangazo Octoba, 2001 kwamba, tunataka tuelimishe wananchi na wafanyabiashara, ambao wanataka wakakague magari huko nje katika magari haya ambayo yametumika ambayo yanatoka Japan, Dubai na Hongkong, waje kwenye mkutano tarehe 8 Machi, 2002. Waliokuwa wanahitaji biashara hiyo, walifika na makampuni yanayotoka nje na wale wa ndani waliandika *applications* zao.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga hoja mkono.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako, kwa kunipa nafasi hii ya kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kabla ya kujibu hoja hizo, napenda kuwashukuru kwa dhati, Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri na yenye manufaa, waliyoitoa kwa kauli na kwa maandishi. Michango hiyo itatusaidia sana na itaendelea kutusaidia katika kuboresha utendaji wetu wa kazi katika nyanja zote.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuishukuru sana Kamati ya Uwekezaji na Biashara, chini ya uongozi mahiri na makini wa Mheshimiwa William H. Shellukindo. Chini ya uongozi Kamati imekuwa mstari wa mbele na imekuwa ikichukua juhudi kubwa katika kuelekeza, kuongoza na kushauri Wizara yangu bila kuchoka. Tunawashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati hii na nachukua nafasi hii kuwahakikishia kwamba, Wizara yangu inathamini sana na kuenzi juhudi kubwa na mchango wao wanaoutoa kwa ajili ya maendeleo sio tu ya sekta ya viwanda na biashara na masoko, bali kwa uchumi wa nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mbunge wa Viti Maalum kupitia Chama cha CHADEMA, kwa mchango alioutoa alipokuwa akichangia hotuba yangu. Ametoa hoja nyingi na amegusia maeneo mbalimbali, nitajitahidi kugusia baadhi yake tu kutokana na ufinyu wa muda.

Mheshimiwa Spika, ili niweze kutoa muda, hoja ambazo sitazijibu wakati nazungumza sasa hivi, napenda kwanza niwatambue Wabunge ambao wametoa michango yao kwa kuzungumza humu humu Bungeni, ambao ni kama wafuatao: Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Ahmed M. Shabiby, Mheshimiwa Mohammed Amour Chombon, Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro na Mheshimiwa Chrisant M. Mzindakaya.

Pia nawashukuru Wabunge waliochangia kwa maandishi, ambao ni wafuatao: Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Devotha M. Likokola, Mheshimiwa Aziza S. Ali, Mheshimiwa Athumani S. Janguo, Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama, Mheshimiwa Masola C. Masola, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mheshimiwa Adam K. Malima, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili, Mheshimiwa Grace S. Kiwelu, Mheshimiwa Martha J. Umbulla na Mheshimiwa Savelina S. Mwijage.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Mwanawetu S. Zarafi, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed,

Mheshimiwa Janet B. Kahama, Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia, Mheshimiwa Salum Ahmed Khamis, Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mheshimiwa Aggrey D.J. Mwanri, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Mohamed R. Abdallah, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Dr. Aisha O. Kigoda, Mheshimiwa Ali Haji Ali, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mheshimiwa Dr. Emmanuel J. Nchimbi, Mheshimiwa Dr. Diodorus B. Kamala, Mheshimiwa Dr. Guido G. Singoda na Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa shukrani hizo kwa Waheshimiwa Wabunge, ningependa pia kwa heshima kubwa, kumshukuru Mheshimiwa Dr. David M. David, Naibu Waziri wangu, ambaye licha ya shughuli nyingi, lakini amekuwa msaada mkubwa kwangu katika kuongoza hii Wizara na katika mchango wake alioutoa kwa kujibu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge. Aidha, namshukuru sana Katibu Mkuu wangu, Ndugu Wilfred Nyachia, pamoja na wataalamu wote, ambao wako pale kwenye *gallery,* ambao wamenisaidia kuandaa majibu ya hoja hizi. Kwa hao wote nasema ahsante sana, natumaini kwamba, Waheshimiwa Wabunge, mtaridhika kwa majibu ambayo nitayatoa na wamesaidia kuyaandaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia hotuba ya Wizara yangu ni wengi na kama nikisema nijibu hoja zao zote, muda wa kuahirisha Bunge utafika kabla sijazimaliza. Majibu nitakayotoa yameandaliwa kwa kuzingatia hoja zilizochangiwa na Waheshimiwa Wabunge, kwa umuhimu na uzito wake. Aidha, zile ambazo sitazigusia, nitatumia utaratibu wa Waheshimiwa Mawaziri wenzangu walionitangulia kwamba, tutaziwasilisha kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nianze kwa kuangalia hoja mbalimbali ambazo zimetolewa na Wabunge. Nitaanza na hoja ambayo imetolewa na Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Msemaji Kambi ya Upinzani, ambayo ilikuwa inasema kwamba, Serikali itoe tamko rasmi Bungeni kuhusiana na matairi yenye ubora hafifu, ambayo yamejaa sokoni, ambayo hayaridhishi viwango.

Mheshimiwa Spika, nataka kutamka kwamba, chini ya Wizara yangu, *Tanzania Bureau of Standards* huwa wanapima matairi yote ambayo yanaingia humu Tanzania, isipokuwa tu labda yale ambayo yanaweza kuwa yamejipenyeza kupitia njia za panya. Lakini hata hivyo, huwa kuna taratibu tunazoziita *surprise visits* kwenye maduka mbalimbali, yanayojulikana kwamba yanauza matairi. Lakini hivyo hivyo tungeshauri Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla, pale mtu ambapo atakuwa na wasi wasi na tairi alilolinunua, atoe taarifa rasmi kwenye taasisi hii ya *Tanzania Bureau of Standards* tuwaagize waweze kufika pale kuchukua hayo matairi ambayo yanawekwa kama *sample,* tuone kama hayo matairi ni ya halali ama ni ya bandia.

Mheshimiwa Spika, vile vile amezungumzia kwamba, *SIDO* imejizatiti katika kutoa mikopo tu, haifanyi kazi yake ya kuwasaidia wajasiriamali wadogo wadogo kuendeleza viwanda. Tunasema kwamba, kutoa mikopo ni mojawapo ya nyenzo ya

kuwawezesha wenye viwanda. *SIDO* haitoi mikopo kwenda kufanya *trading* za umachinga kama tunazozijua. *SIDO* inatoa mikopo kwa sababu ya uzalishaji. Lakini vile vile *SIDO* hutoa huduma nyingine zikiwa ni pamoja na mafunzo kwa wasindikaji wa mazao mbalimbali, wanatoa mafunzo vile vile na kubuni mitambo mbalimbali, ambayo huwa inatumika katika kuongeza uzalishaji wa bidhaa. Lakini bila kuchukua muda mrefu kwa suala hili, nafikiri Waheshimiwa Wabunge ambao walikuwa na bahati ya kuhudhuria Maonesho ya 30 ya *Dar es Salaam International Trade Fair,* wenyewe watakuwa walishuhudia bidhaa ambazo zilikuwa zinaoneshwa pale *SIDO* na kweli tumekwishapata pongezi kutoka kwa Kamati ambayo inatusimamia kwamba, waliridhika na wanaipa moyo taasisi ya *SIDO* kwa kiwango walichofikia.

Mheshimiwa Spika, Msemaji wa Kambi ya Upinzani vile vile amezungumzia utaratibu wa kudai Dola 150, wakati wanakagua magari huko Dubai na kwamba *TBS* inapata fedha kidogo tu ambazo ni Dola 10 peke yake. Ni kweli mkataba sasa hivi ambao tunao kati ya *TBS* na yule anayekagua magari Dubai, kila anayepeleka gari lake kukaguliwa, analipa Dola 150. Mwanzoni mkataba wetu ulikuwa unasema kwamba, atatulipa Dola 5,000 tu kwa mwaka kama leseni ya kumpa kazi. Lakini baadaye tukaona kuwa ili kuongeza mapato na vile vile kutokana na gharama ambazo zinatokana na kazi za kiofisi huku Tanzania, ikabidi kuweka kiwango tena cha *administration fee* ya Dola 10. Kwa hiyo, kwa sasa tunapata Dola 5,000 kwa mwaka, pamoja na Dola 10 kwa kila gari. Nafikiri Mheshimiwa Naibu Waziri, amekwishaligusia hilo, wakati mkataba huu ukiisha wakati tunatangaza, tutajaribu kutafuta kwa ushindani kumpata mtu ambaye labda anaweza kuteremsha kile kiwango cha Dola 150 kwa kukagua gari. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba, kila Mtanzania anapatiwa afueni kwa bidhaa anazoziagiza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, ameuliza Viwanda vya Ngozi kuhusu Mfuko wa Ngozi na kuuliza kiasi gani kimo katika Mfuko wa Ngozi. Mfuko wa Ngozi umekusanya zaidi ya shilingi bilioni 4.5, ambazo ziko Hazina zimetunzwa hazijatumika. Hazijatumika kwa sababu zinategemea kupitishwa kwa Azimio ambalo lazima lipitie hapa Bungeni na Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Kabla hatujaondoka kwenye kikao hiki tunatarajia kwamba, atawakilisha Azimio hilo hapa Bungeni ili Mfuko huu uanze kutumika mara moja.

Mheshimiwa Spika, pamekuwepo hoja mbalimbali kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge mbalimbali, kuhusu viwanda vilivyobinafsishwa. Mheshimiwa Lucy G. Owenya vile vile ameligusia kutoka Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa ameligusia na wengine wengi. Lakini ili kujua maudhui ya hivi viwanda toka ubinafsishaji uanze mwaka 1992 mpaka hivi sasa viwanda vilipobinafsishwa ni 105. Kati ya hivyo viwanda au Mashirika ambayo Serikali imebaki kuwa na hisa ndani ya hivyo viwanda ni 13 baada ya Serikali kuuza hisa zake kwa umma wa Watanzania kwenye viwanda vine vinginevyo, yangekuwa makampuni 17. Makampuni hayo ni Tanga *Cement, Breweries,* Sigara. Hivi sasa tumemaliza mchakato wa kununua hisa zilizokuwa za *Tanzania Portland Cement* ya *Wazo Hill*. Kwa hiyo, Serikali itabaki na viwanda 13 tu ambavyo ina hisa, vingine vyote vitakuwa vimeuzwa moja kwa moja.

Mashirika ambayo Serikali imeuza hisa zake zote asilimia mia moja kupitia *PSRC* au *LART* kwa kufilisiwa ni 88. Waheshimiwa Wabunge hoja hii nimeifafanua zaidi kwa sababu kuna viwanda vingi ambavyo viliuzwa kwa wawekezaji wa nje na wa ndani. Viwanda vilivyouzwa kwa wawekezaji wa nje, hili swali limekuja sasa hivi mchana hatukupata takwimu. Lakini kwa mwangalio wa haraka haraka, viwanda vyote ambavyo vilinunuliwa ama na wageni moja kwa moja ama na ubia kati ya wageni na Watanzania, karibu asilimia 99 vyote vinafanya kazi. Viwanda ambavyo tuna matatizo navyo ni viwanda ambavyo vilinunuliwa na Watanzania. Tatizo tunalifahamu, Watanzania walivinunua hivyo viwanda, pengine wakitegemea baada ya kukipata hicho kiwanda, atatafuta dalali, dalali kama hakupatikana, kiwanda atakuwa amekaa nacho, hajui cha kufanya. Mwingine amenunua kiwanda akitegemea kwamba, kilikuwa kinafanya kazi na baada ya kuingia kwenye hicho kiwanda akakuta kinahitaji mitaji mikubwa sana ili kufufuliwa, kwa hiyo, akakwama. Lakini hata hivyo, Wizara yangu kwa njia moja ama nyingine, huwa tunajaribu kuwatembelea na ikiwezekana kutafuta njia ya kuwasaidia. Mimi binafsi kuna kitu ambacho kinanisumbua sana nacho ni viwanda vya korosho ambavyo asilimia kubwa vilinunuliwa na Watanzania, lakini mpaka sasa hivi vimeshindwa kufanya kazi na sasa hivi tayari wamekwisha tuandikia wanaomba Serikali iwasaidie.

Kawaida hili huwa ni suala gumu kibiashara, kwa sababu baada ya kununua kiwanda unakabidhiwa kiwanda hicho. Baada ya manunuzi unakwenda tena kwa yule uliyenunua kwake, akurudishie pesa uliyompa kusudi uanze kufufua hicho kiwanda. Lakini nafikiri kuna mikakati mbalimbali, ambayo itatumika katika kufufua hivyo viwanda na sisi hatutawatupa hasa viwanda vile ambavyo tunasema ni *strategic* hasa viwanda ambavyo ni vya kuongeza thamani ya mazao ya mkulima, tutajaribu kwa njia moja ama nyingine, kuona namna gani tunaweza kuwasaidia. Kuna wengine ambao wanafikiri kwamba, kiwanda kugeuza kusudio lake ni dhambi. Nasema hapana si dhambi, hili hutegemea biashara. Ameligusia vizuri Mheshimiwa Naibu Waziri, alipokuwa anazungumzia hoja hii. Tunajua kuna viwanda ambavyo vimeweza kugeuza matumizi yake halafu vikaweza kufanikiwa vizuri na sasa hivi tunavisifia. Mfano ni wa kiwanda pale Ubungo ambapo sasa hivi kinatengeneza yale mabomba makubwa, ambayo yanatumika kwenye mradi wa kutoa maji kutoka *Lake Victoria* kwenda Shinyanga. Mwanzoni kilikuwa kinategemea kufanya hivyo, lakini baada ya kushindwa kwa kazi iliyokuwa wameipangia *UFI* kutengeneza zana za kilimo*,* kikabadilisha mwelekeo na sasa kinafanya kazi nzuri na kazi hiyo tunaifurahia.

Kwenye hili vile vile amezungumzia viwanda *specific,* Viwanda vya Magunia Moshi, kweli vilikuwa havijaanza amavinafanya kazi kwa kusuasua. Sababu kubwa inayotolewa ni matatizo ya biashara ya kidunia yalivikumba na sasa hivi vinahitaji msaada. Kweli bidhaa ambayo wanashindana nayo kutoka nje ni bidhaa ambayo imewekewa ruzuku na nchi zinazotoka. Nafikiri baada ya kuweka Kitengo chetu cha *Fair Competition,* tutaweza kutumia njia hiyo na wakati mwingine labda kuweza kuvipa upendeleo maalum, kama tulivyofanya viwanda vya ngozi, ambavyo kwa sasa hivi tunaona vinaanza kufufuka. Sina haja ya kuzungumza mengi juu ya hili, lakini kwa sababu tuko hapa Dodoma, kuna mtu amezungumzia Kiwanda cha *Zuzu Tiles Dodoma*. Anasema hakifanyi kazi baada ya kubinafishwa. Hapana, hiki hakijabinafsishwa, habari

tulizonazo ni kwamba, hiki bado kimo kwenye mikono ya *CDA.* Tutafuatilia *CDA* kuona kwa nini hakifanyi kazi.

Mheshimiwa Spika, Msemaji wa Kambi ya Upinzani amezungumzia kwamba, biashara huria imeifanya nchi yetu kuwa jalala la bidhaa. Sheria ya Alama za Bidhaa *(Mechandise Act No. 2)* ya mwaka 1965 iliyohuishwa na Bunge mwaka 2004, imeanza kutekelezwa kwa kudhibiti bidhaa *fake,* ambazo zinaingizwa hapa nchini. Mfano mwezi wa Julai, 2006 bidhaa *fake* zilizuiliwa bandarini. Kwa hiyo, hii Kamati inayoshughulikia tatizo hili tayari imeshaanza kufanya kazi, bidhaa inapoagizwa wanakwenda kuangalia na wakigundua bidhaa haifai inashikwa na kitu wanachokifanya ni kuziharibu. Sasa hivi tatizo lao kubwa ni sehemu na namna gani ya kuweza kuharibu bidhaa hizo. Hii kazi sio ndogo, inahitaji fedha kama gharama za kuweza kutafuta kuzunguka na ku-*police* hizi bidhaa mbovu ili ziweze kupatikana na kuharibiwa.

Mheshimiwa Spika, vile vile nimeulizwa kwamba, lazima nitoe maelezo juu ya Kampuni ya Meremeta. Wengine wamechangia kwa maandishi, wengine wamechangia kwa kuzungumza na wengine wamechangia kwa kunieleza mimi binafsi. Kampuni hii ilisajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni ya Uingereza huko Uingereza. Kampuni hiyo ilisajiliwa Tawi lake hapa Tanzania tarehe 3 Oktoba, 1977 na kupatiwa *Certificate of Compliance No. 32755.* Kwa kuwa sheria zilizotumika kusajili Kampuni hizo ni za Uingereza, ni sheria hizo hizo zinazotumika kufilisi Kampuni hiyo kama itafilisiwa. Ofisi ya Msajili wa Makampuni *(BRELA),* haina taarifa rasmi ya hatua za kufilisi Kampuni hiyo, hivyo, haitakuwa na taarifa za wadai wanaoidai Kampuni hiyo. Aidha, ikiwa Kampuni hiyo itafilisika, basi mfilisi atateuliwa chini ya taratibu na Sheria za Makampuni za Uingereza na baada ya Kampuni hiyo iliyosajiliwa Uingereza kufilisiwa, *automatically* kwa sababu Tawi la Tanzania limefunguliwa kama Tawi la Kampuni hiyo na lenyewe litakuwa limefilisiwa.

Mheshimiwa Spika, vile vile Msemaji wa Kambi ya Upinzani, amezungumzia juu ya *Tanzania International Container Terminal* na *Mwananchi Gold Mine*, akitaka kujua Wamiliki na Wakaguzi. Naomba kusema kwamba, hili suala halina sababu kubwa sana ya kulileta hapa Bungeni, kwa sababu ni haki ya kila Mtanzania ambayo anaweza kuifanya. Hizi zimeorodheshwa pale *BRELA* ukilipia shilingi 2,000 unapata majibu yake yote. Kwa hiyo, namwomba yeyote ambaye anataka kujua taarifa za wawekezaji, hisa ngapi wanazo Wakurugenzi, akilipia shilingi 2,000 tu *BRELA*, tunaita *Company Search* atazipata taarifa hizo.

Mheshimiwa Spika, labda nisemee jambo moja ambalo walio wengi wangependa nilisemee. Msemaji wa Kambi ya Upinzani, amehoji uhalali wa Kampuni ya *Tanzania Intenational Container Terminal,* kuongezewa muda wa kukodisha *Container Terminal* iliyoko Bandari ya Dar es Salaam. Katika hali ya kawaida, hili suala lingeelekezwa Wizara ya Miundombinu na si Wizara yangu. Ninahisi hili suala limeelekezwa Wizara hii kwa sababu wauliza swali wanajua nina maslahi binafsi nalo. Hivyo, pamoja na kwamba hili suala sio la Wizara yangu, naomba uniruhusu nilijibu, kusudi Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla, wajue ukweli wake.

Mheshimiwa Spika, sote hapa ndani ya Bunge lako tuko wa aina tatu; ama ni wakulima hii ni pamoja na wafugaji na wavuvi; wafanyakazi au wafanyabiashara. Wafanyabiashara na wenyewe unaweza kuwaweka katika makundi kama *traders* au *investors*. Hiki ndicho kigezo kimojawapo *(qualifications)* ya kuwa Mbunge, lazima uwe na kazi. Usipokuwa na kazi, unapoteza hiyo *qualification* ya kuwa Mbunge. Hivyo, mimi mwenyewe kuwa na hisa katika Kampuni yoyote hapa Tanzania si kitu kisicho cha kawaida. Hoja hapa ni kuangalia kama utaratibu na sheria ilifuatwa na kanuni za Utawala Bora zilizingatiwa. *(Makofi)*

Uhalali wa kuongezewa muda Kitengo cha *Container* kinachozungumziwa, ulifuatiliwa kwa karibu na Kamati Husika ya Miundombinu na waliridhika kuwa, Mkataba Mama mwaka 2000 na nyongeza ya Mkataba huo *(addendum)* ya 2005, vyote viliwahusisha wadau wote na kuzingatia masharti ya mkataba mama na havikufanywa kinyemela. Kwa hili suala ambalo unaweza ukauliza na una haki ya kuuliza ni suala la Utawala Bora.

Suala hapa limeulizwa kama hapakuwepo na *conflict of interests*. Swali hapa ni je, kama Waziri nilishiriki katika Baraza la Mawaziri wakati Baraza linajadili Mkataba wa Kampuni tajwa. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Mkataba huu ulijadiliwa na kufanyiwa maamuzi na Baraza la Mawaziri mwezi Juni au Julai, 2005. Wakati huo mimi sikuwa Waziri hivyo, suala la *conflict of interests* halikuwepo.

Mheshimiwa Spika, lakini napenda kukupongeza wewe pamoja na Wabunge wote, kwa sababu kwa mara nyingi hapa Bungeni, Mbunge kama alikuwa anazungumzia ama anatoa hoja ya jambo ambalo linamgusa yeye binafsi, alikuwa anaanza kwa kutaja kwamba, Mheshimiwa Spika hili nina maslahi binafsi. Wewe mwenyewe wakati mwingine wakati unachangia ama unaingilia kati, kama suala linakugusa ulikuwa unatanguliza hivyo hivyo kwamba kwa hili una maslahi binafsi.

Hivyo, naona si ajabu kwa hiyo hata na mimi kama ningekuwa Waziri ili kutekeleza dhana ya Utawala Bora, ingelinibidi kumjulisha Mwenyekiti wa Kikao hicho na kutangaza *conflicts of interests* na hivyo, kuomba nisishiriki katika masuala ya namna hiyo. Nafikiri ndiyo dhana ya *conflict of interests*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la uwekezaji katika kuendeleza Miradi ya Makaa ya Mawe ya Mchuchuma na Chuma cha Liganga ni la muhimu sana Serikali inatambua umuhimu wa rasilimali hii kwa Taifa letu. Ushauri ambao umekwishatolewa na Kamati ya Uwekezaji na Biashara na vile vile vipengele vyote ambavyo ameviweka Msemaji wa Kambi ya Upinzani vyote vinashabihiana na mazungumzo tuliyoyafanya na Kamati ya Uwekezaji na Biashara. Yote tunasema yatazingatiwa wakati wa kumpata au kuwapata wawekezaji katika miradi hii.

Hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto kwamba, Serikali inamkumbatia mwekezaji mmoja, si kweli kwa sababu mchakato wa kuwachambua wawekezaji unaendelea. Baadhi ya wawekezaji, watarajiwa wameanza kulegeza hata masharti yao baada ya kujua kwamba, sasa Serikali tuko *serious,* tuna nia isiyoyumbika ya kuhakikisha

kwamba, miradi hii inaanza katika kipindi hiki cha Awamu ya Nne. Haya ni maelekezo yaliyomo kwenye Ilani ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, kuna masuala mengine ambayo yamejitokeza ambayo tunaulizwa, wamechangia Waheshimiwa Wabunge akiwemo Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Msemaji wa Kambi ya Upinzani na wengine wamekuwa wakisema mara kwa mara kwamba, Tanzania tulipojitoa *COMESA,* tunapata hasara kubwa kwa hiyo lazima turudi *COMESA*. Tanzania ilijitoa *COMESA* tarehe 2 Septemba, 2000. Baada ya kujitoa *COMESA*, yalikuwepo manung'uniko mbalimbali kutoka kwa wafanyabishara ama wa hapa nchini au wa kutoka nje, waliokuwa wanaleta bidhaa Tanzania. Kwa hiyo, mwaka 2004 Wizara ilibidi iunde Kamati ya kufanya uchunguzi wa hilo na vile vile mwaka 2005, Baraza la Wafanyabiashara la Afrika Mashariki, *East African Business Council, TCCIA*, pamoja na *CTI,* nao waliunda Kamati ya utafiti wa suala hilo.

Taarifa ya tafiti zote mbili zinaonesha kwamba, mauzo na manunuzi kati ya Tanzania na nchi za *COMESA,* yalishuka wakati Tanzania tuko bado *COMESA*, toka dola za Kimarekani milioni 82.3 mwaka 1977 hadi kufikia Dola za Kimarekani milioni 59.9 mwaka 2000. Baada ya kujitoa *COMESA*, mauzo yalianza kupanda kutoka dola za Kimarekani milioni 80.8 mwaka 2000 hadi kufikia Dola za Kimarekani milioni 196.6 mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, hivyo dhana ya kuwa nchi inapata hasara kutokana na uamuzi wa Tanzania kujitoa *COMESA* haziungwi mkono na takwimu za biashara. Hata hivyo, Serikali haizibi masikio, tutaendelea kupokea hoja kutoka kwa wadau mbalimbali, hoja za wakati zitakazo jitokeza tutazizingatia.

Mheshimiwa Spika, niende kwa Mheshimiwa Ahmed M. Shabiby, aliyechangia kwamba Masoko ya Kimataifa hayana udhibiti, yanageuka kuwa kero na ni kweli kwamba, tumetumia hela nyingi sana na ametoa mfano wa Soko la Kibaigwa. Tumetumia hela nyingi sana kujenga Soko la Kibaigwa na fedha nyingi tulizozitumia ni za wahisani ili kuweka maisha bora kwa kila Mtanzania. Inakuwa ni aibu sana, kama wale waliotusaidia hizo pesa wakifika, wakakuta watu wanakimbia hilo soko ambalo linapaswa kuwa soko la kisasa. Tunajua kuwa sababu za kukimbia hilo soko ni utamaduni wetu wa kukimbilia bidhaa hafifu kwa sababu ya bei. Tunajua kwamba, Soko la Kibaigwa huenda wanatoza ushuru fulani ili uendeshe biashara pale na soko lingine halitozi ushuru. Vile vile tumegundua kwamba, hili linaweza kuchangiwa na Halmashauri yenyewe, kama itatoza ushuru tofauti kati ya Kibaigwa na masoko jirani.

Taarifa ambazo tunazo ni kwamba, ushuru wanaoutoza kwa mwendeshaji wa Soko la Kibaigwa na anayeendesha masoko ya pembeni, tofauti yake ni kubwa sana. Mimi mwenyewe vile vile nilipata bahati ya kuhudhuria kikao, ambacho alikiitasha Mheshimiwa William V. Lukuvi, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, ambapo kati ya Maazimio yaliyotolewa ni kufunga masoko ya jirani ya Kibaigwa, kusudi tuweke *standards* ya mazao yetu yanayotoka Kibaigwa. Wizara yangu baada ya kusikia hili kutoka kwa Mheshimiwa Ahmed M. Shabiby na kwa kuwa anatoka Jimbo jirani,

tulilifuatilia tuone hatua gani zilichukuliwa baada ya kikao hicho na tuweze kuona namna gani tunaweza kuoanisha haya masoko.

Jambo kubwa la kuzingatia si kuwaumiza wakulima wetu, ila kuwasaidia ili bidhaa zao ziweze kufikika nje ya Kibaigwa na ziweze kutambulika kama Kibaigwa. Nina hakika tulikuwa tumekubaliana kwamba, kwa sababu mazao yanayotoka Kibaigwa ni ya *standard* kubwa sana, ili waweze kuwezeshwa ama waweze kupatiwa ubunifu wa kuweza kuwa na vifungashio au magunia ambayo mahindi yakitoka hapo, yawe yanajulikana yametoka Kibaigwa. Kwa sababu tunajua kwamba, yana soko kubwa sana na yanapochukuliwa yanachanganywa na sehemu nyingine na kusingizia kwamba ni ya Kibaigwa. Amezungumzia vile vile vituo vya mafuta kuwa kwenye makazi ya watu na athari mbalimbali alizozizungumzia katika mchango wake. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, Wizara ya Nishati na Madini, nafikiri hivi karibuni wataleta Muswada ambao utalenga ku-*regulate* hii bidhaa ya *petrol*.

Amezungumzia mambo mbalimbali, ikiwemo kuhoji kwa nini tusifunge viwanda vyetu tukawa tunaagiza bidhaa nje, kwa sababu bidhaa za kutoka nje ni rahisi kuliko bidhaa zetu ambazo tunazizalisha wenyewe. Mheshimiwa Ahmed M. Shabiby namwambia kwamba, kuwa na kiwanda hapa nchini, kina faida nyingi sana ambazo huwezi ukaziweka katika bei yake. Kwanza, tutaajiri Watanzania wenyewe na kupunguza umaskini wa mtu mmoja mmoja katika kaya, kwa wale walioajiriwa katika viwanda hivyo. Lakini pili, mbali ya waajiriwa wa viwanda hivyo, kwa sababu viwanda ambavyo tumekuwa navyo na tunavihimiza na vile ambavyo vitaongeza thamani. Bahati nzuri amezungumzia kama viwanda vya saruji, vinatumia malighafi yote kutoka hapa nchini. Najua mwanzoni viwanda vya saruji vilipoanza, walikuwa wanatoa *gypsum* sikumbuki Australia au kwingineko. Sasa hivi *gypsum* inatoka Makanya na sehemu fulani ya Dodoma na viwanda vingine. Lakini hiyo haijatoa hoja kwamba, viwanda vidhibitiwe ili visiweze kupandisha bei kiholela kusudi mlaji aweze kupata unafuu.

Mheshimiwa Naibu Waziri, alikuwa ameanza kujibu hoja iliyokuwa inagusia kwa nini usione bei ya saruji, bei ya bia au bidhaa mbalimbali imeshuka kwa sababu tu wameanza kutumia gesi na wewe unafikiri kwamba, gesi ni rahisi. Kama umemsikia vizuri amesema tuuangalie vizuri utaratibu wa kupanga bei ya gesi asilia kwa sasa hivi. Kwa sababu sasa hivi bei ya gesi, pamoja na uzalishaji wake hata ukiwa asilimia 50, lakini bei wanayouziwa inaoanishwa ama inakuwa *pegged* kwenye bei ya mafuta machafu ya dunia na bei wanayoi-*pack* kwenye mafuta machafu ya dunia ni asilimia 75. Kwa hiyo, jinsi mafuta machafu yanavyopanda bei, ndivyo vile vile na bei ya gesi inavyopanda bei, hata kama uzalishaji wake haujapanda bei. Tunafikiria sisi pamoja na Wizara ya Nishati na Madini, kutumia chombo chake cha *TPDC* itabidi kuzungumza nao, tuone kitu kama hicho kama kimo ndani ya Mikataba kinaweza kubadilishwa ama hakiwezi kubadilishwa.

Mheshimiwa Mbunge mmoja amezungumzia kwamba, wanapopata hii gesi wanakuwa wamepata umeme mbadala. Hapana, hii gesi hawaitumii kama njia mbadala, wanaitumia tu kwa kuongeza joto badala ya kutumia wengine wanaweza kutumia gesi, wengine mkaa na wengine wakatumia mafuta machafu. Sasa badala yake, wenyewe

wanatumia gesi ambayo ina unafuu lakini kwa bei yake ni kwamba, wana afueni ya asilimia 25 tu. Lakini ukija kuangalia gharama nyingine zinaongezeka na hiyo gesi kwa mfano, kama viwanda vya saruji tumefanya utafiti na tumeona kwamba, gesi ina-*contribute* asilimia 15 tu ya gharama za uzalishaji wao, kwa hiyo, kama umeme utapanda, *transport* itapanda na vitu vingine vitapanda na bei ya gesi itapanda hivyo hivyo, kwa sababu inakuwa *pegged* kwenye bei ya mafuta. Unaweza ukaona kwamba, uafueni huu haupatikani katika bei ya mlaji.

Usumbufu na urasimu bandarini, ameuzungumzia hiyo, ushauri huo tunauchukua. Tunajua Wizara ya Fedha kwa kupitia *TRA* na wadau wengine, kama *Tanzania Port Authority* na hii *SUMATRIA,* ambayo ameiweka na wana mikakati mbalimbali na wamekwisha agiza vyombo mbalimbali za kuweza kuangalia muda gani au kuoanisha kutumia mitambo ya kisasa ili kuweza kupunguza urasimu ambao upo pale bandarini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mohammed A. Chombon, amezungumzia mambo mengi, ametupongeza sana kwa utafiti wa soko la asali. Shukrani hizo tunazipokea na akatuomba kwamba, mpango huo usiishie hapo hapo kwenye asali, uende kwenye mazao mengine, ametoa mfano wa ndizi, maembe, ndimu, machenza na kadhalika. Amesema mwenyewe ana utafiti mzuri wa soko la Ghuba, hivi vitu vinahitajika na sisi tunasema ushauri huo, tumeupokea tutautekeleza. Ili tumpe faraja ni kwamba, sasa katika bajeti hii kama mtaipitisha, tumepanga kufungua Ofisi ya Biashara Dubai ili kuweza kuhudumia Soko la Mashariki ya Mbali.

Vile vile amezungumzia juu ya *packaging, labelling*, ni ushauri mzuri tu, tunaupokea na mpaka sasa hivi kwa sababu amezungumzia alipozunguka kwenye Viwanja vya *Dar es Salaam Trade Fair* aliona kwamba, bidhaa ni nzuri lakini zilikuwa wakati mwingine katika *wrong packaging* au kwenye *package* ya kitu kingine. Tunataka kulitangazia Bunge lako Tukufu kwamba, mpaka sasa hivi kuna mtambo ambao tunaufunga *TBS*, mtambo wa vifungashio na tuna uhakika katika kipindi cha bajeti hii utakamilika ili kuweza kuwasaidia kuwafundisha wawezekezaji wetu wadogo wadogo, namna ya kupata vifungashio bora wanavyoweza kuvitumia katika bidhaa zao. Amezungumzia viwanda vya *cement* kwamba, vimenufaika na gesi badala ya umeme, hili nimeshalizungumzia.

Akazungumzia Soko la Zanzibar kwamba, bidhaa inayotoka Zanzibar ikija huku bara sijui inashindikana kuiingiza; nini kinatokea? Hili suala kama lipo, nitalichukua na nitalifikisha katika Wizara husika, ambayo ni Wizara ya Fedha, kwa sababu wanaohusika ni *TRA*, lakini inaweza kutokea kama vile vitu umevizungumzia hakuna uoanisho katika ile *taxation* ya vitu hivyo, wakati vinaagizwa nje, wakati vinaingia Zanzibar na wakati vinaingia Tanzania Bara. Kama *harmonization* hiyo ipo, nafikiri halitakuwa ni tatizo, lakini kama *harmonization* ipo na bado unapata matatizo hayo, nafikiri tutaweza kuwasiliana baadaye, unipe hiyo bidhaa ambayo mnasumbuliwa, niweze kulifikisha Wizara husika.

Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro, namshukuru sana kwa mchango wake lakini sikushangaa sana kwa sababu huyu ni mtaalam tunayemtegemea, ambaye kwa muda

mrefu sana alikuwa *Board of External Trade,* anafamu sana mbinu zinazotumika katika biashara ya hapa na ya kiulimwengu. Kwa hiyo, mchango wake kila wakati tunauchukua kwa msisitizo ule ule. Tunamshukuru kwa kuweka msisitizo kwamba, kweli hakuna nchi yoyote hapa duniani, ambayo inaweza kuendelea bila viwanda na ujumbe huo huo tuliupokea wakati Mheshimiwa Rais alipoitembelea Wizara yetu, alipokuja kujionea yeye mwenyewe kazi zetu na kutupa majukumu. Kwa hiyo, si suala la kuuliza je, viwanda ni sekta kiongozi? Hapana, hilo ni suala limeandikwa katika Ilani ya Uchaguzi, kwa hiyo, halina mjadala. Kuna umuhimu kama alivyosema wa kuoanisha sera zote alizozitamka pale ili zilenge pale pale na kama Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya alivyozungumza, hatutafikia pale kama hatutaoanisha viwanda na kilimo.

Kwa hiyo, kazi hiyo kubwa ndiyo tunayo sana kati ya Wizara yangu na Wizara ya Kilimo. Mpango wa kilimo tumeupitisha hapa Bungeni na tumehudhuira semina pale kwa hiyo, itakuwa ni Mkakati wa Tanzania nzima ili kuweza kuona ni namna gani, tunaweza kuonisha huo Mpango pamoja na viwanda vyetu. Matatizo niliyokuwa nayaona pale ni kwa kila eneo kulima mazao madogo madogo hivyo, bila kuwa na zao kubwa sana ambalo linaweza kuvutia wawekezaji kuweka kiwanda pale.

Kwanza, kuna vitu viwili; zao kulilima eneo moja kwa wingi unapata unafuu wa kusaidiwa katika *extension services,* kwa sababu unaweza kuwahudumia watu wengi kwa wakati mmoja. Pili, hata kama mazao hayakusindikwa pale pale unayachukua sehemu nyingine kwa wingi sana, kwa hiyo, unaweza kuwa na mpango wa unafuu wa kuyachukua kwa wingi. Lakini tatu, kuna uwezekano mkubwa kwamba, kama gharama za usafirishaji wa mazao yenyewe na wingi wake zinaweza kuwa kichocheo cha yule ambaye ana kiwanda cha mbali kukileta pale pale kwenye eneo ambalo zao linalimwa kwa wingi.

Kwa hiyo, naona katika mpango huo, wakati tunapanga mipango yetu hii, huko kwetu mikoani ningependa, mimi kwangu sizungumzii mambo ya Wilaya na Kata. Kwa sababu ukiwa na mpango wa Wilaya tu peke yake ama na Kata peke yake, Kata hii inaweza kulima alizeti, Kata nyingine ikalima mawese, nyingine ikalima karanga, mwisho wa siku hakuna zao lolote ambalo ni kubwa ambalo unaweza ukavutia viwanda. Nafikiri hii iwe ni mikakati ya Mikoa kama tunataka kujikomboa na mkakati huo.

Amezungumzia juu ya tafiti, taasisi zipewe pesa, hiyo tunamshukuru na tunampongeza kwamba, kila wakati anapochangia bajeti yetu hapa au ama wakati tunaendeleza majadiliano ya bajeti nyingine, uwe ni mkakati huo huo wa Kamati yetu ya Uwekezaji na Biashara, kuweza kuweka msisitizo tu na kutubana na kuhakikisha kwamba, taasisi za tafiti hizi zinapata pesa. Lakini pesa hiyo inategemeana na Mfuko wa Kitaifa ulivyo. Amezungumzia juu ya fursa ambazo tunazizungumzia kwamba, haziwafikii wananchi wa kawaida. Hii tumeitambua kwamba, kuna matatizo, kuna fursa za *AGOA*, *EBA*, China, Japan, Canada, lakini kila mmoja wetu hapa ajiulize na mimi nikiwa mmoja wao, nikiwa kwenye pembezoni mwa Kata yangu kule, nikamwambia kuhusu *AGOA;* je, atajua *AGOA* ni nini?

Si atafikiri sijui ni mnyama gani, hajui ni kitu gani na mimi kwa kujua hilo na fursa nyingine kwa mara ya kwanza katika Maonesho ya 30 ya *Dar es Salaam*

*International Trade Fair,* niliagiza pale Wizarani kwangu, lazima mfungue banda la kutangaza fursa ambazo zinapatikana katika Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na walifanya hivyo. Rai sasa ambayo nitaitoa kwa Wizara zote, kuna Wizara nyingine kama Wizara ya Fedha, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma, zinashiriki. Sasa mimi nitatoa rai na nitaomba ikiwezekana na nitamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, aagize Wizara zote ambazo zinahudumia wananchi wakati wa maonesho kama hayo na wao wafungue, wawe pale ili waweze kuwaonesha wananchi kwa wingi, wanafanya nini na kuna fursa gani katika Wizara zao.

Utafiti wa masoko ni mpana sana na tunajitahidi na sasa hivi tunasaidiwa na mitandao kuweza kuingia kwenye *website,* kuweza kujua lipi na liko wapi tunalolihitaji. Lakini vile vile tutaendelea kila wakati tunapokuwa na nyezo, kuweza kuhakikisha kwamba, tunawatuma wafanyabiashara wetu katika maonesho mbalimbali ya Kimataifa ili waweze kujionea wenyewe yanayofanyika huko na vile vile kuwapata wenzao ambao wanaweza kukubaliana nao ama kununua bidhaa zao au kujua kuwekeza hapa wakawa na ubia pamoja wa kuweza kulitangaza soko letu la Tanzania.

Hapo hapo kuna aliyechangia nafikiri ni Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, kuhusu umuhimu wa kufungua *commercial attaches* nchi mbalimbali, hili tulikuwa nalo, lakini kwa sababu ya ufinyu wa bajeti, hatukuweza kuliendeleza. Kuna maofisa mbalimbali pale kwenye Balozi, ambao wamekabidhiwa dhamana ya kufanya kazi zetu za biashara ingawa wakati mwingine si fani yao.

Tunakubali kwamba, hilo ni dosari kidogo lakini kila mahali ambapo tunakuwa na uwezo, tutafanya hilo. Kwanza, sasa hivi tuna Kituo cha Biashara Dubai, ambacho kinahudumia Kituo cha Biashara London, ambacho kinahudumia Ulaya pamoja na Marekani. Lakini tunajua Marekani ni mbali. Juzi juzi nilikuwa Marekani, Mheshimiwa Balozi alikuwa ananiambia anavyoelemewa Marekani ni kubwa sana, akawa anaomba afadhali angekuwa na mtu wetu, ambaye anasimamia biashara ingeweza kusaidia kwa haraka zaidi. Haya masuala yote tunayazingatia jinsi Mfuko wa Serikali unavyoendelea kuwa mpana, tutaendelea kuliomba hilo ili liweze kukamilika kwamba, tutachagua maeneo *strategic* kama alivyozungumza sio maeneo yote.

Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, vile vile amezungumzia suala la *COMESA.* Nafikiri nimekwisha lizungumzia na cha kuongezea kwa waliozungumza ni kwamba, mimi ulipomaliza kusema hayo kwamba, kuna taarifa kutoka *Confederation of Tanzania Industries,* nilimkimbilia Mwenyekiti wake, alikaa pale Mheshimiwa Reginald Mengi. Nikamkimbilia pale nje nikamwuliza siku hizi mbona tumeanza kutokuwa karibu, hiyo ripoti unaipokea unakaa nayo tu mimi sijaipata. Akasema wala, hata yeye mwenyewe ripoti hiyo hana. Sasa Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto kama una riporti hiyo, ambayo imetolewa na sisi hatujaipata, si mimi wala si Mheshimiwa Leginald Mengi, basi tuipate tutaifanyia kazi, tutaangalia maudhui yaliyomo humo ndani.

Amezungumzia suala zito sana ambalo tunalo la majadiliano juu ya *EPAS*, *SADC* na *EPA,* ambayo mpaka sasa yanaendelea na akaweka msisitizo kwamba, Tanzania lazima tutoke tulipo, nafikiri alikuwa ana maana twende *ESA* kwa sababu *COMESA* haipo katika majadiliano haya. Lakini naweza kukwambia kwamba, hili suala sasa hivi

bado wataalam wengi wanabishana juu ya hilo, halijafikiwa muafaka kama anavyolizungumza. Kuna wengine kwa sababu *configuration* atakayotokea mwisho wa siku ni kwamba, nchi moja haiwezi kuwa katika *custom union* mbili na katika hizi nchi tunazozizungumzia za kanda hizi, zina *custom union,* zina maeneo mawili tu.

Kuna *East African Community* na kuna *Southern African Custom Union*. *COMESA* wala *SADC* hazina *custom union*. Kwa hiyo, kuna wengine ambao wanafikiria kwamba, sasa kwa sababu hizi zina *custom union* kwa nini wengine msijiunge ama na *East Africa* na wengine mkajiunga na *SACU,* mkafanya *configuration* ya kuzungumza nao.

Wengine wanasema kwa nini *COMESA* isiwe *custom union* na *SADC* ikawa ni *custom union*. Lakini vile vile ukija kuingia *COMESA* ama *SADC,* unakuta wanachama wengine wako *COMESA,* wengeni wako *SADC* na wengine wako kote kote. Kwa hiyo, hili suala bado linazungumzwa na sisi tulichozungumza hapa kwa sasa hivi, tunaendesha mazungumzo hayo tukiwa upande wa *SADC, EPA*, hatujaziba masikio yetu kwa sababu kinachotuongoza sisi sote hapa ni maslahi ya nchi yetu. Mahali tunapoona maslahi yetu ndiyo yamelala, ndipo mwisho wa siku tutalala. Kwa hiyo, hilo suala halijafikiwa mwisho, kwa sababu hata wale *negotiators* ambao ni wa kutoka Ulaya, bado wanaangalia *configuration* gani ambazo ni nzuri zaidi.

Suala la Mchuchuma nimelizungumzia na juu ya *economic diplomacy,* tumelisikia. Sasa sitaki nigongewe kengele ya pili, kama nilivyosema, kwa wale Waheshimiwa Wabunge, ambao sikuweza kujibu hoja zao, tunatoa ahadi, watazipata kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa na Kuamuliwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 44 - Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko**

Kifungu 1001 – *Administration and General* .... Sh. 3,545,673,400/=

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *Vote* 44, Programu Namba 10, Kifungu 1001, Kifungu Kidogo 250100 – Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni suala dogo la Sera. Kwanza, nampongeza Waziri kwa kuwa muwazi sana katika majibu yake. Anafanya kazi nzuri, lakini nafikiri kuna maeneo ambayo kidogo yanahitaji ufafanuzi, kwa hiyo, nitamwomba atusaidie. Kifungu cha 63(3)(e) cha Katiba kinasema: "Kumwuliza Waziri yeyote swali lolote kuhusu mambo ya Umma katika Jamhuri ya Muungano, ambayo yako katika wajibu wake."

Wakati alipokuwa akijibu suala la Meremeta, alisema kwamba, twende *BRELA* tukalipe shilingi 2,000/=, tupate taarifa. Mimi nafikiri Bunge hili, lina wajibu wa kupata taarifa bila ya kwenda kulipa shilingi 2,000/=. Ningemwomba tu Waziri, atuahidi kwamba atatuletea hiyo taarifa ya hiyo Kampuni ilivyokuwa *registered*, hao *Share Holders* ni akina nani. Ni wajibu wa Bunge hili kupata taarifa, ningemwomba atupatie taarifa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hata ukisoma *Immunities and Privileges Act* ya Bunge hili Namba 10, inatuwezesha sisi kupata taarifa mbalimbali kutoka Serikalini. Kwa hiyo, ningemwomba Waziri atugawie hiyo taarifa badala ya kutuambia sisi twende *BRELA* kutafuta taarifa. Hili lilikuwa ni suala la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo kwa suala la Kampuni ya Mwanachi, kwa sababu katika maandishi yangu niliyomwandikia, niliomba taarifa ya aina hiyo hiyo. Kwa hiyo, ningeomba hayo mawili anifanyie, mimi sina matatizo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Msimamo ni sahihi kabisa. Mheshimiwa Waziri, itabidi utusaidie baadaye Bunge hili lipate taarifa zilizoombwa na Wabunge. Siyo lazima wapitishe mkondo wa kujitafutia wenyewe, lakini ningependa utamke wewe mwenyewe.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, hatuna tabu ya kutoa taarifa hizi, kwa sababu taarifa hizi zinapatikana kwa Mtanzania yeyote ana haki nazo, wala siyo kwa Bunge tu. Kwa hiyo, nafikiri tutatekeleza kama ulivyoagiza.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *Vote* 44, Programu 10, Kifungu 1001 na *Subvote* 250100 – Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia kuhusu Wizara hii, nilielekeza kwamba, Wizara hii ni muhimu sana katika kuhakikisha kwamba, kuna masoko ya wakulima na sisi tulio wengi hapa tuna-*represent* wakulima. Nikataja kwamba, mwaka huu wakulima kwa mfano, wa Pamba bei imeenda juu kwa sababu makato ya Serikali yamepungua kwa shilingi 10/=. Jambo ambalo kusema kweli, Serikali naisifu sana kwa kufanya jambo hilo. Lakini pia nikasema bado tunalipia utafiti na gharama nyingine za pembejeo. Ninataka Serikali ili kuhakikisha kwamba, wakulima wanapata bei iliyo nzuri na wakulima wakipata bei nzuri, watakuwa na hamasa ya kuweza kulima zaidi. Sasa, nimeona hata katika majumuisho wala hakusema lolote, ndio kusema umuhimu wa jambo hili kwa Serikali, hauonekani hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nimesema kwamba, njia nyingine ya kumsaidia mkulima kumwambia bei leo kutokana na mazao tuliyonayo, Zao la Korosho, Zao la Kahawa, Zao la Pamba, yana *future markets*, yaani bei ya 2007/2008 inajulikana. Sasa, nilikuwa nimemwuliza Mheshimiwa Waziri, kwa nini katika masharti ya leseni ya

wanunuzi, pasiwepo na sharti ambalo linasema wanunuzi wa-*declare* bei yao hata kabla hatujaenda kulima. Hii inawezekana kabisa, maana yake hata *insurance* inawezekana.

Sasa hii ni kwa sababu Serikali ndiyo inatoa leseni, hili jambo wangechangamkia. Lakini naona hawachangamkii kabisa, wako kimya tu, ni kama vile wakulima wako solemba, hakuna anaye waangalia. Naona mambo mengi ya viwanda yanazungumzwa, lakini mkulima tumemhakikishia namna gani mwaka kesho, atapata kipato cha aina yoyote? Kwa hiyo, nilitaka hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nilisema kwamba, *Fair Trading*, katika haya madawa kwa mfano ya Pamba, Korosho, muuzaji mmoja; kuna *fair trading* gani hapo? Kuna *intervention* gani ya Wizara hii; yaani wao wanafikiria kwamba mkulima haoni *competition*? Katika *area* nyingine kuna ushindani, lakini yeye anapewa anachopewa kwa bei inayotakiwa. Sasa Serikali inasema nini na zaidi Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Masoko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndio nataka majibu.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa John M. Cheyo, kwa sababu suala la Pamba huwa analifuatilia kweli kweli na liko karibu na moyo wake. Kwa hiyo, nampongeza kwa kufuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kwamba, bei ya Pamba imekwenda juu. Inawezekana kweli kwa sababu ya makato yaliyopunguzwa lakini vile vile tujue kwamba, bei ya Pamba Duniani na yenyewe imepanda. Zaidi ya hayo, Serikali inaendelea vile vile kuangalia namna gani ya kuboresha sio bei tu ya mkulima inayotangazwa, ili mapato ya mwisho, kipato cha mwisho mkulima anachokiweka mfukoni. Hii ni pamoja na kuangalia *levy* mbalimbali ambazo mkulima alikuwa anatozwa. Mpaka sasa hivi imekwisha tangazwa, nafikiri na Waziri wa Kilimo katika bajeti yake alionesha kwamba, ule mchango wa Bodi ya mazao sasa hivi utakuwa unatolewa na Serikali, haitakatwa toka zao la mkulima. Hiyo ni njia mojawapo ya kuboresha bei ya mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ushauri mwema, amezungumzia masoko ya kisasa ya *futures* ambayo kawaida huwa ni miezi mitatu mitatu na watu wananunua *Futures*. *Futures* katika kununua huwa zinatumika, sijui neno zuri la kiswahili ni kama kinga, *mechanism* ya mtu anapotaka kununua vitu fulani. Kwa sababu sisi soko letu halijawa *advanced* kutekeleza ushauri wake ni vigumu. Hatuko kama la Ulaya, ambapo *future* unawea ukaiuza, wana soko la ku-*trade futures*.

Kwa sababu soko letu halijawa *advanced* namna hiyo, kwa kuanzia tumeweka taratibu za Mfumo wa Stakabadhi ya Maghala, mfumo ambao mkulima anaweza akautumia akaweka bidhaa yake kwenye ghala na sio aiweke tu ikae, atatumia bidhaa yake kwenye ghala akapata pesa za kumwezesha kumfanya aendelee kufanya kile

anachokihitaji mpaka pale bei atakaporidhika iko juu, ndipo anaweza kuuza na akapata faida badala ya kuuza wakati ule ambapo kila mmoja anauza na kupata bei ya chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumza juu ya *fair trade*. Kwa hili baada ya kuruhusu biashara huria, tulikuwa tuna mategemeo kwamba, watu wengi watajitokeza na watu wengi wakijitokeza, wataanza kushindana, kwa hiyo, bei kuwa *regulated* na soko. Lakini pale ambapo si mnunuzi mmoja bali hata kiwanda kimoja ndicho kiko peke yake, tunatambua kwamba kiwanda hicho kina *monopoly*. Tayari tuna *Fair Trade Commission*, mtu yeyote anaweza kulalamika kama anafikiri ya kwamba, wanatumia kuwepo kwao peke yao bila kuwa na ushindani kunawafanya kutoa bei zisizo kuwa za halali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John M. Cheyo, maelezo yalikuwa fasaha.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Hapana!

**MWENYEKITI:** Napenda kukumbusha, naomba ukae. Waheshimiwa Wabunge, Kamati ya Matumizi siyo wakati wa kudai kitu hadi ukipate. Inaelekea wengine wanadhani hivyo, ni wakati wa kudai maelezo. Yanaweza kuwa kwako wewe huridhiki kabisa na maelezo, lakini kama ndio ukweli, hapo ndio mwisho. Ukitaka kudai mpaka upate unachokitaka, sio Kamati ya Matumizi, wala hatuwezi kuitumia Kamati ya Matumizi kuanzisha upya mjadala ambao umekwishapita. Kwa maelekezo hayo mawili, basi nakuruhusu. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naheshimu kauli yako. Lakini alichosema Mheshimiwa Waziri si ukweli. Kwa sababu *Futures* za mazao kama Pamba, kama Kahawa, sio jambo geni. Kwa hiyo, ninapoambiwa kwamba sisi tuko wachanga, tumeuza Pamba sisi tangu hatujazaliwa. Kwa hiyo mambo ya kuniambia sisi hili jambo geni, nashangaa na watanzania wanaosikiliza kwamba hili ni jambo geni na wenyewe wanamshangaa Waziri amekulia wapi! Kwa hiyo, hili inawezekana kabisa, kama Serikali ikiamua na kuweka sharti kwamba kabla hujaruhusiwa kununua Pamba, utuonyeshe bei utakayowapa wakulima mwaka unaokuja. Hili ni jambo zuri kwa sisi wote. Maana yake wakulima watahamasika, halafu watalima zaidi. Kuna ubaya gani? Waziri Mkuu juzi alikuwa anatuomba tulime mpaka tufikishe marobota milioni moja. Njia ya kupata marobota milioni moja, ni kuambiwa mwaka kesho pesa zenu ni hizi, sasa hii inawezekana. Sasa Waziri anaponiambia kwamba, hili ni jambo geni, mimi nashangaa! Lakini kama anataka tuje tuzungumze baadae tufundishane, niko tayari. Lakini lazima wakulima waangaliwe katika Bunge hili. Hiyo, moja. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, hakunielewa pia. Nazungumza juu ya dawa. Jambo hili, *we are not talking about* Kiwanda cha Dawa za Pamba kiko Magomeni na kingine kiko hivi. *No!* Hili ni jambo geni, ni *International Trade*. Kuna makampuni *ICI, HERTZ, SIMBAGAIGE* na mengine. Kama isingekuwa Sheria ya Serikali kwamba, dawa zote zinunuliwe na mtu mmoja ambaye ni Bodi ya Pamba, basi tungekuwa na ushindani huo. Ndio kitu ambacho nilikuwa najaribu kumweleza Mheshimiwa Waziri. Kama hajalielewa, mimi niko tayari kusubiri, lakini nitauliza tena, kwa sababu wakulima wanataka watendewe haki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nadhani Mheshimiwa John M. Cheyo, uliyosema ni halali kabisa, yanaelezeka sasa vizuri. Pengine ni vyema kama Mheshimiwa Waziri badala ya kuchukua muda mrefu sana wa Kamati, angekubali kwa ile *dialogue spirit* kwamba, *point* hizi ni nzuri, zinamsaidia mkulima. Sasa kama zinawezekana, hatujui. Lakini Serikali iyachukue ili yaweze kutazamwa. Pitisha kupitia Masoko.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea ushauri wako na mimi binafsi ningependa sana kujifunza, ili kujua kama kuna *Futures* ambazo zinaweza kutumika ili ku-*hedge* kwa mwaka mmoja. Kwa sababu nilipokuwa shuleni najifunza *Finance*, sikuweza kuona yeyote ambaye anaweza ku-*hedge* kwa mwaka mmoja mbele. Lakini kama anazifahamu, nitafurahi sana nitamwona Mheshimiwa John M. Cheyo, aweze kunifundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la Pamba nilikuwa sikulielewa vizuri, lakini kwa sababu hili linahusu sana sana Wizara ya Kilimo, kupitia kwangu nitalifikisha.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote* 44, *Program No*. 10, *Subvote* 1001 – Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilichangia kwa maandishi na nilitaka ufafanuzi katika jambo ambalo linalalamikiwa na wafanyabishara wengi wadogo wadogo nalo ni kuhusu kwa nini Wizara inatoa leseni kwa hawa wawekezaji kutoka nje, ndugu zetu wa Kichina, kwa sababu hawa wanafanya kazi ya kuuza bidhaa ndogo ndogo ambazo sasa hivi wanauza vijana wetu Wamachinga? Inasemekana kwamba, biashara hizi ni *Sub-standard*, zina maandishi ya Kichina ambayo Watanzania wengi hawaelewi, inawezekana kwamba dawa zimesha-*expire* lakini zinanunuliwa hivyo hivyo. Kwa hiyo, tungependa ufafanuzi kidogo, kwa nini basi waruhusiwe wawekezaji kutoka nje kuuza vitu hivi vidogo vidogo ambavyo sisi wenyewe tunaweza kuuza? Ahsante.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu hoja ya Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, kama ifuatavyo: Hili tatizo tumeshalisikia sana limezungumziwa sana hapa Bungeni na kuna kipindi ambacho Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani alilizungumzia vile vile. Sisi kama Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, hatuna uhusiano wa moja kwa moja wa kumpa *status* ya mtu kuishi hapa nchini. Akishapewa *status* ya *category 'A'* kuja hapa nchini na akapewa kibali cha kuishi hapa nchini, hawezi akaja kuomba leseni ukamkatalia, kufuatana na sheria ambayo tunayo kwa sasa na haijabadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hili tumelisikia likisemwa sana, sisi pamoja na ushirikiano wa Wizara ya Mambo ya Ndani, kuchunguza hao wanaozungumziwa tuweze kubaini wana vibali vya *category* gani vya kuishi hapa nchini kama njia ya mwanzo ya kuweza kutatua tatizo hilo.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *Vote* 44, *Program* ya 10, *Subvote* 1001, Kifungu kidogo 250100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu, nilizungumzia suala la ubinafsishaji wa hivi viwanda na katika jibu la Mheshimiwa Waziri, alijibu ambapo kwa mfano, Kiwanda cha Zuzu alisema hakiko katika Wizara yake, kiko chini ya *CDA*. Lakini kuna viwanda vingine nategemea bado viko katika Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilitaka kujua kwamba, kwa mujibu wa kazi ya Wizara ambayo inawajibika kufuatilia sana hivi viwanda vilivyobinafsishwa na kutatua matatizo yanayojitokeza mle ili viwanda vile kuhakikisha vinafanya kazi na Serikali inapata pato linalohusika. Katika majibu yake, viwanda ambavyo vimeshauzwa, ubinafsishaji wenyewe akasema kwamba, Serikali haina la kufanya tena.

Hapo kidogo mimi nashangaa, kwa sababu lengo la Serikali kubinafsisha viwanda hivi sio kuvitupa moja kwa moja. Mle mna ndugu zetu, ambao wangeweza kupata ajira, mle Serikali ingeweza kupata mapato na inakuwaje ikiwa kwa kawaida hata hizi hati za viwanja vidogo vidogo tu, hapana chochote mtu akiwa hajakiendeleza ananyang'anywa. Lakini ikiwa kiwanda kizima na muwekezaji ameshindwa kukiendeleza, inakuwaje? Labda niulizie kwa upande mwingine, hizi Sheria za *PSRC* wakati wanapobinafsisha hivi viwanda, hakuna kifungu chochote kwamba huyu mtu ameshindwa kufanya kazi, Serikali ifanye nini? Naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba kumpongeza Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa kwa hoja yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hiyo anaitoa kwa nia nzuri. Kweli wakati kiwanda kinabinafsishwa na kisiweze kufanya kazi, kila mmoja anasikitika. Hii ni pamoja na Serikali na watu waliozunguka kiwanda hicho, ambao wangetarajia kazi kutokana na kiwanda hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyozungumza Mheshimiwa Waziri wakati ananisaidia kujibu hoja, kweli kuna matatizo ya kisheria. Matatizo ya kisheria yanaendana na *ownership* ambayo kuielewa vizuri huwa nawatolea mfano. Kama mimi ni MwislamuItikadi kali nikakwambia nakuuzia teksi yangu hii, wakati unaendesha barabarani, usimbebe mama yeyote. Tunaweza tukawekeana mkataba na ukaniuzia hiyo teksi, lakini baada ya kuniuzia, nikabadilisha *registration* ikawa kwenye jina langu. Nikiingia barabarani, nikambeba mama, ukinigusa naweza nikakupeleka mahakamani wanakufunga, kwa sababu sio ya kwako tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wakati tunajadili namna ya kubinafsisha vitengo mbalimbali vilivyobaki, tulichukua muda mrefu, tena kwa uchungu kama aliouzungumzia Mheshimiwa Mbunge, tukimwomba Mheshimiwa *Attorney General* kwa nini kile kipengele cha kunyanganya walioshindwa Mradi uliobinafsishwa asikiweke? Lazima ukiweke kusudi yule atakayeshindwa tumnyang'anye. Akasema, kwa sheria zetu tulizonazo hapa, kukiweka si tatizo, tunaweza tukakiweka, lakini ukitaka kumnyang'anya, atakupeleka mahakamani na tutamlipa mara mbili au zaidi kwa kiwanda

kile alichoshindwa kukiendesha. Hili linaendana na sheria ile ya *ownership right* kwa vile itakuwa imekwishakuwa *property* yake.

Kama alivyozungumza, mfano kama mtu amechukua kiwanda cha kutengeneza juisi ya machungwa, kama machungwa yote yamekauka kwenye eneo hilo na wewe umng'ang'anie kwamba lazima atengeneze juisi ya machungwa tu, atakuambia hapana. Vile vile bei ya juisi ya machungwa ikiteremka na akaona hana faida kuitengeneza, itabidi asitishe ghughuli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri sheria zetu kama alivyosema, tutaziangalia. Kuna viwanda ambavyo kweli wana nia ya kuviendeleza lakini sera zetu zilikuwa hazijaangalia mambo mbalimbali, ambayo yanawakwaza, mfano hili linaathiri viwanda vya ngozi. Kweli vilichelewa kuanza kwa sababu tulikuwa hatujabadilisha sera fulani fulani. Nimesema kwamba, Tamko litatoka hapa Bungeni. Vile vile tunao wanaolalamika, viwanda vya magunia mmevizungumzia sasa hivi. Wanafikiria kwamba, sera zetu zilizopo sasa hivi haziwaweki kuwa katika *fair competition*. Maoni hayo tunapoyapokea, kazi yetu ni kuyachambua na kuangalia pale ambapo nia ni ya kweli, tutaweza kumsaidia mwekezaji huyo, kusudi aweze kufufua hicho kiwanda, bila kukwazwa na sera zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Mohamed Haib Juma Mnyaa, kwa mawazo hayo, tunayapokea na tunaendelea kuyatekeleza. *(Makofi)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza hoja yangu kidogo, Mheshimiwa Waziri aweze kunijibu. Niko kwenye *Vote* 44, *Program* 10, *Subvote* 1001, Kifungu kidogo 250100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia hoja hii kwa maandishi, nilimwomba Mheshimiwa Waziri atueleze mambo mawili:-

Kwanza, niliomba atueleze kwamba kiwanda cha *Tanganyika Packers* kilichoko Dar es Salaam ambacho sasa hivi kwa muda mrefu hakijafanyi kazi. Kiwanda hiki ambacho kilisaidia sana kutoa soko kwa mazao ya mifugo na sasa hivi tuna tatizo kwamba, mazao mengi ya mifugo hapa Tanzania hayana soko, wafugaji wanafuga, hawana sehemu ya kuuza mazao yao. Lakini mpaka ssa hivi, sijui Serikali ina mpanga gani na kiwanda hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilipenda kujua kwamba, kama matumizi ya kiwanda hiki yamebadilika, je, nini hatima ya majengo yaliyoko pale *Tanganyika Packers* kwa kuwa yako pale, yanaozea pale na ni nguvu za Wananchi wa Tanzania? Ninaomba maelezo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Suala kama hili limewahi kuulizwa hapa Bungeni na akalijibu Mheshimiwa Waziri wa Mifugo. Ningependa kurudia maudhui ya majibu yake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha *Tanganyika Packers,* tunaweza kusema siyo kiwanda, eneo la *Tanganyika Packers*, limekwisha binafsishwa kwa muwekezaji ambaye anataka kuweka pale *Estates* za vitu mbali mbali. Sababu za kubadilisha matumizi yake, kama alivyoshauri Waziri wa Wizara ya Mifugo, kiwanda cha nyama mahali ambapo kinakuwa, lazima wawe na eneo la kutosha ili ng'ombe ama mbuzi au watakaokuwa wanachinja, waweze kuwatunza pale kabla ya kukichukua machinjioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hicho kiwanda kiko katikati ya mji, kimezungukwa na watu, hakina tena maeneo ya kuweza kuwatunza hawa wanyama. Kwa hiyo, huwezi ukakiendeleza kama kilivyokuwa *Tanganyika Packers*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muwekezaji amekwishapatikana, amekwishanunua na malengo yake ni kujenga *Real Estate* na kuweka Hoteli ya Kisasa, *Conference Centre* na mambo mengine, kama muwekezaji alivyoyaweka kwenye *Certificate* aliyopewa na *TIC* wakati anaomba kuwekeza hapa nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, bado hujaridhika?

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, bado sijaridhika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya kutosha kama ninavyofahamu, inatakiwa kuwepo kwenye *abbatoir* au sehemu yenye machinjio na sasa hivi Serikali ina mpango wa kujenga Machinjio ya Kisasa Dar es salaam. Ninavyofahamu, nyama inatolewa kwenye machinjio inapelekwa kiwandani kwa ajili ya kusindikwa. Iweje Waziri atuambie kwamba, inatakiwa maeneo ya kutosha pale? Halafu pia kiwanda hicho kimefanya kazi kwa muda mrefu na kimesaidia sana Tanzania, wakati huo kikiwa kwenye hali hiyo hiyo; leo kwa nini Serikali ituambie kwamba nafasi ni ndogo, hakiwezi kufanya kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado ninaomba majibu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sijui kama kuna maelezo ya ziada, kwa sababu ukweli ndio huo. Hapana, Waheshimiwa, narudia, kutumia Kamati kudai unalolitaka ni kinyume kabisa cha kanuni. Hebu tushughulike na *reality* yenyewe. Kiwanda hiki kimebinafsishwa, kilivyobinafishwa ni kwa misingi ya matumizi mengine na ardhi yote pale imegawanywa. Sasa tutakaa Wabunge tunabisha tu kwamba hiyo haikuwa! Sasa hiyo, inaweza kuwa ni *post-mortem*, lakini hiyo sio kazi ya Kamati ya Matumizi. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. *Vote* 44, *Program* 10, *Subvote* 1001, *Item* 250100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichangia kwa maandishi. Nampongeza Waziri amejitahidi kujibu, lakini muda haukutosha. Kwa hiyo, ninaomba tu anisaidie kupata maelezo juu ya hoja yangu hii moja tu, walau kati ya nyingi ambazo nilikuwa nimeuliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo ya machimbo ya dhahabu au ya almasi kunakuwepo kodi inayolipwa na wale wachimbaji kwenye Halmashauri, maana yake ni Serikali za Mitaa. Pesa zile zinatumika katika kuchangia maendeleo ya wananchi wa maeneo yale. Sasa, katika Ziwa Victoria, kunavuliwa samaki wengi sana na leo nilikuwa nasoma Gazeti la Mwananchi kwamba, samaki wameongezeka kutoka tani laki 7.9 kufikia tani karibu milioni 1.1. Hali hii inaonesha kwamba, itavutia wavuvi wengi sana kuendelea kuvua katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo wananchi ambao wanaishi katika ziwa hilo, wakiwemo wa Jimbo la Muleba Kaskazini, Kata za Bumbile na Gozba, wakiwemo wanaozunguka ziwa katika Wilaya ya Bukoba Vijijini, Bukoba Mjini, Muleba, Mwanza, Sengerema na kadhalika, ni wananchi ambao kimsingi ni wavuvi na maisha yao ni ya chini.

Viwanda vile haviwezi kuwekwa katikati ya ziwa, vinawekwa kando. Sasa napenda kuuliza, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, imefikiria vipi kuwasaidia wavuvi ili viwanda vile vitoe kodi, kodi ile itumike kuanzisha Mfuko na Mfuko huo usaidie wale wananchi wanaozunguka yale maeneo na hasa wavuvi kupata huduma za jamii, ambazo zinawapa shida sana ikiwemo elimu, afya na hata katika kununua zana za uvuvi? Naomba maelezo. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Wabunge wamesimama Kanuni Namba 21(iv), nisingependa niisome yote, lakini inasema kwamba: "Iwapo hoja ya kuongeza muda wa kikao itatolewa na kukubaliwa, kwa maana ya Wabunge 10 kusimama na kuunga mkono…" Kwa hiyo, nataka nichukue nafasi hii kwa sababu watu wengi sana waliomba kusimama kwa ajili ya kujadili hiyo hoja ya Wizara hii, nitoe hoja ya kuongeza muda wa nusu saa wa Kamati ya Matumizi kwa ajili ya kuendelea kujadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mwongozo wa Mwenyekiti ni kama ifuatavyo: Katika kitabu hicho hicho cha kanuni, ukiangalia Kanuni ya 21(vi), hoja kama hiyo ni lazima ikubaliwe na Kiongozi wa Shughuli za Serikali, kwa maana ya Waziri wa Nchi ndiyo anaitoa.

Naomba mnisikilize. Hata mwanzo nimesema kanuni hizi zina matatizo, lakini ndiyo zinatufunga. Hivi sasa ndiyo tunafanya kazi ya kuzibadili. Sasa, ruhusa hiyo ni lazima uisome na 21(vi), ambayo nayo inachanganya tena na historia imeonesha kwamba, wakati wote hoja kama hii imeingia kwenye mkondo wa 21(vi), ambayo inahitaji Waziri wa Nchi wa masuala ya Bunge ndiyo aweze kutoa hoja ya kuahirisha. Kwa hiyo, hii inashindikana kwa leo na kwa hiyo tutaendelea hivyo hivyo tu.

Waziri, ufafanuzi wa hoja za Mheshimiwa Ruth B. Msafiri.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Ruth B. Msafiri kwa jinsi anavyowatetea wapigakura wa Muleba na wa Bukoba Vijijini ili nao waweze kufaidika na rasilimali inayopatikana kwenye maeneo yao. Amelinganisha zile kodi ama yale mafao ambayo yanatolewa na Makampuni ya Migodi ili kuwapa watu ambao wako katika maeneo ya mgodi na hili la samaki.

Ukiliangalia kwa makini kuna tofauti kubwa sana. Tofauti iliyopo ni kwamba, hawa wenye madini hawanunui hayo madini kutoka kwa wananchi wa maeneo hayo. Kwa hiyo, hawawezi kuwapandishia ama kuwashushia bei wale wananchi kwa sababu ya ku-*compensate* hiyo kodi ambayo wanailipa kwa Serikali. Hilo inabidi uliangalie kwa makini kwa sababu ukiliweka kwenye viwanda vya samaki na viwanda hivyo hivyo ndiyo vinanunua samaki kwa wale wale wavuvi, vitawapunguzia bei wavuvi ili waweze ku-*compensate* hiyo gharama ambayo baadaye watailipa kwa Serikali. Kwa hiyo, kuna utata ingawa ni hoja nzuri, tutaipeleka, tutaangalia kama inawezekana.

Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, tumia dakika kama moja na nusu tu kwa sababu karibu tunafikia *guillotine*.

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niondoe tu hilo ombi langu la kuongea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa kweli sasa bado dakika kumi na kwa hiyo itabidi tuingie katika kupitisha mafungu haya bila mjadala wowote. Waheshimiwa Wabunge, mtaona umuhimu wa kushughulikia hizi kanuni na ndiyo maana nimeunda Kamati, kwa sababu ni kweli kuna kazi ya kufanya hapa. Ningependa sana kutoa muda, lakini kanuni zinatupeleka mkondo huu, ambao hauwezeshi kuweza kufuatilia mambo ya Serikali vizuri.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 – *Finance and Accounts* ... ... .... ...... Sh. 223,539,000/=
Kif. 1003 – *Policy and Planning* …. … …. …. Sh.1,995,377,100/=
Kif. 2001 – *Industry* …. ….. ….. ….. ..... ..... ....Sh.5,348,918,800/=
Kif. 3001 – *Commerce* … ….. …. ….. .... ...... Sh.3,385,661,600/=
Kif. 3002 – *SADC* …. …. ….. ….. ….. … ... Sh. 144,592,089/=
Kif. 3004 – *Trade Practices Bureau Agency* …. … Sh. 191,407,500/=
Kif. 3005 – *Trade Practices Tribunal* …. …. ….. Sh. 255,000,000/=
Kif. 4002 – *Marketing Development* ….. ….. Sh. 738,508,600/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MATUMIZI YA MAENDELEO**

Kif. 1001 – *Administration and General* …. ….. Sh. 150,000,000/=
Kif. 1003 – *Policy and Planning* ….. ….. ….. … Sh. 946,000,000/=
Kif. 4002 – *Marketing Development* …. ….. …… Sh.1,906,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge limekaa kama Kamati ya Matumizi, limeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, kwa mwaka wa 2006/2007 kwa mafungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo basi, Bunge lako Tukufu linayakubali makadirio hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa mwaka 2006/2007 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, kuna matangazo machache hapa. Tangazo kutoka Wizara ya Kilimo limeletwa na Naibu Waziri, Mheshimiwa Christopher K. Chiza kwamba, wakati wa Semina ya *ASDP*, ule Mpango Kabambe wa Mambo ya Kilimo, kuna baadhi ya Wabunge hawakupata makabrasha muhimu ya Semina hiyo, kwa sababu mbalimbali; hawakuwepo na kadhalika. Kutokana na umuhimu wa kuuelewa Mradi huu mkubwa, Wizara ya Kilimo, imeandaa makabrasha ya kutosha kwa wale ambao hawajayapata na yote wanaweza kuyapata kupitia Ofisi ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa hiyo, mtaelekezwa.

Mheshimiwa Christopher K. Chiza, ameacha namba yake ya simu hapa, sasa sijui kwa haraka kama watu wanaweza kushika ni 0744 759117, ni rahisi sana. Nashauri Mheshimiwa Naibu Waziri, uweke tangazo pia linaloelekeza mahali ambapo wanaweza kukupata kwa urahisi ili waweze kupata hayo makabrasha. Waheshimiwa Wabunge, nimepokea malalamiko mawili yanayopingana. Moja ni kutoka Chombo cha Habari cha *ITV,* wakilalamika kwamba, tarehe 02 Agosti, 2006, Mheshimiwa Adam K. Malima, Mbunge wa Mkuranga alipokuwa anachangia, hakuwatendea haki. Lakini wakati huo huo, nimepokea barua kutoka kwa Mheshimiwa Adam K. Malima anasema kwamba,

matangazo ya *ITV* kukanusha kile alichosema hayakumtendea haki. Kwa hiyo, nimeita pande zote mbili, wameniletea makaratasi yao na upande wa *TV* wameleta na kanda. Namkabidhi Mheshimiwa Juma Suleiman Nh'unga, Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ili aweze kulitazama suala hili kwa mapana na kuweza kuleta kwangu taarifa ili tuweze kutenda haki. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nikumbushie tu juu ya ratiba ilivyo. Kesho ni Sikukuu ya Nane Nane. Lakini Wizara ya Maliasili na Utalii, imeandaa onesho muhimu sana kwa namna ya *presentation,* saa moja jioni kwenye ukumbi wetu wa zamani na Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuwa ni mgeni rasmi. Waheshimiwa Wabunge, mnaombwa kuhudhuria kwa sababu itatusaidia sana kupata uelewa zaidi kuhusu utalii katika nchi yetu. Ratiba baada ya hapo sasa inakuwa Jumatano tarehe 09 Agosti, 2006, tutasikiliza Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Alhamisi tarehe 10 Agosti, 2006 itakuwa ni zamu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kwa wiki hii tunahitimisha Ijumaa, kwa kumsikiliza Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, akiwasilisha sasa makadirio ya Wizara yake, hiyo ni tarehe 11 Agosti, 2006. Mengine zaidi tutakuelezeni kuhusu wiki ijayo, ambayo ndiyo ya mwisho ya kufunga Shughuli za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, niseme tu siku ya Jumatano Mheshimiwa Job Y. Ndugai, saa 7.30 mchana atanikabidhi matokeo ya kazi waliyoifanya ya kurekebisha Kanuni za Bunge. Naomba Wajumbe wote wa Kamati ya Kanuni, wawepo kwenye ofisi pale Ukumbi wa Spika, ili kwa pamoja tuweze kupokea na hapo tuanze mchakato wa kushauri upande wa Serikali na vikao vingine ili tuweze kuzirekebisha hizi kanuni zetu, ambazo kwa kweli hata ninyi wenyewe mnaona, zinaendelea kutupa shida katika kufikia kupata tu majibu ya maswali ambayo wanauliza wananchi na ninyi ndiyo mnauliza kwa niaba yao. Nawashukuru sana Kamati wamefikia tamati, tulikuwa tunauliza mara kwa mara, sasa tunapata majibu. Natumaini kutakuwa na ushirikiano wa pamoja ili tuwe na kanuni bora zaidi kuliko zilizopo hivi sasa, tuendeshe Bunge kwa namna ambayo inakidhi haja ya kisasa na matazamio ya wananchi. *(Makofi)*

Mwisho kabisa, nilitangaza wakati natangaza mwisho wa mgogoro wa Yanga kwamba, Yanga ndiyo *club* kubwa hapa nchini. Hiyo ni kweli, lakini ni kweli kwa idadi ya wanachama. Bado ukweli unabaki kwamb, *club* bora nchini ni Simba. *(Kicheko/Makofi)*

Baada ya kusema hayo, sasa naliahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.47 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano,*
*Tarehe 9 Agosti, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*